# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao



1

Njozi ya Zamani yananena Sasa


2

Huku mawazo yake yakiwa mbali, msomi mmoja alikuwa akisafiri kwa treni hali akiwa amebobea katika usomaji. Mwangalizi (conductor)akapita akiulizia tiketi. Msomi akachomeka mkono wake katika mifuko yote bali hakuipata. Akaanza kutafuta tena kama kwa hasira .
Hivyo mwangalizi akasema, kwa upole, Usijali, bwana, utakapoipata, itume kwa kampuni. Nina hakika unayo. Msomi alijibu kwa hofu Lakini huelewi imenipasa kuipata sasa! Ninaihitaji ile tiketi ili nifahamu ni wapi ulimwenguni ninakoelekea! Mamilioni ya watu ulimwenguni wanauliza, Ni wapi ulimwenguni tunakoelekea? Wakati ujao yaelekea haueleweki. Wamechanganyikiwa. Wanashangaa dunia yetu inaelekea wapi. Hatuhitaji kuwa na wasiwasi tena. Miaka elfu mbili na mia sita iliyopita ndoto ya mfalme wa zamani ilielezea historia ya dunia Yetu.



3

Wanasayansi wanasema ya kwamba sisi sote huota ndoto kwa kawaida mara kadhaa kila usiku.
Lakini ndoto zetu nyingi, hatuzikumbuki.


4

Pengine ndoto ya kukumbukwa zaidi iliyopata rekodiwa katika historia ilitokea usiku mmoja zaidi ya miaka 2,600 iliyopita katika ufalme wa kale wa Babeli.
Kisa cha ndoto kimeandikwa vema, kiliandikwa na kisha kikaelezwa na mtu aliyepitia katika uzoefu wake.

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao



5

Kitabu cha Biblia cha Danieli, sura ya pili, kinaeleza kisa.
Hata hivyo, mtu aliyepata ndoto hii, mfalme mwenye nguvu Nebukadneza, hakuweza (au asingeweza) kukumbuka kile alichokiota! Alijua haikua ndoto ya kawaida. Alijua ndoto hii yenye fumbo lazima ilikuwa na tafsiri ya muhimu sana.
Na kwa kweli, ilikuwa hivyo!


6

Mungu alikuwa amempatia ndoto iliyokuwa ikitupatia kwa ufupi historia ya dunia--hasa ya Ulaya na Mashariki ya Kati--tokea nyakati za Nebukadneza hadi mwisho wa wakati!


7

Mungu ashukuriwe ya kwamba alishiriki pamoja nasi kile ambacho kipo katika wakati ujao.
Babeli, ufalme wa kwanza wa dunia, ulikuwa ndiwo mkubwa kuliko falme zote, wenye utajiri kuliko zote, na wenye nguvu kuliko falme zote katika ulimwengu wa wakati ule.
Ulikuwa pia na mfalme aliyekuwa na nguvu kuliko wote.
Huyu kiongozi wa watu alikuwa amefaulu kwa kutumia nguvu kuwaweka chini maadui zake mmoja baada ya mwingine hadi ufalme wake uliposimama kama Malkia wa mataifa.


8

Katika mwaka wa pili wa utawala wake, Mfalme Nebukadneza alikweda kitandani huku akijiuliza kama ufalme wake ungedumu kwa muda mrefu kiasi gani.
Yeye, kama watawala wengine, alitaka kujua juu ya wakati ujao.
Usiku ule, Mungu alitizama chini toka mbinguni na akachagua kumkabidhi huyu mtawala wa kiimla aliyekuwa pia mkarimu sura ya wakati ujao.

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao


9

Wakati mfalme alipoamka toka katika usingizi wake wa mang'amung'amu, alikuwa na wasiwasi.
Alikuwa ameona ndoto, na alijua kwamba ilikuwa na jambo la muhimu sana, lakini hakuweza kukumbuka ni jambo gani?
Kwa Wababeli ndoto zilikuwa na umuhimu sana, na mfalme alitaka kujua ndoto na tafsiri yake.


10

Kwa kweli, alikuwa na wanajimu, wachawi, waganga, na wasihiri.
Hakika wangeweza kumwambia ilikuwa na nini (hiyo ndoto) na maana yake.
Licha ya kuwa ni mapema sana, waliitwa mahakamani.
Walipoingia na kusimama mbele za mfalme, aliwaambia



11

(Fungu: Danieli 2:3)
...Nimeota ndoto, na roho yangu imefadhaika hata niijue tafsiri yake.
Danieli 2:3


12

Watu hawa walikuwa kama wengi wanaojidai kujua na kutabiri juu ya wakati ujao.
Wangeliweza kukisia katika kutafsiri ndoto,
lakini kwa kweli hawakujua maana ya ndoto.
Walisimama kwa muda. Hatimaye wakasema,



13

(Fungu:Danieli 2:4)
....Ee Mfalme, uishi milele; tuambie sisi watumishi wako ile ndoto, nasi tutakuonyesha tafsiri yake.
Lakini ujasiri wao ulipotea mara, wakati huyu mfalme mwenye kutakabari, hali akiwa amechoshwa na uchuuzi wao, aliposema,



14

(Fungu: Danieli 2:5,6)
Mfalme akajibu, akawaambia Wakaldayo, (uamuzi wangu ni thabiti):

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao



15

Neno lenyewe limeniondoka; msiponijulisha ile ndoto na tafsiri yake, mtakatwa vipande vipande,



16

na nyumba zenu zitafanywa jaa.



17

Bali kama mkinionyesha ile ndoto na tafsiri yake, nitawapa  zawadi



18

na thawabu na heshima nyingi; basi nionyesheni ile ndoto na tafsiri yake.'
Mafungu 4-6.



19

Kwa mara nyingine wakajaribu kumfanya mfalme aeleze ndoto. Mfalme alikuwa amewang'amua sasa ya kwamba walikuwa walaghai. Aliwatisha tena, hatimaye wakakiri,



20

(Fungu: Danieli 2:10, 11)
Wakaldayo wakajibu mbele ya mfalme, wakasema, 'Hapana mtu duniani awezaye kulionyesha neno hili la mfalme;



21

kwa maana hapana mfalme, wala bwana, wala liwali, aliyetaka neno kama hili kwa  mganga, wala kwa mchawi wala kwa Mkaldayo



22

....wala hapana mwingine awezaye kumwonyesha mfalme neno hilo ila miungu,wasio na kikao pamoja na wenye mwili.
Danieli 2:10,11.

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao



23

Biblia yasema mfalme alighadhibika na kuwaamuru askari wake kuwaua wenye hekima wote.


24

Bahati mbaya, Danieli na vijana watatu wa Kiebrania pamoja naye walikuwa katika kundi la wenye hekima, ingawa hawakuwepo pamoja na wenye hekima wakati mfalme alipodai maelezo ya ndoto yake.

Wakati askari walipokuja kumchukua Danieli ili wakamuue, alishtuka,lakini akaomba muda ili apate kuwasiliana na Mungu ambaye makazi yake hayakuwa pamoja na wenye mwili, na kuuliza hekima ya kumfahamisha mfalme ndoto yake. (Mafungu 12 - 15).


25

Mfalme, kwa sababu ya heshima yake kwa huyu kijana mwaminifu, alimpatia Danieli muda wa kuzungumza na Mungu wake -- Mungu wa uumbaji. Wajibu mkubwa kiasi gani uliwekwa mabegani mwa Danieli.

Siyo tu maisha yake na ya rafiki zake watatu yaliwekwa rehani, bali pia maisha ya wenye hekima wote wa Babeli!

Danieli alirejea nyumbani mwake ambapo alieleza hali.


26

Wote walililia rehema za Mungu wa mbinguni ili kufunua siri hii, ili wasiuawe pamoja na wenye hekima wengine wote wa Babeli.

Ulikuwa ni mkutano wa maombi wa muhimu kiasi gani huu!

Vijana wa Kiebrania wanne wakisali kwamba Mungu afunue ndoto ya mfalme mpagani kabla ya tarehe ya kutisha! (Mafungu 16 - 18).

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao


27

Biblia yasema ya kwamba Mungu wa Danieli usiku ule ule alifunua hii ndoto ya siri katika njozi ya usiku.
Mungu wa mbinguni hakushindwa kusikia na kuheshimu sala zile!
Hivyo Danieli akambariki Mungu wa mbinguni na kusema,



28

(Fungu: Danieli 2:23)
Nakushukuru, nakuhimidi, Ee Mungu wa baba zangu, uliyenipa hekima na uwezo,



29

ukanijulisha hayo tuliyotaka kwako; maana umetujulisha neno lile la mfalme. Fungu la 23.
Kulikuwa na shangwe kiasi gani mioyoni mwa Danieli na marafiki watatu wa Kiebrania!
Danieli alikwenda haraka kwa mkuu wa mauaji, Arioko, kama Biblia isemavyo:



30

(Fungu: Danieli 2:24)
Basi Danieli akaenda kwa Arioko, aliyewekwa na mfalme kuwaangamiza wenye hekima wa Babeli;



31

Alikwenda akamwambia hivi: Usiwaangamize wenye hekima wa Babeli. Niingize mimi mbele ya mfalme, nami nitamwonyesha mfalme ile tafsiri.
Danieli 2:24


32

Danieli alipokuja mbele za mfalme, Nebukadneza alimuuliza kama alikuwa anaweza kumfahamisha kile yeye mfalme alichokiota--pamoja na tafsiri yake.
Hebu tutazame jinsi Danieli alivyomjibu mfalme:

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao



33

(Fungu: Danieli 2:27,28)
Ile siri aliyoiuliza mfalme, wenye hekima hawawezi kumfunulia mfalme; wala wachawi wala waganga, wala wanajimu;




34

Lakini yuko Mungu mbinguni afunuaye siri, naye amemjulisha mfalme Nebukadneza mambo yatakayokuwa siku za mwisho... (Mafungu 27 - 28).



35

Tambua ya kwamba Danieli hakutaka sifa kwa ajili ya ujuzi wake.
Alijua kwamba ni Mungu pekee awezaye kufunua juu ya wakati ujao.



36

(Fungu: Isaya 46:9,10)
Bila ya shaka alikuwa amejifunza Isaya 46:9,10:
...Maana mimi ni Mungu, wala hapana mwingine; mimi ni Mungu, wala hapana aliye kama mimi;



37

nitangazaye mwisho tangu mwanzo,na tangu zamani za kale mambo yasiyotendeka bado; nikisema, Shauri langu litasimama, nami nitatenda mapenzi yangu yote.


38

Hekima ilitoka kwa Mungu, aliyechukua nafasi hii kueleza kwa ufupi historia ya dunia kwa zaidi ya miaka 2,600 kwa Mfalme Nebukadneza na kwetu.
Kwanza, Danieli anaeleza uhalisi wa ndoto hii ambayo mfalme aliiota:



39

(Fungu: Danieli 2:29)
Wewe, Ee mfalme, mawazo yako yaliingia moyoni mwako kitandani pako ya mambo yatakayokuwa halafu;



40

na yeye afunuaye siri amekujulisha mambo yatakayokuwa. [katika siku za baadaye]
Danieli 2:29.

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao



41

(Fungu: Danieli 2:31)
Kisha, Danieli anaeleza ndoto:
Wewe, Ee Mfalme, uliona, na tazama, sanamu kubwa sana.



42

Sanamu hii, iliyokuwa kubwa sana, na mwangaza wake mwingi sana,ilisimama mbele yako; na umbo lake lilikuwa lenye kutisha.
Fungu 31.



43

Je, si waweza hata kumsikia mfalme akisema kwa msisimko,
Ndiyo, ndiyo-ndiyo hiyo! sanamu ya kutisha, ikisimama juu kuliko vyote!
Danieli anaieleza ndoto kwa uwazi kiasi kwamba Nebukadneza hana shaka hiyo ndiyo ndoto ile ile aliyoiota.



44

(Fungu: Danieli 2:32,33)
Kisha Danieli anaendelea:
Na sanamu hii kichwa chake kilikuwa ni cha dhahabu safi; kifua chake na mikono yake ni ya fedha; tumbo lake na viuno vyake ni vya shaba;



45

miguu yake ni ya chuma; na nyayo za miguu yake nusu chuma na nusu udongo.



46

Kwa mshangao, Nebukadneza anasikiliza Danieli anapoeleza sehemu zote zitengenezazo sanamu sawasawa kabisa na jinsi alivyoiona katika ndoto.
Kichwa kilikuwa ni dhahabu safi ing'aayo.
Kifua pamoja na mikono, ilikuwa ni madini yenye upungufu kidogo wa mng'ao (ukilinganisha na dhahabu) - Fedha.
Tumbo na viuno vyake vilikuwa shaba.
Miguu yake ilikuwa chuma, na nyayo zilikuwa mchanganyiko wa udongo na chuma.

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao



47

(Fungu: Danieli 2:34,35)
Nawe ukatazama hata jiwe likachongwa bila kazi ya mikono,



48

nalo jiwe hilo likaipiga sanamu miguu yake, iliyokuwa ya chuma na udongo, likaivunja vipande vipande.



49

Ndipo kile chuma, na ule udongo, na ile shaba, na ile fedha, na ile dhahabu, vilivunjwa vipande vipande pamoja



50

vikawa kama makapi ya viwanja vya kupepetea wakati wa hari; upepo ukavipeperusha hata pasionekane mahali
pake;



51

Kilichofuata mfalme lazima alishtuka kuona jiwe likitoka mbio mahali asipopajua na likiwa na kasi kubwa sana, likaipiga miguu ya sanamu, likaisaga saga, na kisha kwa mshindo likaivunja vunja na kuiponda ponda sanamu nzima hadi ikawa mavumbi laini kiasi kwamba upepo ulifutilia mbali bila kuacha alama.



52

(Fungu: Danieli 2:35)
Na lile jiwe lililoipiga hiyo sanamu likawa milima mikubwa likaijaza dunia yote.
Danieli 2: 29-35

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao



53

Ndiyo,Danieli, lazima mfalme alisema, jiwe lilikatwa bila ya mikono ya mtu na kusaga sanamu na kuwa mlima ulioijaza dunia.
Ndoto nzima ilikuwa tu kama jinsi mfalme alivyoiota. Fikiria jinsi Nebukadneza alivyoshangaa kuelezwa na huyu kijana aliyeheshimika ndoto yake kwa undani kabisa kama jinsi alivyoiona yeye mwenyewe!


54

Jambo moja lazima lilikuwa bayana kabisa kwa mfalme, hakuna mtu ambaye angeweza kufunua hili kwa Danieli, hakuna mtu awezaye kueleza kile alichokiota mtu mwingine! Ingekuwa tu imetokea kwa uwezo wa ki-ungu.



55

Yawezekana kabisa mfalme alijihoji kwamba ndoto hii ilikuwa na uhusiano gani naye. Twaweza kuwa na wazo la namna iyo hiyo. Hata hivyo, ndoto ya Nebukadneza, inatabiri kuinuka na kuanguka kwa mataifa muhimu ya dunia.
Falme zilizowakilishwa katika ndoto hii zimeathiri kwa njia fulani kila taifa duniani, hasa nyakati hizi za kisasa.



56

Kwa maneno machache tu, Mungu alifupisha mambo muhimu ya historia tangu wakati wa Babeli - miaka 600 kabla ya Kristo - hadi kilele cha historia ya Dunia.
Hatimaye, Danieli anafikia katika kiini cha ndoto.



57

(Fungu: Danieli 2:38)
Huku akimkabili mfalme usoni, Danieli alisema: Wewe u kichwa kile cha dhahabu.
Fungu la 39.
Babeli ilikuwa kichwa -- taifa la dhahabu safi!
Tabasamu la ridhaa lazima lilitokea usoni mwa mfalme aliposikia maneno haya.


# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao


58

Ushindi wa kijeshi pamoja na fahari ya sanaa ya Babeli ilizidi zote. Wanahistoria wanathibitisha ya kwamba dhahabu ilikuwa ni alama iliyostahili kuwakilisha ufalme wa Babeli.



59

Dhahabu ilitumika kwa wingi katika kupamba majengo ya Babeli. Tazama maelezo ya mwanahistoria mmoja juu ya jiji hili kuu la kale:



60

Likiwa katika bustani ya mashariki; likiwa limejengwa katika mraba kamili...likiwa na handaki au mfereji kulizunguka.......



61

malango yake ya shaba, bustani zake zikiwa zimeinuka tuta juu ya tuta...ikulu zake mbili za kifalme.......



62

Pale, nchi yote ikiwa imelala chini yake, malkia katika utukufu usio na kifani.......



63

lilisimama jiji hili, makao makuu yanayostahili ya ufalme uliowakilishwa na kichwa cha dhahabu.
- Uriah Smith, Unabii wa Danieli na Ufunuo, Uk. 33, 34.



64

Bustani za ajabu za Babeli zilikuwa kati ya Maajabu Saba ya Ulimwengu wa Kale!

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao


65

Kama Danieli angelikuwa mwanasiasa hodari akijaribu kujijengea jina lake katika Babeli, angeachia ufasiri wake wa ndoto hapa. Lakini Danieli alikuwa na ujumbe ambao Mungu alitaka ufunuliwe kwa dunia--ujumbe ambao haukuwa kwa wakati wake tu, bali pia ambao ungekuwa muhimu hadi mwisho wa historia ya Dunia.



66

(Fungu: Danieli 2:39)
Hivyo Danieli kwa unyenyekevu lakini kwa ujasiri alitamka kwa mfalme hivi:
Na baada ya zamani zako utainuka ufalme mwingine mdogo kuliko wewe;
Danieli 2:39.


67

Yawezekana kabisa tabasamu ya mfalme ilipotea upesi mara aliposikia maneno hayo ya Danieli. Mtawala huyu mwenye kiburi wa Babeli yawezekana hakuruhusu kamwe wazo la kwamba taifa jingine lolote lingepata kuitawala dunia.



68

Kwa kweli, wanaakiolojia wamechimbua bamba za udongo zilizoandikwa na Nebukadneza maneno haya:



69

Ngome za Esagila na Babeli niliziimarisha na kuthibitisha jina la utawala wangu milele.



70

(Fungu: Danieli 4:30)
Biblia yasema ya kwamba Nebukadneza mwenye kiburi akanena, akasema, 'Mji huu sio Babeli mkubwa,



71

nilioujenga mimi, uwe kao langu la kifalme, kwa uwezo wa nguvu zangu, ili uwe utukufu wa enzi yangu?' Danieli 4:30
Hata hivyo, Mungu alisema ya kwamba mamlaka nyingine ingeinuka ambayo ingeuondoa ufalme wa dhahabu wa Babeli.
Na Danieli aliishi na kushuhudia hilo likitokea.



72

Wakati wa utawala wa Belshaza, mjukuu mwenye majivuno na kiburi wa Nebukadneza, Koreshi Mmedi aliuzingira Babeli.



73

Mwezi wa Oktoba 13, 539 K.K., ufalme wa dhahabu wa Babeli ulifikia mwisho usio na utukufu!


74

Tambua ya kwamba Mungu alikuwa ametabiri kwa yakini kabisa na nani na jinsi gani jiji lingetwaliwa. Karibia miaka 200 kabla ya kuanguka kwa Babeli,



75

(Fungu: Isaya 45:1)
Mungu, kupitia kwa nabii Isaya , alisema:
Haya ndiyo BWANA amwambiayo Koreshi, Masihi wake, ambaye nimemshika mkono wake wa kuume, ili kutiisha mataifa mbele yake



76

nami nitalegeza viuno vya wafalme; ili kufungua milango yake, hata malango hayatafungwa.
Isaya 45:1.



77

Mungu alieleza hata kwamba ni nani ambaye angeitenda kazi hii: Koreshi Mmedi, miaka 150 kabla ya kuzaliwa kwake.

1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao



78


Koreshi asingeweza kuvunja kuta, kwani zilikuwa ndefu sana, na nene sana, hivyo akabuni njia nyingine:
Angeligeuza mwelekeo wa maji ya mto ambao ulikuwa ukipita katikati ya jiji, na jeshi lake lingepita chini ya mto (pakavu) hadi walipopata njia ya kuingilia jijini.
Mtu fulani, kwa sababu ya uzembe au usaliti, aliacha malango ya ndani makubwa ya shaba bila ulinzi na yakiwa wazi!


79

Askari wa Koreshi waliingia jijini na kumuua mfalme na waheshimiwa wake walipokuwa wakinywa mvinyo kwa kutumia vyombo vya dhahabu vilivyochukuliwa na Mfalme Nebukadneza wakati alipoliteka jiji la Yerusalemu.
Alikuwa amepora vyombo vya dhahabu toka kwa hekalu la Sulemani, miaka ya nyuma.


80

Danieli alikuwa ametabiri ya kwamba baada ya ufalme wa Babeli, ufalme mwingine ulio mdogo kwa Babeli, uliowakilishwa kwa kifua na mikono ya fedha, ungechukua madaraka.



81

Serikali ya Wamedi na Waajemi ilikuwa kwa kweli ndogo kwa Ufalme uliotukuka wa Babeli, lakini ulitawala Mashariki ya Kati kwa karne mbili.
Danieli alitabiri ya kwamba ufalme wa fedha ungekuwa na mipaka yake pia:



82

(Fungu: Danieli 2:39)
...Na baada ya zamani zako....ufalme mwingine wa tatu, wa shaba, utakaoitawala dunia yote.
Danieli 2:39
Je, hili lilitokea? Kweli, hakika!

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao


83

Utabiri wa sanamu hii ya madini, tumbo la shaba na kiuno cha  shaba, ulitimia wakati Jenerali aliyetukuka , Aleksanda Mkuu, alipomshinda Dario wa tatu wa Uajemi katika Pambano la Arbela mwaka wa 331 KK na hivyo ufalme wa tatu ukawa Uyunani!


84

Katika umri wa ujana wa miaka 25, kijana Aleksanda akawa mtawala wa moja ya falme kubwa sana iliyowahi kuwepo duniani.



85

Mwana historia wa Kiyunani Arian, akiandika juu ya Aleksanda, alisema,
Nina amini  ya kwamba hakukuwa na taifa,  jiji, wala watu....ambapo jina lake halikufika...




86

Yaonekana kwangu ya kuwa kumekuwa na mkono wa kimbingu uliopelekea kuzaliwa kwake na matendo yake.
- Maktaba ya Kihistoria, kitabu cha 16, sura ya 12.


87

Sawa sawa kabisa na madini ya tatu katika ndoto ya Nebukadneza,  silaha ambazo kwa wingi zilivaliwa na jeshi la Kiyunani lililokwenda kwa miguu , zilitengenezwa kwa shaba.


88

Aleksanda alikufa kwa homa kabla ya siku yake ya kuzaliwa ya mwaka wake wa 33.
Baada ya kufa kwake, ufalme wake ulidhoofika na kugawanyika sehemu kadhaa hadi hatimaye;



89

Juni 22, 168 K.K.,katika Pambano la Pydna, ufalme wa Aleksanda Mkuu ulimalizika, miaka 144 baada ya kufa kwake.
-Historia ya Rumi, kitabu cha 3, Sura ya 10.

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao



90

Sasa unakuja utawala wa kutisha kuliko zote kati ya hizi falme za kale.
Unakumbuka kwamba Mungu alitabiri ya kwamba kungekuwa na falme nne za dunia, moja baada ya nyingine.




91

Kwa kweli, miguu ya chuma ilieleleza vyema mamlaka katili iliyokuwa ikiangamiza ya  ufalme wa nne wa dunia.
Hivi ndivyo Danieli alivyoeleza kwa mfalme:



92

(Fungu: Danieli 2:40)
Na ufalme wa nne utakuwa na nguvu mfano wa chuma...... (Danieli 2:40).


93

Kaisari wake walijiita miungu na walidai ibada na kicho toka kwa watu wote.
Ulikuwa wakati huu wa utawala wa Kirumi  wakati matukio mawili yenye umuhimu sana yalipotokea katika taifa hili.


94

1. Yesu alizaliwa katika Bethlehemu.
Alikuwa ni Gavana wa Kirumi aliyetoa tamko la kuwaua watoto wote wa kiume waliokuwa na umri wa miaka miwili kwenda chini katika Bethlehemu.
Alitarajia kumuua Yesu . Na


95

2. Yesu alisulubiwa katika Yudea, chini ya mamlaka ya Kirumi.
Liwali wa Kirumi aliruhusu Yesu ahukumiwe.
Yesu alipigiliwa msalabani na askari wa Kirumi,  na muhuri wa Kirumi uliwekwa juu ya kaburi la Yesu kujaribu kumzuia humo.
Sasa mfumo wa unabii ukabadilika.
Hakuna UFALME WA DUNIA mmoja ambao ungefuatia ule wa Rumi.

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao



96

(Danieli 2:41,43)
Danieli aliandika: Na kama vile ulivyoziona hizo nyayo za miguu na vidole vyake, kuwa nusu udongo wa mfinyanzi, na nusu chuma,




97

ufalme ule utakuwa ufalme uliogawanyika.….



98

...watajichanganya nafsi zao kwa mbegu za wanadamu; lakini hawatashikamana,



99

kama vile chuma kisivyoshikamana na udongo. Danieli 2:41,43


100

Kwa maneno mengine, nabii alitabiri, hakutakuwa na ufalme wa tano wa dunia, bali utakuwa ni mgawanyiko wa ufalme wa chuma wa Rumi utakaotokea.



101

Rumi ilikuwa igawanyike katika falme kadhaa


102

Nyuzi nyuzi za chuma za huu ufalme mkubwa wa Rumi ambao ulitawala kwa karibu miaka 600 zilisambaa.

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao


103

Kwa njia ya anasa, mchafuko wa kisiasa, na uozo wa maadili, Rumi ilipoteza msimamo wake na nguvu yake, ikawa mawindo rahisi kwa makabila makorofi yaliyoanza kuvamia ufalme kati ya 351 B.K. na 476 B.K.



104

Mfalme Augustus aliondolewa, na Rumi ikagawanyika katika sehemu ndogo ndogo nyingi zilizowakilishwa na nyayo na vidole vyake vilivyokuwa mchangayiko wa chuma na udongo katika ile sanamu.



105

(Fungu: Danieli 2:43)
Na kama ulivyokiona kile chuma kimechanganyika na udongo wa matope, watajichanganya nafsi zao kwa mbegu za wanadamu;



106

lakini hawatashikamana, kama vile chuma kisivyoshikamana na udongo.
Danieli 2:43.
Uvamizi wa hawa wakorofi katika Rumi uliigawanya falme.
Migawanyiko hii iliyowakilishwa na nyayo za chuma na udongo, ilitengeneza misingi ya mataifa yaliyopo Ulaya leo.



107

Kumi kati ya hayo makabila makatili yanaorodheshwa hivi na wanahistoria wengi:
Alamanni - Wajerumani, Burgundians - Waswisi, Franks - Wafaransa, Lombards - Waitalia, Saxons - Waingereza



108

Suevi - Wareno, Visigoths - Wahispania
kisha Heruli, Osrogoths, Vandals - wamepotea au kuchanganyika na mataifa mengine yaliyowazunguka.

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao



109

Tamko la Mungu ya kwamba hizi falme kamwe hazitaunganika kama ufalme wa dunia tena linazuia kile haya mataifa yanachokifanya.




110

Ulaya itasalia katika mgawanyiko. Kamwe hawatakaa pamoja!
Hata pamoja na soko la Ulaya na Fedha ya aina moja, bado wamegawanyika.




111

Alisema kwamba hata kama watajichanganya na mbegu za wanadamu. Kwa maneno mengine, jamii za kifalme zingeoana.



112

Katika Ikulu ya Denmark, kipo kielelezo kionyeshacho familia za kifalme za Ulaya.
Wote walikuwa na undugu! walitarajia ingezuia vita.
La, hilo halikufanikiwa.



113

Hawakuweza kupatana. Hivyo, vita vingi vilivyokuwa Ulaya vilikuwa ni ugomvi wa kifamilia! Mungu alitabiri ya kwamba wasingeliweza kushikamana. Walijaribu kuuweka Ufalme wa Kirumi pamoja tena, lakini hili lisingedumu, kama jinsi chuma na udongo visivyoweza kushikamana!



114

Fikiria juu ya majaribio mengi ambayo yamefanyika ili kuunganisha mataifa ya Ulaya yawe pamoja tena. Nini kilitokea kwa hawa ambao wangelikuwa viongozi wa dunia, hawa waliojaribu kuiunganisha Ulaya iliyogawanyika?

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao



115

Charlemagne - ALISHINDWA, Charles V - ALISHINDWA, Louis XIV - ALISHINDWA, Napolioni - ALISHINDWA, Kaiser Wilhem - ALISHINDWA, Hitler - ALISHINDWA
Akiwa uhamishoni katika kisiwa cha Elba, Napolioni -- Yule shujaa mkubwa wa Ufaransa katika miaka ya mapema  1800-- alikiri ya kwamba Mungu alikuwa amemzidi mno.
Mungu alikuwa amewazidi mno wote!



116

Mungu alikuwa amesema, HAWATASHIKAMANA!
Kauli nzuri ifaayo kwa kumbukumbu ya wale ambao - wangekuwa - watawala wa dunia!
Hata hivyo, watu bado wanajaribu kuunganisha nchi za Ulaya pamoja, lakini haziwezi kuungana pamoja, kama jinsi Mungu alivyosema!
Wanaweza kukutana pamoja, bali hawawezi kushikamana!



117

Lazima Nebukadneza alishangazwa na haya mabadiliko katika unabii.
Mungu alitabiri maangamizi ya falme kuu nne za dunia. Alitabiri ya kwamba Rumi ingefuatiwa na mataifa kadhaa,  saba kati yao yakiwa yamewakilishwa katika Ulaya Magharibi leo -- baadhi yakiwa yenye nguvu, baadhi dhaifu, lakini yote yakiwa yamegawanyika bila matumaini.


118

Kitu gani kingefuatia?
Huku akidhihirisha furaha na ujasiri, Danieli sasa alifikia kilele cha kushtua katika kutafsiri ndoto  ya sanamu hii kuu ya madini. Aliandika



119

(Fungu: Danieli 2:44, 45)
Na katika  siku za wafalme  hao, Mungu wa mbinguni atausimamisha  ufalme ambao hautaangamizwa milele.




120

wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele.




121

Na kama vile ulivyoona ya kuwa jiwe  lilichongwa mlimani bila kazi ya mikono--




122

na ya kuwa lilivunja-vunja kile chuma, na ile shaba na ule udongo, na ile fedha,  na ile dhahabu;




123

basi Mungu aliye mkuu amemjulisha mfalme mambo yatakayokuwa baadaye; na ndoto hii ni ya hakika na tafsiri yake ni thabiti.
Danieli 2:44, 45.



124

Tukio kuu litakalofuata katika jukwaa la historia ya mwanadamu litakuwa ni kuja kwa mara ya pili kwa Kristo na kusimamishwa kwa ufalme Wake, uliowakilishwa na jiwe lililochongwa bila kazi ya mikono.
Ufalme wake utawekewa msingi, siyo kwa mikono ya wanadamu, bali kwa mkono wenye nguvu wa Mungu -- ufalme utakaoijaza dunia nzima.




125

(Fungu: Ufunuo 11:15)
Hapo utakuwa umetimizwa unabii,
.....Ufalme wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu ......naye atamiliki hata milele na milele.
Ufunuo 11:15.




126

Tazama matukio ya mwisho yaliyomo katika unabii huu wa  kushangaza wa Kitabu cha Danieli:

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao



127

Kuja kwa Yesu mara ya Pili.



128

Mataifa ya dunia yatafikia mwisho.




129

Mungu atasimika Ufalme Wake.




130

Ufalme huu utadumu milele.



131

Yesu atatawazwa kama Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana.



132

Anakuja duniani kutawala ufalme wa milele.


133

Wakati Danieli alipomaliza kumueleza mfalme tafsiri ya njozi yake hii ya kutisha, Mfalme Nebukadneza aliinuka kutoka kwenye kiti chake cha enzi na kwa unyenyekevu akajilaza chini mbele za Mungu mkuu wa Danieli, ambaye hekima yake na uwezo wake vilikuwa vimedhihirika kwa nguvu kiasi kile.

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao




134

(Fungu: Danieli 2:47)
Mfalme alimwambia Danieli, ...Hakika Mungu wenu ndiye Mungu wa miungu, na Bwana wa wafalme, awezaye kufumbua siri,......
Danieli 2:47.
Kweli, Mungu wa Danieli ndiye Mungu ninayemtaka awe Mungu wangu -- Mungu anayeshikilia maisha ya kesho mikononi Mwake!




135

Kwa kutumia hili sanamu kubwa la madini lililoonwa na Nebukadneza katika ndoto yake karne sita kabla ya kuzaliwa kwa Kristo, Mungu alifunua siri za karne zilizokuwa zinakuja!



136

Ndiyo, rafiki, Ndoto hii ni ya hakika, na tafsiri yake ni thabiti!
Safari imekaribia kuisha!
Tukio kuu linalofuata ni la Kristo kuja katika mawingu kusimika ufalme Wake wa milele.




137

Falme zilizowakilishwa na dhahabu, fedha, shaba, na chuma zote zimepita katika historia.
Na tukio linalofuata la utukufu ni la kuja kwa Bwana wetu hivi karibuni!



138

Amepanga kesho ya kupendeza ambayo imewezekana tu kwa njia ya msalaba uliomwagikiwa damu pale Kalvari.
Ni kipindi kifupi tu hadi haya yote yatakapotimia.
Sasa hivi Mungu anaandaa ufalme Wake na wale watakaokuwa sehemu ya ufalme ule.

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao



139

Twaweza kuwa na uhakika ya kuwa tutakuwa sehemu ya huo kama tu, kwa imani, tutatenda kile ambacho yule mwizi msalabani alitenda alipokuwa amening'inia kati ya mbingu na dunia akiwa karibu na Yesu.
Asingeweza kuja karibu zaidi na Yesu, lakini alijua ya kwamba alikuwa mdhambi na kwamba alihitaji kuokolewa toka kwa dhambi alizokuwa amezitenda.
Alimtizama Mwokozi wa ulimwengu na kuona damu ikichuruzika usoni pake toka katika kipaji chake kilichochomwa na miiba.
Moyo wake uliguswa. Alikiri dhambi zake na kulia,



140

(Fungu: Luka 23:42)
Ee Yesu! Unikumbuke wakati utakapoingia katika ufalme wako.
Luka 23:42.
Na Yesu alimpatia uhakika ya kwamba angekuwa naye katika Ufalme.


141

Wewe, pia, waweza kusali sala ile na kupokea uhakika ule ule ya kwamba utakuwa pamoja na Kristo katika Ufalme wake ambao utasimikwa hapa duniani hivi karibuni.



142

(Fungu: Mathayo 25:34)
.....Njoni enyi mliobarikiwa na Baba yangu; pokeeni Ufalme mliotayarishiwa tangu kuumbwa kwa ulimwengu. ...


143

Dunia hii haipo mikononi mwa mwanadamu.
Ipo mikononi mwa Mungu. Twaweza kukabili wakati ujao kwa ujasiri mkuu. Kristo atakuja hivi karibuni.
Jiwe lililokatwa bila mikono ya mtu litaliponda sanamu.
Falme za dunia zitaanguka.
Mungu ataleta ufalme wake wa Milele, wenye kudumu.

# 1 - Jinsi ya Kuujua Wakati Ujao



144

Waweza kuwa na matumaini yote katika Mungu huyu.
Waweza kumtegemea Mungu huyu.
Waweza kutulia kwa usalama kabisa mikononi mwake.
Anakuita leo.
Anakualika uje leo.
Anavuta moyo wako sasa.
Je, ungependa kusema, Ndiyo, Bwana, Nitakutegemea wewe kikamilifu. Ninatoa maisha yangu kwako sasa hivi tunaposali?

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!



1

Kuukabili Wakati Ujao Bila Hofu


2

Mchana mmoja mzuri wa kiangazi, baba na binti yake wa umri wa miaka tisa walikuwa wakiogelea baharini. Walikuwa wakiruka ruka katika mawimbi kwa muda wakati ghafla maji yalipoanza kupwa kwa nguvu.

Kwa upesi yalimchukua huyu binti mdogo kwa umbali. Babake hangeweza kumfikia. Binti alihitaji msaada kama alikuwa arejee kwenye pwani.

Kwa nasibu, badala ya kughafulika, baba aliita, Elea na ogelea kwa utulivu; usiogope. Nitarejea kukuchukua.

Kisha akaondoka mbio kufuata mtumbwi. Baba alipofika mahali pale alipomuacha binti,sasa akiwa amekuja na waokoaji, moyo wake ulivunjika. Binti yake hakuwa pale. Alikuwa amesombwa hadi mbali katikati ya bahari. Lakini walipomfikia hatimaye, msichana alikuwa akielea tu kwa utulivu kama babake alivyomuelekeza.


3

Baadaye aliulizwa jinsi gani aliweza kusalia kwa utulivu hivyo peke yake, mbali katikati ya bahari. Binti alijibu, Nilitenda tu kile ambacho Baba aliniambia nifanye. Nilijua atarejea, na sikuogopa. Tumaini la yule binti mdogo jasiri lilimtunza hai; lilimuwezesha kuendelea na hatimaye kuokolewa. Tumaini kuu linalotunza imani yetu kama wakristo ni tumaini kwamba Baba yetu wa mbinguni yu tayari kuiokoa sayari hii iliyoko katika ukingo wa uharibifu.

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!



4

(video: sek. 10) Hivi karibuni mwanasayansi mashuhuri alitaja hofu yake kwamba dunia yaweza isidumu miaka elfu mingine.
Alisema kwamba uchafuzi wa anga la dunia unaofanywa na wanadamu utasababisha joto kupanda duniani,


5

na hali hii itasababisha mawimbi ya joto la kufisha duniani na mabara kupata mafuriko kwa sababu ya kuyeyuka kwa barafu iliyopo katika ncha za dunia. Lakini wengine wanadhani dunia itaisha kwa namna tofauti.



6

(Video: Sek. 5) Baadhi husema tutajiangamiza wenyewe kwa vita ya Nyuklia.


7


Wengine wanasema tutaishiwa chakula na raslimali kwa sababu ya mlipuko wa idadi ya wakazi duniani.


8

Bado wengine husema twaweza kufutiliwa mbali wakati nyota kubwa yenye mkia ama kimwondo vitakapogongana na dunia.


9

Na kisha wapo wale wafikiriao ya kwamba siku moja wageni tokea sayari nyingine watawasili na kutuangamiza sisi sote. Wengi wetu, kwa kweli, tunayo mambo mengi zaidi ya kutufadhaisha.


10

Tunapambana na majaribio ya kupata riziki au mapatano na wengine, au maradhi na huzuni na mauti.

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!



11

Kwa wengi wetu, pengine tulio wengi zaidi, maisha siyo rahisi. Ni magumu kiasi kwamba nyakati fulani twaweza kujikuta tukitamani mara kwa mara dunia iishe!

Kwa kweli maisha hayakuumbwa ili yajaze maumivu na njaa na uchovu na msongo. Tunataka dunia iliyo bora!



12

Naam, rafiki yangu, kuna habari njema! Dunia hii INAelekea mwisho. Na IPO dunia nzuri inayokuja!



13

Karibu kila mmoja wetu angependa kujua jinsi gani na lini dunia itaisha.

Je, itaisha wakati wetu - ama miaka elfu au elfu kumi tokea sasa?



14

Na ni nani aliye sahihi kuhusu JINSI itakavyokwisha? Hakuna upungufu wa manabii wanao toa utabiri wao.




15

Lakini tatizo ni kupata manabii ambao utabiri wao ni sahihi - manabii ambao kwa kweli unabii wao unatimia!

2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!



16

(Video: Sek 15) Lakini je, wajua ya kwamba YUPO ambaye unabii wake umetimia - kila mmoja hadi wa mwisho katika huo?
Yule ambaye aweza kutuambia kwa hakika jinsi dunia inavyofikia mwisho - na kama itamalizika hivi karibuni au itadumu kwa miaka elfu zaidi?
Haipaswi kushangaza yeyote kujua ya kwamba yeye aliyeiumba dunia hii - yeye aliyekuwepo ikianza - ndiye pia ajuaye lini itaisha.
Na marafiki, Yesu Kristo, Mungu wa uumbaji, kupitia katika Neno Lake, aweza kutuchukua hadi muda ujao. Yeye ni Kiongozi wa kuaminika.
Ni nani ambaye angeweza kujua juu ya MWISHO wa dunia kuliko yeye aliyeIANZISHA?


17

Biblia yatuambia juu ya tukio la muhimu katika maisha ya Yesu Kristo.
Siku moja wanafunzi walimchukua pembeni na kumuonyesha majengo ya hekalu, ambayo yalikuwa tu yamejengwa upya na serikali ya Kirumi.


18

Lilikuwa moja ya majengo ya thamani katika Ufalme wote wa Kirumi - jengo zuri sana!
Baada ya kulitazama jengo, Yesu alitoa kauli ya kushangaza kwa wanafunzi. Alisema,



19

(Fungu: Mathayo 24:2)
...Hamyaoni haya yote? Amin, nawaambieni,



20

halitasalia hapa jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomoshwa.
Mathayo 24:2


21

Hili lilikuwa jengo kuu kuliko yote katika taifa la Kiyahudi, na Yesu alitabiri ya kwamba lingebomolewa kabisa.

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!


22

Wanafunzi walishtuka!
Na walipoenda juu kwenye mlima wa Mizeituni, walimuuliza Yesu swali ambalo sisi sote tungeuliza:



23

(Fungu: Mathayo 24:3)
Yesu alipokuwa ameketi juu ya mlima wa Mizeituni, wanafunzi walimwendea faraghani, wakamwuliza, Twambie mambo haya yatatukia lini?



24

Ni ishara gani itakayoonyesha kuja kwako na mwisho wa nyakati?
Mathayo 24:3


25

Unaona, wanafunzi walihisi kwamba kama jengo hili lilikuwa libomolewe, basi ingekuwa na uhusiano na kuja kwa Kristo na mwisho wa dunia.


26

Lakini katika kitabu cha Mathayo, sura ya 24, tunaona kwamba Yesu alikuwa akinena juu ya matukio mawili tofauti.


27

Moja ya hayo ni kuja kwa mara ya pili kwa Yesu - kuja kwake hapa duniani katika utukufu na usimikaji wa ufalme wake hapa katika sayari Dunia.



28

(Video: Sek 6) Jingine, hata hivyo, lilikuwa lile ambalo lingeonwa na watu wengi walio hai wakati ule.
Hili lilikuwa liwe uangamivu wa jiji la Yerusalemu na hekalu.
Sasa Yesu akaendelea kuwaambia wanafunzi kile ambacho kilikuwa kitokee kwa hekalu.

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!



29

(Fungu: Mathayo 24:15-16)
Alisema katika Mathayo 24:15,16; Basi hapo mtakapoliona chukizo la uharibifu, lile lililonenwa na nabii Danieli,



30

Kidokezo, limesimama katika 'Patakatifu' (asomaye na afahamu).



31

ndipo walio katika Uyahudi na wakimbilie milimani.



32

Danieli alikuwa ametabiri ya kuwa Yerusalemu ingeangamizwa.
Lakini sasa Yesu anawakumbusha wanafunzi wake maonyo ya nabii Danieli yangetimizwa karibuni.



33

Utabiri wa Danieli (Fungu: Mathayo 24:17-18 HNKK)
Alisema katika Mathayo 24:17,18: Aliye juu ya paa la nyumba yake asishuke kuchukua kitu nyumbani mwake. Aliye shambani asirudi nyuma kuchukua vazi lake.




34

Aliye shambani asirudi nyuma kuchukua vazi lake.


35

Kwa maneno mengine, Aliwaambia kukimbia ili kuokoa maisha yao, kwani walipoona majeshi yakizingira Yerusalemu, uangamivu ulikuwa umewadia.

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!



36

(Fungu: Luka 21:20)
Katika Luka 21:20, Yesu alisema: Mtakapoona mji wa Yerusalemu umezungukwa na majeshi, ndipo mtambue ya kwamba wakati umefika ambapo mji huo utaharibiwa.
Kisha akaendelea kuwaambia ya kwamba popote walipoona majeshi hayo, walipaswa kukimbia.



37

(Fungu: Luka 21:22, 24)
Kwa maana siku hizo ni siku za adhabu, ili yote yaliyoandikwa yatimie.



38

Wengine watauawa kwa upanga, wengine watachukuliwa mateka katika nchi zote



39

Na mji wa Yerusalemu utakanyagwa na watu wa mataifa mengine, hadi nyakati zao zitakapotimia. Luka 21: 22,24




40

Katika mwaka wa 66 BK, takriban miaka 33 baada ya Yesu kutoa utabiri huu, majeshi ya Kirumi, chini ya Cestius, Gavana wa Kirumi wa Shamu, alikuja kutuliza



41

ghasia iliyokuwa imezuka ndani ya Yerusalemu. Walipokuwa wamelizingira jiji, hata hivyo, jiji lilijikinga na uharibifu wa jeshi la Kirumi,



42

majeshi ya Kirumi yalirudi nyuma, yakikata tamaa kwa kushindwa kuliteka jiji.

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!



43

(Video:Sek 6) Wale waliofuata maelekezo yaliyotolewa na Yesu walifaulu kukimbia maangamivu ya jiji la Yerusalemu, na hawakuuawa wakati jiji liipochukuliwa na majeshi ya Kirumi


44

Takriban watu 1,100,000 waliuawa katika uvamizi wa kutisha. Walishindwa kufuata maelekezo ya Yesu ya kutoroka wakati jeshi la Kirumi liliporudi nyuma mwaka wa 66 BK.
Hili ni fundisho kubwa juu ya umuhimu wa kujifunza unabii na kuzitilia maanani dalili za nyakati.
Wale waliomuamini Kristo na kuziangalia dalili alizozitabiri waliokolewa, wakati wasioamini waliangamia.
Hivyo ndivyo itakavyokuwa mwisho wa dunia - waumini wanaokesha wataokolewa, wakati wasiojali na wasioamini wataangamia.



45

Habari gani juu ya hekalu la fahari? Tito, jenerali wa Kirumi aliyekuwa kiongozi katika kuliteka Jiji la Yerusalemu, alikuwa ametoa maagizo ya kutoliangamiza hekalu, lakini mmoja wa askari wake alitupa mwenge kupitia mlangoni uliokuwa ukiwaka moto,


46

Kidokezo na hekalu likawa tanuru liwakalo moto! Hakuna jiwe lililosalia juu ya jingine.


47

Utabiri wa Yesu kwa wanafunzi wake miaka 40 kabla ya maangamizi ya Yerusalemu yalitimia kikamilifu. Je,tutazidharau dalili alizotupatia Yesu kuhusu mwisho wa dunia, ama tutatii maonyo na kuwa tayari kwa kile kijacho mbele?
Tutajuaje wakati mwisho wa dunia ukiwa karibu sana?
YESU ANATUPATIA ISHARA ZILIZOWAZI .

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!



48

Hebu tuziangalie baadhi ya hizi dalili za nyakati!
Katika Mathayo 24:7, Kristo alisema,



49

(Fungu: Mathayo 24:7)
Taifa moja litapigana na taifa lingine; ufalme mmoja utapigana na ufalme mwingine.



50

Hapa na pale patakuwa na njaa na mitetemeko ya ardhi. Mathayo 24:7.
Karne ya ishirini ilikuwa ya umwagaji wa damu kuliko nyingine yoyote katika historia ya mwanadamu.



51

(Video : sek 20) Vita Kuu ya Kwanza ilishuhudia watu milioni 20 wakitolewa kafara katika madhabahu ya vita. Vita Kuu ya pili ilishuhudia maangamizi ya watu milioni 50.
Ingawa kila mmoja alidhani vurugu na chuki vingeisha, bado tunavyo vita.
Inaonekana ya kwamba dunia imekuwa kichaa. Hii ni mojawapo ya dalili za nyakati.



52

Mataifa yananena juu ya amani hali yakiandaa vita.
Unabii mwingine wa Biblia uhusuo amani na maandalizi unasema:



53

Watu watakapokuwa wanasema: 'Kuna amani na salama, 'ndipo uharibifu utakapowaangukia ghafla! 1 Wathesalonike 5:3.
Tunanena amani, lakini hakuna amani!
Kila mtu anataka amani! Lakini ni maneno matupu!


54

Biblia yasema kwamba katika nyakati za mwisho za dunia hii, mwanadamu atakuwa na uwezo wa kuiangamiza dunia.

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!





55

(Fungu: Ufunuo 11:18)
Watu wa mataifa waliwaka hasira, maana wakati wa hasira yako umefika...... Ni wakati wa kuwaangamiza wale wanaoangamiza dunia. Ufunuo 11:18.
Kamwe wanadamu hawakupata kuwa na uwezo wa kuangamiza mada halisi ambayo ndiyo iliyotumika kutengeneza dunia.



56

Pamoja na ugunduzi wa bomu la nyuklia, mwanadamu sasa anao uwezo wa kuiangamiza hata dunia.



57

Magaidi tayari wamekwisha pata njia ya kununua au kuiba baadhi ya silaha hizi za nyuklia ambazo zimelindwa sana. Baadhi ya hivi vyombo vya kufisha tayari vimepotea na kuishia katika mikono ya mtu au watu wanaosubiri kuviuza au kuvitumia.




58

Gazeti linaloheshimika sana lilishaeleza ya kwamba taarifa za jinsi ya kutengeneza bomu la nyuklia zipo katika maktaba nyingi muhimu duniani. Zipo karibu kama jinsi ilivyo kubonyeza tu kitufe katika kompyuta.




59

Ni nani aliye nazo na watafanya nini siku hizi za karibuni? Siyo kubwa kuliko sanduku tu la nguo, zaweza kuwekwa popote, na moja ya hizo yaweza kuteketeza moja ya majiji makuu ya dunia.




60

Bwana alisema kutakuwa na maafa ya kila namna siku za mwisho.




61

(Mathayo 24:7) Kutakuwa na njaa ….
Taifa moja litapigana na taifa lingine; ufalme mmoja utapigana na ufalme mwingine. Hapa na pale patakuwa na njaa na mitetemeko ya ardhi.

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!



62

Na zipo njaa mahali  pengi duniani.



63

Inakadiriwa  kwamba watu milioni 57 watakufa njaa katika mwaka huu mmoja.  Hao ni watu 156,000 watakao kufa kila siku  kutokana na njaa.



64

Kati ya mabilioni ya watu katika sayari dunia, asilimia 60 wana upungufu wa lishe, na asilimia 20 wataishia katika kufa njaa.
Yesu alisema ya  kuwa kutakuwa na njaa kama mojawapo ya dalili za mwisho.



65

Vyanzo vyenye takwimu vinatuambia kwamba wakati idadi ya watu izidipo uzalishaji wa chakula, basi njaa duniani, vifo kwa sababu ya njaa, maradhi ya jumuiya na  magomvi juu ya chakula havizuiliki.
Twawezaje kulisha ma bilioni ya watu watakaoongezeka, wakati theluthi mbili ya  wakazi wa dunia sasa wako katika njaa?



66

(Fungu: Luka 21:25)
Yesu alielezea mashaka ya saa ya mwisho ya dunia kwa kusema kwamba kutakuwa  ...katika nchi dhiki ya mataifa,wakishangaa...
Luka 21:25



67

Yesu alisema  ya kwamba kutakuwa na uharibifu:

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!



68

(Fungu: Mathayo 24:7)
Kutakuwa na njaa, maradhi, na matetemeko ya nchi mahali mahali.
Neno lililotumika kwa kiingereza pestilence lina maanisha kulingana na kamusi , pigo au ugonjwa mgeni.


69

Yapo mapigo mengi licha ya kile ambacho madawa ya kisasa yanakitenda.



70

UKIMWI, malaria, niumonia, kifua kikuu, ebola, kaswende, kisonono na kipindupindu.



71

Kidokezo Shirika la Afya la Dunia sasa linakadiria kwamba tunao watu milioni 40 wenye virusi vifahamikavyo kama H.I.V.
Mataifa mazima yatafutiliwa mbali kama hakuna njia itakayofanyika kuisimamisha hali hii.



72

Dalili nyingine ya nyakati inaonekana katika uchafuzi wa mazingira.
Biblia ilitabiri ya kwamba dunia ingezeeka. Katika Isaya 51:6, Mungu alisema,



73

(Fungu: Isaya 51:6)
Inueni macho yenu mbinguni, mkaitazame nchi chini;



74

Kidokezo Maana mbingu zitatoweka kama moshi, na nchi itachakaa kama vazi.
Ni maelezo yapi yaliyo bora zaidi yawezayo kutolewa yakieleza anga na nchi zinavyotikisika hadi mwisho!

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!



75

Kidokezo Anga katika majiji yetu mengi limejazwa na kemikali zenye sumu tunazozivuta na kuzipitisha kwenye mapafu yetu.




76

Kidokezo Vibao vilivyowekwa katika majiji mengi vinatuonya juu ya hatari ya anga lililochafuka.




77

Kidokezo Mahali pengi sasa maji si salama kunywa, kwa sababu ya vitu hatari ndani yake.




78

Limekuwa tatizo gumu sana kupata mahali pa kutupa mabaki ya Atomiki.
Watenda kazi katika eneo moja la kiwanda cha atomiki wako katika kulipwa fidia kwa sababu ya sumu ambayo imewatesa.



79

Ni wapi tutakapoweza kupata nishati na maji safi na hewa safi? Tutapata wapi chakula?




80

Pamoja na uongezekaji wa kasi wa idadi ya wakazi wa dunia, mwanadamu anakabili matatizo mazito katika kuishi Duniani!




81

(Fungu: Luka 21:25)
.... Na katika nchi dhiki ya mataifa wakishangaa........




82

Biblia yasema pia juu ya muongezeko wa matetemeko.

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!



83

(Fungu: Mathayo 24:7)
Kutakuwa  na ........matetemeko ya nchi mahali mahali. Mathayo 24:7
Tumeona uongezekaji mkubwa sana wa idadi ya matetemeko yanayotokea.




84

Kila mwaka tunayo matetemeko makuu 6,000 duniani.




85

Katika miaka 90 ambayo imepita peke yake, tumekuwa na maafa 1,500,000.



86

Kidokezo Katika kipindi kifupi tu kilichopita, tumeona matetemeko yakichukua  maisha ya watu 20,000 hadi 30,000 katika ngurumo moja.
Wengi wenu mtakumbuka  matetemeko ya hivi karibuni ambayo nchi mbalimbali zimeyapitia.




87

(Luka 21:11,25)
Biblia yasema, Kutakuwa na matetemeko makubwa ya nchi;  na  njaa na tauni mahali mahali;



88

Kidokezo na mambo ya kutisha na ishara kuu kutoka mbinguni........



89

Tena kutakuwa na ishara katika jua, na mwezi, na nyota; na katika nchi dhiki ya mataifa

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!



90

wakishangaa kwa uvumi wa bahari na msukosuko wake.
Luka 21:11,25.



91

Tambua ya kwamba inasema upepo na mawimbi vitakuwa vikiunguruma.
Duniani kote, tumeona hali ya hewa isiyo ya kawaida.
Tufani, zinazokuja na mawimbi yajaayo na kupwa; vimbunga; visulisuli; volkano - haya yote yanaongeza idadi ya uharibifu kiasi cha kutisha katika vitu na maisha ya watu.



92

Biblia inatupa dalili nyingine. Hali za maadili wakati wa mwisho.
Yesu alilinganisha hali ya dunia katika siku za mwisho na ile ya Sodoma na Gomora, miji miwili kati ya miji miovu sana ya dunia iliyopata kuwepo.
Mungu hatimaye aliiangamiza kwa moto toka mbinguni.



93

Itakuwa kama ilivyotokea wakati wa Lutu. Watu waliendelea kula na kunywa, kununua na kuuza, kupanda mbegu na kujenga.
Ndivyo itakavyokuwa siku ile Mwana wa Mtu atakapofunuliwa.



94

.........Hivyo ndivyo itakavyokuwa siku ile atakayofunuliwa Mwana wa Adamu.
Luka 17:28-30.



95

(Fungu: Yuda1:7)
Yuda aliandika, ....Kama vile Sodoma na Gomora na miji iliyokuwa kando - kando, waliofuata uasherati.....

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!


96

Paulo, akinena juu ya hali za maadili  ambazo ziliipa tabia miji  hii ,alisema,



97

(Fungu: Warumi 1:26,27)
Hata wanawake wakabadili matumizi ya asili kwa matumizi yasiyo ya asili.




98

Nao wanaume hali kadhalika, waliyaacha matumizi ya  mke ya asili wakawakiana tamaa wao kwa wao.



99

Wanaume wanafanyiana mambo ya aibu....
Warumi 1:26,27.



100

Watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye majivuno, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiowatii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi;



101

watu wasio na upendo wao kwa wao, wasio na huruma, wachongezi, walafi na wakali; wasiopenda mema,



102

wasaliti, wakaidi na wenye kujivuna; wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu.



103

Kwa nje wataonekana kama watu wenye kumcha Mungu,  lakini wataikana nguvu yake.
2 Timotheo 3:2-5

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!



104

(Fungu: 2 Timotheo 3:13)
Je, yawezekana hali ikawa mbaya zaidi? Ndiyo , nasikitika kusema;
Lakini watu wabaya na wadanganyaji wataendelea na kuzidi kuwa waovu, wakidanganya na kudanganyika.



105

Mojawapo ya dalili muhimu alizotaja Yesu ulikuwa ujio wa makristo na manabii wa uongo.
Kristo alionya kuhusu makristo na manabii wa uongo ambao wangetokea ili kuudanganya ulimwengu.



106

(Fungu: Mathayo 24:23-24)
Basi, mtu akiwaambieni siku hizo: Kristo yuko hapa au Yuko pale, msimsadiki.



107

Maana watatokea makristo wa uongo na manabii wa uongo. Watafanya ishara kubwa na maajabu ya kuweza kuwapotosha



108

hata ikiwezekana, wateule wa Mungu. Mathayo 24:23-24



109

(Fungu: Mathayo 24:26) [Union version]
Basi wakiwaambia, Yuko jangwani, msitoke; Mathayo 24:26.
Hakutakuwa na hitaji la kwenda popote, kwani Yesu alisema,



110

(Fungu: Mathayo 24:27)
Kwa maana kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi,

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!



111

hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu. Fungu 27



112

(Fungu: Ufunuo 1:7)
Na tena tunaambiwa;
Tazama! Yuaja na mawingu! Kila jicho litamwona, hata wale waliomchoma. Makabila yote duniani yataomboleza juu yake. Naam! Amina.


113

Tutamwona akija! Hakuna atakayehitaji kutuambia, wakati Yesu anakuja na malaika zake watakatifu!



114

Dalili ya mwisho na iliyo kuu zaidi kuliko dalili nyingine zote alizozitoa Yesu ilikuwa ni injili kwa ulimwengu wote.
Kati ya dalili zote hii ndiyo pekee ambayo haijatimilika.



115

(Fungu: Mathayo 24:14)
Mathayo 24:14 Yesu anasema, Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; HAPO NDIPO ULE MWISHO UTAKAPOKUJA.


116

Katika kitabu cha Ufunuo, tunaona ya kwamba Mungu analielezea hili tamko kuu.



117

(Fungu: Ufunuo 14:6)
Kisha nikaona malaika mwingine akiruka katikati ya mbingu,

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!



118

mwenye injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi,




119

na kila taifa na kabila na lugha na jamaa.
Ufunuo 14:6
Je , unatambua ya kwamba unaona utimilifu wa unabii usiku wa leo katika mkutano huu?
Hii ni sehemu ya mahubiri ya injili ya milele kwa kila kiumbe.


120

Injili inatangazwa kwa njia ya TV, redio, mikutano ya kiinjilisti, mtandao wa kompyuta, mafundisho ya Biblia ya mtu mmoja mmoja, na shule kwa njia ya posta dunia nzima.


121

Danieli amesema ya kwamba, ujuzi utaongezeka.
Katika siku za mwisho za historia ya dunia hii, kitabu cha Danieli kimefunuliwa,
na hili litaleta kuongezeka kwa maarifa juu ya mpango wa Mungu kwa ajili ya dunia hii pamoja na uongezekaji mkuu wa ujuzi katika dunia ya kisayansi.



122

Wakati unakwisha!
Dhambi zilizopelekea maangamizi ya dunia wakati wa Nuhu zipo leo.



123

Mtu anaonekana kujitahidi sasa katika kujiangamiza mwenyewe, kama jinsi matukio yanavyothibitisha.
Yesu alizifananisha siku zetu na siku za Nuhu.


124

Watu walioishi siku za Nuhu walikuwa wakihangaika kufanya kazi muda wote ili wapate riziki na kutenda mambo yao ya kila siku bila kuwa na muda wa mambo ya kiroho.

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!




125

(Fungu: Mathayo 24:37-39)
Yesu alisema katika Mathayo 24:37-39:
Kwa maana kama ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu.



126

Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya gharika watu walivyokuwa wakila, na kunywa,




127

wakioa na kuolewa, hata siku ile aliyoingia Nuhu katika safina,



128

wasitambue, hata  Gharika ikaja, ikawachukua wote,




129

ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu.


130

Yesu alisema kwamba kuja Kwake mara ya pili kutakuwa kama ilivyokuwa siku za Nuhu.
Watu watakuwa na wakati mzuri, lakini hawana muda na Mungu! Watakuwa wanaopenda anasa kuliko kumpenda Mungu.


131

Chembe za mwisho za mchanga ndani ya bilauri la kioo la wakati zinamalizia kutiririka.
Hivi karibuni Mwana wa Mungu atapasua anga lililojaa nyota, akiwa amezungukwa na malaika wasiohesabika kwa wingi.
Mungu anaitizama kwa shauku siku ile,  si kwamba aiangamize dunia, bali ili  awachukue watu wake nyumbani. Makao yanasubiri. Yapo tayari!

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!


132

Tunapotazama ishara duniani leo, twaweza kuona kwa hakika kiasi gani tu karibu na kuja kwa Yesu. Mambo sasa yanafanana sana na jinsi yalivyokuwa wakati Yesu alipokuja duniani mara ya kwanza. Mungu alitoa ishara nyingi wakati ule ili watu wajue wakati ambao Yesu alikuwa aje duniani.




133

(Video: sek 7) Mapigo ya saa yalikwenda ta-ta-ta-ta kwa miaka 4000, na Mungu akatuma hata malaika na watu wenye hekima ili kuwafahamisha watu juu ya kuja kwake.



134

(Fungu: Yohana 1:11)
Lakini inasikitisha kusema, Alikuja kwake, wala walio wake hawakumpokea. Hawakuwa tayari kwa ajili yake.


135

Marafiki, ametupatia dalili hizi zote zituambiazo kwamba anakuja upesi. Yesu alisema,



136

(Fungu: Mathayo 24:33-34)
Nanyi kadhalika, myaonapo hayo yote, tambueni ya kuwa yu karibu, milangoni!



137

Amin, nawaambia, kizazi hiki hakitapita, hata hayo yote yatakapotimia.
Mathayo 24:33,34


138

Je,tutampokea safari hii - au atasikitishwa tena? Muda umekwenda, na hatari zi nyingi. Hakuna wakati wa kupoteza.

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!


139

Merikebu ya moshi ya Amerika ya kati ilikuwa imeondoka toka kwenye bandari ya New York na ilikuwa ikienda kusini ndani ya Atlantiki ikielekea kwenye mfereji wa Panama wakati ilipovuja kwa kutoboka. Merikebu nyingine iliona ishara ya kulemewa toka kwa ile iliyo kuwa ikivuja, hivyo ikawahi ili kusaidia. Nahodha wa meli iliyokuja kusaidia akatuma ujumbe, tatizo gani?
Jibu likaja: Tuna shida ya ukarabati na tunazama. Subiri karibu hadi asubuhi!
Nahodha aliyetaka kuokoa aliona merikebu ikididimia majini akajibu, Wacha nichukue abiria wako kwenye merikebu yangu sasa.
Lakini giza lilikuwa likitanda, na nahodha wa merikebu ya Amerika ya kati hakutaka kuhatarisha yeyote kwa kuhamisha abiria gizani. Hivyo akarudia, Subiri karibu hadi asubuhi.
Huyu nahodha mwingine akatuma ujumbe mwingine akisisitiza kwamba lazima hatua ichukuliwe sasa. Lakini alikataliwa. Ikabidi asalie akingoja kwa mbali kidogo ndani ya giza lililokuwa limetawala.
Wahudumu katika meli hii waliweza kuona taa za merikebu ya Amerika ya kati zikiishia katika mawimbi.
Kama saa moja na nusu baadaye, walishuhudia huku wakiwa wamepigwa na butwaa zile taa zikitokomea kabisa.
Merikebu ilikuwa imezama, na wote waliokuwemo ndani yake waliangamia.

# 2 - Ishara Usizoweza Kuzidharau!


140

Kungoja kwaweza kuleta matokeo ya upotevu wa milele.
Zipo nyakati ambazo unapaswa kufanya uamuzi sasa.
Nahodha wa Amerika ya Kati alidhani hakukuwa na shida kusubiri hadi asubuhi.
Alikosea sana.
Biblia yasema, Leo ni siku ya wokovu.
Usingoje. Usikate tamaa. Usichelewe.
Kwa nini usifanye uamuzi kwa ajili ya Kristo sasa hivi?
Je, hutauinua moyo wako kwa Mungu sasa hivi na kumuomba akuandae kwa kuja kwa Kristo hivi karibuni?
Je, kuna chochote katika maisha yako ambacho chaweza kukuzuia usiwe tayari kwa ajili ya marejeo ya Kristo hivi karibuni?
Kwa nini usikitoe hicho sasa hivi tunapoomba?
Kama kweli u makini juu ya kumkubali Kristo, je, waweza kuinua mkono wako sasa hivi na kusema, Ndiyo, Bwana, nataka kuwa tayari kukupokea unapokuja tena.

# 3 - Kuepa Kukuu



1


Siku Utakayo ingia Katika Kutokufa


2

Mary alikuwa amechoka. Lilikuwa juma lenye kazi nyingi sana. Maisha yake yalikuwa kama msukumo mmoja wa kimbunga cha shughuli. Huku akiendesha kutoka kwenye duka, alipiga kona toka kwenye barabara kuu akaingia katika kibarabara kidogo cha vumbi kilichoelekea  nyumbani kwake.


3

Ghafla nyota yenye mkia ilionekana kama kumwagika kwenye anga katika hili giza la usiku. Nyota zilizokuwa zikirushwa tena kwa ung'avu ziliziangaza mbingu.



4

Kwa sababu ya kutozoea pia muonekano wa nyota katika mtindo huo, alikikanyaga zaidi kiongeza mwendo (accelerator). Mara ile aliwaza, Huu ni mwisho wa dunia! Kristo anakuja!  Yote ninayohitaji ni kufika nyumbani na kuwa na mtoto wangu. Akizungumzia hili tukio baadaye, Mary alisema, Nilipoona mbingu ziking'aa hivyo, nilidhani Yesu alikuwa anakuja wakati ule ule.



5

Hivi umepata kufikiri kwa undani kwamba dunia itafikia mwisho siku moja? Kama umepata kuwaza hivyo, yawezekana umepata kujiuliza  itaishaje. Je, nyota yenye mkia itamwaga vipande vyake kuashiria mwisho?



6

Baadhi ya watu wanafikiri dunia itafikia mwisho katika vita vya nyuklia - kwamba wanadamu watajiangamiza wenyewe na uhai wote duniani.

# 3 - Kuepa Kukuu


7

Wengine wanafikiria ya kwamba kutakuwa na mlipuko wa idadi ya wakazi wa dunia kwa kiasi kwamba dunia haitaweza kuhifadhi watu wengi kiasi hicho, kisha njaa kali kwa watu wengi itafuata.


8

Na bado wengine wanao wasiwasi ya kwamba labda siku moja kimondo au nyota yenye mkia itaigonga dunia na kuiangamiza.



9

Lakini je, wajua ya kwamba muda mrefu uliopita, Biblia ilitabiri bayana juu ya jinsi dunia itakavyokwisha? Na rafiki, habari njema ni kwamba jamii ya binadamu haitaangamia kwa sababu ya vita au njaa au hata kwa sababu ya kugongana na kiumbe kingine chochote angani.


10

Badala yake, Biblia yasema ya kwamba dunia itaisha kwa kuja kwa utukufu kwa Yesu Kristo hapa duniani! Atarejea kwa dunia hii hii aliyoiacha karibia miaka 2,000 iliyopita, na atarejea kuufikisha wakati mwisho wake na kuuleta umilele.


11

Inapendeza kugundua jinsi watu wanavyofikiri juu ya yale yatakayotokea wanapoulizwa kama wanafikiri kuja kwa Yesu kutakuwaje.


12

Ndiyo, rafiki, Mfalme Yesu anakuja upesi, na hakuna mashaka ya kuwa matatizo ya dunia hii yako juu zaidi ya uwezo wa kibinadamu -
ya kwamba Kristo pekee na Baba yake wanao uwezo wa kunyoosha matatizo ya Sayari Dunia!
Utakuwa mbaraka mzuri kiasi gani wakati Mfalme akija!

# 3 - Kuepa Kukuu


13

Wakati mtume Paulo alipokuwa mfungwa katika giza, gerezani Mammertine palipokuwa  na unyevu nyevu, akisubiri muuaji aje kumkata kichwa, aliandika ya kwamba,



14

(Fungu: Tito 2:13)
Tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu.
Tito 2:13.
Paulo aliandika hii barua ya kutia moyo kwa Tito, mwanae wa kweli katika imani, ili kumkumbusha Tito juu ya  kuja kwa utukufu kwa Bwana wetu.


15

Kama unaona kwamba maisha yako yana usiku wenye giza la mambo ya kukatisha tamaa,  tazama juu na kumbuka lile tumaini lenye baraka- kuja kwa mara ya pili kwa Kristo hapa duniani - hilo litanyoosha mambo!



16

Tukio linenwalo zaidi katika Agano Jipya ni la kuja kwa Kristo mara ya pili.
Karibu kila fungu katika mafungu 25 linalo jambo la kusema juu ya tukio hilo.
Kristo alitumia muda zaidi akinena juu ya tukio hilo kuliko somo lingine lolote katika Agano Jipya.
Yapo mafungu mawili katika Agano Jipya ambayo kila  anayeiamini Biblia anapaswa kuyajua.



17

(Fungu: Yohana 3:16)
Pengine moja linalofahamika zaidi ni Yohana 3:16 ;
Kwa Maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwana wake wa pekee, ili kila amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.



18

ili kila amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.
Ya pili ni ahadi nzuri ya Yesu aliyoitoa muda mfupi kabla ya kusulubishwa kwake na kupaa:

# 3 - Kuepa Kukuu



19

(Fungu: Yohana 14:1)
Yesu aliwaambia, Msifadhaike mioyoni mwenu. Mwaminini Mungu, niaminini na mimi pia.



20

Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; la sivyo ningalikwisha waambieni. Sasa nakwenda kuwatayarishieni makao.



21

Na nikienda na kuwatayarishieni makao, nitarudi



22

na kuwachukua kwangu, ili nanyi muwepo nilipo mimi.
Yohana 14:1-3.


23

Kwa muda wa karne nyingi sasa, wakati wowote kukata tamaa,  na matatizo, au mauti vinapowatisha wafuasi wa Kristo,


24

hii nyota ya tumaini - ahadi ya Kurudi kwake - imewaletea tumaini na uwezo wa kuvumilia. Wafuasi wa Yesu daima wametazamia kwa shauku utimilifu wa ahadi hii.



25

(Fungu: 2 Timotheo 4:7,8)
Baadaye katika maisha yake,  mnyongaji akiwa si mbali sana toka alipokuwa Paulo, alitamka: Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda;



26

baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana , mhukumu mwenye haki,

# 3 - KUEPA KUKUU



27

atanipa siku ile; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake.
2 Timotheo 4:7,8


28

Paulo aliweza kuukabili kwa ujasiri kabisa upanga wa muuaji katika siku ile ya hatima yake kwa sababu alikuwa na imani katika ahadi ya kurejea kwa Kristo!


29

Naam, Yesu ATArejea!
Na rafiki, ahadi ya Yesu kwa wanafunzi wake inatuhusu sisi wote.
Yesu atakuja!


30

Wakati wanafunzi walipouliza ni zipi dalili za kuja kwake na za mwisho wa dunia, Yesu alitoa kwa undani maelezo ya matukio yatakayochukua nafasi kabla ya kuja kwake.



31

(Fungu: Mathayo 24:4,5)
Hebu tulisome:
Yesu akawajibu, Jihadharini msije mkadanganywa na mtu. Maana wengi watatokea na kulitumia jina langu wakisema: 'Mimi ndiye Kristo,' nao watawapotosha watu wengi.



32

Maana wengi watatokea na kulitumia Jina langu, wakisema, 'Mimi ndiye Kristo' nao watawapotosha wengi.
Mathayo 24:4,5.
Katika fungu la 24, Yesu anafafanua swala hili.



33

Maana watatokea  makristo wa uongo na manabii wa uongo. Watafanya ishara kubwa na maajabu ya kuweza kuwapotosha

# 3 - Kuepa Kukuu



34

ikiwezekana hata wateule wa Mungu.



35

Kama hatujui kutofautisha - jinsi ya kutambua kilicho bandia - twaweza kujiunga na mlaghai, tukidhani yeye ni Kristo!
Yesu alionya ya kwamba itatokea! Na hakua anazungumzia juu ya viuongo uongo vidogo vidogo vichache.


36

Ni wazi alikuwa akizungumza juu ya miigo ya ajabu ya nafsi fulani, iliyopangwa vema na kwa ustadi na kutekelezwa kiasi kwamba karibu dunia nzima itadanganyika! Unaona, hawa walaghai watatenda miujiza - kuponya wagonjwa na kutoa vielelezo vinavyozidi akili za kibinadamu kuelewa ili tu kuunga mkono madai yao!


37

Hatutakosea kuja halisi kwa Kristo! Hakuna ambaye angefanya hilo. Lakini tungeweza kuchukuliwa na Kristo bandia na kudanganywa kabla ya kuonekana kwa Kristo!
Tafakari juu ya hili.


38

Mwovu atawatumia ma kristo wa uongo na manabii wa uongo ili kujaribu kuchanganya watu juu ya kuja mara ya pili.



39

(Fungu: 2 Wakorintho 11:13,14)
Maana, hao ni mitume wa uongo, watendao kazi kwa hila wanojigeuza kuwa mitume wa Kristo.

# 3 - Kuepa Kukuu



40

Wala si ajabu! Maana hata shetani mwenyewe hujigeuza kuwa mfano wa  malaika wa nuru!
2 Wakorintho 11:13,14.
Mwovu atadiriki kujibadilisha mwenyewe na kufanya onyesho la kuja kwa bandia kwa Yesu.



41

Kila mara yupo anayeibuka mahali fulani akidai kuwa Kristo.
Wanaweza kuvaa mavazi kama yale watu wanayofikiria kwamba Yesu aliyavaa.
Wananena kwa sauti ya wema, na tamu.
Wananukuu mafungu kwa wingi.
Wanaonekana kuwa na hekima sana.
Baadhi yao wanavutia  ufuasi wa watu wengi sana wanaoamini ya kwamba Kristo amekuja duniani tena.
Lakini hakuna kati ya watu hawa aliye Kristo.
Twaweza kukwambia hilo kwa uhakika kamili.
Na kwa nini?
Mtu wa namna hiyo aweza onekana kama ambavyo ungemtegemea Yesu aonekane.
Aweza nena kama jinsi ambavyo ungemtegemea Yesu anene.


42

Anaweza aponye watu na kufanya ishara kuu na maajabu, na jaribu laweza kuwa kubwa kiasi cha kuwa na wasi wasi na kile Biblia isemacho.  Ila hatupaswi kuamini fahamu zetu - kile tusikiacho, tuonacho, na tujisikiavyo!


43

Kuna muongozo mmoja tu ulio salama usaidiao kutambua kama mhusika ndiye kweli ama ni mlaghai - Biblia.



44

Hebu tutafakari dalili chache au vielelezo vilivyo pekee vihusuvyo kuja kwa Kristo mara ya pili ili tusije tukadanganywa!

# 3 - Kuepa Kukuu



45

Kuja kwa Kristo Mara ya Pili ni Kuja Kuliko Dhahiri



46

(Fungu: Mathayo 24:27)
maana, kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana magharibi, hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu.
Mathayo 24:27.
Kwa kweli, katika Ufunuo 1:7 tunasoma,



47

(Fungu: Ufunuo 1:7)
Tazama, yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona.......


48

Walaghai waweza tokea hapa na pale, lakini hakuna mmoja wao awezaye kuja katika mawingu ya mbinguni kwa namna ambayo kila jicho litamwona.


49

Baada ya Yesu kumaliza kazi yake hapa duniani, alikuwa tayari kupaa kwenda mbinguni.


50


Aliwachukua wafuasi wake wa karibu  nje hadi katika Mlima wa Mizeituni, na baada ya kuwaelekeza wanafunzi wake na kuwaaga,  ghafla akachukuliwa kwenda mbinguni.



51

Hebu tutambue kile Biblia inachokisema juu ya hili tukio.

# 3 - KUEPA KUKUU



52

(Fungu: Matendo 1:9-11)
Akiisha kusema hayo, walipokuwa wakitazama, akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao.




53

Walipokuwa wakikaza macho mbinguni, yeye alipokuwa akienda zake, tazama, watu wawili wakasimama karibu nao, wenye nguo nyeupe,



54

wakasema, 'Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni,



55

Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni.'
Matendo 1:9 - 11.


56

Malaika wawili kutoka kwa Mungu walikuwa wamekuja kuwahakikishia wanafunzi ya kwamba ile ahadi Yesu aliyowapa ingetimia.
Yesu alikuwa amesema wazi kile ambacho WANGEKIONA:



57

(Fungu: Luka 21:27)
Halafu, watamwona Mwana wa Adamu akija katika wingu, mwenye nguvu na utukufu mwingi. Luka 21:27.


58

Hakuna atakayehitaji kukutaarifu wakati Yesu akija. Utamwona akija mawinguni. Lakini zipo ishara zingine ambazo mwovu hawezi kuziiga. Kristo hatatokea tu ghafla mahali fulani porini au toka kwa chombo fulani kitokacho angani.

# 3 - Kuepa Kukuu



59

Yesu Hatakuja Tena Peke Yake - Litakuwa Tukio La Utukufu !



60

(Fungu: Mathayo 25:31)
Yesu alisema, Wakati Mwana wa Adamu atakapokuja katika utukufu wake na malaika wote wakiwa pamoja naye, ndipo ataketi juu ya kiti chake cha enzi kitukufu.
Mathayo 25:31.



61

(Fungu: Mathayo 24:31)
Kwa nini Yesu analeta malaika pamoja naye? Anatoa jibu: Naye atawatuma malaika wake wenye tarumbeta la kuvuma sana,




62

Nao watawakusanya wateule wake kutoka pande zote nne za dunia, toka mwisho huu wa mbingu hadi mwisho huu.
Mathayo 24:31.


63


Ndiyo Yesu atasindikizwa na malaika watakatifu - wakijaza anga na utukufu usioelezeka.
Sasa wajua kwa nini watu hawa wajiitao kuwa Kristo hawawezi kuwa yeye!
Wangekuwa na wakati mgumu wa kujaribu kuiga marejeo ya Yesu!
Hakuna awezaye!
Lakini yapo matukio zaidi yahusianayo na kuja kwa Yesu.



64

Kutakuwa Kuja Kwenye Kusikika kwa Mshindo - na Watakatifu Waliokufa Watafufuliwa Toka kwa Wafu

# 3 - KUEPA KUKUU



65

(Fungu: 1 Wathesalonike 4:16)
Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu.



66

na parapanda ya Mungu..…nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza.
1 Wathesalonike 4:16.


67


Hivyo je, unaona, kuja kwa Kristo hakutakuwa tu kuonekanako dhahiri bali pia kutasikika - kila mmoja atasikia.
Mwito wa Mungu utapenya kiasi ambacho pamoja na sauti ya tarumbeta, wafu waliokufa katika Kristo watafufuliwa  na kutoka katika makaburi yao.


68

Je waweza kufikiria furaha itakayo kuwepo wakati makaburi yatakapofunguka na familia zitakapoungana?


69

Je, waona jinsi itakavyokuwa vigumu kwa Shetani kuiga kuja halisi kwa Kristo?



70

Kuna habari  nzuri zaidi!
Tambua  kinachotokea kwa wenye haki walio hai wakati Kristo ajapo mara ya pili:



71

(Fungu: 1 Wathesalonike 4:17)
Kisha sisi tulio hai,tulio salia, tutanyakuliwa  pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani;

# 3 - Kuepa Kukuu



72

na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.
1 Wathesalonike 4:17.




73

Wafuasi waaminifu wa Yesu wananyakuliwa pamoja na waliofufuliwa kumlaki Bwana hewani.
Litakuwa unganiko la furaha kiasi gani kwa familia nyingi.



74

Paulo anatufafanulia kwa undani zaidi juu ya kile kitakachotokea Yesu akija:



75

(Fungu: 1 Wakorintho 15:51 - 53)
Angalieni, nawaambia ninyi siri;....sote tutabadilika,



76

kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho, maana parapanda italia,



77

na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika.




78

Maana sharti huu uharibikao uvae kutokuharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa.
1 Wakorintho 15:51-53.


79

Mungu atampatia kila mfuasi wa Yesu karama Yake ya upendo - uzima wa milele.
Karama zingine zote hazina maana bila ya karama hii ya kutokufa.

# 3 - Kuepa Kukuu



80

(Fungu: Wafilipi 3:20, 21)
Na kuna kitu kingine ambacho Mungu atawapatia watu wake:
........Tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo;



81

atakayeubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu, Wafilipi 3:20,21.
Mwili kama wa Kristo.
Hakuna tena maumivu kuugua - au ugonjwa.
Ni habari ipi ingelipendwa zaidi ya hii?



82

Kuna kundi jingine la watu. Kuja kwa mara ya pili haitakuwa habari njema kwao. Sikiliza Biblia inavyoelezea matukio ya mwisho ya kutisha ya historia ya dunia.



83

(Fungu: Ufunuo 6: 14-17)
Mbingu zikaondolewa kama ukurasa ulivyokunjwa;



84

na kila mlina na kisiwa kikahamishwa kutoka mahali pake.



85

Na wafalme wa dunia, na wakuu, na majemadari, na matajiri, na wenye nguvu, na kila mtumwa, na mwungwana,



86


wakajificha katika pango na chini ya miamba ya milima;

# 3 - Kuepa Kukuu



87

wakiiambia milima na miamba,
Tuangukieni,tusitirini mbele za uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, ....



88

Kwa maana siku iliyo kuu, ya hasira yake, imekuja; naye ni nani awezaye kusimama?
Ufunuo 6:14-17.




89

(Fungu: Ufunuo 16:18)
Pakawa na umeme, na sauti na radi na palikuwa na tetemeko la nchi kubwa




90

ambalo tangu wanadamu kuwako juu ya nchi hapakuwa namna ile jinsi lilivyokuwa kubwa tetemeko lile. Ufunuo 16:18.


91

Tetemeko hili litabomoa majiji ya dunia.
Hakuna awezaye kukosa tetemeko kama hili linapoashiria kuja kwa Kristo!


92

Yesu alionya ya kwamba kuja Kwake kutakuwa katika wakati ambao hakuna anayetarajia.
Alisema pia ya kwamba watu watakuwa wakihangaika kupoteza maisha yao katika anasa za kipumbavu.



93

(Fungu: Mathayo 24:30)
Katika Mathayo 24:30, tunaambiwa ya kwamba wakati Yesu atakapokuja, ..mataifa yote ya ulimwengu wata...omboleza...

# 3 - Kuepa Kukuu


94

Hiki ndicho Yesu alichosema kingetokea kwa wale wasiokuwa tayari kwa ajili ya siku ile!
Wanapotea-na wanajua!
Ni picha ya huzuni kiasi gani, na hali ingeweza kuwa vingine.
Rafiki, siku ile itakuwa ya kweli!
Hakutakuwa na kuamka toka usingizini na kukuta kwamba ilikuwa ndoto tu - la!


95

Hakuna lililo la muhimu duniani zaidi ya kuwa tayari kumlaki Yesu atakapokuja.
Inashangaza jinsi zilivyo dhaifu hazina za dunia tunazozithamini sana!
Tetemeko moja tu, vyote vitakwisha!



96

(Luka 21:36)
Basi,  kesheni ninyi kila wakati, mkiomba, ili mpate kuokoka katika haya yote yatakayotokea,



97

na kusimama mbele za Mwana wa Adamu.
Luka 21:36



98

(Yesu anakuja tena)
Hebu tufanye mapitio  ya haraka ya yale ambayo tumejifunza pamoja katika Biblia:



99


Manabii wa Uongo na makristo  watajaribu kudanganya kila mtu.



100

Mwovu atatokea kama malaika wa nuru.

# 3 - Kuepa Kukuu



101

Kuja kwa mara ya pili hakutakuwa siri.




102

Kila jicho litamwona Yesu akija.



103

Malaika watakafifu wote watakuja pamoja na Yesu.



104

Atakuja na sauti ya parapanda.




105

Atakuja na sauti ya Malaika Mkuu.




106

Waliokufa wakiwa wenye haki watafufuliwa.



107

Wenye haki watakaokutwa hai watabadilishwa bila kuonja mauti.



108

Wenye haki wote watapewa kutokufa.

# 3 - Kuepa Kukuu



109

Wasiomcha Mungu wote duniani wataomboleza watakapomuona Yesu.



110

Tetemeko kuu litaiangamiza dunia.



111


Waliopotea wote watauawa.


112

Nusu haijaelezwa, wala kalamu ya mwanadamu haijachora, wala mawazo hayajaelewa uzuri na utukufu wa kuja kwa fahari kwa Kristo mara ya pili! Lakini tungependa kushirikiana nanyi jinsi ambavyo waandishi na wasanii wanavyopiga picha mawazoni mwao na kuieleleza juu ya kuja kwa Yesu-kutakuwaje-na jinsi mawazo yanavyoiweka picha kulingana na jinsi Biblia inavyoeleza.


113

Katika wakati ambapo hakuna atakayetarajia, Yesu atarejea! Sauti ya Mungu, kama mvumo wa radi, inaenea duniani kote ikitangaza siku na saa ya kuja kwa Mwana wake.


114

Mbingu zinakunjwa kama karatasi, nchi inatetemeka mbele zake, na kila mlima na kisiwa vinasogezwa toka mahali pake.


115

Mara kunatokea upande wa mashariki wingu dogo jeusi, kama nusu ya mkono wa mtu.

# 3 - Kuepa Kukuu


116

Lile wingu likaribiapo zaidi na dunia linang'aa zaidi na zaidi na linaonekana na utukufu zaidi hadi lilipokuwa wingu kubwa likiwa na upinde kama wa mvua juu yake. Hali wakiwa kimya watu wa Mungu wanatazama hili tukio, na kuduwaa. Linaduwaza!


117

Anga limejazwa na sura zenye kung'aa kwa nuru, elfu kumi mara elfu kumi, na maelfu ya maelfu ya malaika wakimzunguka Yesu akiwa kwenye kiti chake cha enzi!


118

Uzuri wake wote unazifunika mbingu na walipokaribia zaidi na dunia, 'kila jicho' linamuona Mfalme anayekuja!
Hakuna taji ya miiba inayokiharibu kile kichwa kitakatifu, lakini taji ya utukufu imetulia katika kipaji chake kitakatifu. Na katika vazi lake na katika paja lake jina limeandikwa, 'Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.'


119

Na wafalme wa dunia, na watu wakuu, na matajiri, na mabaharia wakuu, na wakuu kati ya watu, na kila mtumwa na kila aliye huru, walililia miamba na milima iwaangukie na iwafiche mbali na uwepo wa Mwana-Kondoo.


120

Wale waliowatesa na kuwaua watu wa Mungu na wale waliomkejeli na kumkataa Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu, waliopaza sauti, waliopaza sauti, 'Msulubishe! Msulubishe!' wameinuliwa ili wasimame mbele za Yesu. Mioyo yao inayeyuka, magoti yao yanagongana, na kwa sauti ya kuogofya sana, katika kilio cha kukata tamaa wanaita,



121

'YEYE NI MWANA WA MUNGU. NDIYE MASIHI WA KWELI.'

# 3 - Kuepa Kukuu


122

Sasa, wanamtazama Yeye katika utukufu wake wote, na bado hawajamuona Yeye akiwa ameketi katika mkono  wa kuume wa Mamlaka.


123

Wale waliodhihaki dai lake kuwa Mwana wa Mungu wameduwaa.
Pale yupo Herode mwenye majivuno aliyecheka cheo chake cha kifalme na kuwaamuru  askari wenye kudhihaki wamuwekee taji Yesu kama mfalme.


124

Pale wapo watu wale ambao kwa mikono yao yenye kufuru waliweka  juu ya mwili wake  lile vazi la zambarau, na juu ya kichwa chake taji ya miiba, na katika mkono wake usio na ugomvi fimbo ya kifalme ya kejeli,  na  ndiyo walioinama  mbele zake kwa mzaha wenye kufuru.


125

Watu waliompiga na kumtemea  mate Mfalme wa Uzima sasa wanageuka toka katika macho yake yapenyayo na wanatafuta kutoroka toka kwa utukufu wenye nguvu kuliko zote wa uwepo wake.


126

Wale waliomchoma misumari katika mikono yake na miguu yake, askari waliomchoma ubavuni mwake, wanatazama alama hizi kwa hofu na majuto.
Kwa  uwazi  wa kutisha  makuhani na watawala wanakumbuka matukio ya Kalvari. Huku wakitetemeka kwa hofu kubwa wanakumbuka sasa, wakitingisha vichwa vyao kwa mzaha  wa kishetani walitamka kwa sauti: 'Aliwaokoa wengine; Yeye Mwenyewe Hawezi Kujiokoa.


127

Kama kweli Yeye ni Mfalme wa Israeli, na  ashuke sasa toka msalabani, nasi tutamwamini. Alimwamini Mungu; hebu na amuokoe sasa kama anamtaka.'

# 3 - Kuepa Kukuu


128

Wale ambao wangemuangamiza Kristo na watu wake waaminifu sasa wanashuhudia utukufu unaowaangukia. Katikati ya tisho lao wanasikia sauti ya watakatifu wakipaza sauti kwa furaha na kusema,



129

(Fungu: Isaya 25:9)
'.....Tazama, huyu ndiye Mungu wetu; Ndiye tuliyemngoja naye atatuokoa.'



130

Kati ya kulewa lewa kwa dunia, miali ya radi, na ngurumo za radi, sauti ya Mwana wa Mungu inaita watakatifu waliolala.
Anatazama makaburi ya wenye haki, kisha, akiinua mikono Yake kuelekea mbinguni, Anapaza sauti yake: 'Amkeni, amkeni, amkeni, ninyi mlalao katika mavumbi, na muondoke!'


131

Katika dunia nzima wafu wataisikia sauti yake, na wale watakaoisikia wataishi. Na dunia nzima itavuma kwa mshindo wa jeshi kubwa la ajabu la kila taifa, kabila, lugha na jamaa.


132

Kutoka katika nyumba ya gereza la wafu wanakuja, wakiwa wamevikwa na utukufu usiokoma, wanapaza sauti zao:' Ewe mauti U wapi uchungu wako? Ewe kaburi, u wapi ushindi wako?'
Na wenye haki walio hai na watakatifu walio hai sauti zao zinaungana katika sauti kubwa ndefu ya shangwe ya ushindi. Dosari zote na ulemavu vimeachwa kaburini. Ah, ukombozi wa ajabu! Ulionenwa kwa muda mrefu, umetarajiwa kwa muda mrefu, umetafakariwa na matarajio yaliyo na shauku, lakini haukueleweka kikamilifu.


133

Watakatifu walio hai wanabadilishwa 'kwa sekunde moja, kufumba na kufumbua.' Sauti ya Mungu iliposikika walitukuzwa; sasa wanavishwa kutokufa na pamoja na watakatifu walio fufuliwa wananyakuliwa juu kumlaki Bwana wao hewani.

# 3 - Kuepa Kukuu


134

Malaika wanakusanya watakatifu wake toka pande nne za dunia, toka mwisho mmoja wa mbingu hadi mwingine. Watoto wadogo wanabebwa na malaika watakatifu na kupelekwa hadi kwa mikono ya mama zao.


135

Marafiki waliotengana kwa muda mrefu kwa sababu ya mauti wanaungana, wasiachane tena, na huku wakiimba nyimbo za furaha wanapaa juu kwa pamoja kwenda kwa Jiji la Mungu.


136

Na wanapopaa kwenda mbinguni msafara mkubwa wa malaika unapaza sauti, 'Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenye Enzi.' Na waliokombolewa wanashangilia, 'Haleluya' wanapoendelea kusonga kulielekea Jiji Takatifu.


137

Kabla ya kuliingia Jiji Takatifu, Mwokozi anawapatia wafuasi wake vielelezo vya ushindi na kuwavisha nembo zenye hadhi ya ufalme wao. Umati huu wote ulio mkubwa wa waliokombolewa kila jicho linatazama utukufu wake ambaye' sura yake iliharibiwa kuliko mtu yeyote, na umbo lake zaidi ya wana wa watu.'


138

Juu ya vichwa vya washindi, Yesu mwenyewe kwa mkono wake wa kuume anaweka taji ya utukufu. Kwa kila mmoja kuna taji yenye jina lake 'jina jipya' na maandishi 'Utakatifu kwa Bwana.'
Furaha isiyoelezeka inajaza kila moyo, na kila sauti inainuliwa kwa ajili ya sifa ya shukrani.

# 3 - Kuepa Kukuu


139

Mbele za umati huu uliobadilishwa, ni Jiji Takatifu. Yesu anafungua wazi malango ya lulu, na mataifa ambayo yameshika amri na kuwa na subira ya Yesu yanaingia.
Pale wanashuhudia Paradiso ya Mungu, nyumba ya Adamu kabla hajatenda dhambi.
Kisha ile sauti, iliyo tamu kuliko muziki wowote uliopata ingia masikioni mwa sikio linalokufa, inasikika ikisema: 'Pambano lenu limekwisha.'



140

(Fungu: Mathayo 25:34)
'Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu;' Mathayo 25:34.


141

Hili ni tumaini letu. Hii ni hatima yetu. Haya ni maisha yetu yajayo.
Twaweza kuishi na Kristo mbinguni milele.
Tukiukosa umilele, tumekosa kila kitu.
Tukiikosa mbingu, tumekosa kila kitu.
Kama hatukujiandaa kwa ajili ya kuja kwa Kristo karibuni sana, tutalikosa tukio kubwa kuliko yote katika historia ya karne zote.
Yesu anasema .. Njoo upate msamaha.
Njoo upate rehema.
Njoo upate nguvu za kushinda dhambi zako.
Njoo uupate umilele.
Njoo uingie kwenye ufalme wangu.
Je, utasema ndiyo kwa mwito wake sasa hivi?
Kama unatamani kuishi kwenye ufalme wake milele, simama sasa hivi tunaposali.

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?



1

Vumbua Mafumbo ya Maisha.


2

Yamkini ungekuwa unaishi kando kando ya bahari. Asubuhi moja unadamka na kuamua kutembea kwenye mchanga huu wa pwani.
Ni mandhari yenye kuvutia. Miali ya jua linalochomoza inarukaruka. tokea majini. Mawimbi yanagonga kwenye pwani.


3

Utembeapo kwa utulivu katika pwani, unagundua seti ya alama za nyayo mchangani mbele yako. Kisha unagundua seti ya pili na ya tatu ya alama hizi za nyayo.  Unatizama mbali kadiri uwezavyo kwenye pwani lakini huoni mtu yeyote.
Je, hizi nyayo zinakwambia nini? Kwa urahisi tu zinasema - ingawa huwezi kuona yeyote, kuna aliyekuwepo pale.
Yupo aliyetembea kwenye pwani kabla yako.
Hebu nikuulize swali jingine.


4

Usimamapo nje ya nyumba na kutizama mazingira, unaona nini?
Nyasi, miti, vilima au milima, maua, chemichemi za maji au maziwa, labda wanyama.


5

Na usimamapo hapo, je, umesimama juu ya nini?
Ndiyo, umesimama kwenye ardhi - usoni mwa nchi.


6

Tizama juu,  waona nini?

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?


7


Wakati wa mchana, waweza kuona jua, anga, ama mawingu.


8

Usiku, waweza ona maelfu ya maelfu ya nyota - ama pengine mwezi.


9

Imefikaje hapa?
Ulifikaje hapa?
Nani aliyewatengeneza?


10

Baadhi ya watu husema uhai ulianza tu na chembehai za kawaida ndani ya maji-
Hizo chembehai zikakuwa hadi zikawa vijitu vidogo sana vitokanavyo na muunganiko wa chembehai nyingi.
Kisha vile vijitu vidogo vikabadilika kwa miaka mamilioni na kuwa viumbe vidogo ambavyo vingeweza kusogea tokea baharini hadi kwenye nchi kavu, ambapo viliota miguu.



11

Mamilioni ya watu wakati wote wameamini jambo la tofauti kabisa kuhusu jinsi ulimwengu , dunia, na viumbe hai vyote vilivyopata kuwepo.
Wanaamini ya kwamba Muumbaji-Mungu alivitengeneza vyote.
Lakini Mungu gani?


12

Watu wanaabudu miungu mingi leo: Buddha, Mohamed, Shinto, miungu ya kihindu na mingineyo.
Wafuasi wa miungu hii hudai ya kwamba miungu yao ndiyo mikuu.

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?


13

Lakini je,wajua ya kwamba kati ya miungu yote duniani, ni mmoja tu anayedai kuwa Muumbaji wa kila kitu?
Na Mungu huyo ni Mungu wa Biblia Takatifu.
Hivyo tunataka kutafuta kwa kadiri tutakavyoweza kutokea kwenye Biblia kuhusu Mungu wa viumbe vyote.


14

Uonapo nyumba, je, umepata kuwaza wakati wowote ya kwamba kwa namna fulani nyumba hiyo imejitengeneza yenyewe?
La. Unatambua ya kwamba yupo aliyeitengeneza nyumba hiyo.


15

Uonapo barabara, je, unadhani ya kwamba barabara hiyo imejitengeneza tu yenyewe - ama ya kwamba yupo aliyeitengeneza? Na barabara na nyumba ni rahisi kwa mbali sana ukilinganisha na ulimwengu na watu. Hivyo utazamapo watu na wanyama na nyota, je, haileti tu maana kuhitimisha ya kwamba yupo aliyevitengeneza vyote?
Yupo aliyevisanii vitu hivi, kisha akaviumba.


16

Tutaanza kujifunza juu ya Mungu anayedai kuwa Msanii na Muumbaji wa kila kitu.
Hebu tuanze na kile ambacho kitabu chake, Biblia,kinasema kuhusu kazi Yake katika kuumba dunia hii na ulimwengu wetu.
Kwanza hebu na tutazame kile kilichotokea siku ya kwanza.



17

(Fungu: Mwanzo 1:1)
Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi.
Mwanzo 1:1



18

(Fungu: Mwanzo 1:3)
Kisha Mungu akasema, 'Iwe nuru'; ikawa nuru.
Mwanzo 1:3

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?



19

(Picha za somo la pili: Mwanzo 1:4,5)
Mungu akaiona nuru, ya kuwa ni njema; Mungu akatenga nuru na giza.




20

Ikawa jioni ikawa asubuhi siku moja.
Mwanzo 1:5
Siku ya kwanza ya juma Mungu aliumba dunia. Aliumba nuru na kuanza mzunguko wa mchana na usiku.



21

(Fungu: Mwanzo1:6) Siku ya Pili
Mungu akasema, 'Na liwe anga katikati ya maji, likayatenge maji na maji.'
Mwanzo 1:6



22

(Fungu:  Mwanzo 1:7)
....na ikawa hivyo.
Mwanzo 1:7




23

(Fungu: Mwanzo 1:8)
Mungu akaliita lile anga Mbingu. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya pili. Mwanzo 1:8
Katika siku ya pili, Mungu alitengeneza anga lililo juu yetu, na kutenganisha maji katika nchi na maji katika mawingu na anga.



24

(Fungu  Picha 2: Mwanzo 1:9) Siku ya Tatu
Mungu akasema,' Maji yaliyo chini ya mbingu na yakusanyike mahali pamoja, ili pakavu paonekane';



25

na ikawa hivyo.
Mwanzo 1:9

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?



26

(Fungu  Picha 2:  Mwanzo 1:11)
Mungu akasema, 'Nchi na itoe  majani, mche utoao mbegu,




27

na mti wa matunda uzaao matunda kwa jinsi yake, ambao mbegu zake zimo ndani yake, juu ya nchi; ikawa hivyo.




28

(Fungu: Mwanzo 1:13)
Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya tatu.
Mwanzo  1:13
Siku ya tatu Mungu aliifanya chi kavu kutokea, akaumba bahari, na kuifunika dunia kwa  uhai wa mimea.




29

(Fungu  Picha 3: Mwanzo 1: 14,15) Siku ya Nne
Mungu akasema, 'Na iwe mianga katika mbingu  ili itenge kati ya mchana na usiku;



30

nayo iwe ndiyo dalili na majira na siku na miaka;



31

tena iwe ndiyo mianga katika anga la mbingu itie nuru juu ya nchi'; ikawa hivyo.
Mwanzo  1:14,15



32

(Fungu  Picha 2: Mwanzo 1:18, 19)
Mungu akaona ya kuwa ni vyema.

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?



33

Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya nne.
Mwanzo 1:19.
Katika siku ya nne Mungu alifanya jua na mwezi vikatokea angani. Aliziumba nyota pia.



34

(Fungu Picha 2: Mwanzo 1:20) Siku ya Tano
Mungu aliumba nini siku ya tano?
Mungu akasema, 'Maji na yajawe kwa wingi na kitu kiendacho chenye uhai,



35

na ndege waruke juu ya nchi katika anga la mbingu.'
Mwanzo 1:20



36

(Fungu: Mwanzo 1:23)
Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya tano.
Mwanzo 1:23. Katika siku ya tano, Biblia yasema, Mungu alifanya ndege na samaki na viumbe wengine wa majini.



37

(Fungu Picha 2: Mwanzo 1:24) Siku ya Sita
Siku ya sita ya uumbaji ilikuwa ya muhimu zaidi hadi hapa:
Mungu akasema,' Nchi na izae kiumbe hai kwa jinsi zake;



38

mnyama wa kufugwa, nacho kitambaacho, na wanyama wa mwitu kwa jinsi zake'; ikawa hivyo.
Mwanzo 1:24



39

(Fungu Picha 5: Mwanzo 1:26,27)
Mungu akasema,' Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu;

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?



40

wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama,



41

na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi.
Mwanzo 1:26



42

Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba;



43

mwanamume na mwanamke aliwaumba.




44

(Fungu Picha 2: Mwanzo 1:31)
Mungu akaona kila kitu alichokifanya, na tazama, ni chema sana.



45

Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya sita.
Mwanzo 1:31
Siku ya sita - siku Mungu alipofanya wanyama, na halafu uumbaji wa juu kuliko wote - mtu - wanadamu.


46

Adamu na Hawa hawakutokana na mfumo wa mabadiliko ama kutokea tu kwa nasibu. Biblia inasema ya kwamba Mungu aliisanii miili yao kwa mfano wake.

4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?


47

Yeye ni  Mhandisi Mkuu - Msanii Mkuu mwenye Ujuzi - yeye aliyetufanya tukawepo!
Siku ya Saba
Katika siku ya saba,  kazi ya Mungu  ya uumbaji ilimalizika, hivyo akapumzika. Pia Akaiweka siku ya saba kuwa ya pekee kama Sabato ya pumziko.



48

(Fungu Picha 3: Mwanzo 2:1,2)
Basi mbingu na nchi zikamalizika, na jeshi lake lote.



49

Na siku ya  saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya,



50

akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya.
Mwanzo 2:1,2



51

Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na  kuifanya. Tutazungumza zaidi juu ya hii Sabato ya pumziko ya siku ya saba huko mbeleni.


52

Hivyo hapo tumepata  mtizamo kwa  ufupi uonyeshao jinsi Mungu alivyoumba dunia na kila kilichomo ndani yake, tukiwemo sisi wanadamu.


53

Hebu tumuangalie kwa ukaribu zaidi jinsi huyu Msanii na Muumbaji alivyo wa kushangaza kwa kweli:


# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?


54

mwili wa mwanadamu unatupatia kielelezo cha kushangaza cha usanii na msanii.


55

Fikiria juu ya sehemu moja tu ya mwili wa mwanadamu - jicho:



56

(Video: Sekunde 10)
Wanasayansi wanatuambia ya kwamba ubunifu mzuri sana wa chamba na kioo cha jicho hufanya hata Kamera zilizo za kisasa zaidi duniani kuonekana kama visanamu cha mtoto cha kuchezea kwa ulinganifu.


57

Jicho linabadili nuru kuwa ujumbe, ubongo unaelewa katika namna ambayo hata maabara zilizoendelea sana za dunia haziwezi kuiga. Chembehai za Ubongo hubadili jumbe hizi kuwa muujiza wa uonaji - jambo ambalo hakuna kingine chochote hapa duniani kinachokaribia utendaji wake.


58

Jicho la mwanadamu hutupatia kithibitisho cha Muumbaji anayetaka sisi tuone uzuri ambao ameufanya katika ulimwengu wote.
Si ajabu mtunga Zaburi aliandika:



59

(Fungu: Zaburi 139:14)
Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa
kwa jinsi ya ajabu ya kutisha;



60

Matendo yako ni ya ajabu,
Na nafsi yangu yajua sana. Zaburi 139:14
Mwili wa mtu na mawazo yake ni muunganiko wa vitu vingi na imewezekana tu ukawa hivyo kutokana na Msanii mwenye hekima sana.

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?


61

Lakini vipi juu ya ulimwengu?  Ni kithibitisho gani tulichonacho kwamba Mungu mwenye kusanii alikuwa mtendaji katika kuumba ulimwengu wote?


62

Isaya, nabii wa injili,  anatupa changamoto sisi sote kutoweka macho yetu katika mambo madogo tu  na badala yake kuipa mtizamo kazi ya Mungu inayoonekana katika anga.



63

(Fungu  Picha 2: Isaya 40:26)
Inueni macho yenu juu, mkaone; ni nani aliyeziumba hizi; aletaye nje jeshi lao kwa hesabu;



64

aziita zote kwa majina; kwa ukuu wa uweza wake,




65

hapana moja isiyokuwepo mahali pake.
Isaya  40:26


66

Je, umepata kutizama juu angani ukiangalia nyota zisizohesabika zilizo juu yako?  Je, umepata kujiuliza zilipotokea  zote hizo na kustaajabu juu ya uwingi wake?


67

Mungu alitumia kielelezo  kinachotusaidia kuelewa kwa ubora zaidi kidogo juu ya ukubwa wa jambo hili.
Alipata kumchukua Ibrahimu, baba wa jamii ya kiarabu na ya kiyahudi, na kamuweka mahali nje na kumpa changamoto ya kuhesabu nyota.

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?



68

(Fungu: Mwanzo 15:5)
Tazama sasa mbinguni, kuzihesabu nyota, kama ukiweza kuzihesabu. Ndivyo utakavyokuwa uzao wako.
Mwanzo 15:5.


69

Hivi karibuni, mtaalamu wa nyota, alisema, kama ungeweza kuhesabu chembe moja moja za mchanga katika pwani zote duniani, ungepata kwa kukadiria idadi iliyo sawa na idadi ya nyota zilizoko katika mbingu.



70

Safari ijayo ukienda kwenye pwani, jaribu kuhesabu ndoo iliyojaa mchanga. Bora uwe na  muda wa kutosha! Je, yashangaza ya kwamba Mfalme Daudi alisema,



71

(Fungu  Picha 2: Zaburi 8: 3,4)
Nikiziangalia  mbingu zako, kazi ya vidole vyako, Mwezi na nyota ulizoziratibisha;



72

mtu ni kitu gani hata umkumbuke, Na binadamu hata umwangalie?
Zaburi 8:3,4



73

(Video: Sek. 20) Je, umepata kujiuliza kama Mungu aliye na uwezo mkubwa kiasi hicho anayetawala  na kushikilia ulimwengu mkubwa kiasi hicho anahusika nasi na matatizo yetu hapa Duniani? Bado Yesu anasema kwamba hakuna hata shomoro (zuwaridi) mmoja aangukaye  chini bila ya Mungu kutambua.

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?



74

(Fungu: Mathayo 10:31)
Kwa hiyo msiogope; ninyi mu wa thamani kuliko shomoro wengi.
Na kwa kusisitiza zaidi juu ya Upendo wa Mungu na uangalizi wake,
Yesu alisema,



75

(Fungu: Mathayo 10:30)
Lakini kwa upande wenu, hata nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa zote.
Mathayo 10:30.
Mungu wa ajabu kiasi gani!


76


Ni haki gani aliyo nayo Mungu wa Biblia kudai ya kwamba kila mmoja anapaswa kumuabudu yeye pekee?
Mungu wa Biblia na wa Ukristo anadai ya kwamba Yeye anastahili ibada na sala kwa sababu Yeye ni Muumbaji-Mungu.


77

Kama Yeye ndiye hicho anachodai, na Yeye ni Muumbaji, basi Anastahili ibada zetu, je, unakubaliana na hilo?


78

Wakati Yohana, mmoja wa wanafunzi wa Kristo na mwandishi wa kitabu cha mwisho cha Biblia, Ufunuo, alipokuwa kwenye njozi kisiwani Patmo, alipewa kuona chumba chenye kiti cha enzi mbinguni.
Angalia aliyoona:



79

wale wazee ishirini na wanne hujiangusha mbele ya huyo aliyeketi juu ya kiti cha enzi na kumwabudu huyo ambaye



80

anaishi milele na milele, na huziweka
taji zao mbele za kiti cha enzi na kusema:

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?



81

Umestahili wewe, Bwana wetu na Mungu wetu, kuupokea utukufu na heshima na uweza;



82

Kwa kuwa wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi yako vilikuwako, navyo vikaumbwa.
Ufunua 4:10, 11


83

Hawa wazee mbele za kiti cha enzi cha Mungu wanamsifu na kumwabudu kwa sababu Yeye ni Muumbaji. Hii ni sababu pia twapaswa kumuabudu Mungu wa mbinguni juu.


84

Yeye ndiye aliyeiumba dunia na sisi wote. Lakini, waweza uliza, tunacho kithibitisho gani kingine kuwa Mungu ni Muumbaji? Mungu Yeye mwenyewe hutuambia ya kwamba tunavyo vithibitisho vinavyotuzunguka pote ya kwamba Yeye ndiye Muumbaji.



85

(Fungu Picha 2: Rum. 1:20)
Tangu Mungu alipoumba ulimwengu, uwezo wake wa milele na uungu wake, ingawa havionekani kwa macho, vinafahamika wazi. Watu wanaweza kuyajua mambo hayo kutokana na vitu hivyo alivyoumba Mungu. Kwa hiyo hawana njia yoyote ya kujitetea!



86

Hata uwezo wake wa milele na Uungu wake.
Warumi 1:20
Tangu uumbaji, kumekuwa na vithibitisho katika viumbe vyote kwamba Mungu ndiye Mtengenezaji wa vyote hivi.


87

Kama tulivyoona swala la nyayo katika mchanga. Tulijua yupo aliyekuwepo pale hata kama tulikuwa hatujamwona.

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?


88

Na mara uonapo vyote hivi vikikuzunguka ambavyo vilipaswa kuumbwa na fulani ili viwepo, hivyo vyawa kama nyayo zikuambiazo Yupo aliye hai aliyetengeneza hivi vyote.


89

Mungu Baba, kama Biblia imuitavyo, hakuwa peke yake katika kazi Yake ya uumbaji.



90

(Fungu: Mwanzo 1:26)
Katika Mwanzo inasema, Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu......
Injili ya Yohana inaliendeleza hili zaidi.



91

(Fungu Picha 3: Yohana 1:1-3)
Hapo Mwanzo, Neno alikuwako; naye alikuwa na Mungu, naye alikuwa Mungu.



92

Tangu mwanzo Neno alikuwa na Mungu.



93

Kwa njia yake vitu vyote viliumbwa, hakuna hata kitu kimoja kilichoumbwa bila Yeye kujua.



94

(Fungu: Yohana 1:14)
Naye Neno akawa mwanadamu, akakaa kwetu. Nasi tumeuona utukufu wake, utukufu wake yeye aliye Mwana wa pekee wa Baba; amejaa neema na ukweli.



95

utukufu wake Yeye aliye Mwana wa pekee
wa Baba, amejaa neema na ukweli.
Yohana 1:14.

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?



96

Biblia inanena juu ya kile tukijuacho kama Uungu: Mungu Baba, Mungu Mwana, Mungu Roho Mtakatifu. Uungu ni nafsi tatu, wote wanawaza sawa, ingawa kila mmoja ni nafsi inayojitegemea.


97

Yesu alishirikiana na Baba kuumba kila kitu.




98

(Fungu: Waefeso 3:9)
tena niwaangazie watu wote waone jinsi mpango wa Mungu uliofichika unavyotekelezwa. Mungu aliye Muumba wa vitu vyote alificha siri hiyo yake tangu milele,
Kila karama nzuri na iliyo kamili ambayo mwanadamu amepata kuwa nayo ama atakayopata kuwa nayo inatokana na Muumbaji atoaye kwa wanadamu wote mibaraka yote hiyo.



99

Mungu hakumuumba tu mtu kwa mfano wake na kumpatia ulimwengu mzuri wa kuishi ndani yake, bali pia hujali sana mahitaji ya mwanadamu:



100

(Fungu: Zaburi 145:15,16)
Macho ya watu wote yakuelekea wewe nawe huwapa chakula chao kwa wakati wake.



101

Waufumbua mkono wako, wakishibisha kila kilicho hai matakwa yake.
Zaburi 145:15, 16.



102

Hebu tutizame njia chache tu jinsi Mungu anavyojali mahitaji ya viumbe wake.
Tafakari juu ya maji unayokunywa. Ni ya zamani kuliko ihramu--mazee kama vilima.

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?


103

Maji yaweza kuchafuliwa na madawa ama takataka, lakini acha jua liyageuze kuwa hewa ama liyainue na kuyapeleka angani,


104

yanakuwa masafi tena na kufaa kutumika tena na tena, kwa kusambazwa na mvua, umande au theluji. Ni mpango wa ajabu kiasi gani wa mfumo wa maji ambao Mungu aliusanii!


105

Kisha kuna chanzo kikuu cha nishati kilichopo angani-jua! Tafakari kwa muda mfupi:


106

Kama jua lingelikuwa kubwa kidogo kuliko lilivyo ama karibu na dunia kidogo zaidi ya lilivyo, maziwa yetu yangechemka na kutoweka.



107

Kama jua lingelikuwa dogo kidogo ama mbali kidogo zaidi ya lilivyo sasa, anga letu lingeganda. Kwa namna yoyote kati ya hizo, kusingekuwa na uhai Duniani.
Bali Mungu si tu kwamba aliumba vitu vyote, Anavihifadhi vitu vyote pia!
Hewa tunayoivuta ni karama ya Mungu: Biblia yasema,



108

(Fungu: Ayubu 12:10)
Ambaye nafsi ya kila kilicho hai iko mikononi mwake, Na pumzi ya wanadamu wote.
Ayubu 12:10.


109

Mungu aliusanii ulimwengu, na alijua tu kanuni iliyo sahihi kwa ajili ya hewa tunayoivuta ili ihifadhi maisha yetu na kutupa afya Duniani.

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?



110

Alijua kiasi halali cha  mchanganyo wa Nitrojeni, Oksijeni, Argon, na Kabon Daioksaid  katika anga. Hilo lisingelitokea tu!


111


Hakuna mwisho katika maajabu ya mambo ya asili ya dunia-hakuna mwisho kwa uangalizi wa Mungu kwa viumbe vyake. Fikiria juu ya uhamiaji wa ndege wa angani, ni moja ya vitendawili vikuu katika mambo ya asili.


112

Yawezekanaje ndege wenye uzito wa pungufu ya wakia moja  kusafiri maili maelfu bila kupumzika, hadi kufikia tuo walilolipanga hata kabla hawajaliona?


113

Samaki wawezaje  kupata vijito mahali maisha yao yalipoanzia, maili 1,200  zakuvuka katika bahari isiyo na mipaka bayana?
Walijifunzaje kujua wakati na mahali pa kwenda?



114

Nani aliyefundisha nyuki kutengeneza sega la asali ambalo ni shani ya kihandisi, na wakiwa na ubongo usioweza kuzidi kichwa cha sindano?
Nani aliye Mbunifu nyuma ya yote haya? Ayubu anatuambia:



115

(Ayubu 12:7-9)
Lakini sasa waulize hao wanyama, nao watakufundisha;  Na nyuni (ndege) wa angani  nao watakuambia;



116

au nena na nchi, nayo itakufundisha; nao samaki wa baharini watakutangazia.

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?



117

Katika hawa wote ni yupi asiyejua, Kwamba ni mkono wa BWANA uliofanya haya?
Ayubu 12:7-9.
Ndiyo, Mungu aliyafanya yote!
Kwa kweli, wajibu wetu na wasaa wa kumwabudu Mungu umejengwa katika ukweli ya kwamba Yeye ni Muumbaji na kwa sababu yake vitu vyote vinapata kuwepo.



118

(Zaburi 100:3)
Jueni ya kwamba BWANA ndiye Mungu; Ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake;



119

Tu watu wake na kondoo wa malisho yake.
Zaburi 100:3.
Mungu ajua mahitaji yetu, na Anao uwezo wa kutupatia mahitaji hayo!



120

(Yeremia 32:17)
Yeremia anasema, Aa! Bwana MUNGU, tazama , wewe umeziumba mbingu na nchi,kwa uweza wako mkuu na kwa mkono wako ulionyooshwa;



121

hapana neno lililo gumu usiloliweza.


122

Je, hilo halikupi amani mawazoni kujua kwamba Mungu aweza kushughulikia kila kitu katika ulimwengu na katika maisha yako binafsi pia? Hakuna tatizo lililo dogo sana lisiloweza kuletwa kwa Mungu wa Ulimwengu. Mungu ajua kila kitu - hata anayajua yote kabla ya wakati wake.



123

(Isaya 46:9)
Anasema, Mimi ni Mungu, wala hapana aliye kama mimi;

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?






124

nitangazaye mwisho tangu mwanzo, na tangu zamani za kale mambo yasiyotendeka bado.
Isaya 46:10



125

Ni amani na ujasiri kiasi gani tuwezao kuwa nao kwa kujua kwamba hakuna liwezalo kutokea kwetu lililogumu sana kwa Mungu kulishughulikia. Lakini bora kuliko yote,




126

(Fungu: 1 Yohana 4:8)
Mungu ni upendo.
Yesu alisema:




127

(Fungu: Yohana 16:27)
maana yeye (Baba) mwenyewe anawapenda ninyi...




128

(Sek. 10 za video) Je, inakushangaza ya kwamba Mungu mkuu aliyeumba na anayehifadhi ulimwengu mkubwa kiasi hicho, aweza kujihusisha nawe binafsi? Inaduwaza kutafakari uwezo wa Mungu usio na kikomo, Hekima yake yenye kina, na uwezo wake wa kuwa mahali pote.
Bali upendo ni kitu tuwezacho kukielewa. Na hakuna chochote duniani kote kiwezacho kututenga na upendo wa Mungu!




129

(Fungu: Warumi 8:38, 39)
Maana ninajua hakika kwamba hakuna kitu kiwezacho kututenganisha na upendo wake: wala kifo, wala uhai; wala malaika, au nguvu nyingine za mbinguni;




130

wala yanayotokea sasa wala yatakayotokea baadaye,

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?



131

wala ulimwengu wa juu, wala  wa chini kabisa, hakuna kiumbe chochote kitakachoweza kututenga na upendo wa Mungu kwetu



132

kwa njia ya Kristo Yesu Bwana wetu.
Warumi 8:38,39.


133

Mungu anatupenda tunapopendeka - bali pia tunapokuwa hatupendeki. Je, unatambua hilo? Anatupenda bila kujali kama tu weusi ama weupe, wanaume ama wanawake, wazuri ama wabaya.
Hakuna aliye kama hivyo!
Bali la muhimu kuliko yote, Anatupenda milele!



134

(Fungu: Yeremia 31:3)
Naam, nimekupenda kwa upendo wa milele.



135

(Fungu: Zaburi 100:5)
Daudi aliandika:...BWANA ndiye mwema; na Rehema zake (pia upendo wake) ni za milele. Zaburi 100:5. Mungu kamwe hakati tamaa juu yetu! Yu pamoja nasi kila wakati tunapoishi na kamwe hatatuacha! Na kana kwamba kungelikuwa bado na mashaka kuhusu upendo wake, Mungu anaeleza kwa njia rahisi ili tuelewe kwa urahisi pia:



136

(Fungu: Isaya 49:15, 16)
Je, mwanamke  aweza kumsahau  mtoto wake anyonyaye, hata asimhurumie mwana wa  tumbo lake?



137

Naam, hawa waweza kusahau, lakini mimi sitakusahau wewe!

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?



138

Tazama,nimekuchora katika vitanga vya mikono yangu;.....
Isaya 49:16.


139

Mungu alijaribu kueleleza Upendo wake kwa mwanadamu, bali maneno na ujumbe uliotumwa na manabii na malaika haukutosha.
Hatukuupata ujumbe.


140

Hivyo Mungu akamtuma Mwanae. Yesu alikuwa ni ufunuo mkamilifu wa nafsi na tabia ya Baba Yake.



141

(Fungu: Yohana 14:9)
Yesu akamwambia, Filipo, nimekaa nanyi muda wote huu, nawe hujanijua? Aliyekwisha niona mimi amemwona Baba. Unawezaje basi, kusema: <Tuonyeshe Baba?>


142

Kama kweli twataka kujua Mungu alivyo na jinsi anavyohisi kutuhusu sisi, twahitaji kujifunza maisha ya Yesu. Alichukua asili yetu,
ili afikie mahitaji yetu.
Alihubiri habari njema kwa maskini.
Aliponya waliovunjika mioyo na kuwapa vipofu kuona.


143

Aliwalisha wenye njaa na kula pamoja na watu majumbani kwao. Aliwasamehe dhambi na kuwapa tumaini  kwa ajili ya siku za usoni.


# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?


144

Uso wake ulikuwa wa kwanza kwa watu kuuona.
Sauti yake ya kwanza kwa wengi kuisikia.
Alisambaza uhai na furaha pote vijijini na mijini alipotembelea.
Maisha yake yalikuwa ya kujikana nafsi na uangalifu wa kujali wengine.


145

Tunapoiangalia aibu, kebehi, na udhaliilishwaji Aliouvumilia, Kifo chake Kalvari na moyo wake uliovunjika, tunaanza kuelewa kidogo juu ya upendo wa Mungu kwa watoto wake.



146

(Fungu: Yohana 3:16)
Maana Mungu aliupenda ulimwengu hivi hata akamtoa Mwana wake wa pekee,



147

ili kila amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.
Yohana 3:16.


148

Huyu Mungu wa Ulimwengu ni nani?
Yeye ni Muumbaji mwenye Uwezo.
Yeye ni Mpaji wa kushangaza.
Yeye ni Msanii wa ajabu.
Yeye ni Baba mwenye Upendo.

# 4 - Ni kwa Nasibu au kwa Kupanga?



149

Miaka mingi iliyopita mvulana mdogo alipatwa na ajali mbaya. Alikimbizwa hospitali akiwa mahututi. Kijana alihitaji kupewa damu moja kwa moja kwenye mishipa. Hakuna aliyepatikana ili kutoa damu yake kwa ajili ya huyu kijana.
Babake alikuwa na aina hiyo hiyo ya damu na akakubali kutoa damu.
Tabibu akaanza kutoa damu toka kwa mkono wa baba na kuiingiza moja kwa moja kwa kutumia mrija kupitia mkononi mwa mtoto. Damu ilipoendelea kumiminika moja kwa moja ikiingia kwenye mwili wa mtoto uliokuwa umetulia tuli, baba alimuangalia Tabibu na kusema, Mganga, kama unahitaji toa yote. Mganga, nipo tayari kutoa damu yangu yote kwa ajili ya mtoto wangu.


150

Baba yetu wa mbinguni alitizama ulimwengu Aliouumba na akauona jinsi ulivyopotea katika dhambi.
Alitoa yote ambayo mbingu zingelitoa kupitia kwa Mwanae.
Yesu alisema, Baba, kama unahitaji, chukua yote. Chukua kila tone la damu yangu kumuokoa mtoto wangu, binti yangu, rafiki yangu.


151

Unawezaje kuupa mgongo upendo wa namna hiyo? Mungu mwenye uwezo wote,mwenye upendo alikuumba.
Wakati jamii ya wanadamu ilipotenda dhambi, alitoa yote kwa ajili yako.
Wewe ni wa muhimu Kwake. Anakupenda kwa upendo wa kushangaza.
Tunapoinamisha vichwa vyetu kusali usiku wa leo, je ungependa kuinua mkono wako na kusema, Bwana, Ninafungua moyo wangu kwa upendo wako sasa hivi. Ahsante kwa kuniumba mimi na kunikomboa. Ninatoa maisha yangu kwako sasa hivi.



1

Maana Yake Kwako Leo


2

Miaka kadhaa iliyopita ndugu mmoja aitwaye Marsh alitambua ya kwamba shangazi yake alikuwa amefariki na alimhusisha katika wosia wake. Wosia ulisomeka hivi: Kwa mpendwa Steven Marsh, ninakuachia Biblia yangu kubwa pamoja na vyote ilivyo navyo, pamoja na masalio ya mali yangu. Naam, baada ya kulipa madeni, fedha kiasi tu cha mali yote ndiyo iliyosalia.
Hiyo fedha ilimalizika upesi, na ndugu Marsh alisalia tu na ile Biblia kubwa, aliyokuwa ameiweka kwenye kasha kwenye chumba cha juu kabisa cha ghorofa. Steven Marsh ilibidi astaafu katika ujira mdogo. Aliishi katika umaskini kwa miaka thelathini.

5 - Siri za Magombo ya Kale

# 5 - Siri za Magombo ya Kale



3

(Video: sek 9) Hatimaye, akiwa katika umri wa miaka ya 90, aliamua kuhamia nyumbani kwa mwanae. Wakati akifunga mizigo yake, aliiona  Biblia ya shangazi yake  na akaanza kuipekua.
Bw.Marsh alishangaa kukuta noti za fedha zikiwa kimesambaa katika kurasa mbalimbali.
Alihesabu zaidi ya dola elfu tano za kimarekani fedha taslimu, fedha nyingi sana wakati huo.
Mtu huyu alikuwa amekaa muda mrefu sana wa maisha yake katika ufukara wakati angelikuwa tajiri.
Kulikuwa na hazina pale pale katika vidole vyake ndani ya Neno la Mungu.
Je, yawezekana pia ya kwamba sisi pia,tunayo hazina ya ajabu  katika vidole vyetu?
Wapo mamilioni wanaoamini ya kwamba Biblia ni kitabu cha kushangaza zaidi kilichowahi kuandikwa.
Wanasadiki ya kwamba Biblia ni kitabu kilicho vuviwa na Mungu na kinayo maelekezo yasaidiayo kupata uzima wa milele.
Watu wa kila taifa, na lugha, na jamaa wamelikubali neno la Mungu kama libadilishalo maisha, kama tunu ya thamani.
Watu wengine wanayo mashaka mazito. Wanayo maswali mengi.


4

Sasa je, vipi juu ya kitabu kinachouzwa sana kuliko vyote duniani - Biblia Takatifu? Je, yaweza kuaminiwa? Je, inasema ukweli? Je, iko sahihi? Baadhi ya watu husema waweza kuiamini Biblia bila wasiwasi wowote. Wengine husema huwezi. Ni nani aliyesahihi?



5

Na jibu ni la muhimu, kwa sababu kama Biblia NI ya kweli, basi uiamini usiiamini inasalia kuwa swala la uzima na mauti!
Kama Biblia ni ya kweli, hatima yako nzima ya milele inategemea kama unaiamini na kuikubali. Kile unachokiamini kuhusu Biblia kinafanya tofauti yote katika kile unachokiamini kuhusu Mungu.
Kuna mahali pamoja tu peke yake uwezapo kupata picha safi na bayana ya Mungu, na hapo ni kwenye Biblia. Kwa kweli, hiyo ndiyo sababu Biblia ilitolewa kwetu.


6

Inatuambia juu ya Mungu asiyeonekana ambaye twaweza tu kumjua kwa kusoma ujumbe  ambao ameutuma kupitia kwa manabii wake na Mwana wake kumfunua Yeye Mwenyewe kwetu.


7

Hivyo hebu na tuangalie kitabu hiki kikuu, Biblia, kinachoitwa pia Neno la Mungu, na tuone kama twaweza kuthibitishiwa kama ni cha kweli au la, kama chaweza kuaminiwa ama la.



8

Biblia kwa kweli si tu kitabu kimoja, bali ni maktaba nzima ya vitabu ndani ya jalada moja.
Biblia inavyo vitabu 66 vilivyoandikwa nyakati tofauti na  waandishi tofauti kwa zaidi ya miaka 1,600.
Kuna vitabu 39 katika Agano la Kale na vitabu 27 katika Agano Jipya.


9

Watu tofauti tofauti arobaini na watano waliandika vitabu hivi, na bado tunaona kwao maafikiano  ya kushangaza yawezayo kuelezewa tu na ukweli ya kwamba walikuwa na chanzo kimoja cha yale waliyoyaandika.
Huu mwafaka ulio kamili ulitokea hata ingawa wengi wa hawa waandishi wa vitabu hivi  hawakupata hata kuonana.

5 - Siri za Magombo ya Kale

# 5 - Siri za Magombo ya Kale


10

Walitokana na shughuli au taaluma mbalimbali. Baadhi walikuwa wavuvi, baadhi walikuwa wachungaji wa kondoo, baadhi wafalme, baadhi viongozi wa serikali, baadhi wakulima, baadhi wahubiri, baadhi mawaziri, mganga pia - watu tokea aina zote za maisha.



11

(Video: sek. 13) Bado unaona kuna umoja kamili na upatano kati ya vitabu walivyoandika. Ni muujiza, hakika!
Huu mwafaka waweza tu kuelezeka kwa kutambua ya kwamba Mungu alitupatia Kitabu hiki ili aweze kuwasiliana nasi juu ya mapenzi yake kwetu.



12

(Fungu: 2 Petro 1:21 HNKK)
Maana hakuna ujumbe wa kinabii unaotokana na matakwa ya binadamu, bali watu walinena ujumbe wa Mungu wakiongozwa na Roho Mtakatifu.



13

(Fungu: 2 Timotheo 3:16 - 17)
Mtume Paulo aliandika:
Maandiko yote Matakatifu yameandikwa kwa uongozi wa Mungu, na yanafaa katika kufundishia ukweli,



14

kuonya, kusahihisha makosa, na kuwaongoza watu waishi maisha adili



15

ili mtu anaye mtumikia Mungu awe mkamilifu, na tayari kabisa kufanya kila tendo jema.
2 Timotheo 3:16,17.
Sababu iliyomfanya Mungu achague mbinu hii ya mawasiliano - kunena nasi katika njia ya maandishi-ni hii- njia iliyokuwepo awali ya mawasiliano kati Yake na mwanadamu ilikuwa imekatwa na dhambi.

# 5 - Siri za Magombo ya Kale


16

Wakati Mungu na mwanadamu walipotembea na kuzungumza pamoja Edeni,  hakukuwa na hitaji la nabii kuandika kile ambacho Mungu alitaka mtu ajue.



17

Wakati Adamu alipotenda dhambi, alijificha mbali na Mungu, kwani aliogopa na alikuwa na hatia kutokana na kile alichokuwa amekitenda. Mungu alipomuuliza Adamu wapi alipokuwa, Adamu alijibu,



18

(Fungu: Mwanzo 3:10)
....Nalisikia sauti yako bustanini,
nikaogopa,......nikajificha.
Mwanzo 3:10.



19

Mungu hakuendelea  tena  kuzungumza uso kwa uso. Alichagua kufunua yale aliyotaka tuyajue kupitia kwa manabii wake, kupitia kwa Mwana Wake.



20

(Fungu: Amosi 3:7)
Hakika Bwana Mungu hatafanya neno lolote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri Yake.


21

Mungu alimvuvia Musa kuandika kitabu cha Ayubu na vitabu vya awali vitano vya Agano la Kale, ambavyo kwa pamoja vinaitwa Sheria.
Hii ilikuwa nyakati za miaka ya 1500 KK.


22

Wakati huu Israeli ilikuwa imekuwa hadi kufikia taifa kubwa lenye watu milioni kadhaa na Mungu alihitaji kuwasiliana mapenzi Yake katika  namna ya maandishi.
Huu ndio wakati sahihi ambapo maandishi ya ki-alfabeti, kuacha yale kutumia picha , yaligunduliwa.

# 5 - Siri za Magombo ya Kale



23

Watu wangeweza sasa kusoma Amri Kumi ambazo Mungu aliandika kwa vidole Vyake mwenyewe na Kitabu cha Sheria ambacho Musa aliandika kwa niaba ya Mungu.





24

Lakini swali linasalia: Je,Biblia bado ni sahihi na ya kutegemewa, kama vile Mungu alivyoitoa?
Hadi mwaka 1947, maandishi ya awali kuliko yote ya Agano la Kale zilikuwa nakala tokea mwaka wa 900 B.K.




25

gombo la Isaya lililopatikana lilionekana kurudi nyuma hadi mwaka wa 125 K.K.
Lilikuwa limenakiliwa zaidi ya miaka elfu kabla maandishi ya zamani zaidi kupatikana hadi wakati huo.
Lilikuwa na Kitabu kizima cha Isaya.





26

Bwana Frederic Kenyon, mmoja kati ya walio sifika katika taaluma yao na raisi wa Chuo cha Uingereza cha maarifa ya mambo ya kale (Akiolojia) alitaarifu hivi:
Kwenye sura moja yenye maneno 166 kuna neno moja tu (lenye herufi tatu) liletalo utata na hii ikiwa ni baada ya miaka elfu ya mpisho,




27

na neno hili halina uzito kiasi cha kubadili maana ya ujumbe!




28

Bw Frederic Kenyon anaiweka hivi:




29

Mkristo aweza kuchukua Biblia nzima katika mkono wake na kusema bila hofu au kusitasita ya kwamba anashikilia mkononi mwake Neno la kweli la Mungu,

# 5 - Siri za Magombo ya Kale




30

lililorithishwa bila kupoteza jambo muhimu toka kizazi hadi kizazi katika karne zote.




31

Bw Kenyon alitoa kauli hii baada ya kutumia maisha yake katika utafiti mkubwa wa ushuhuda wa jinsi Biblia ilivyo pitishwa (ilivyo pishwa) na athari ambazo zaweza kuwa zilipatikana kutokana na mpisho huo kwa ujumbe ulio Kitabuni.



32

Wakosoaji wa Biblia karne moja iliyopita walikuwa wamepata sababu nyingi zilizozua mashaka juu ya Biblia, lakini lawama hizi nyingi zimenyamazishwa na koleo la wachimbuzi wa mambo ya kale.




33

Hadi karne ya kumi na tisa, machache sana yalikuwa yakifahamika juu ya nyakati zilizopita isipokuwa kwa yale ambayo Biblia ilikuwa imeyasema kuzihusu.





34

Historia ya kale ilionekana kufungwa milele ndani ya maandishi ya picha zisizo za kawaida za Misri. Kwa sababu hakuna hata mmoja kule Misri, wala duniani kote, aliyeweza kuyafumbua.




35

Kisha mwaka 1798, Napolioni aliongoza safari ya kijeshi hadi Misri.
Akiwa na askari wake 38,000, Napolioni alichukua wasanii mia, wataalamu wa lugha, na wanasayansi ili wamsaidie kuelewa kwa ubora zaidi historia ya nchi hii iliyomkanganya.



36

Kila mahali, waliona kumbukumbu za zamani- maandishi yasiyosomeka kwa urahisi, sanamu na makaburi yaliyopambwa na kuta za mahekalu. Napolioni na wasomi wake walishangaa haya maandishi ya picha yalikuwa na ujumbe gani wa siri.

# 5 - Siri za Magombo ya Kale


37

Mwaka mmoja baadaye, 1799, uvumbuzi muhimu kuliko wote uliokuwa umefanyika hadi wakati huo katika maarifa ya mambo ya kale ulifanyika.



38

Mmojawapo kati ya askari wa Napolioni alifukua kile kilichokuja fahamika kama Jiwe la Rosetta, jiwe jeusi -lenye sentimeta 122 za urefu na sentimeta 76 upana (futi nne kwa futi mbili na nusu) hilo lingefungua fumbo la maandishi ya picha na kufunua siri zilizofichika kwa karne nyingi.


39

Jiwe la Rosetta hivi sasa limewekwa katika jumba la makumbusho la Uingereza.



40

Huu ubamba wa mwamba, uliofukuliwa karibu na mji wa Rosetta - mahali matawi ya mto yanapoingilia baharini, ulikuwa na tamko la kale katika lugha tatu tofauti:




41

Hieroglyphic (maandishi ya picha), kidemo cha Misri, na Kiyunani.
Kwa kweli, wasomi waliweza kutafsiri kwa urahisi maandishi ya kiyunani, bali lugha ya picha ilikuwa kitu kingine.



42

Hata hivyo, miaka ishirini baadaye, mwaka wa 1822, kijana mwenye akili sana wa Kifaransa kwa jina la Jean Francois Champollion aliistua dunia kwa kuvumbua lugha ya picha iliyoko kwenye Jiwe la Rosetta.


43

Hivyo hazina kubwa ya Misri ya kale ikafunguliwa kwa wasomi wa dunia.

# 5 - Siri za Magombo ya Kale



44

Lakini jambo la muhimu zaidi, historia ya Misri iliyokuwa imesahauliwa kwa muda mrefu sasa iliyathibitisha maandiko.
Mawe yalilia ya kwamba kile Biblia ilichokisema kilikuwa ni kweli!


45

Kadiri wachimbuzi wa mambo ya kale wanavyoendelea kuchimba, ndivyo wanavyozidi kupata shuhuda za historia ya Biblia kwa kupata rekodi za kihistoria za tamaduni zilizopita.



46


Uvumbuzi wa karibuni wa Tell Marduk, umesisimua ulimwengu wa akiolojia.
Jiji hili lilikuwa likiitwa Ebla katika Syria- na hili eneo liliwahi kuwa la jamii iliyokuwa tajiri na iliyoerevuka ya takribani watu 300,000.


47

Tangu uvumbuzi wa Magombo ya Dead Sea hakujawahi kuwa na msisimko mkubwa kiasi hicho kwa wasomi wa eneo hili hapo uvumbuzi huu ulipofanyika!
Lakini ni jambo la kusisimua zaidi kwa wanafunzi wa Biblia.


48

Katika shule ya uandishi iliyounganika na ikulu ya jiji, vibao vya udongo na vipande vipande vingine 14,000 vilivyoandikwa vilipatikana, na vilionyesha kuwa vya nyakati za 2300 KK.
Ofisi ya kumbukumbu ya serikali ya zamani kuliko zote ilikuwa na rekodi rasmi za ufalme wa Ebla kwa zaidi ya karne moja.


49

Baadhi ya wanahistoria walikuwa wamehoji kama Waebrania walikuwa wameendeleza sanaa ya uandishi ulipofikia wakati wa Musa.
Hadi kufikia karne ya kumi na tisa, hakuna ushuhuda wa kihistoria uliokuwa umepatikana kulihakikisha hilo.

# 5 - Siri za Magombo ya Kale


50

Hata hivyo, bamba(mbao) za mawe za Ebla na zingine zaonekana kurudi nyuma katika historia hadi kabla ya wakati wa Musa.
Kwa kweli, wanaakiolojia wamevumbua maktaba nzima ambazo muda wake unaonekana kurudi nyuma hadi karne kadhaa kabla ya Musa.


51

Mbao za mawe za Ebla zinaeleza juu ya kisa cha Uumbaji na kisa cha Gharika.
Pia yaliyotajwa ni majina na sehemu ambazo zinashabihiana na zile za kibiblia: Esau, Ibrahimu, Israeli, Sinai, hata Yerusalemu.


52

Lakini jambo lakushangaza zaidi ni kutajwa kwa majiji ya dhambi mawili- Sodoma na Gomora.
Kabla ya uvumbuzi wa hizi mbao za mawe, hakuna kumbukumbu yoyote ya kihistoria ya miji hii iliyokuwa imefahamika isipokuwa katika Biblia.
Hivyo, hizi zilidhaniwa kuwa ni sehemu za kubuni tu.


53

Hata hivyo, vitabu vingi itabidi viandikwe tena, kwani uvumbuzi huu kwa kweli unathibitisha majina mengi ya kijiografia ya wakati huo.



54

Baadhi ya waandishi itawabidi wakubali ya kwamba Mwanzo ni zaidi ya nyimbo tu za kale na mapokeo.
Uvumbuzi kule Ebla na penginepo umethibitisha ukweli wa Biblia!



55

(Fungu: Zaburi 119:160)
Daudi anasema, Jumla ya Neno lako ni kweli..



56

(Fungu: Isaya 45:19)
Mungu anasema katika Isaya 45:19: ...Mimi, BWANA, nasema haki; nanena mambo ya adili.

# 5 - Siri za Magombo ya Kale


57

Wanasema ya kwamba wafu hawasemi hadithi.
Wanasema!
Hadithi zinazosisimua kuliko hadithi za kubuni.
Tamaduni zilizokufa zamani zinanena kutoka kwenye makaburi ya mavumbi, zikihakikisha usahihi na kuaminika kwa Neno la Mungu.



58

Hadi karne ya kumi na tisa, baadhi ya wasomi waliamini ya kwamba Malkia Semiramis aliijenga Babeli.
Wakati huo huo katika Biblia, Danieli alimnukuu Mfalme Nebukadneza akisema,



59

(Fungu: Danieli 4:30)
.....Mji huu siyo Babeli mkubwa  nilioujenga mimi?
Ni nani aliyekuwa sahihi?



60

Mwaka 1899, Robert Koldewey alianza kuchimbua mabaki ya zamani ya Babeli, akafukua makumi elfu ya matofali yaliyokuwa yametengenezwa kwa kuchomwa kwenye tanuru, yote yakiwa na muhuri wa Mfalme Nebukadneza, yote yakiwa yamechukuliwa toka kwa kuta na mahekalu ya jiji!



61

Mbao ya jiwe ya kikabari,  iliyoelezea mafanikio ya Nebukadneza, ilipatwa pia na wana akiolojia wa Babeli.



62

Katika huo, mfalme alisema,Ngome za Esagila na Babeli  niliziimarisha na kuthibitisha jina la utawala wangu  milele.



63

(Fungu: Danieli 4:30)
Biblia yasema ya kwamba Nebukadneza mwenye kiburi akanena, akasema, 'Mji huu sio  Babeli,

# 5 - Siri za Magombo ya Kale



64

mkubwa nilioujenga mimi, uwe kao langu la kifalme, kwa uwezo wa nguvu zangu,ili uwe utukufu wa enzi yangu? Danieli 4:30


65


Maandishi ya Nyumba ya India Mashariki, sasa yakiwa London, yalitenga safu sita kwa ajili ya maandishi ya Babeli na hapa kuweka maelezo juu ya miradi mikubwa ya ujenzi wa Nebukadneza.
Hapa tena koleo likatetea Neno la Mungu.


66

Fumbo jingine la historia ya kidunia lilikuwa la kukosekana kwa Belshaza kama mtawala wa Babeli. Biblia ilimtaja Belshaza kama mtawala wa Babeli aliyeshuhudia maandiko katika ukuta wa ukumbi wa sherehe.
Je, yeye alikuwa tu ni matokeo ya ubunifu wa akili nzuri ya Danieli? La hasha!


67

Nabonidus, mrithi wa Nebukadneza mkuu, alikuwa amekabidhi ufalme kwa mwanae Belshaza, alipokuwa awe mbali huko Tema Uarabuni kwa miaka kumi.




68

Bamba zitokanazo na uvumbuzi wa wanaakiolojia zinasema kwamba ufalme ulikabidhiwa kwa hakika kwa Belshaza, mwana mrithi wa kifalme.
Hapa ni yale yaliyokuwa yameandikwa:



69

Na kwa Belshaza mwana aliyetukuka, mzao wa mwili wangu, weka kicho cha uungu mkuu katika moyo wake; na asiipe dhambi nafasi;



70

hebu na aridhike na uhai; na hebu kicho cha uungu mkuu kikae katika moyo wa Belshaza, mwanangu mpenzi mzaliwa wa kwanza.
Mungu Hunena kwa mwanadamu wa Kisasa, Uk.154.

# 5 - Siri za Magombo ya Kale



71

(Fungu:Danieli 12:4)
Je si jambo la kupendeza ya kwamba mwisho ya kitabu cha Danieli, tunasoma:
Lakini wewe,Ee Danieli, yafunge maneno haya, ukakitie muhuri kitabu, hata wakati wa mwisho:



72

wengi wataenda mbio huko na huko, na maarifa yataongezeka.
Danieli 12:4.
Maarifa yangeongezeka siyo tu katika ulimwengu wa kisayansi.
Maarifa yangeongezeka pia katika kuwa na usahihi wa Neno la Mungu.



73

Matofali na mizinga, bamba za mawe na nyaraka za kale - zilizochimbuliwa na wanaakiolojia - vyote vinahakikisha ya kwamba kile Biblia ikisemacho ni kweli!


74

Hata hivyo, kingine kinachothibitisha kwa nguvu ya kwamba Biblia ni Neno la Mungu lililo vuviwa ni uwezo wake wa kutaja mambo ya usoni.




75

(Fungu: Isaya 46:9 - 10)
..Mimi ni Mungu, wala hapana aliye kama mimi,



76

nitangazaye mwisho tangu mwanzo, na tangu zamani za kale mambo yasiyotendeka bado.
Isaya 46:9,10.


77

Ndiyo, Mungu anapolifungua pazia la wakati,akitupatia muonjo wa wakati ujao, anaonyesha kwa dunia ya kwamba Biblia si tu kitabu cha kawaida. Ni Kitabu Chake.

# 5 - Siri za Magombo ya Kale


78

Kabla ya Babeli kufikia kilele cha ukuu wake na utukufu,  Kitabu cha Mungu kilitabiri kuanguka kwake:



79

(Fungu: Isaya 13:19)
Na Babeli, huo utukufu wa falme, uzuri wa kiburi cha Wakaldayo,



80

utakuwa kama Sodoma na Gomora hapo Mungu alipoiangamiza.
Isaya 13:19.
Biblia ilitabiri hata mamlaka ambayo yangeuangusha ufalme huu mkuu.



81

(Fungu: Yeremia 51:11)
BWANA ameziamsha  roho za wafalme wa Wamedi; kwa sababu shauri lake ni juu ya Babeli auangamize; Yeremia 51:11.


82

Jina la mtu ambaye angeongoza majeshi dhidi ya Babeli lilitabiriwa miaka 150 kabla yake kuzaliwa, na pia jinsi ambavyo angelitenda.



83

(Fungu: Isaya 45:1)
Haya  ndiyo BWANA amwambiayo Koreshi, masihi wake, ...nita.....fungua milango mbele yake,.......
Isaya 45:1.
Je, unabii wa Biblia ulitimizwa?
Hata kila herufi!



84

Katika Ukumbi wa  Kiajemi wa  Jumba la Makumbusho la Uingereza  umesimama ule 'mzinga' wa Koreshi--uliogunduliwa katika mabaki ya Babeli. Katika huu mzinga wa udongo, Koreshi anaelezea juu ya ushindi wake!
Maelezo yako sahihi hata kwa undani!

# 5 - Siri za Magombo ya Kale



85

Biblia haikutabiri tu juu ya maangamivu ya Babeli, ilieleza pia yafuatayo:




86

(Fungu:Yeremia 51:37)
Na Babeli utakuwa magofu.... Yeremia 51:37.




87

(Fungu: Isaya 13:20-21)
Isaya aliandika:
Hautakaliwa na watu tena kabisa...




88

Lakini huko watalala hayawani wakali wa nyikani; na nyumba zao zitajaa bundi.......
Isaya 13:20,21.



89

Mungu peke yake ndiye ambaye angeliweza kuona wakati unaokuja na kutabiri kwa usahihi kiasi hicho juu ya hatima ya Babeli mkuu.
Mvumbuzi Austen H. Layard anaelezea juu ya eneo la Babeli ya kale:



90

Malundo yenye sura mbaya ya takataka yanafunika ekari nyingi za uso wa nchi....mahali pa pweke na penye uchafu uliokithiri.



91


Bundi wanaruka toka kwenye vichaka vilivyosambaa, na mbweha wachafu wananyatanyata kupitia kwenye mifereji.
Mavumbuzi Kati ya Mabaki ya Ninawi na Babeli, Uk. 413.

# 5 - Siri za Magombo ya Kale



92

Kuhusu utukufu wa zamani wa Babeli, hakuna kilichosalia ila jina lake katika kibao kando ya barabara.
Malundo makubwa yaliyosambaa juu ya mabaki ya Babeli ya kale ni kithibitisho hakika cha uvuvio na ukamilifu wa Biblia.



93

(Fungu: Isaya 40:8)
Twaweza kukubaliana na nabii:
Majani yakauka, ua lanyauka;
Bali neno la Mungu wetu litasimama milele.
Isaya 40:8.


94

Rafiki, kama Mungu aweza kuona mbele karne nyingi kama ilivyokuwa kwa falme za kale, je, twaweza kutilia mashaka hata kidogo uwezo wake na hekima ya kutabiri kwa usahihi kile kilichopo mbeleni katika maisha yetu? Vigumu!


95

Kwa kweli, unabii wa Biblia unatupatia upendeleo wa kuvuta mapazia, na kuangalia wakati ujao kupitia kwa macho ya Mungu, na kupata picha halisi ya utatuzi wake kwa matatizo yanayotishia uhai wa mwanadamu katika Sayari Dunia.


96

Biblia ni zaidi ya historia inayoaminika, ni zaidi ya vithibitisho vya kisayansi, ni zaidi ya unabii uliotimizwa.
Kama isingelikuwa hivyo, isingelikuwa neno jinsi watu walivyoitendea.


97

Neno kuu la Kitabu, kiini chake kabisa, ni taarifa ya kile kilichofanyika katika kilima chenye mawe mawe nje ya Yerusalemu zaidi ya karne kumi na tisa zilizopita. Kile tunachoamini kuhusu lile tukio kinafanya tofauti!

# 5 - Siri za Magombo ya Kale





98

Ama Mwana wa Mungu Aliye Hai alikufa katika msalaba ule au la.
Ama alikuwa Yeye ambaye Biblia inasema alikuwa au la!
Kalvari ilikuwa ni ndoto tu au halisi?
Inafanya tofauti, na tunahitaji kujua!



99

Pengine kielelezo kikuu zaidi ya vyote kwamba Biblia ipo kama inavyodai ni uwezo uliomo katika Kitabu wa kubadiili maisha.
Uwezo huo umefungwa katika mtu mmoja--Yesu Kristo! Yesu alisema,




100

Mwayachunguza maandiko,kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia.
Yohana 5:39




101

Yesu alikuwa akinena kuhusu Agano la Kale, kwani Agano Jipya halikuwa limeandikwa bado! Na unapofungua kurasa za Agano la Kale, utagundua kwamba zinatabiri juu ya Masihi ajaye na kueleza Utume wake wa upendo na wokovu.




102

Halafu akawaambia, Hii ndiyo maana ya maneno niliyowaambia nilipokuwa pamoja nanyi: kwamba ilikuwa lazima kukamilisha




103

yote yaliyoandikwa juu yangu katika Sheria ya Musa na katika vitabu vya manabii na katika kitabu cha Zaburi.
Luka 24:44.



104

Agano la Kale lilitabiri juu ya Kristo, na Agano Jipya ni kisa cha maisha yake.
Hivyo unaona, Biblia nzima ni ufunuo wa Yesu Kristo, aliyekuja kuonyesha sayari iliyokuwa katika uasi jinsi ya Baba yake alivyo.

# 5 - Siri za Magombo ya Kale



105

Hiyo ndiyo sababu Biblia inaitwa Neno Lililo hai la Mungu.
Inabeba nguvu ya kushangaza pamoja nayo popote iendapo - nguvu inayobadili maisha, inayobadili tabia ya mwanadamu, itoayo nguvu kwa wadhaifu, moyo mkuu kwa waliovunjika moyo na tumaini kwa wanaokufa.
Katika historia yote, uwezo wa Biblia kubadili watu umehakikishwa tena na tena. Watu waliotawaliwa na hasira wamebadilishwa kuwa wenye amani kwa nguvu ya Biblia.


106

Watu waovu na waliotawaliwa na tamaa wametakaswa na kuwa safi.
Walevi wameokolewa kutoka katika ulevi, wezi toka katika wizi, waongo toka katika kudanganya.
Huhitaji kuangalia mbali leo kuona wauaji wa kutisha gerezani ambao wamebadilishwa na kuwa Wakristo wenye furaha kwa njia ya nguvu ya Biblia.


107

Huhitaji kutizama mbali kuona ndoa zilizokuwa zikielekea moja kwa moja katika talaka,ambazo sasa zimeokolewa na kujazwa na upendo mpya kwa njia ya nguvu ya Biblia.
Hakuna awezaye kusoma Biblia kwa uaminifu, kila siku, bila ya Kitabu cha Mungu kumbadilisha.
Na kama utatumia wakati kila siku kusoma Biblia, rafiki yangu, itakubadilisha pia.


108

Yesu alitumia muda wake akibadilisha watu.
Hicho ndicho kiini cha dini ya Kikristo. Na hicho ndicho kiini pia cha Biblia, siri ya uwezo wake.



109

(Fungu: Yohana 8:32)
Yesu alijua ni nguvu gani inayobadili watu:
Tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru. Yohana 8:32.

# 5 - Siri za Magombo ya Kale



110

Ni kweli iwekayo watu huru-- inayobadili watu!
Ni kweli imfanyayo mlevi kuacha kunywa vileo na kuwa baba mwenye upendo.
Ni ukweli umwekao huru mtumiaji wa madawa ya kulevya.
Kukiwa na udanganyifu mwingi kiasi hiki duniani leo, tunahoji, Ukweli ni nini?



111

(Fungu: Yohana 17:17)
Yesu alitoa jibu:
(Iamini Biblia) Neno lako ndiyo kweli. Yohana 17:17.
Biblia, Neno la Mungu, ni kweli!
Nguvu ya Neno hilo yaweza badili mioyo ya wanaume na wanawake.


112

Lakini Neno la Mungu laweza kubadili wale tu waliotayari kubadilishwa--wale waliotayari kumkubali Mtu aliyetajwa humo Kitabuni, Yesu Kristo.
Na mamilioni ya watu wamebadilishwa kadiri walivyojifunza Biblia.
Hakuna nguvu inayozidi hii katika dunia igusayo mioyo na kubadilisha maisha.
Unaona rafiki, kile tufanyacho na Kitabu, huleta tofauti.
Ni zaidi ya kitabu cha kubeba kanisani au cha kurembesha kwenye kabati za nyumba zetu!
Ni zaidi ya taarifa isaidiayo ama ushauri wa maana
Ni Mungu anenaye na mioyo yetu.
Ni barua yake ya upendo kwa watoto wake katika Sayari Dunia.
Ndani yake kuna siri ya kuishi, siri ya furaha ya kudumu, na amani ya mawazo.

# 5 - Siri za Magombo ya Kale



113

(Video Sek 12) Hebu  niwape kisa juu ya uwezo wa neno la  Mungu wa kubadili maisha.
Miaka mingi iliyopita, kulikuwa na meli iliyoitwa Bounty.  Mwaka 1790, Nahodha Bligh na kikosi cha mabaharia wake waliondoka Uingereza ili kuleta shehena ya miche ya mifenesi ili kuipandikiza katika visiwa vya magharibi ili kuwa chakula rahisi kwa watumwa.



114

Kwa sababu ya uongozi wa kikatili wa Bligh na jinsi alivyowatendea vibaya mabaharia wake,  kulizuka uasi, na Fletcher Christian,kiongozi wa uasi, aliwatenga  Bligh pamoja na mabaharia 18 katika mtumbwi mdogo.
Walifaulu kupata njia ya kurudi hadi Uingereza kwa sababu pia ya uzoefu wa nahodha Bligh wa kusafiri majini.



115

Mabaharia waliosalia katika Bounty hawakuwa na wakati mzuri sana, bali waliishia katika kisiwa kisicho na wakaaji cha Pitcairn.



116

Waliichoma meli - Bounty, ili wasionekane.
Walipokuwa Tahiti, Bligh alikuwa amechukua wanawake kadhaa na watoto na wanaume wenyeji wachache.
Taabu iliwafika waasi hawa  walipokuwa wakijifunza kutengeneza pombe. Kulikuwa na mauaji na uhalifu na  kwa muda mfupi kulikuwa na mtu mmoja tu, John Adams, pamoja na wanawake na watoto.

# 5 - Siri za Magombo ya Kale



117

John Adams alitafuta hadi alipoona Biblia ya Bounty ambayo ilikuwa katika sanduku. Alianza kuisoma na kadiri alivyoendelea kuisoma badiliko kubwa lilimjia. Alitambua ya kwamba wajibu mkubwa ulikuwa umemjia ili kuwasaidia watoto hawa kuwa na maisha mazuri yajayo.
Alianza kuwaelimisha jinsi ya kusoma na kuandika na jinsi ya kuishi.
Mabadiliko ya kushangaza kati ya wakazi wote kisiwani uliweka mvuto kwa mashua zilizokuwa zikipita, kisha serikali ya Uingereza, na hatimaye dunia nzima.


118

Biblia yaweza kubadili maisha yako pia rafiki. Tusomapo Biblia, Roho Mtakatifu yule yule aliyevuvia waandishi wa Biblia kuandika neno la Mungu karne nyingi zilizopita, hubadili maisha yetu tunapojifunza.
Njoo kwa neno la Mungu ukiwa na mawazo yaliyofunguka katika imani isiyogawanyika kisha sema:
Ee Bwana, nionyeshe kweli yako, nami nitaifuata.
Ee Bwana, funua mabadiliko yoyote ninayohitaji kufanya katika maisha yangu.
Ee Bwana, natamani kukuona kama Mwokozi abadiliye maisha mwenye upendo, na mwenye kusamehe katika kurasa za neno lako.


119

Ndiyo, rafiki, si kitabu tu-ni mwandishi wa kitabu aletaye tofauti
Tunapopata picha ya yule mwandishi, imani yetu itakua.
Kwani kumjua ni kumpenda na kumuamini.

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI  HIKI?



1

Yawezekanaje Mungu wa upendo akayaruhusu?


2

Clara Anderson alikuwa  mjakazi  jijini San Francisco, na Clara alikuwa mwanamke muungwana sana - na pia mwaminifu sana.
Siku moja baada ya kuwa mtendakazi kwa muajiri mmoja kwa miaka 15, alitoweka.
Muajiri wake hakujua alipokwenda.  Alikuwa tu kama aliyetokomea toka machoni pa watu.
Kisha kwa namna ya ajabu, baada ya siku za kutafuta, idara ya jiji  ya ustawi wa jamii ikampata. Clara alikuwa katika mpango wa 'mgomo wa kula hadi kufa' katika kificho cha mlima nje ya San Fransisco. Akasema, Nataka kufa. Niacheni. Wakati mwandishi wa habari aliyemkuta alipomhoji, Clara alisema,
Tazama , hakuna anayenijali. Mimi ni kijakazi tu - mmoja tu kati ya maelfu  katika jamii watendao kazi za kinyonge. Maisha yangu hayana thamani. Sina ndugu wa karibu, sina jamaa, sina marafiki. Mimi ni mpweke kiasi kwamba sihitaji kuishi. Hakuna ninaye mdhani kuwa wa karibu nami - sina niwezaye kuzungumza naye, hayupo niwezaye kufungua moyo wangu kwake. Hivyo niacheni tu nife, kwa sababu hakuna kwa kweli anayejali.

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI  HIKI?


3

Hakuna anayejali! ndicho kilio cha wanaume na wanawake katika sayari iliyo pweke.
Hivi karibuni katika utafiti kuhusu Mungu, watu waliulizwa, Kama ungemuuliza Mungu swali moja, hilo swali lingelikuwa lipi?
Vipi wewe? Kama ungemuuliza Mungu swali moja, lingelikuwa lipi? Tazama jinsi ambavyo mamilioni wangeuliza:
Mungu , je, kweli unanijali? Kama wewe ni mwema hivyo, kwa nini kuna maradhi mengi kiasi hiki?
Mbona mahangaiko na mauti duniani?
Mbona kuna kuvunjika moyo hivi na huzuni?
Mbona kuna njaa, mafuriko, maafa yatokanayo na nguvu za asili, na vita?


4

Tuanatazama mazingira na tunatambua nguvu za kiovu zilizomo duniani.
Kila mahali kuna maafa ya kutisha yanayotokea kila siku.



5

(Video Sek. 15) Ni nani anayewajibika kwa sababu ya maafa, shida, na taabu  katika dunia?
Watu wengi humlaumu Mungu kwa matatizo wanayopitia.
Mara kwa mara utawasikia wakiuliza swali, Kwa nini Mungu alitenda hivi kwangu?



6

Hebu tutizame kile ambacho Biblia inasema juu ya pambano kuu linaloendelea kati ya nguvu za wema na zile za uovu.
Waweza kuuliza, Kama Mungu haleti shida zote hizi na huzuni duniani, ni nani anayewajibika kwa maafa yote haya tunayoyashuhudia?


7

Biblia  inasonda kundi  lenye makosa!
Yesu alieleza kisa juu ya mkulima alliyepanda mbegu  ndani ya shamba, lakini mimea ilipokua,

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI HIKI?


8

kulikuwa na magugu ndani ya shamba.



9

(Fungu: Mathayo 13:27)
Watumishi wa yule mwenye shamba wakamwendea, wakamwambia, "Mheshimiwa, bila shaka ulipanda mbegu nzuri katika shamba lako.



10

Sasa magugu yametoka wapi?"
Walitaka kujua, magugu yalitokea wapi.



11

(Fungu: Mathayo 13:37)
Yesu akawaambia, Mpanzi wa zile mbegu nzuri ni Mwana wa Mtu.




12

Lile shamba ni ulimwengu. Zile mbegu nzuri ni watu wale ambao ufalme wa mbinguni ni wao,lakini yale magugu ni wale watu wa yule mwovu.



13

Adui aliyepanda yale magugu ni ibilisi.
Mathayo 13:37-39
Mavuno ni mwisho wa nyakati na wavunaji ni malaika.



14

Unaona, wakati Mungu anapojaribu kuonyesha wema kwa kila mmoja, kuna nguvu nyingine itendayo kazi duniani iletayo maafa, misiba, mauti, na maradhi kwa maisha ya wana wa Mungu.

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI HIKI?



15

Kitabu cha mwisho cha Biblia, Ufunuo, kinatuambia jinsi mambo yalivyoanza ili tuwe na ukweli hakika juu y kile kilichotokea mbinguni na kusababisha taabu kubwa namna hii katika Sayari Dunia. Tutagundua chanzo cha uovu. Waweza kushangaa, lakini kulipata kuwa na vita mbinguni!



16

Kisha kukazuka vita mbinguni: Mikaeli na malaika wake walipigana na hilo joka, nalo likawashambulia pamoja na malaika wake.



17

na joka hilo halikuweza kuwashinda, na hatimaye hapakuwa na nafasi tena juu mbinguni kwa ajili yake na malaika wake.



18

Basi joka hilo kuu likatupwa nje. Joka hilo ndiye yule nyoka wa kale ambaye huitwa pia ibilisi au shetani. Ndiye anayeudanganya ulimwengu wote;



19

Naam, alitupwa duniani, na malaika wake pamoja naye.
Ufunuo 12:7-9.


20

Sasa, tazama jinsi huyu joka, au mwovu anavyotambulishwa katika Ufunuo 12:3,4:



21

Ishara nyingine ikatokea mbinguni: joka kubwa jekundu na lenye pembe kumi na vichwa saba;

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI HIKI?



22

na kila kichwa kilikuwa na taji.



23

Joka hilo liliburuta kwa mkia wake theluthi moja ya nyota za anga na kuzitupa duniani...


24

Ni wazi kwamba theluthi moja ya malaika wa mbinguni walimfuata mdanganyifu katika uasi wake dhidi ya Mungu.
Lakini hebu tuchunguze zaidi juu ya huyu malaika aliyeanguka aitwaye Lusifa.
Katika Agano la Kale anatajwa kama Mfalme wa Tiro, na yasema hivi juu yake:



25

(Fungu: Ezekieli 28:12 -14)
Bwana MUNGU asema hivi: Wewe wakitia muhuri kipimo, umejaa hekima, na ukamilifu wa uzuri.
Ezekieli 28:12




26

Ulikuwa ndani ya Adeni, bustani ya Mungu; kila jiwe la thamani lilikuwa kifuniko chako....
Ezekieli 28:13



27

Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye...ukawa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu;



28

umetembea huko na huko kati ya mawe ya moto.
Ezekieli 28:14

6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI HIKI?

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI  HIKI?


29

Lusifa alikuwa malaika mkamilifu, aliyeumbwa kwa ukamilifu kwa namna zote.
Alikuwa malaika aliyesimama mbele za Mungu kama kerubi afunikaye.


30

Lusifa alishikilia nafasi iliyotukuka huko mbinguni. Katika pande zote mbili za kiti cha rehema au cha enzi cha Mungu kulikuwa na malaika wawili-mmoja kulia na mmoja kushoto. Mmoja wa hawa alikuwa Lusifa.


31

Hakuridhika kwa kuwa karibu hivyo na Mungu.
ALITAKA KUWA MUNGU!
Kitu kilitokea kwa Lusifa katika uhusiano wake wa karibu na Mungu. Mungu alimwambia Lusifa,



32

(Fungu: Ezekieli 28:15)
Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata uovu ulipoonekana ndani yako.
Ezekieli 28:15




33

(Fungu: Ezekieli 28:17)
'Moyo wako uliinuka kwa sababu  ya uzuri wako; umeiharibu hekima yako kwa sababu ya mwangaza wako...;
Ezekieli 28:17.


34


Huyu malaika mzuri, aliyetukuka akajipenda nafsi. Alitamani utukufu na heshima iliyomstahili Mungu pekee. Akawa na uchu wa madaraka. Akawa na ujasiri wa kumpa changamoto Muumbaji hata katika swala la utawala wa ulimwengu! Sikiliza kwa makini:



35

(Fungu: Isaya 14:12-14)
Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni,  Ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa..........

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI  HIKI?




36

Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu.....



37

.......Nitafanana na Yeye Aliye juu.
Isaya 14:12-14


38

Maneno haya ya kiburi yalipoendelea kumiminika toka midomoni mwa Lusifa,  upendo ulio kamili na amani ya mbinguni vikavunjwa vunjwa katika mamilioni ya vipande vidogo vidogo vya uchoyo.


39

Haikuchukua muda hadi Lusifa alipoanza kusambaza roho ya kutoridhika kati ya malaika wengine.
Pole pole bali kwa uhakika, aliharibu upendo wa Mungu na haki yake.


40

Kama tunda lililooza kwenye tenga, uasi wake ulienea kwa malaika wengine mbinguni.
Pengine unashangaa kwa nini Mungu hakumuangamiza Shetani wakati ule.
Mungu angeweza kuwaangamiza Lusifa na malaika waliojiunga naye katika  uasi kwa muwako mmoja tu wa kupofusha, lakini kama angefanya hivyo, viumbe wote wangemtumikia kwa hofu.

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI HIKI?


41

Hebu tufikirie kama Mungu angeondoa uhuru wetu wa uchaguzi na kutufanya sote kuwa kama mashine.
Wangapi kati yenu wenye watoto?
Je, ungependa mtoto - mashine? Ungefurahiaje mtoto uliyemtia ufunguo ndiye atende kila utakacho?
Mtoto wako angeamka asubuhi na kukariri maneno:
Ndiyo ,Mama, Nitakula wali wangu.
Ndiyo, Baba, Nitasafisha nyumba.
Unayo mashine iliyo kama mtu--imetulia, chuma, mashine isiyo na akili.
Huna mtoto wewe.
Je, ungependa aina hii ya mtoto? Ni wazi la.
Vivyo hivyo Mungu.


42

Mungu ni Mungu wa upendo. Aweza tu kuwa na furaha katika mahusiano ya upendo na viumbe Vyake ambapo wanamwabudu kwa sababu wanampenda na kumuamini.


43

Shetani alikuwa ametoa changamoto kwa sheria za Mungu na haki yake, lakini Mungu hakuwa ameweka sheria hizi kwa mabavu ili aonyeshe ni nani aliye mkubwa! Aliziweka kulinda viumbe Wake, kuhakikisha amani yao na furaha.



44

Sheria zake ni kama taa na alama zionyeshazo mwendo kasi ulio salama vyote vikiwa vimepangwa kwa ajili ya usalama wetu na kwa ubora wetu.
Bali huyu aliyeheshimika kati ya malaika wote alidhani ya kwamba angeweza kuendesha ulimwengu kwa ubora kuliko Mungu Muumbaji wake!


45

Shetani, adui wa Mungu , alijifanyia 'mwovu' ndani yake!

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI  HIKI?



46

(Video: Sek. 10) Mungu anampa kila mtu uwezo wa kutii  ama kutotii.
Kutokana na haki na upendo, Mungu amemruhusu Shetani kueleleza kwa ulimwengu jinsi ambavyo angeuongoza ulimwengu.
Hatuelewi jinsi yote haya yalivyotokea wakati Mungu alikuwa mwema na mwenye upendo kwa wote.


47

Pambano lililoanza mbinguni halijaisha, limebadilisha tu viwanja!
Sasa Dunia ni eneo ambamo pambano kuu kati ya wema na uovu lingepiganwa, ambapo shetani angeeleleza aina yake ya serikali na jinsi ambavyo angeliiongoza dunia.



48

Lakini kwa nini Dunia? Kwa nini sayari yetu ikawa ....




49

(Fungu: 1 Wakorintho 4:9)
.... tumekuwa tamasha mbele ya ulimwengu wote, mbele ya malaika na watu.
1Wakorintho 4:9.


50

Dunia ilikuwa ndipo tu imetoka mikononi mwa Muumbaji,  ikiwa inang'aa  na ikiwa kamilifu, nzuri kuliko maelezo.
Ni wazi Shetani alifikiri vivyo pia, kwani aliiona dunia hii kama tunu ufaayo kuikamata.
Angejaribu kuikamata sayari hii ikiwa katika uzuri uwezao kuvunjika - dunia ambayo ndipo  imezaliwa.


51

Ingawa Adamu na Hawa, baba na mama wa wanadamu, waliumbwa wakamilifu, hawakufanywa wawe juu kuliko uwezekano wa kutenda makosa.
Walikuwa huru kuchagua kumpenda na kumfuata Mungu ama kutojali  maelekezo Yake.
Lakini utii wao ulipaswa kujaribiwa, na jaribu hilo lingewekwa kwenye mti. Mungu alionya,

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI  HIKI?



52

(Fungu: Mwanzo 2:16,17)
Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula;



53

walakini  matunda ya mti wa ujuzi wa mema  na mabaya usile,  kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika.
Mwanzo 2:16,17.
Hilo laonekana kuwa lilikuwa ombi la busara. Lazima walijihisi salama kabisa. Lakini mtu  yuko katika hatari kubwa akutwapo bila kujilinda kwa sababu hujihisi yu salama.


54

Hicho ndicho kilichotokea kwa Hawa.
Shetani alitumia uwezo wake upitao akili ya mwanadamu ili kumdanganya.
Shetani hutenda kazi hadharani kwa nadra. Yeye ni mdanganyifu sana.
Anatumia mifumo ya jamii, watu, au hata nyoka!


55

Kwa sababu hiyo Paulo anasema:



56

(Fungu: Waefeso 6:11-12)
 Vaeni silaha anazowapeni Mungu mpate kuzipinga mbinu mbaya za Ibilisi.



57

Maana vita vyenu si kati
yetu na binadamu, bali ni vita dhidi ya jeshi ovu  la ulimwengu wa roho; tunapigana na watawala, wakuu na wenye nguvu




58

wanaomiliki ulimwengu huu wa giza.
Waefeso 6:11,12.

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI HIKI?


59

Hawa alidanganywa.
Hakudhani maneno yaliyotoka kwa nyoka yalitoka kwa Shetani.
Mwovu, akinena kupitia kwa joka, alimwambia,



60

(Fungu: Mwanzo 3:1)
....Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani?
Mwanzo 3:1.



61

(Fungu: Mwanzo 3:2-4)
Hawa akajibu, Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula;



62

lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani



63

Mungu amesema, 'Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa.'



64

Nyoka akamwambia mwanamke, 'Hakika hamtakufa.'
Mwanzo 3:2-4


65

Hawa alipokuwa akimsikiliza joka, lazima lilipita wazo ghafla kichwani kwamba alikuwa akinena tofauti na na jinsi Mungu alivyowaambia.
Pengine kwa kuhisi ya kwamba alionekana kuchanganyikiwa, joka kwa upesi aliongeza,

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI HIKI?



66

(Fungu: Mwanzo 3:5)
Kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya.
Mwanzo 3:5


67

Mwovu alipendekeza ya kwamba Mungu hakufanya haki, kwamba alikuwa akizuia kitu fulani kizuri. Kuwa kama Mungu ilikuwa tamaa kubwa iliyomla Shetani na kuwa chanzo cha maanguko yake. Sasa Hawa pia aliliona kuwa wazo zuri pia; na kwa kwa haraka bila kufikiri, aliuzika.




68

(Fungu: Mwanzo 3:6)
Mwanamke alipoona kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho,




69

nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika matunda yake akala...
Mwanzo 3:6.


70

Akampa na mumewe, naye akala.


71

Adamu na Hawa wakashindwa jaribio la Mungu la upendo na utii, na haikuchukua muda mrefu kwa wao kugundua ya kwamba kuna jambo limeharibika.

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI HIKI?


72

Shetani alikuwa ameteka nyara dunia iliyozaliwa karibuni! Tangu wakati huo, akadai cheo cha , Mfalme wa Dunia hii.
Mtawala wa sayari iliyo katika uasi!
Adamu na Hawa walikuwa wameisikiliza sauti ya mwovu.


73

Kadiri siku hii ya msiba mkubwa ilipokuwa inafikia mwisho, Mungu akaja jioni wakati wa jua kupunga kama kawaida yake, akiwaita Adamu na Hawa. Hadi sasa, huu ulizoeleka kuwa wakati wa furaha mno wa siku - fursa ya kutembea na kuzungumza na Mungu moja kwa moja Yeye aliyewaumba. Lakini katika siku hii walikimbia na kujificha vichakani!



74

Hatimaye Adamu akachomoka pole pole kutoka nyuma ya vichaka katika bustani na kukiri kosa.



75

Muhtasari (Fungu: Mwanzo3:10)
....Nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi, nikajificha.
Mwanzo 3:10.


76

Muhtasari Adamu alikuwa hajapata kuogopa kabla ya hapo, lakini hicho ndicho dhambi inachofanya. Inamfanya mtu amuogope hata Mungu.



77

(Fungu: Mwanzo 3:11)
Mungu akajibu, ...Je! Umekula wewe matunda ya mti niliokuagiza usiyale?
Fungu 11.
Adamu akajibu:

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI  HIKI?




78

(Fungu: Mwanzo 3:12)
...Huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala.
Mwanzo 3:12
Saa chache kabla ya hapo, Adamu alikuwa tayari kufa pamoja na  Hawa.
Sasa alimlaumu na pia akamlaumu Mungu kwa kumuumba. Jinsi gani dhambi inavyovunjavunja upendo uliomkamilifu!


79

Lakini Hawa naye hakushindwa kushitaki. Mungu alipomuuliza juu ya kile alichokuwa ametenda, alijibu,




80

Muhtasari (Fungu: Mwanzo 3:13)
....Nyoka alinidanganya, nikala.
Mwanzo 3:13.
Hawa alimshutumu Mungu pia! Kwa maneno mengine, alikuwa anasema,  Ni nyoka uliyemuumba ndiye aliyeniingiza taabuni.


81

Siku ile ile Adamu na Hawa wakawa chini ya kifo! Ili kuwazuia Adamu na Hawa wasile matunda ya mti wa uzima, Mungu akawaondoa kutoka kwenye nyumba yao ya bustani.
Mwovu alisema ya kwamba wasingekufa, bali Biblia yasema,



82

Muhtasari (Fungu: Mwanzo 5:5)
Siku zote  za Adamu alizoishi ni miaka mia kenda na thelathini, naye akafa. Mwanzo 5:5
Wakiwa wamechelewa kabisa waligundua ya kwamba mwovu alikuwa



83

…... ni mwongo na baba wa huo.

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI  HIKI?





84

Ni rahisi kumlaumu Mungu kwa sababu ya huzuni za ulimwengu na uharibifu, lakini ukweli ni kwamba Shetani ndiye anayewajibika na kuleta maangamizi.



85

(Video Sek. 10) Yeye ndiye aliyeleta taabu kwa sayari hii na ndiye ambaye amekuwa akisababisha dhambi na  mateso tangu hapo. Yesu alimfichua mwovu na jinsi anvyotesa watu.


86

Alipokuwa akifundisha kwenye Sinagogi Sabato moja, Alimuona mwanamke aliyekuwa amejikunja kwa ulemavu  wa kudhoofisha.
Akiwa ameguswa na mazingira  yake ya kusikitisha, Yesu akamponya.


87

Watawala mara moja wakamshutumu kwa sababu uponyaji ulifanyika siku ya Sabato - Siku takatifu ya ibada ya Mungu. Lakini angalia jinsi alivyotetea matendo yake:



88

(Fungu: Luka 13:16)
 Na huyu mwanamke aliye wa uzao wa Ibrahimu, ambaye Shetani amemfunga miaka kumi na minane hii



89

haikupasa afunguliwe kifungo hiki siku ya Sabato? Luka 13:16


90

Yesu alisema kuwa Shetani alikuwa amemfunga huyu mwanamke kwa miaka 18.
Shetani ndiye aliyekuwa na hatia! Kwa kweli, Shetani ndiye nguvu mbaya  iliyo nyuma ya  maradhi yote na mateso, huzuni kubwa, na mauti!

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI  HIKI?



91

Pengine hakuna mahali katika Biblia tuwezapo kuona mkakati wa  Shetani kwa wazi zaidi kuliko ulivyo fichuliwa katika sura ya kwanza ya kitabu cha Ayubu, katika mazungumzo kati ya mwovu na Mungu.



92

Ilikuwa wakati fulani baada ya kuanguka kwa Shetani  kwamba wana wa Mungu walikwenda kujihudhurisha  mbele za Bwana. Shetani naye akaenda kati yao.
Fikiria hili! Mkutano wa wana wa Mungu, na Shetani akaja bila kualikwa!



93

(Fungu: Ayubu 1:7)
BWANA akamwuliza Shetani, 'Umetoka wapi wewe?'
Ayubu 1:7
Kwa maneno mengine,ni nani aliyekualika? Una haki gani ya kuwa hapa? Ndipo Shetani akamjibu Bwana,



94

(Kwa nini Mateso) Natoka katika kuzunguka-zunguka duniani, na katika kutembea huku na huku humo.
Ayubu 1:7
Shetani alidai miliki juu ya Sayari Dunia. Alikuwa amenyakua nafasi ya Adamu!



95

Adamu anaitwa mwana wa Mungu  (Angalia Luka 3:38), kama tu wale wengine waliokuja siku ile  kwa ajili ya mkutano na Mungu.


96

Je, yawezekana ya kwamba walikuwa ni viongozi wa dunia zingine, kama jinsi ambavyo Adamu alikuwa awali kiongozi wa ulimwengu wetu?
Kwa vyovyote vile, dai la Shetani la kuwakilisha Dunia halikupita bila kupingwa. Bwana akamwuliza Shetani;

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI HIKI?



97

(Fungu: Ayubu 1:8,9,11)
..... 'Je! umemwangalia huyo mtumishi wangu Ayubu? kwa kuwa hapana mmoja aliye kama yeye duniani,




98

mtu mkamilifu na uwelekevu, mwenye kumcha Mungu na kuepukana na uovu?'



99

Ndipo Shetani akamjibu BWANA, na kusema, Je!, huyo Ayubu yuamcha BWANA bure?




100

Lakini nyosha mkono wako sasa, uyaguse hayo yote aliyo nayo, naye atakukufuru mbele za uso wako!'


101

Ni changamoto kubwa kiasi gani! Siku hiyo Shetani alidai ya kwamba sababu pekee ambayo kwayo Ayubu alimtii Mungu ilikuwa ni kwa sababu ya yale ambayo Mungu alimtendea, na si kwa sababu alimpenda na kumtumaini Mungu.



102

(Fungu: Ayubu 1:12)
BWANA akamwambia Shetani,' Tazama, yote aliyo nayo yamo katika uwezo wako; lakini usinyoshe mkono wako juu yake mwenyewe.'



103

Basi Shetani akatoka mbele za uso wa BWANA. Ayubu 1:12.
Shetani aliondoka, akiwa na shauku ya kutia mikono yake katika mali ya Ayubu.


104

Mara mapigo yakaanza kuanguka:
Kwanza: Waseba wakaiba ng'ombe wa Ayubu na kuwaua wafanyakazi wake.

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI  HIKI?


105

Pili: Radi ikapiga, na kua kondoo wake na wachungaji wake.


106

Tatu: Wakaldayo walikuja na kuteka nyara ngamia wa Ayubu.


107

Nne (habari ya kuvunja moyo mno): kimbunga kiliipiga nyumba ya kijana mkubwa wa Ayubu. Karamu ilikuwa ikiendelea, na watoto wote kumi wa Ayubu waliokuwemo wakauawa!


108

Maskini Ayubu! alidhani kwamba Bwana alikuwa amechukua mali yake na kusababisha msiba wote huo. Hakuelewa ya kwamba mwovu ndiye alikuwa ametenda hiyo! Hata ingawa alizidiwa na huzuni, uaminifu wa Ayubu kwa Mungu haukubadilika.




109

(Fungu: Ayubu 1:21)
Akasema, ....BWANA alitoa, na BWANA  ametwaa; jina la BWANA  na libarikiwe.
Ayubu 1:21
Ingawa hakuelewa misiba iliyoangamiza mali zake na watoto, Ayubu alidumu tu kutumaini wema wa Mungu.
Lakini Shetani alikuwa hajamaliza.
Akampa Mungu changamoto tena akisema,



110


(Fungu: Ayubu 2:4-6)
...Naam, yote aliyo nayo mtu atayatoa kwa ajili ya uhai wake.



111

Lakini sasa nyosha mkono wako,uuguse mfupa wake na nyama yake,naye atakufuru  mbele za uso wako.

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI  HIKI?



112

BWANA akamwambia Shetani, Tazama, yeye yumo mkononi mwako; lakini tunza tu uhai wake.
Ayubu 2:4-6



113

Jaribu lilikuwa tayari limeanza! Je, Ayubu angesalia kuwa  mwaminifu kwa Mungu wakati makali yatakapozidi kuwa makali, ama atamwacha Mungu?




114

(Fungu: Ayubu 2:7)
Basi Shetani akatoka mbele za uso wa BWANA,



115

akampiga Ayubu na majipu mabaya tangu wayo wa mguu hata utosi wa kichwa.
Ayubu 2:7


116

Kama umewahi kupata na jipu, unajua jinsi ambavyo jipu moja tu linavyoweza kuuma.Fikiria sasa kitendo cha kufunikwa na majipu toka utosini hadi wayo wa mguu!



117

Hata ingawaje  Shetani alikuwa amempokonya Ayubu mali yake, watoto wake, na afya yake, Ayubu alisalia mwaminifu kwa Mungu. Mtu wa namna gani huyu! Biblia inasema,



118

Katika mambo hayo yote  Ayubu hakufanya dhambi, wala hakumwazia Mungu kwa upumbavu.
Ayubu 1:22



119


Ni nani aliyemuumiza Ayubu?
Ni nani aliyemletea mapigo Ayubu?
SHETANI!

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI HIKI?



120

Ni nani aliyeiba mifugo yake na kuua watumishi wake?
SHETANI!




121

Ni nani aliyeleta kimbunga kilichoteketeza wana na binti zake?
SHETANI!



122

Bwana anaweza kuruhusu matatizo yaje ili kujaribu utii na upendo wetu,



123


bali SHETANI ndiye mwenye hatia kwa ajili ya uovu wote uliopo kwenye Sayari Dunia!


124

Wewe nami tumekutwa katikati ya pambano linalokanganya la ulimwengu, ugomvi kati ya mamlaka na uasi, kati ya Muumbaji na Shetani, muasi wa kwanza.
Sisi si watazamaji. Tunahusika, tupende tusipende.



125

Dhana kwamba Shetani ni hadithi tu ama mvuto fulani tu, hutuacha tukiwa hatukujiandaa kabisa kukabiliana na kiumbe mwenye akili kama alivyo.



126

Kitabu cha Ufunuo kinasema:



127

(Fungu: Ufunuo 12:12)
Kwa hiyo shangilieni, enyi mbingu, nanyi mkaao humo. Ole wa nchi na bahari!

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI  HIKI?



128

Kwa maana yule Ibilisi ameshuka kwenu mwenye ghadhabu nyingi, akijua ya kuwa ana wakati mchache tu.
Ufunuo 12:12

Kwa sababu hiyo, furahini enyi mbingu na vyote vilivyomo ndani yenu. Lakini, ole wenu nchi na bahari, maana Ibilisi amewajieni akiwa na ghadhabu kuu, kwa sababu anajua kwamba siku zake zilizobakia ni chache.
Petro aliandika onyo hili:



129

(Fungu: 1 Petro 5:8)
Muwe na kiasi na kukesha kwa adui, Ibilisi, kuwa mshitaki wenu  kama simba angurumaye huzungukazunguka akitafuta mtu ammeze.



130

akitafuta mtu ammeze.
1 Petro 5:8


131

Lakini hata ingawa Shetani hutenda ubaya zaidi, Mungu wa uumbaji anao mpango wa kuumba upya ambao umjumuisha  Mwana wake Yesu- Mwana wake wa thamani  aliyekuwa hiari kufa  ili kulipa deni letu ili tuwe na uzima wa milele.


132

Biblia inasema Shetani huja kama simba angurumaye.


133

Shetani alitenda kazi kupitia kwa Mfalme Herode ili kumuangamiza mtoto Kristo (Akashindwa).

6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI  HIKI?

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI HIKI?



134

(Video: Sek. 10) Shetani alikuja kwa Yesu jangwani, akijifanya kuwa malaika kutoka mbinguni akiwa na majaribu makuu matatu (Akashindwa).


135


Shetani alichochea halaiki ya watu ili wamwangamize Yesu pale Kalvari (Alikuwa adui aliyeshindwa milele).


136

Ingawa kulikuwa na Kalvari, kulikuwa pia na ufufuo! Mungu Asifiwe!
Hivyo ndivyo ilivyokuwa ya kwamba Mungu alimtoa Mwanae; na Mwana akajitoa mwenyewe, ili kubatilisha hatima yako na yangu.
Ilikuwa ni saa ya ushindi, siku ya kutamka uhuru kwa ajili ya wafungwa wote wa mwovu katika Sayari Dunia.



137

Siku hiyo Shetani akawa adui aliyeshindwa! Kristo kwa mauti yake akapata haki ya kuangamiza uovu wote na mateso.
Paulo aliandika katika Waebrania 2:14:



138

(Fungu: Waebrania 2:14)
Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo



139

ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi.

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI  HIKI?




140

Shetani alidhihihirisha mbele ya wenye ufahamu wote wa ulimwengu  kuwa yeye ni kiumbe wa jinsi gani.
Na bado anaendelea kudhihirisha jinsi ambavyo angeuendesha ulimwengu.
Vimbunga, matetemeko, mafuriko, uhalifu, maradhi, huzuni, na maumivu!
Haya tunayaona




141

Lakini nguvu isimamayo nyuma ya yote haya bila kuonekana kwa macho ni ile  kazi ya Shetani ipitayo akili ya mwanadamu.




142

Haya maafa siyo matendo ya Mungu-  haya ni matendo ya mwovu.



143

Waweza kuwa unashangaa juu ya masikitiko, huzuni, na matatizo katika maisha yako binafsi.
Waweza kuwa unashangaa juu ya kifo cha mtoto ama  mpendwa na kuuliza  Yu wapi Mungu?




144

Biblia inafundisha ya kuwa Mungu yupo.
Yupo katikati ya huzuni zako masikitiko,  na matatizo.
Na atakuja muda si kitambo  kushughulikia tatizo la dhambi na mateso.



145

Habari njema  ni kwamba sayari hii nzuri, iliyotekwa na Shetani, i karibu kuokolewa.
Ufahamu huu wapaswa kunyamazisha hofu za abiria wenye shauku,  juu ya sayari  iliyokwenda kombo!
Mungu anao mpango wa kumwangamiza Shetani-- mwovu mdanganyifu-- na tutajifunza kwa hakika jinsi  huo mpango ulivyo katika mikutano yetu ijayo.
Hebu tuone kile ambacho Biblia inasema juu ya Shetani:

6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI  HIKI?

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI HIKI?



146

(Fungu: Ezekieli 28:16,18)
.....Nami nimekuangamiza, Ewe kerubi ufunikaye.......



147

Basi nimetokeza moto kutoka ndani yako;



148

nao umekuteketeza, nami nimekufanya kuwa majivu juu ya nchi...
Ezekieli 28:18
Dhambi na taabu vitapotea milele.


149

Ndiyo, rafiki, Yesu anakuja upesi! Siyo kama mtu wa chini wa Galilaya, siyo kama aliyetukanwa, aliyetemewa mate, na aliyekataliwa. Siyo kama mtu anayening'inia msalabani,


150


bali kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana akiwa na haki ya kutawala! Lazima tuwe tayari kukutana naye maana kama tukikosa hilo, tumekosa kila kitu!



151

Utii wako uko wapi? (Video Sek. 12) Swala leo ni, Ni nani tutakayemwamini? Ni nani tutakayemfuata? Mungu mwenye upendo -au malaika aliyeanguka? Mistari inachorwa;
Ulimwengu nzima unagawanywa katika sehemu mbili.

Uko upande wa nani?


152

Kwa kila moyo usiotulia, moyo mpweke, kwa kila roho inayoumia, yenye hatia, kwa watoto wake wote katika sayari dunia iliyo katika uasi, Yesu anatoa mwaliko wa upendo:

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI  HIKI?



153

(Fungu: Mathayo 11:28)
Njoni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.



154

(Fungu: Yohana 6:37)
Wote anipao Baba watakuja kwangu;  ye yote ajaye kwangu, sitamtupa nje kamwe
Yohana 6:37
Je, hii si habari ya ajabu?

# 6 - KWA NINI MAHANGAIKO MAKUBWA KIASI HIKI?


155

Katikati ya misiba ya maisha, simanzi, huzuni na kukata tamaa, Yesu yuko hapo.
Anaelewa simanzi uliyo nayo sasa hivi.
Yesu anaelewa unachokipitia mwili wako unaporaruliwa na ugonjwa.
Anajua maumivu.
Aliyapitia wakati watu wakatili walipopigilia misumari yenye kukwaruza katika mikono Yake.
Anajua upweke.
Aliupitia wakati aliponing'inia peke yake katika giza msalabani.
Anajua umaskini.
Aliupitia alipotembea katika barabara zenye vumbi za Palestina akiwa na chakula kidogo tu huku akiwa hana mahali pa kupaita nyumbani.
Njoo kwake leo.
Atakupatia tumaini jipya na moyo mkuu.
Hapa kuna habari nzuri kuliko zote.
Siku moja hivi karibuni Yesu huyu atakuja tena na kukomesha taabu zote za maisha.
Atakuja tena kuanzisha ulimwengu mpya.
Dhambi na wadhambi wataangamizwa.
Hatimaye Shetani, atashindwa kwa ujumla kabisa.
Yesu anatamani kukurejesha wewe kwa familia ya Mungu, kukupatia wewe uzima wa milele kwenye sayari iliyofanywa mpya.
Lakini uamuzi lazima ufanyike--Ni nani atakayekuwa Mkuu na Bwanawako ?
Rafiki, uamuzi huu ni swala la kufa na kupona!
Je, hutachagua sasa hivi kumruhusu Kristo awe Mfalme wako?
Anasubiri. Mikono yake imefunguliwa wazi.
Anasema, Njoo! Njoo! Njoo!
Je, waweza kuinamisha kichwa chako tunaposali na kusema, Naam, Yesu, ninakuja?

# 7 - Uhai wa Mtu  Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.



1

Anaweza Kubadilisha Maisha Yako, Pia.


2

Watu wawili walikuwa wanasafiri maili mamia toka upande mmoja hadi wa pili wa Marekani kwa treni. Kwa vile safri yao ilikuwa ndefu sana kiasi hicho, walipitisha muda kwa kuzungumzia kila kitu kilichokuja katika mawazo yao.
Wakazungumzia hali ya hewa.
Wakazungumzia  siasa.
Wakazungumzia maisha yao ya awali utotoni, familia zao na ndoa zao.
Maongezi yao hatimaye yakageukia dini.
Mtu mmoja alikuwa asiyemwamini Mungu. Mwingine alikuwa Mkristo.
Mtu mmoja hakuamini juu ya Mungu kabisa.
Mwingine alikuwa na imani thabiti sana kwa Mungu.
Mtu mmoja hakupata kusoma Biblia kamwe.
Mwingine aliisoma kila  mara.

# 7 - Uhai wa Mtu Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.



3

Somo la mjadala wao mchana ule wa wakati wa hari lilikuwa Yesu Kristo.
Mwenye kumkana Mungu alimuuliza rafiki yake Mkristo maswali muhimu na ya nguvu. Maswali kama:
Kwa nini wewe ni Mkristo? Je, hii siyo tu ajali ya kijiografia?
Ilitokea tu ukazaliwa katika nchi ya Kikristo, sawa?
Yesu ana tofauti gani na mtu yeyote mwingine mkuu?
Je, Yesu ni zaidi ya mwalimu wa maadili ama mwanafalsafa mnyofu?
Je, unawezaje kuwa na hakika kuwa Yesu yu yote yale aliyodai kuwa?
Wawezaje kuwa na hakika ya kwamba Yesu ni Mungu na kwamba toleo lake la uzima wa milele ni halisi?
Maswali ya yule mtu asiye mwamini Mungu mchana ule wenye wa wakati wa hari kwenye treni ni mazuri.
Rafiki yake, Mkristo, akashiriki baadhi ya majibu pamoja naye.
Hakuna swali katika mawazo yangu kwamba yapo majibu ya msingi kabisa kwa maswali haya na kuelewa haya majibu humaanisha uzima wa milele.




4

Ulimwengu wetu kwa hakika umekuwa na sehemu yake ya watu mashuhuri. Watu ambao wametoa mchango wao kufanya kufanya ulimwengu mahali bora zaidi.



5

Wafalme, maraisi, viongozi wa kidini, na wa kijeshi, wanasayansi na wasanii wameacha alama zao katika ulimwengu.
Wanayo majina mashuhuri ulimwenguni kote.

# 7 - Uhai wa Mtu  Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.


6

Jina moja linasimama juu ya mengine yote.
Hata historia imegawanywa katika miaka kabla na baada ya kuzaliwa kwake.
Jina lake ni Yesu.
Yesu ni jina mashuhuri kuliko yote katika historia.
Lakini ni jambo moja kuwa umesikia jina lake, na jingine kujua ya kwamba yeye ni nani hasa.


7

Wakati Yesu alipokutana na wanafunzi wawili njiani kwenda Emau siku ya Jumapili ya ufufuo,
Wawili miongoni mwa wanafunzi walikuwa wanastajabia.
Usiku huu ningependa kukutambulisha zaidi sana kwa Yesu wa historia.
Yesu wa Biblia. Hebu tuanzie mwanzo.  Yawezekana unashangaa-Huyu Yesu ni nani? Je yukoje tofauti?
Je, alikuwa tu mtu mwema, mwalimu wa maadili au mwanafalsafa wa maadili?
Wawili miongoni mwa wanafunzi walikuwa wanastaajabia mambo haya pia.


8

Wakati Yesu alipokutana na wanafunzi wawili njiani kwenda Emau siku ya Jumapili ya ufufuo,


9

Aliwaonyesha unabii ambao ulikuwa umetimizwa siku chache tu zilizopita.



10

(Fungu: Luka 24:25,27)
 Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyoyasema manabii!.........



11

Akaanza kutoka Musa na manabii wote,

7 - Uhai wa Mtu  Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.

# 7 - Uhai wa Mtu Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.



12

akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.
Luka 24:25,27



13

Hebu tutazame vithibitisho vinavyohakikisha ya kwamba Yesu ni Masihi.



14

MUUJIZA WA KUZALIWA KWAKE
Muda mrefu kabla ya Yesu kuzaliwa kupitia kwa Mariamu, Isaya alitabiri:



15

(Fungu: Isaya 7:14)
Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara:



16

Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanueli.
Isaya 7:14



17

(Video: Sek. 5) Yesu anayo majina mengi, Imanueli, Yesu, Mwokozi, Kristo, na Masihi. Unabii wa Isaya kuhusu Yesu kuzaliwa toka kwa bikira ulikuwa umeandikwa zaidi ya miaka 600 kabla hajazaliwa. Malaika alinukuu unabii huu huu kama kithibitisho kwamba Yesu ni Masihi.
Hebu tutazame jinsi malaika alivyoeleza kuzaliwa kwa Yesu toka kwa bikira Mariamu.

# 7 - Uhai wa Mtu  Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.



18

(Fungu: Mathayo 1:18)
 Basi, hivi ndivyo Yesu Kristo alivyozaliwa: Maria, mama yake, alikuwa ameposwa na Yosefu. Lakini kabla hawajakaa pamoja kama mume na mke, alionekana kuwa mja mzito kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.



19

lakini kabla hawajakaa  pamoja kama mume na mke, alionekana kuwa mja mzito kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.
Mathayo 1:18



20

MAHALI PA KUZALIWA



21

(Fungu: Mika 5:2)
....Bethlehemu,...kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli...
Mika 5:2
Ni jambo lisilo la kwaida ya kwamba Yesu alizaliwa Bethlehemu, mji ule ule ambao unabii ulitabiri miaka 700 kabla.



22

(Fungu: Mathayo 2:1)
 ..Yesu alizaliwa mjini Bethlehemu, mkoani Yudea,....... Mathayo 2:1.
Agano Jipya linahakiki utimilifu wa unabii wa Mika.
Yesu alikuwa zaidi ya mtu mzuri, zaidi ya mwalimu wa maadili, na zaidi ya mwanafalsafa mnyofu.
Alikuwa mtakatifu Mwana wa Mungu.
Alizaliwa na bikira kama nabii Isaya alivyotabiri.
Alizaliwa Bethlehemu kama nabii Mika alivyotabiri.

7 - Uhai wa Mtu  Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.

# 7 - Uhai wa Mtu Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.


23

Unabii wa Biblia unafunua wazi mambo muhimu ya ndani ya maisha ya Kristo miaka mamia kabla hayajatokea. Unabii huu ulitimia kikamilifu. Wakati Adamu na Hawa walipotenda dhambi, Mungu alikuwa na mpango. Upendo wake ulimsababisha Yesu - Mwanae - kuja duniani, aishi maisha makamilifu na kufa kwa sababu ya dhambi zetu. Alichukua nafasi yetu ili tupate uzima wa milele kama tungekubali Mpango wake wa kuwa Mwokozi wetu.
Huu unaitwa MPANGO WA WOKOVU.


24

Karibu miaka 2000 iliyopita wenye hekima (mamajusi) kutoka Mashariki walijifunza maandiko. Walisoma juu ya mfalme mkuu aliyekuwa atokee na walijua ulikuwa wakati wake wa kuwasili.


25

Walijua ulikuwa wakati na nyota ilikuwa ni ishara ya Mfalme mpya aliyekuwa azaliwe.
Ndani ya Bethlehemu walimkuta na wakainama na kumwabudu Yesu.



26

(Fungu: Luka 2:7)
[Mariamu] akajifungua mtoto wake wa kwanza wa kiume, akamvika nguo za kitoto,



27

na kumlaza katika hori, kwa sababu hapakuwa na nafasi kwa ajili yao katika nyumba ya wageni. Luka 2:7


28

Hapakuwa na nafasi kwenye nyumba ya wageni, hivyo Yesu alilazwa kwenye chombo cha kuwekea chakula cha ng'ombe. Alizaliwa mhitaji.

# 7 - Uhai wa Mtu  Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.


29

Mama yake alikuwa mwema sana, na pia kijana wakati malaika alipomwambia alikuwa amzae Mwana wa Mungu.



30

Ingawa Alikuwa  Mwana wa Mungu, Alikuwa Mungu kama alivyo Baba yake.
Mtume Paulo anasema alikuwa sawa na Mungu na akachukua umbo la mtumwa akafanana na mwanadamu.



31

(Fungu: Wafilipi 2:6)
...Alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho,



32

bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa,



33

akawa na mfano wa mwanadamu.
Wafilipi 2:6,7


34

Yesu alikuwa kama sisi na kuishi hapa duniani. Lakini alikuwa mtakatifu, msafi, na bila mawaa, ili ayatoe maisha yake ili tuupate uzima wa milele. Katika masaa 24 ya mwisho ya maisha ya Kristo, kila kipengele cha sehemu nyingi za unabii uliotajwa karne za zamani kilitimia.



35

Chukua mfano wa KUSALITIWA na Yuda.

# 7 - Uhai wa Mtu Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.



36

(Fungu: Zaburi 41: 9)
Msiri wangu tena niliyemtumaini,Aliyekula chakula changu, Ameniinulia kisogo chake.
Petro alimuuliza Yesu kwamba ni nani aliyekuwa amsaliti, Yesu akajibu,



37

Yesu akajibu, Yule nitakayempa kipande cha mkate nilichochovya katika sahani, ndiye. Basi, akatwaa kipande cha mkate, akakichovya katika sahani, akampa Yuda, mwana wa Simoni Iskarioti.



38

UJIRA ALIOLIPWA MSALITI




39

....Basi wakanipimia vipande thelathini vya fedha. Zekaria 11:12



40

(Fungu: Mathayo 26:14,15)
Kisha, Yuda Iskarioti, mmoja wa wale kumi na wawili, akaenda kwa makuhani wakuu,



41

akawaambia, 'Mtanipa kitu gani kama nikimkabidhi Yesu kwenu? ' Wakamhesabia sarafu thelathini za fedha.



42

KUPIGWA KWAKE NA KUDHALILISHWA



43

(Fungu: Isaya 50:6)
Naliwatolea wapigao mgongo wangu, na wang'oao ndevu mashavu yangu;

# 7 - Uhai wa Mtu  Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.






44

sikuficha uso wangu usipate fedheha na kutemewa mate.
Isaya 50:6




45

(Fungu: Mathayo 26:67)
Kisha wakamtemea mate usoni, wakampiga.
Wengine wakiwa wanampiga makofi,
Mathayo 26:67




46

WALIICHOMA MIKONO YAKE NA MIGUU YAKE




47

(Fungu: Zaburi 22:16)
.... Wamenizua (wamenichoma)mikono na miguu.
Zaburi 22:16
Baada ya ufufuo wa Kristo, Tomaso (au Toma), mmoja wa wanafunzi Wake aliyekuwa na mashaka kwamba Alikuwa Amefufuka, alishuhudia mwenyewe ya kwamba mikono ya Kristo na miguu yake kweli ilikuwa imechomwa. Alisema,




48

(Fungu: Yohana 20:25)
....Nisipoona mikononi mwake alama za misumari, na kutia kidole changu katika kovu hizo,




49

......Sitasadiki.
Yohana 20:25




50

ALIHESABIWA PAMOJA NA WAKOSAO
Tazama jinsi huu unabii wa Kristo ulivyotimizwa moja kwa moja:

# 7 - Uhai wa Mtu Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.



51

(Fungu: Isaya 53:12)
....alihesabiwa pamoja na hao wakosao.
Isaya 53:12



52

Pamoja naye waliwasulubisha wanyang'anyi wawili, mmoja upande wake wa kulia na mwingine upande wake wa kushoto.




53

Hapo yakatimia Maandiko Matakatifu yanayosema, 'Aliwekwa kundi moja na waovu.'
Marko 15:27,28



54

WALILIPIGIA KURA VAZI LAKE
Mfalme Daudi alinena juu ya kile ambacho kingetokea kwa vazi la Yesu miaka 1000 kabla ya Yesu kufa:



55

(Fungu: Zaburi 22:18)
Wanagawanya nguo zangu,
Na vazi langu wanalipigia kura.
Zaburi 22:18



56

(Fungu: Yohana 19: 23,24)
Askari.....walizichukua nguo zake, wakazigawa mafungu manne.......,



57

Kanzu hiyo ilikuwa imefumwa kwa kipande kimoja tu, bila mshono.



58

Wakashauriana:Tusiipasue, ila tuipigie kura, itakuwa ya nani.'
Yohana 19:23,24

# 7 - Uhai wa Mtu Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.



59

MANENO YAKE MSALABANI




60

(Fungu: Zaburi 22:1)
Mungu wangu, Mungu wangu, Mbona umeniacha? Zaburi 22:1. Linganisha fungu hili la Agano la Kale na Mathayo 27:46:



61

(Fungu: Mathayo 27:46)
Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha? Yesu alinena maneno haya kabla tu ya kifo chake saa ya tisa.



62

Unabii mwingi ulizidi kabisa uwezo wa kibinadamu wa Yesu kuutimiza.



63

Asingeweza kupanga mahali pa kuzaliwa Kwake



64

namna ya kuzaliwa,



65

Kusalitiwa Kwake,



66

ama matukio yaliyozingira kifo chake.

7 - Uhai wa Mtu Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.

# 7 - Uhai wa Mtu Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.


67

Yesu alikuwa kwa kweli kama alivyosema -- Masihi. Alipokuwa akining'inia katika ule msalaba wa kikatili, mwenye majeraha ya vipigo, misumari katika mikono na miguu Yake, pamoja na taji ya miiba, akikebehiwa na kukejeliwa,


68

Angeweza kuita malaika elfu kumi kuiangamiza dunia na kumuweka huru.
Asingeweza kujiokoa Yeye mwenyewe na sisi pia!


69

Je wakati fulani unashangaa kama yupo anayekujali kweli?
YESU ANAKUJALI!
Alilihakikisha zamani katika kilima nje ya Yerusalemu!
Upendo mkubwa kiasi gani!
Unavunja mioyo yetu yenye kiburi.
Angeita malaika elfu kumi, lakini Mungu,ashukuriwe hakuwaita!
Badala yake Alikufa kwa ajili yake na mimi!



70

Swali la muhimu kabisa ni hili, Yesu ni nani Kwako?


71

Yesu alikuja katika sayari yetu ili kuishi maisha makamilifu.
Alikuja ili pia afe mauti yaliyotustahili,
ili tuishi milele!
Biblia yasema kuhusu kafara Yake,



72

(Fungu: Isaya 53:3-7)
Alidharauliwa na kukataliwa na watu;
Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko......

# 7 - Uhai wa Mtu Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.





73

Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu,
Alichubuliwa kwa maovu yetu;....Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.



74

Sisi sote kama kondoo tumepotea.......



75

Alionewa ........wala hakufunua kinywa chake;
kama mwana - kondoo apelekwaye machinjoni.
Isaya 53:3-7


76

Hapa tunamuona Yesu akitajwa kama Mwana kondoo.
Anaitwa Mwana kondoo sehemu nyingine nyingi katika Biblia.



77


(Fungu: Ufunuo 13:8)

Ufunuo 13:8 inanena juu ya kitabu cha uzima cha Mwana - Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia.



78

(Fungu: Ufunuo 5:8,12)
..Wazee ishirini na wanne wakaanguka mbele za Mwana - kondoo.....



79

[wakisema] 'Astahili Mwana- Kondoo aliyechinjwa. '
Ufunuo 5:8,12
Yesu Mwana-Kondoo alituokoa sisi sote toka katika mauti ya milele na ametupatia uzima wa milele badala yake.

# 7 - Uhai wa Mtu Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.



80

(Fungu: Warumi 6:23)
Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti;



81

bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.
Warumi 6:23


82

Adamu na Hawa walitenda dhambi na wakatenganishwa na Mungu.
Ilimpasa Mungu kuwatoa toka katika nyumba yao ya bustanini na hawangeweza tena kula matunda ya Mti wa Uzima.
Uzima wao ungepungua pole pole hadi hatimaye wangelikufa.



83

(Fungu: Mwanzo 3:24)
Basi akamfukuza huyo mtu, akaweka makerubi, upande wa mashariki wa bustani ya Edeni,



84

na upanga wa moto uliogeuka huko na huko, kuilinda njia ya mti wa uzima.
Mwanzo 3:24


85

Mungu aliwaambia mpango Wake wa kuwaokoa.



86

(Fungu: Mwanzo3:15)
Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako[wafuasi wa Shetani] na uzao wake [wafuasi wa Kristo];

# 7 - Uhai wa Mtu Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.






87

huo [Yesu] utakuponda kichwa [cha Shetani], na wewe [Shetani] utamponda kisigino [cha Yesu]. Mwanzo 3:15



88

KUPONDA: kuna maana gani?



89

Neno la kiebrania litumikalo kama kuponda lina maanisha gandamiza au saga.
Kusaga kichwa cha mtu ni jambo zito zaidi kuliko kuponda kisigino cha mtu.
Kristo alikuwa awe ndiye mshindi juu ya Shetani.
Mungu alifanya jambo jingine kumkumbusha mtu juu ya mpango Wake wa kuwaponya.


90

Aliuanzisha mfumo wa kafara.
Walikuwa waonyeshe imani yao kwa Mwana-Kondoo wa Mungu (Yesu) ambaye siku moja angekufa ili kuwapatia uzima wa milele.


91

Biblia haituambii bayana wapi mfumo huu wa kafara ulipoanzia.
Adamu na Hawa walikuwa uchi na Mungu akawatengenezea mavazi toka kwa ngozi. Katika sura inayofuata mara, Kaini na Habili wanaleta kafara.



92

(Fungu: Mwanzo 4:4,5)
Habili naye akaleta wazao wa kwanza wa wanyama wake na sehemu zilizonona za wanyama,



93

BWANA akamtakabali Habili na sadaka yake. Mwanzo 4:4

# 7 - Uhai wa Mtu  Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.



94

..bali Kaini [Mungu] hakumtakabali, wala sadaka yake. Kaini akaghadhibika sana.
Mwanzo 4:5
Habili alimleta mwana-kondoo aliyemwakilisha Mwana-Kondoo wa Mungu,  bali Kaini alileta matunda ya nchi.
Kafara ya Kaini haikuonyesha imani katika Mwana - Kondoo wa Mungu aliyechinjwa.



95

(Fungu: Waebrania 9:22).
.....Pasipo kumwaga damu, hakuna ondoleo.
Waebrania 9:22


96

Wakati Mungu alipowaleta wana wa Israeli toka Misri, aliwafundisha mafundisho mengi kupitia kwa hekalu alilomtumia Musa kulijenga.
Hekalu, au  hema ya kukutania, ilikuwa ni nakala ya Hema halisi iliyoko mbinguni.


97

Moja ya sherehe hizi ilikuwa ni Pasaka.


98

Katika siku ya 14 ya mwezi wa kwanza, watu walikuwa wameelekezwa kumchinja mwana kondoo na kupaka damu ya mwana kondoo  katika miimo ya milango yao.
Ilikuwa ishara ya kwamba walikuwa wamefunikwa kwa damu ya Mwana-Kondoo.


99

Usiku ule malaika anayeangamiza alipita juu ya nyumba zilizokuwa zimewekwa damu na hakuumiza yeyote aliyekuwa ndani.

# 7 - Uhai wa Mtu Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.


100

Pasaka ilikuwa iwakumbushe ya kwamba damu ya Mwana - Kondoo pekee ndiyo iwezayo kutukomboa toka katika uharibifu.
Wanyama ambao walitolewa kafara wasingeweza kutakasa toka dhambini.
Bali imani ya watu katika kafara ya Mungu ingewaokoa toka dhambini.



101

(Fungu: Waebrania 9:26)
.....Yeye ametokea mara moja tu, kuondoa dhambi kwa kujitoa yeye mwenyewe dhabihu.
Waebrania 9:26




102

Maana damu ya fahali na mbuzi haiwezi kamwe kuondoa dhambi.
Waebrania 10:4


103

Yohana Mbatizaji alimtangaza Masihi na kuelekeza kwa Yesu na kusema,



104

(Fungu: Yohana 1:29)
Huyu ndiye Mwana-kondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya ulimwengu!


105

Mfumo wa kafara wa sherehe za kiyahudi ulilenga mbelekwa Masihi - Mwana-Kondoo wa Mungu. Damu liyomwagika ya kila mwana kondoo katika zama za Agano la Kale, ilikuwa kwa karne kadhaa ikiwakilisha damu ya Yesu iliyomwagwa kwa ajili yetu.

# 7 - Uhai wa Mtu Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.


106

Yesu ni Mwokozi wa Ulimwengu.
Yesu anaridhia.
Yesu anasamehe.
Yesu anatuokoa kutoka kwenye hatia.
Yesu anatufundisha jinsi ya kuishi.
Yesu ameishi maisha kielelezo kwetu.
Yesu anatia nguvu maisha yetu.
Yesu anatubadilisha tokea ndani.
Yesu anatupatia maisha mapya.


107

Wakati Bwana Ernest Shackleton alipofanya mojawapo ya majaribio yake ya kuvuka Bahari ya Antarctica mwaka 1914, meli yake, Endurance, ilijigonga kwenye mwamba wa barafu. Kundi la hawa mabaharia liliambaa ambaa kwa siku kadhaa hadi walipofika katika kisiwa kilichoitwa Kisiwa cha Tembo.
Shackleton aliwaongoza watu hawa kusimika kambi pale; mahali ambapo wangeweza pia kutunza riziki zao na kujaribu kuipita baridi iliyokuwa inakuja. Lakini aligundua mara ya kwamba hakuna ambaye angekuja kuwaokoa. Hakuna aliyejua mahali walipokuwa. Walikuwa wametengwa na dunia kwa sababu ya Bahari yenye dhoruba ya Antarctica iliyokuwa inaganda kwa baridi. Kulikuwa na tumaini moja tu la kuokolewa: Ilipasa mmoja avuke ile bahari ili apate msaada.
Shackleton alianza kutengeneza mtumbwi wenye futi ishirini uliokuwa uende mwendo wa Nyangumi kwa ajili ya safari. Toka kwa waliojitolea, alichagua watu sita. Walikuwa wavuke maili mia nane za Bahari yenye machafuko ili kufikia kituo cha Norway kinachoshughulikia nyangumi ambacho kipo kwenye kisiwa kilichokuwa kimeganda cha Georgia Kusini.

# 7 - Uhai wa Mtu Mmoja Ulibadilisha Ulimwengu.



108

Ilionekana kuwa kazi isiyowezekana katika kipindi chenye dhoruba kuliko vingine vyote katika mwaka.Lakini Shackleton aliondoka na watu wake. Kwa siku kadhaa walijikunja wakajifunika na hili turubali la muda, huku wakiwa wamelielekeza gubeti kuelekea kwenye mawimbi makali, wakiomba upepo usije pasulia mbali tanga lao.

Walivumilia baridi - iliyopenya hadi mifupani, mifuko ya kulalia iliyoganda kwa baridi, maji ya barafu yaliyotiririka katika migongo yao, njaa na kiu. Siku kumi na nne baada ya safari yao kuanza wakati wote walipokaribia kufa kwa sababu ya kuwa nje kwenye baridi na kiu, waliona magenge meusi ya Georgia ya Kusini!

Shackleton alikuwa amefanikiwa kupita; hivi karibuni meli ingekuwa njiani kwenda kuwaokoa watu wake waliosalia wakiwa wamekwama. Mungu alipotizama chini katika hatari yetu na kutuona tulivyotengwa katika kisiwa, tukizungukwa na bahari kubwa ya dhambi, Alijitumbukiza katika bahari hii iliyochafuka Yeye Mwenyewe. Alijitwika Mwenyewe uovu wa mwanadamu unao ua, wenye uzito wa barafu.



109

Hakuna mtu yeyote katika ulimwengu kama Yesu. Yeye peke yake ndiye awezaye kutuokoa. Ndiye pekee awezaye kuondoa hatia na kubadilisha maisha yetu. Ndiye pekee awezaye kutupatia uzima wa milele.

Je, waweza kuinua mkono wako sasa hivi na kusema, Ndiyo, Yesu, Ninakukubali leo kama Bwana na Mwokozi. Ndiyo ,Bwana, Ninaamini ulikufa kwa ajili yangu. Ndiyo Bwana, ninatoa maisha yangu kwako. Inua tu mkono wako ninapoomba kwa ajili yako.

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele




1

Siri ya Kutokufa




2

Nchi ilitikisika. Mtetemo wenye nguvu ulituma mawimbi yake katika jiji zima. Majengo ya ofisi yalibomoka na nyumba zilianguka. Vituo vya Afya, mashule na makanisa yote yaliharibiwa.
Tetemeko la ardhi mwezi wa Februari 2001 ndani ya El Salvador liliua karibu watu 3,000 papo hapo. Maelfu waliachwa bila makazi.
Waokoaji walitenda kazi bila kuchoka mchana na usiku wakitafuta watu waliokumbwa. Waliwapata wachache tu waliosalia hai.
Baada ya kuchimba kwa siku nne mfululizo, walikuwa wakijiandaa kukata tamaa katika msako wao wakati mmoja wao alipotambua nusu ya mkono uliotokeza kati ya kifusi. Ilishtua zaidi hasa wakati mkono uliposogea polepole.
Waokoaji wakachimba nguvu zaidi.
Iliwachukua karibia masaa manne kumtoa mwanamume huyu wa makamu hivi toka chini ya vifusi. Alikuwa hai. Alikuwa amedumu kwa siku nne bila chakula wala maji. Baadaye hospitalini, aliulizwa kwa jinsi gani aliweza kuishi katika hali ngumu ya ajabu kiasi hicho.
Jibu lake, Nilinuia kuishi. Nilikokota pumzi. Sikutaka kufa. Niliamini msaada ulikuwa njiani.



3

Tulizaliwa na shauku hii ya kuishi. Wewe na mimi tulikuwa nayo wakati tulipoingia hapa duniani. Kila mmoja ambaye amepata kuishi amepata kuwa nayo. Yawezekana ni tamaa kubwa kuliko zote tulizo nazo. Sisi wanadamu tumeunganishwa pamoja na tamaa ya uhai.

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele


4

Na wakati maisha ya mwanadamu yanapokuwa hatarini, watu hujaribu mambo ya ajabu, ya kishujaa ili kuokoa wengine.
Yaweza kuwa mtoto ambaye ametumbukia kisimani.
Au watu waliomo ndani ya meli iliyokwama baharini kwa matatizo.


5

Ama mkweaji wa mlima aliyekwama katika ukingo wa mwamba kando kando ya mlima.
Ama watu walionaswa katika vifusi vitokanavyo na tetemeko. Lakini maisha ya watu yakiwa hatarini watu hukimbia kuokoana.


6

Bado ukweli ambao hakuna mmoja wetu apendaye kuufikiria - lakini ni ukweli tu hata hivyo ni kwamba - maisha ya kila mmoja wetu yapo hatarini.
Siyo hatarini tu, pia.
Kila mmoja wetu amehukumiwa kifo.




7

(Fungu: Warumi 6:23)
Kwa maana mshahara wa dhambi ni kifo; lakini zawadi anayotoa Mungu ni uzima wa milele katika kuungana na Kristo Yesu, Bwana wetu.


8

Dhambi ni sumu - inaua.
Inatisha. Kwa nini? Kwa sababu inatutenganisha sisi na chanzo cha uzima wote - Mungu Mwenyewe, aliyetuumba.
Na kila mmoja wetu ametenda dhambi.



9

(Fungu: Warumi 3:23)
Watu wote wametenda dhambi na wametindikiwa utukufu wa Mungu.



10

(Fungu: Warumi 3:10 - 12)
....Hakuna mwenye haki hata mmoja.

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele



11

Hakuna afahamuye; Hakuna amtafutaye Mungu.



12

Wote wamepotoka.......Hakuna mtenda mema, la hata mmoja.
Warumi 3:10 -12.


13

Wazazi wetu wa awali, Adamu na Hawa,ambao kutokea kwao  jamii yote ya kibinadamu imekuwepo, walichagua kujitoa wenyewe toka kwa Mungu kwa kutomtii na kwenda njia yao wenyewe.



14

(Fungu: Warumi 5:12)
Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni,na kwa dhambi hiyo mauti;




15

na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi. Warumi 5:12


16

Matokeo ya asili ya dhambi ni mauti.
Asilimia ya watu wanaokufa kutokana na dhambi ni asilimia 100.
Adamu alikuwa afe kwa sababu ya dhambi.
Hivyo pia wote waliowazao wake  - kila mmoja wetu akiwemo.


17

Hivyo sisi sote tumo ndani ya shimo.
Tumenaswa na hatuna msaada.
Tumehukumiwa kufa isipokuwa kama mtu atatuokoa.
Habari mbaya ni kwamba tumo hukumuni isipokuwa kama  atakuwepo atakayetuokoa.
Habari njema ni kuwa Yupo ambaye ametuokoa!

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele



18

(Fungu: Waefeso 2:8,9)
Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu;



19

wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu. Waefeso 2:8,9.
Ndiyo, sote tumetenda dhambi.
Hakuna wasiwasi juu ya hilo!
Tunatenda dhambi kwa kila tendo la ubinafsi, neno, au hata wazo.



20

Fikiria jinsi ambavyo tumetenda dhambi mara nyingi kiasi kisichohesabika!
Na tatizo letu si tu dhambi ambazo tumezitenda-ni ukweli kwamba- sisi tu wadhambi!


21

Mtu mwenye tatizo la kufisha ambaye kwamwe hatambui tatizo lake au kutafuta msaada wa kiafya atakufa.
Na hiyo ndiyo hatima ya wadhambi wanaoshindwa kutambua hali yao ya kiroho na kutafuta msaada.



22

(Fungu: Isaya 59:2)
Maovu yenu [dhambi] yamewafarakanisha ninyi na Mungu wenu. Isaya 59:2.
Mungu ni chanzo cha uzima wote, na Adamu alipotenda dhambi alianza kufa.
Sisi sote tumo katika hukumu ya kifo.
Lakini Mungu wa Upendo hakutuambia tu matokeo ya dhambi bila kutupatia tumaini la wokovu!
Hii ndio habari njema!



23

(Fungu: Warumi 6:23)
Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu, Bwana wetu.

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele



24

Wokovu ni karama.
Hatuistahili.
Wala hatuwezi kuupata huo wokovu kwa matendo yetu mema, na pia hatuwezi kuununua kwa gharama yoyote.


25

Watu walio wengi wanaamini ya kwamba wanadamu wanapokea msamaha kwa kutenda matendo mema zaidi.
Watu wanaketi katika vitanda vya misumari, wakiamini ya kwamba kwa kutesa miili yao wanaweza kuipata neema ya Mungu.


26

Baadhi ya watu hujipiga na kujijeruhi miili yao kwa mijeledi na minyororo, wengine hujitesa kwa ndoano kali, na


27

wengine hutembea miguu mitupu katika makaa ya mawe ya moto wakitafuta upendeleo wa Uungu kwa vitendo visivyo vya kawaida vya kuudhalilisha mwili.


28

wengine huamini wanapata sifa zinazostahili maisha yajayo kwa kujenga mahekalu au kwa kuwalisha watu watakatifu,


29

na kwa wengine pia, hakuna furaha zaidi au njia iliyo bora zaidi ya kupata upendeleo wa Mungu zaidi ya kwenda kuhiji Mecca au kufa kwa kuutetea uislamu.


30

Wakristo wengi bila kujua wanatenda jambo lilo hilo. Wanahudhuria kanisani, wanatoa sadaka, na kufuata ile Sheria ya Dhahabu ya Biblia , wakidhani ya kwamba watapata upendeleo toka kwa Mungu na hivyo kuustahili uzima wa milele.
Lakini je, hilo lawezekana?

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele


31

Je, mtu , kwa njia ya adhabu ya kimwili ya namna fulani, mateso ya kiakili au tendo la wema, aweza kumhonga Mungu ili ampatie msamaha  na uzima wa milele?


32

Je, tunaupata wokovu kama matokeo ya kuufanyia kazi au kama  matokeo ya mtu ashindapo tuzo fulani au medali ya dhahabu ?



33

(Fungu: Waefeso 2:8,9)
Biblia Yasema,
Kwa Maana, mmeokolewa kwa neema kwa njia ya imani ambayo haitokani na nafsi zenu, bali ni kipawa cha Mungu.



34

wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu. Waefeso 2:8,9.


35

Hatuwezi kujiokoa sisi wenyewe kwa matendo yetu wenyewe - sharti tutegemee neema ya Mungu na upendo wake na wema wake, anaotupatia bure. Kama tungeweza kuufanyia kazi wokovu, basi usingekuwa karama (zawadi).


36

Fikiri  muajiri wako angekukabidhi bahasha huku akisema ana zawadi kwa ajili yako.


37

Kama ukigundua ni hundi ya mshahara wako  wa majuma mawili yaliyopita ya kazi (au nchi zingine - hundi ya mshahara wako wa mwezi), ndiyo iliyomo ndani, je, hiyo ingelikuwa zawadi?
SIVYO KAMA UMEFANYIA  KAZI!

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele


38

Lakini kwa nini Mungu mkuu atawalaye ulimwengu



39

anajihusisha hivyo na watu katika sayari iliyoko nje huko katika anga?
Kwa nini hakumuacha tu huyu mtu mbinafsi, muasi na kuacha ateseke na matokeo ya dhambi zake?



40

(Fungu: 1 Yohana 4:8)
Jibu linapatikana katika waraka wa kwanza wa Yohana:
Mungu ni upendo.


41

Baadhi yenu ni wazazi.


42

Baadhi yenu mnajua maana ya kuwa na mtoto mgonjwa halafu aanze kulia mchana na usiku. Unajaribu kila njia kufanya mambo yawe bora, lakini hakuna kinachoonekana kusaidia.
Unatembea katika sakafu/zulia, unamuimbia mtoto, na kujaribu kila aina ya ushauri unaoupata toka kwa marafiki,lakini hakuna kinachoonekana kufanya kazi. Lakini hebu nikuulize swali:
Hata kama umechoka kiasi gani, hata kama mtoto yu mgonjwa kiasi gani, je umepata hata mara moja kufikiria kumtoa mtoto kwa mtu mwingine au kumuacha ateseke peke yake?



43

La ? Kwanini? Kwa sababu unampenda huyu mtoto mdogo asiyejiweza zaidi kwa sababu ya maumivu na taabu ambayo ameipitia.
Hivyo ni kama jinsi Mungu alivyo!

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele


44

Watoto wake kwenye sayari dunia walipatwa na ugonjwa wa dhambi,


45

na maumivu na taabu  wanayoipitia kwa sababu ya huo ugonjwa vinamfanya Mungu awapende zaidi.



46

Kamwe Mungu hajafikiria kutuacha na kwenda zake! Kamwe Mungu hajafikiria kutuacha tuteseke na tufe tu kwa sababu ya matokeo ya uasi wetu.



47

(Fungu: 2 Petro 3:9)
Yeye (Bwana) ana saburi kwa ajili yenu, maana hapendi hata mmoja wenu apotee, bali huwavuta wote wapate kutubu.  2 Petro 3:9.


48

Bila kujali jinsi gani ulivyo mwema au mbaya, Mungu anakupenda na anataka kukuokoa.
Hapendi ufe.


49

Hata hivyo, sisi sote tumetenda dhambi.
Sisi sote tumeasi dhidi ya Mungu na kuvunja sheria yake.


50

serikali za kidunia haziwezi kuvumilia uvunjwaji wa sheria  na bado zikadumu kwa muda mrefu.

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele


51

Wavunja sheria huadhibiwa.
Lakini kuivunja sheria ya Mungu ni jambo lililo zito zaidi, kwa sababu dhambi hututenganisha na Mungu - Yeye ambaye peke yake aweza kutusaidia na kutuokoa!


52

Hata ingawa Mungu ni Mungu wa upendo wa milele, Yeye pia ni Mungu wa haki.
Katika Mlima wa Sinai alijieleza Mwenyewe:



53

(Fungu: Kutoka 34:6,7)
...BWANA, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli;



54

mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi; wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe.
Kutoka 34:6,7.


55

Je, hakuna utatuzi? Je, hakuna njia ya kutokea?
Ndiyo ipo njia ya kutokea!
Mungu mwenye upendo alipata njia ya kutuokoa na bado akawa mwenye haki.


56

Alipata aliye mkamilifu kuwa badala yetu kufa katika mahali petu,akilipa adhabu kwa ajili ya dhambi zetu ili tupate kuishi.
Yohana, mwanafunzi aliyependwa, anaeleza sababu:



57

Kwa Maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwana wake wa pekee,

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele




58

ili kila amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.
Yohana 3:16.


59

Yesu alikuja kuishi hapa duniani kama mwanadamu, akikabili matatizo na majaribu ambayo kila mwanadamu amepata kuyapitia.
Aliishi maisha ya utii ulio kamili.
Halafu, kama mwakilishi wa wanadamu asiye na dhambi, Kristo kwa kujitolea alijitwika hatia ya kila mtu ambaye angepata kuishi, na kufa kwa niaba yao.



60

(Fungu: Warumi 5:19)
Paulo aliandika, Kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja, watu wengi walifanywa wenye dhambi,



61

kadhalika kwa kutii kwa mtu mmoja wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki.
Warumi 5:19.


62

Mauti ya Yesu hayakuwapo ili kumridhisha Mungu mwenye hasira.
Yesu alijitolea kufa ili kutuokoa toka dhambini mwetu, na Mungu alitupenda sana kiasi cha kuwa tayari kumtoa Mwana wake wa pekee kwa ajili yetu.
Yesu alikuwa Mwana Kondoo wa Mungu, Mwana Kondoo wa kafara!

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele




63

Kama watu wa Mungu waliochaguliwa, Wana wa Israeli, walitanga jangwani karibu na Mlima Sinai baada ya kuokolewa toka Misri na Musa, huku wakishuhudia kila siku, kwa ishara na sherehe, kielelezo cha mpango wa Mungu wa kuokoa mwanadamu aliyeanguka. Hema la jangwani, lililojengwa kwa maelekezo halisi ya Mungu pamoja na huduma zilizoanzishwa na Mungu, vilidumu kumkumbusha mwanadamu Kalvari iliyokuwa ikija usoni - kileleni pa mlima ambapo Yesu angekufa, mahali ambapo Mwana-Kondoo wa kweli angetolewa kafara kwa ajili ya mwanadamu, akiwapatia wote tumaini na uhakika wa msamaha na wokovu.


64

Mdhambi alikuja, akileta mnyama wa kafara. Aliweka mkono wake juu ya kichwa cha mnyama na kukiri dhambi yake.
Kisha alichukua kisu akamuua, ikiwakilisha kwamba dhambi zake zilisababisha mauti ya Mwana-Kondoo wa kafara, aliyemwakilisha Yesu.



65

Haipendezi, ndiyo. Lakini msalaba wa Kalvari ulioleta ahadi ya uzima wa milele kwa moyo wa mwanadamu ulichukiza zaidi.
Hata hivyo, kwa tendo hili Mungu alieleleza ya kwamba dhambi huleta mauti, ama kwa mdhambi ama kwa kafara isiyo na hatia.


66

Watu wa Mungu nyakati za Biblia walitoa kafara kuonyesha imani yao kwa mauti iliyokuwa ikija ya Mwana wa Mungu, Yeye ambaye angekufa badala ya mwanadamu kama mwakilishi wake.

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele



67

(Fungu: Yohana 1:29)
Yesu alikuwa kafara ya kweli. Yesu alipokuja kubatizwa, Yohana alisema, ..…Tazama Mwana-kondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya ulimwengu! Yohana 1:29. Ni dhihaka  kubwa kiasi gani kwamba baadhi ya watu aliokuja kuwaokoa walipanga kumuua!
Yesu alipigwa, alikebehiwa, na kuhukumiwa kusulubishwa kwa njia iliyokuwa mbaya kuliko zote za kunyonga.



68

(Fungu: 1Petro2:22)
Hata hivyo kama Biblia isemavyo,
Yeye hakutenda dhambi, wala hila haikuonekana kinywani  mwake alikufa kwenye ule msalaba!
1 Petro 2:22.


69

Kristo alisulubishwa katika kipindi cha Pasaka. Ilikuwa ni desturi ya watawala wa Kirumi wakati huu kumuweka mmoja wa wahalifu huru kama kitendo cha kuonyesha itibari. Umati ukamchagua Baraba na kumuacha Yesu afe badala yake.


70

Katika mauti, Yesu aliwekwa sawa na wadhambi. Alisulubishwa kati ya wevi wawili!
Na Mungu alipoweka juu yake dhambi za dunia nzima,



71

(Fungu: Mathayo 27:46)
Alilia, ...Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?
Mathayo 27:46.
Alihisi utengano wa kutisha ambao dhambi huleta. Yesu hakuweza kuubeba uchungu wa kutengana na Baba.
Ulimvunja moyo wake.

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele



72

(Fungu: Marko 15:31)
Nao makuhani wakuu pamoja na walimu wa Sheria walimdhihaki wakisema, Aliwaokoa wengine, lakini kujiokoa mwenyewe hawezi!
Marko 15:31.


73

Na hiyo ilikuwa kweli!
Hangeweza kujiokoa Mwenyewe na bado aokoe wengine.
Alikuwa Mungu akilipa gharama ya jamii iliyopotea, sheria iliyovunjwa, mshahara wa dhambi.
Hivyo ndivyo Mungu alivyokuwa, akiwa na upendo ambao usingeweza  kuridhishwa hadi mtu aliporejeshwa kwenye familia Yake, alimtoa Mwana Wake wa pekee ili afe badala ya mwanadamu, kama Mwakilishi wake.



74

Yesu alitendewa  inavyotustahili ili sisi tutendewe anavyostahili.
Alihukumiwa kwa sababu ya dhambi zetu  na kufa mauti yetu ili tuupate uzima wa milele.
Kwa njia hii Mungu angetupa uzima wa milele na bado angekuwa mwenye haki.
Siyo kwa sababu ya chochote chema tulichokitenda, lakini kwa sababu Mungu aweza kutupatia heshima kwa sababu ya kile alichokitenda Kristo - kwa sababu ya maisha  yasiyo na dosari aliyoishi.



75

(Fungu: Waefeso 2:8)
Paulo, mtume kwa wamataifa, alisema,
Kwa maana mmeokolewa  kwa njia ya imani.
Waefeso 2:8.
Imani hii ni kiini cha wokovu.


76

Wakati askari magereza wa Filipi alipomuuliza Paulo afanye nini ili apate kuokolewa, Paulo alijibu,

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele



77

(Fungu: Matendo 16:31)
Mwamini Bwana Yesu nawe utaokolewa pamoja na jamaa yako yote.
Matendo 16:31.



78

Hata hivyo, kukubali tu katika mawazo yako ya kwamba Kristo aliishi duniani haitoshi. Hiyo si imani iokoayo.
Kuna zaidi kuliko hilo.



79

(Fungu: Yakobo 2:19)
Biblia yasema kwamba Mashetani nao waamini na kutetemeka. Yakobo 2:19.


80

Kumwamini Yesu ni zaidi ya kukubali ya kwamba alikufa zaidi ya miaka 1900 iliyopita.
Biblia yasema,




81

( Fungu: Mithali3: 5,6)
Mtumaini BWANA kwa moyo wako wote,
wala usizitegemee akili zako mwenyewe;




82

Katika njia zako zote mkiri yeye,
Naye atayanyosha mapito yako.
Mithali 3:5,6.
Je, unamwamini? Je, kweli unamwamini? Kiasi cha kutosha kumruhusu atawale maisha yako?


83

Imani inayookoa ni tegemeo kwa kafara ya Kristo kama malipo kamili na yasiyo na upungufu kwa ajili ya gharama kwa kila dhambi ambayo tumepata kuitenda.
Ina maana ya kuamini kwamba si kile tuwezacho kutenda kituokoacho, bali ni kile Kristo alichotenda kwa ajili yetu Kalvari.

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele



84

Hakuna mwanadamu awezaye kujivuna ya kwamba alijiokoa mwenyewe.
Utukufu wote ni wa Mungu!
Ni neema kwa upande wa Mungu na imani kwa upande wetu:
Kumtegemea Mungu kikamilifu - kwa kupenda sisi wenyewe kumruhusu Yeye atawale maisha yetu.



85

Kupokea wokovu ni rahisi kiasi hicho, bado wengi hufanya kuonekane kuwa ngumu sana na kwenye kutatanisha.
Swali tupaswalo kulijibu ni lile lile lililomjia askari magereza wa Filipi wakati alipomlilia Paulo na Sila usiku ule wa kutisha wakati tetemeko lilipofungua malango yote ya gereza:



86

(Fungu: Matendo 16:30)
Nifanye nini nipate kuokoka?



87

Kuna kweli nne tu za wokovu upaswazo kuzijua ili upate kuokolewa.
Nne tu.



88

(Fungu: Waefeso 2:8,9)
KWELI NA. 1: Wokovu ni zawadi ya bure.
Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.
Waefeso 2:8,9.
Sasa swali ni hili, Kwa nini wokovu unapaswa kuwa zawadi ya bure?
Sababu kwanini inapaswa kuwa zawadi ya bure inatuleta kwenye kweli nambari mbili.

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele



89

(Fungu: Warumi 3:23)
KWELI NA. 2: Sisi sote tumetenda dhambi.
Warumi 3:23 inasema, Kwa sababu wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.


90

Hii ina maana kwamba siistahili hiyo karama.
Sistahili wokovu.
Unaona, nimetenda dhambi.
Nimepungukiwa na utukufu wa Mungu.
Kama wokovu unategemea wema wangu, basi kamwe siwezi kuupata, kwa sababu nimetenda dhambi - kamwe siwezi kuwa mwema vya kutosha.
Hii ndiyo sababu halisi kwa nini wokovu unapaswa uwe karama ya bure, itolewayo bure kwangu, kwa sababu siwezi kuufanyia kazi na siwezi kuustahili.
Sisi sote tumetenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.



91

(Fungu: Warumi 6:23)
KWELI NA. 3 Tatizo: Dhambi humaanisha mauti.
Warumi 6:23 Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti.
Hilo ndilo tatizo kubwa tunalolikabili sote.
Mimi ni mdhambi ; kwa hiyo ninastahili mauti.
Sistahili karama ya wokovu.
Sistahili karama ya bure.
Ndiyo maana inapaswa iwe karama ya bure, unaona, kwa sababu sisi sote tumetenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.
Tatizo ni kwamba mimi kama mdhambi ninastahili kufa. Lakini Mungu anaufumbuzi kwa tatizo hili.



92

(Fungu: Warumi 5:8)
KWELI NA.4: Utatuzi: Yesu alikufa kwa ajili yetu.
Warumi 5:8 anasema,
Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi maana wakati tulipokuwa bado tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu.
Je, hilo siyo zuri ? Yesu alikufa kwa ajili yangu, mdhambi. Na rafiki, alikufa kwa ajili yako pia!

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele



93

Kweli nne rahisi. Hebu tufanye mapitio:



94

1. Wokovu ni karama ya bure.



95

2. Sisi sote tumetenda dhambi.



96

3. Tatizo: Dhambi humaanisha mauti kwetu.




97

4. Utatuzi: Yesu alikufa kwa ajili yetu, ikimaanisha uzima kwa ajili yetu kama tukimkubali Yeye kama Mwokozi wetu.


98

Tulipokuwa tungali wenye dhambi, Yesu alikufa kwa ajili yetu. Je, hamumpendi rafiki zangu?
Je, hamumpendi kwa kufa kwa ajili ya dhambi zako na dhambi zangu?
Je, hamumpendi kwa kutupatia sisi ile karama ya bure ya wokovu?


99

Sasa waweza uliza, Nawezaje kuikubali ile karama ya bure?

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele



100

(Fungu: Ufunuo 3:20)
Biblia inatupatia jibu la swali hilo kwenye Ufunuo 3:20.
Tazama! nasimama mlangoni na kubisha hodi.
Kama huyu mwenye uzima wa milele akibisha hodi kwenye mlango wa nyumba yako, Je, unamuacha nje - au utamkaribisha ndani?


101

Ni dhahiri, utafungua mlango na kumkaribisha ndani!
Unaona, kwa kumpokea Yesu, tunapokea karama ya uzima wa milele anaouleta.
Je, hilo si jema?
Yesu anataka kuja katika maisha yetu.
Tunamkaribisha ndani.


102

Hivi ndivyo tuipokeavyo hiyo karama ya bure.
Kwa urahisi tu tunanyoosha mikono na kusema, Ahsante, Yesu! Ingia maishani mwangu. Ingia moyoni mwangu.
Tawala maisha yangu - tawala moyo wangu.
Na wakati Yesu aingiapo ndani, tunamkubali kama Rafiki, kama Mwokozi wetu, kama Bwana wetu na Mkuu wetu.



103

Mambo mawili muhimu hutokea tuanapomuomba Yesu aingie mioyoni mwetu - tunapomkubali katika maisha yetu.



104

(Fungu: 1 Yohana 1:9)
Kwanza, tunaziungama dhambi zetu na kupokea msamaha wake.
tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki , hata atuondolee dhambi zetu



105

na kutusafisha na udhalimu wote. 1 Yohana 1:9.
Rafiki, hii ni ahadi nzuri.

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele


106

Bila kujali tulichokitenda au tulikokuwa , hata kama tumekuwa na maisha ya namna gani, hata kama tumekuwa wadhambi wabaya zaidi ya wote twaweza kuja kwa Yesu na kukubali karama ya bure ya wokovu. Twaweza kuungama dhambi zetu na kupokea msamaha wote ulio kamili.


107

Biblia inatuambia ya kwamba Yesu alizitupilia dhambi zetu ndani ya vilindi vya bahari, zisikumbukwe tena.



108

Wapenzi, Yesu anaposamehe, anasahau.
Je, ipo dhambi yoyote ambayo umewahi kuungama kwa Mungu, na bado unajihisi hukumu na kulemewa na hatia.
Labda unahisi ya kwamba ipo dhambi ambayo ni kuu sana kwa Mungu kuisamehe.
Twapaswa kuamini kile Mungu anachokisema.
Katika 1 Yohana 5:10 maneno yako wazi kabisa kwetu ya kwamba kama tusipomwamini Mungu, tunamfanya kuwa muongo.



109

(Fungu: 1 Yohana 5:10)
Anayemwamini mwana wa Mungu anao huo ushuhuda ndani yake; asiyemwamini Mungu, anamfanya kuwa mwongo, kwa kuwa hakuamini huo ushuhuda ambao Mungu ameshuhudia Mwanawe.



110

asiyemwamini Mungu, anamfanya kuwa mwongo,



111

kwa kuwa hakuamini huo ushuhuda ambao Mungu amemshuhudia Mwanawe. 1 Yohana 5:10.
Yesu anapoahidi kwamba atatusamehe dhambi zetu na kuondolea mbali hatia yetu, atatenda hakika alichokisema.

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele



112

Yesu anaposamehe, anasahau, na tunapaswa kusahau, pia!



113

(Fungu: Matendo 3:19)
Katika maneno ya Petro yaliyo katika Matendo 3:19: Tubuni basi  mrejee ili  dhambi zenu zifutwe ....


114

Unaona, tunakuja kwa Yesu, tunakubali karama ya bure ya wokovu, tunamkaribisha katika maisha yetu, na jambo la kwanza litokealo  ni kwamba anatusamehe na kututakasa anatuosha,  anazitupilia dhambi zetu katika vilindi vya bahari.
Je, hilo si jambo zuri, rafiki zangu?
Je, humpendi Mwokozi wako na wangu?
Lakini kuna jambo jingine linalotokea tunapomkaribisha Yesu mioyoni mwetu.




115

Anatupatia uwezo wa kushinda dhambi zetu na kuwa zaidi na zaidi kama alivyo - kutembea katika nyayo zake.
Mwivi haibi tena.
Mwongo haongopi tena.
Mlevi halewi tena.



116

(Fungu: Yohana 1:12)
Tambua katika Yohana 1:12:
Bali  wote waliompokea  aliwapa uwezo wa kuwa watoto wa Mungu,



117

Ndio wale waliaminio jina Lake.
Anatupatia uwezo wa kuwa watoto wake, wana wake na binti zake.  Hatuendelei kutawaliwa na Shetani. Hatudumu kuwa watoto wa giza.

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele



118

Atatupatia uwezo wa kutembea katika nyayo zake. Tunapomuamini, tunapoikubali ile karama ya wokovu, atatupatia uwezo wa kuwa washindi.


119

Kama tukijikwaa na kuanguka baada ya kupokea ile karama, atatusamehe tena na tena.
Kisha atatupatia uwezo wa kuwa washindi-kuwa zaidi na zaidi kama Yesu.
Ni njia ya ukuaji kujifunza kuwa na imani na ujasiri na tegemeo katika Yesu Mwokozi wetu. Hatutakuwa wakamilifu bali tutasamehewa . Shetani si tena bwana wetu. Yesu ni Bwana wetu.

8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele


120

Unaona, kuamini kuna maana ya kuwa na imani na tegemeo, na kukubali ile karama ya wokovu. Anatusamehe dhambi zetu na Yeye pia anatupatia uwezo wa kutembea katika nyayo zake.


121

Tunapoitikia abishapo mlangoni mwa mioyo yetu na kumkaribisha Yesu ndani, anasafisha mioyo yetu michafu na kutusamehe.
Anatupatia pia uwezo wa kubadilika na kuishinda dhambi na kuwa zaidi na zaidi kama Yeye.


122

Na kama Yesu akiishi ndani yetu, twaweza kujua kwa uhakika ya kwamba tunao uzima wa milele.
Je, ulilijua hilo?

Hatuhitaji kuwa na wasi wasi kama tutaokolewa na kuishi milele na Yesu.



123

(Fungu: 1 Yohana 5:12,13)
Yeye, aliye naye Mwana anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu, hana huo uzima.

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele



124

Nawaandikieni mpate kujua kwamba mnao uzima wa milele ninyi mnaoamini jina  Mwana wa Mungu,



125

ili mpate kujua kwamba mnao uzima wa milele. 1Yohana 5:12,13.


126

Yesu anataka tujue -hapa tena sasa- kwamba tunao uzima wa milele.
Twaweza kujua sasa tena hapa ya kwamba tunapomualika Yesu katika mioyo yetu, tunapokea uhakika wa wokovu wetu.
Yesu anatoa mwaliko kwa kila mmoja kila mahali, ili kwamba



127

(Fungu: Yohana 3:16)
kila amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.
Yohana 3:16.
Pengine unajihisi kwamba wewe u mwenye dhambi asiye na matumaini, lakini  hilo si kweli!
Mungu aweza kubadili hali isiyowezekana kabisa  na kuifanya ushindi.
Hakuna maisha yaliyo mabaya sana, au dhambi iliyo kubwa sana, ambayo Kristo hawezi kuisamehe!

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele




128

Desemba 31, 1995, John Clancy, askari mkongwe wa zima moto Jijini New York, aliongoza kikosi chake na kuingia katika jengo tupu la kupangisha liliokuwa likiteketea kwa moto katika eneo la Manhattan lenye ulevi mwingi. Moto ulipozidi nguvu za wazimaji, askari wazima moto walikuwa na wasiwasi ya kwamba yawezekana yupo aliyesalia ndani ya jengo, ingawa waliokuwa wakilitumia sasa walikuwa tu wahuni, watumiaji wa madawa ya kulevya, walevi, na makahaba.

Hata hivyo, Clancy na wenzake waliamua kuingia ndani ya miali hii kama ya tanuru katika mpango wa kusaka na kuokoa. Jengo lilikuwa limejazwa na moshi, kiasi cha kufanya uwezekano wa kuona kuwa karibu asilimia sifuri. Askari wazima moto walikuwa wakiweka hatarini maisha yao ili kutafuta wahuni ambao walikuwa wakilitumia jengo hili kama makazi yao ya muda. Ghafula, dari ya ghorofa ya pili ikaanguka, ikamnasa John Clancy. Wenzake wakahangaika sana ili kumtoa toka kwenye tanuru la moto, lakini walipofanikiwa hatimaye kumtoa nje, walikuwa wamechelewa sana.

Mwili wake ulikuwa umeunguzwa kiasi cha kuwa vigumu kutambulika. Siku ya mwisho ya mwaka 1995 ilikuwa siku ya mwisho ya maisha ya huyu mpiganaji jasiri katika moto. Aliacha nyuma mke aliyekuwa mjamzito wa miezi sita na mipango ya baadaye waliyokuwa wakiipanga pamoja. John Clancy aliamini ya kwamba maisha yote yalikuwa ya thamani; hivyo alikuwa tayari kuweka hatarini maisha yake mwenyewe ili kuokoa yeyote alliyekuwemo kwenye jengo. Aliacha usalama wa nyumba yake ili aingie kwenye hatari ya moto mkali. Aliingia kwenye miali ya moto kuokoa maisha ya wengine akapoteza yake.

Kujitoa kwake katika kuwajibika kulimgharimu maisha yake.

Hangeweza kusimama kivivu huku akijua wengine walikuwa wakifa.

Undani wa kisa hiki ulipochunguzwa, wachunguzi

waligundua ya kwamba moto ulikuwa umeanzishwa na mtu ambaye huwasha mioto makusudi; kama vile nyumba,nk. Edwin Smith, mmoja wa watu wajulikanao kama wa chini na wa nje aliyetajwa kuwemo ndani ya jengo, ndiye aliyeuwasha moto huu. Ukweli mzito ni huu, John Clancy alikuwa akijaribu kuokoa mtu aliye choma lile jengo. Alitoa maisha kwa ajili ya mteketezaji. Kielelezo kizuri kiasi gani cha Yesu Kristo.


129

Yesu aliacha usalama wa nyumba yake ya mbinguni na kujitumbukiza katika joto kali la moto wa dunia hii.
Mwokozi wetu alining'inia msalabani, na mioto ya dhambi ilimchoma kabisa.
Kwa uchaguzi wetu sisi wenyewe tulitenda dhambi. Tuliweka dunia hii katika moto kwa hasira zetu, kwa kutokuwa waaminifu, kwa tamaa zetu, kwa uzinzi wetu, kwa udanganyifu wetu.
Kristo alikufa ili tupate kuishi.
Alipitia miali ya moto ya dhambi katika msalaba ili sisi tusiupitie ukali wa miali ya jehanamu Yesu atakapokuja kuchoma dhambi milele.
Leo Yesu anataka kukupa uhakika ya kwamba waweza kuishi milele.


130

Anasikiliza na kusubiri.
Kwa nini usiufungue mlango wa moyo wako leo na kumkaribisha Yeye ili aingie na awe Mwokozi na Bwana wa maisha yako?
Anasubiri! Anasikiliza!
Kuna jambo moja ambalo Yesu hawezi kulifanya, nalo ni kukulazimisha wewe ufungue mlango wa moyo wako kwa ajili yake.
Ametupatia kila mmoja wetu uwezo wa kuchagua.
Sisi wenyewe tunapaswa kuufungua mlango!
Ataingia kwa furaha kama tukifungua mlango!
Rafiki, je, ungependa kulifanya hilo hivi sasa?
Je, ungependa kumualika Yesu moyoni mwako bila kusubiri zaidi?

# 8 - Kuzaliwa ili Kuishi Milele




131

Kama ndivyo, basi hebu tusali pamoja.




132

Mungu Mpenzi, ninatambua ya kwamba mimi ni mdhambi na ninahitaji msaada.




133

Ninataka kumkubali Yesu kama Mwokozi wangu na Bwana.



134

Ninataka kujibu anapobisha  na kumkaribisha ndani ya moyo wangu hivi sasa.



135

Tafadhali samehe kila dhambi niliyoitenda. Tafadhali tawala maisha yangu kikamilifu.


136

Ninataka Yesu aje moyoni mwangu  auoshe kabisa na kisha anisaidie nipate kuishi kwa ajili yake. Ahsante kwa kusikia na kujibu sala yangu, katika jina la Yesu, Amina.

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri




1

Hakimu yu Upande Wako



2

James wa kwanza, mmoja wa Wafalme wa Uingereza, anatajwa akiwa katika kujaribu nafasi yake kama hakimu. Kwa uangalifu kabisa alisikiliza upande mmoja wa kesi. Alikuwa karibu kabisa aamue kufanya uamuzi wake alipoamua kusikiliza upande wa pili wa kesi.

Kisha hali akiwa amekanganyikiwa kabisa, hakujua la kufanya. Watu aliowadhania kutokuwa na hatia, sasa walionekana kuwa na hatia. Watu walioonekana mwanzo kuwa na hatia sasa walionekana kutokuwa na hatia. Matokeo yake aliacha nafasi ya uhakimu katika hali ya kukata tamaa.


Mfalme James wa kwanza akaliweka hivi,

Ningeendelea vizuri sana kwa kusikia upande mmoja peke yake, lakini wakati pande zote mbili ziliposikika kwa roho yangu, sijui sahihi ni ipi.

Hakimu aliyechanganyikiwa atakuwa na wakati mgumu kufanya uamuzi ulio sahihi.

Mungu ni hakimu asiye na upendeleo, anayetumia haki kikamilifu na aliye sahihi.

Hachanganyikiwi kabisa anapotuhukumu.




3

Biblia inatufundisha ya kwamba kila mmoja wetu anayo kesi inayotusubiri mbele za Mungu.

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri



4

Hata sasa, tunapewa mwito wa kwenda hukumuni ili kutoa taarifa ya jinsi ambavyo tumeishi na yale ambayo tumeyatenda.
Kila mwanamume na mwanamke ambaye amewahi kuishi anayo kesi inayomsubiri mbele za baraza ya hukumu ya Mungu -- mahakama ya juu kuliko zote katika ulimwengu.
Mtume Paulo anasema juu ya miadi ambayo dunia nzima lazima iitunze:



5

(Fungu: Matendo 17: 31)
Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu...... Matendo 17:31.
Hakuna atakayekuwa na udhuru. Hakuna awezaye kukwepa mwaliko huo.
Biblia inataja wazi ya kwamba kila mmoja lazima awepo:



6

(Fungu: 2 Wakorintho 5:10)
Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo......
2 Wakorintho 5: 10.


7

Tuamini tusiamini.
Tupende tusipende.
Tujiite Wakristo au la.
Haijali ni nani lazima sote tuwepo.
Mungu hana upendeleo.
Tunapoitwa na mahakama ya mbinguni, lazima tuwepo. Kwa nini?
Paulo anatoa jibu:



8

(Fungu: Warumi 14:12)
Basi ni hivyo, kila mtu miongoni mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu.
Warumi 14:12.

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri




9

Uamuzi wa mahakama ya mbinguni utaweka muhuri wa milele kwa hatima ya kila mtu.
Na uamuzi hautabadilishwa, kwani hakuna mahakama ya juu zaidi ya rufani!



10

Lakini kabla ya tamko la mwisho kutolewa, ama hukumu kupitishwa, lazima kuwe na kesi au upelelezi.
Hebu tufungue Biblia na tuone picha ya hii baraza ya hukumu, au kutaniko la mahakama, kule mbinguni.
Nabii Danieli aliandika:



11

(Fungu: Danieli 7:9,10)
Nikatazama hata viti vya enzi  vikawekwa, na mmoja aliye mzee wa siku  ameketi;



12

mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele  za kichwa chake kama sufu.




13

kiti cha enzi kilikuwa miali ya moto, na gurudumu zake  moto uwakao.



14

Mto kama wa moto
ukapita mbele zake;



15

Maelfu elfu wakamtumikia,

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri



16

na elfu kumi mara elfu kumi wakasimama mbele zake;
hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa.
Danieli 7:9,10.


17

Hapa Danieli anaona picha ya Mungu, Baba, au Mzee wa Siku, akiwa ameketi kwenye kiti chake cha enzi cha milele, huku akiwa amezingirwa na malaika wengi wasiohesabika.
Sasa ona kile alichokiona Danieli kilichofuatia katika njozi yake:



18

( Fungu: Danieli 7:13)
Nikaona katika njozi za usiku, na tazama,



19

mmoja aliye mfano wa mwanadamu, akaja pamoja na mawingu ya mbingu!



20

Akamkaribia huyo mzee wa siku, wakamleta karibu naye.
Danieli 7:13.


21

Hapa Mwana wa Mungu anaonekana akiwa amesimama mbele za Mzee wa Siku.
Ni jinsi gani hii inafanana na mahakama hapa Duniani!
Yupo Hakimu anayeendesha kesi yote: Mzee wa Siku.
Wapo mashahidi: malaika watakatifu ambao wameona na kurekodi kila kitu.
Na waliosimama mbele za kiti cha enzi ni Yesu - Wakili wa mwanadamu, kama Yohana alivyoandika:

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri





22

(Fungu: 1 Yohana 2:1)
.....tunaye Mwombezi
kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki.
1 Yohana 2:1.



23

Naam, wasema, kila mmoja anaonekana kuwa pale lakini yule atakaye hakikiwa (hukumiwa)! Hii inaleta maana, lakini hebu na utangalie kile Biblia inachokisema:



24

(Fungu: Danieli 7:10)
...hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa.
Danieli 7:10.
Ni wazi vitabu hivi vina taarifa za matendo ya wale wanaosimama ili kuhakikiwa, kwani Sulemani aliandika:



25

(Fungu: Mhubiri 12:14)
Kwa maana Mungu
ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya.
Mhubiri 12:14.



26

(Fungu: Malaki 3:16)
Malaki anaongezea: Ndipo wale waliomcha BWANA waliposemezana wao kwa wao. Naye BWANA akasikiliza, akasikia;



27

na kitabu cha ukumbusho kikaandikwa mbele zake, kwa ajili ya hao waliomcha BWANA, na kulitafakari jina lake.
Malaki 3:16.
Mungu anatambua kila wakati mioyo yetu inapovutwa kwake. Ananukuu kila neno la kutia moyo tulitoalo kwa mtu mwingine na kila tendo la wema.
Mfalme Daudi pia alijua juu ya taarifa kwani alisema:

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri



28

(Fungu: Zaburi 56:8)
Uyatie machozi yangu katika chupa yako;
(Je! Hayamo katika kitabu chako?) Zaburi 56:8.
Mungu anajua juu ya simanzi za ndani zaidi za maisha yako pia.
Kwa kweli, Mungu anajua yote yanayotuhusu, kwani Daudi aliandika pia:



29

(Fungu: Zaburi 139:1,3,16)
Ee BWANA, umenichunguza
na kunijua.



30

.....Umeelewa na njia zangu zote.



31

......Chuoni mwako
ziliandikwa zote pia, Siku zilioamriwa
kabla hazijawa bado.
Zaburi 139:1,3,16.


32

Wakati Mungu ajua yote yanayotuhusu, siyo lazima kwake kutunza taarifa kwa faida yake.
Taarifa zinatunzwa kwa faida ya ulimwengu, hivyo kuna kithibisho dhahiri cha upendo wa Mungu na haki kwa kila kesi.
Uwajibikaji wetu kwa Mungu ni wazo uchaji.


33

Kila mmoja lazima atoe taarifa kwa ajili ya karama iliyo ya muhimu kuliko zote - maisha! Hiki ndicho Sulemani alichosema alipoandika:



34

(Fungu: Mhubiri 11:9)
Wewe kijana, uufurahie ujana wako, na moyo wako ukuchangamshe siku za ujana wako;

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri



35

ukaziendee njia za moyo wako, na katika maono ya macho yako,



36

lakini ujue wewe ya kwamba kwa ajili ya hayo yote Mungu atakuleta hukumuni.
Mhubiri 11:9.



37

(Fungu: Mathayo 12:36,37)
Mathayo aliandika:....Kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu.



38

Kwa kuwa kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa.
Mathayo 12:36,37.



39

Mtu mmoja amekadiria ya kwamba mtu wa kawaida hunena kwa juma  maneno ya kutosha  kujaza kurasa 320!
Katika miaka 60, hilo lingemaanisha vitabu zaidi ya 3,000!


40

Je maktaba yako ya vitabu ingelisema nini katika hukumu?
Na zaidi ya hapo, hata nia  zilizopelekea maneno hayo na matendo yote yatawekwa wazi ili yaonekane:



41

(Fungu: 1 Wakorintho 4:5)
......Atayamulikisha yaliyo sitirika ya giza, na kuyadhihirisha mashauri ya mioyo.....
1 Wakorintho 4:5.

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri


42

Hakutakuwa na kufuta, wala kufunika funika chochote siku ile!
Watu wanaweza kudanganya marafiki zao na hata familia zao, lakini hakuna awezaye kumdanganya Mungu.
Yeye husoma siri za moyo!


43

Unaona, siku yetu ya hukumu ikifika, tutajikuta katika moja ya sehemu mbili:
Ama taarifa yetu yote ya kushindwa kwetu wakati wa uliopita itakuwa imefunikwa na damu ya Yesu, ama taarifa yetu itasimama kutuhukumu.
Na kwa kweli, siyo jinsi tunavyojiita, lakini jinsi tulivyo halisi na yale tuyatendayo ndivyo viletavyo tofauti!



44

(Fungu: Mathayo 16:27)
Tunaambiwa ya kwamba wakati Yesu akija, ....ndipo atakapomlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake. Mathayo 16:27.
Matendo yetu mema siyo msingi wa wokovu wetu, neema ya Mungu ndiyo msingi. Lakini matendo yetu hufunua kama mioyo yetu imekabidhiwa kwa Mungu.




45

Sasa, pengine unasema, Kama tunaokolewa kwa neema, kwa nini tunahukumiwa kwa matendo yetu?
Hilo ni swali zuri!
Dk. Sakae Kubo aliandika hivi karibuni:



46


Hebu na tufikirie ingekuwa na maana gani kama hukumu haingekuwa na msingi katika matendo.



47

Mungu angelituhukumu kwa msingi upi,
ngozi yetu, rangi yetu, daraja letu katika jamii, elimu yetu, muonekano wetu, talanta yetu, nguvu zetu,

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri



48

ushirika wetu kanisani, au tu kwa sisi kumkiri Kristo hadharani? Mungu anaweza tu kutuhukumu kwa matendo yetu, mema au mabaya.
Mwito Wako Mahakamani, uk.20.



49

Haya ni matokeo yanayokuja yenyewe kama matunda ya moyo uliojaa upendo kwa Mungu na kwa mwanadamu.
Ni uhusiano wa upendo na Yesu ambao unachochea wafuasi wake kutenda matendo mema.
Akihitimisha katika Kitabu cha Mhubiri, Sulemani alisema:



50

(Fungu: Mhubiri 12:13,14)
Hii ndiyo jumla ya maneno yote yamekwisha sikiwa:



51

Mche Mungu, nawe uzishike amri  zake: Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu.



52

Kwa maana Mungu ataleta hukumuni..........
Mhubiri 12:13,14.
Kwa sababu uhusiano wa mtu na Kristo utahukumiwa kwa mwenendo wake, lazima kuna kiwango dhahiri ambacho mwenendo hupimwa kwacho.


53

Katika taratibu za sheria zetu hapa duniani, kusudio la kawaida la mahakama ni kuhakikisha kama uhalifu umetendeka -- kama sheria imevunjwa.
Pale tu inapohakikishwa kwamba sheria imevunjwa ndipo mtu anapopatikana na hatia.


54

Katika hukumu ya Mungu kuna sheria au kiwango, na Yakobo analiweka wazi kuwa ni sheria ipi itakayoinuliwa.

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri



55

(Fungu: Yakobo 2:12)
Semeni ninyi,
na kutenda kama watu watakaohukumiwa kwa sheria ya uhuru.
Yakobo 2:12.

---



56

(Fungu: Yakobo 2:11)
Katika fungu lililopita, Yakobo anataja amri mbili, Usizini, na Usiue.
Hivyo ni wazi, Amri Kumi za Mungu ni sheria iitwayo Sheria ya Uhuru ambayo kwayo maisha ya watu yatahukumiwa.

---



57

Hukumu itadhihirisha tu sehemu gani tunasimama katika pambano kuu kati ya Kristo na Shetani.
Je, tupo na Kristo?
Je, tumemruhusu aishi ndani yetu?

---


58

Je, tumekuwa na upendo wa juu kwa ajili yake na mapenzi yake kama inavyoelezwa katika Amri Kumi?
Je, ni tamaa yetu kufuata mapenzi yake kwa uwezo wake?
Je, ameandika sheria yake katika mioyo yetu?

---


59

Unaona, wahamiaji wanapotamani kuwa raia wa nchi, wanatakiwa waape kuwa watii kwa nchi ile, waahidi kuwa raia watiifu na kuzishika sheria za nchi ile.

---



60

Vivyo hivyo na Wakristo. Wakati wanapomkubali Kristo na kutamani kuwa raia wa ufalme wake, Mungu anawauliza kuahidi kumpa upendo na utii yeye na kuzishika sheria za serikali yake.

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri



61

Hata hivyo, siyo raia wote wanaosalia kuwa waaminifu kwa maagano yao.
Baadhi kwa nje huonekana kuwa raia wema wa nchi, lakini baadaye hukutwa wakiwa waharibifu.
Hili linapohakikishwa, uraia wa mtu huyo huondolewa na mtu huyo huondolewa katika nchi.



62

Vivyo hivyo, siyo Wakristo wote wanaosalia kuwa waaminifu katika maagano yao.
Haitoshi kuitwa mwenye haki sasa, tunapaswa kusalia tukiwa waaminifu kwake hadi ajapo/
Haitoshi kujidai ya kwamba tu wafuasi wa Kristo, lazima turuhusu maisha ya Yesu yasiyo na upungufu wowote ya utii na uaminifu yawe ndani yetu.



63

(Fungu: Mathayo 7:21)
Yesu alisema, Si kila mtu aniambiaye, 'Bwana, Bwana,' atakayeingia katika ufalme wa mbinguni;



64

bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Mathayo 7:21.
Pambano zima kati ya wema na uovu, kati ya Kristo na Shetani, linahusu tabia ya Mungu ya upendo.


65

Na sheria ni kiwango cha tabia ile katika maandishi.
Mshangao kidogo ya kwamba inaonekana sana katika hukumu ya mwisho!


66

Lakini ukweli wa kushangaza zaidi ambao unafahamika kwa Wakristo ni kwamba mahakama ya mbinguni inaendelea hivi sasa!
Kwa hakika, kitabu cha mwisho cha Biblia, Ufunuo, hufunua ya kwamba hukumu ya Mungu inaendelea sasa hivi.

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri



67

Hii ndiyo sababu, katika sura za mwisho za Kitabu cha Ufunuo, Yohana anaeleza kwa ufupi onyo la mwisho kwa dunia na mwaliko katika maneno haya:



68

(Fungu: Ufunuo 14:6,7)
Kisha nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu,



69

mwenye  injili ya  milele, awahubiri hao wakaao juu  ya nchi-



70

na kila taifa  na kabila  na lugha na jamaa----




71

akasema kwa sauti kuu,  'Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja;



72

Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji.'
Ufunuo 14:6,7.



73


Utatambua ya kwamba ujumbe huu  hausemi hukumu itakuja, unasema, saa ya hukumu imekuja.

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri




74

Sehemu ya pili ya ujumbe huu unaokuja katika sehemu kuu tatu, ni mwito kwa watu wa Mungu watoke katika mifumo ya kidini bandia ambayo itakuwepo katika siku za mwisho.
Sehemu ya mwisho ya ujumbe huu wa mwisho kwa dunia inawaonya watu wa Mungu kuwa macho wasiabudu mamlaka ya mnyama ya Ufunuo 13.



75

(Fungu: Ufunuo 14:9,10)
....Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake.



76

Yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa,...
Ufunuo 14:9,10.
Sasa, tazama fungu la 14 na la 15, ambayo hufuatia tangazo la ujumbe wa malaika watatu:



77

(Fungu: Ufunuo 14:14,15)
Kisha nikaona, na tazama, wingu jeupe, na juu ya wingu hilo ameketi mmoja, mfano wa Mwanadamu,



78

mwenye taji ya dhahabu juu ya kichwa chake, na katika mkono wake mundu mkali.



79

Na malaika mwingine akatoka katika hekalu, akimlilia kwa sauti kuu yeye aliyekuwa ameketi juu ya lile wingu,



80

'Tia mundu wako, ukavune; kwa kuwa saa ya kuvuna imekuja;

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri



81

kwa kuwa mavuno ya nchi yamekomaa.'
Ufunuo 14:14,15.



82

Mavuno ya dunia ni nini? Ni mwisho wa dunia. Mavuno yanahusu kuja kwa Kristo mara ya pili.Ni kitu gani ambacho hutokea kabla ya kuja kwa mara ya pili kwa Yesu? Hukumu ya Mungu.
Hukumu yake inafunua kwamba ni nani aliye tayari kwa ajili ya kuja kwake. Lakini lazima tutulie na kulichunguza somo hili kwa undani zaidi. Labda unashangaa kuwa hukumu hii ilianza lini?




83

Ufunguo unapatikana katika unabii wa pekee sana katika Kitabu cha Danieli!



84

(Fungu: Danieli 8:14)
Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakaswa.
Danieli 8:14. Huu ni unabii wa muda mrefu kuliko wote katika Biblia.



85

(Fungu: Ezekieli 4:6)
Katika unabii tunaona ya kwamba siku inawakilisha mwaka.
siku moja kwa mwaka mmoja, nimekuagiza.
Ezekieli 4:6. Hivyo siku 2300 huwakilisha miaka 2300.



86

Miaka 2300 ni sehemu ya unabii wenye mambo mengi sana unaopatikana katika kitabu cha Danieli sura za 7,8, na 9.

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri




87

Unabii huu unasonda tarehe halisi ya ubatizo na kusulubishwa kwa Bwana wetu.
Pia hufunua wazi kabisa wakati halisi wa hukumu kuanza.



88

Siku hizi za kinabii 2300 au kipindi hiki cha miaka 2300 kilianza wakati wa amri ya Mfalme Artashasta kurejesha Yerusalemu na kuujenga upya uchumi wake. Wana wa Israeli walikuwa wamekaa mateka katika Babeli kwa miaka 70 na walitamani kwenda nyumbani na kujenga upya jiji lililopendwa


89

Hatimaye, katika mwaka wa 457 K.K., Mfalme alitoa tamko liliokuwa likisubiriwa kwa muda mrefu. Miaka elfu mbili na mia tatu kutokea tarehe ile, huishia katika mwaka wa 1844 B.K.

Sasa hebu turejee katika fungu letu. Hata siku elfu mbili na mia tatu za kinabii au miaka halisi, ndipo hekalu litakapotakaswa. Tumeona ya kwamba unabii huu unakwenda hadi mwaka wa 1844. Utakaso wa hekalu ni nini?



90

Mwaka wa 1844 kile ambacho Biblia inakieleza kama Saa ya Hukumu ya Mungu ilianza. Mshale uligonga katika saa halisi. Waweza uliza, Hukumu inahusianaje na utakaso wa hekalu ambao Danieli alitabiri utatendeka mwishoni mwa siku 2300?



91

Utakaso wa hekalu ni nini? Huu una uhusiano gani na hukumu? Biblia inaeleza juu ya mahekalu mawili - moja la hapa duniani, na lingine la mbinguni.


92

Katika Israeli ya kale, watu walileta kafara zao kila siku hekaluni.

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri


93

Pale waliungama dhambi zao na kutoa uhai wa mwana-kondoo kuonyesha imani yao kwa mauti iliyokuwa ikija mbele yao ya Yesu, Mwana wa Mungu.


94

Leo, kama tukitenda dhambi, tunamuomba Mungu atusamehe dhambi zetu kwa sababu Yesu alikufa mahali petu ili alipe deni la dhambi.


95

Hata hivyo, kabla ya Kalvari, watu hawakuwa na kafara ya kuitizama nyuma yao, hivyo badala yake kwa imani walitizama mbele  wakati Mwana-Kondoo wa Mungu angelikufa kwa ajili yao.
Kwa kitendo cha kutoa kafara ya mnyama asiye na hatia, walitambua imani yao katika Mwokozi ambaye angekuja na kufa ili afanye iwezekane kwao kupata msamaha.


96

Kisha kwa ishara dhambi zao zilihamishiwa hekaluni na kuhani aliyenyunyiza damu toka kwa mnyama mbele za pazia la Patakatifu Sana ndani ya hekalu.



97

Kisha siku moja kila mwaka, wana wa Israeli waliiadhimisha siku takatifu na ibada takatifu iliyoitwa Siku ya Upatanisho au utakaso wa hekalu. Kwa wana wa Israeli, hii ilikuwa ni siku ya hukumu.


98

Siku kumi kabla ya Siku ya Upatanisho, tarumbeta zililia, zikiwakumbusha wana wa Israeli ya kwamba ulikuwa wakati wao wa kufanya hesabu ya maisha yao--kutubu na kuungama dhambi zao.
Wote walioshindwa kufanya hivyo wallihamishiwa mbali na kambi.



99

Kwa maana siku hiyo upatanisho utafanywa kwa ajili yenu, ili kuwatakasa;

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri



100

nanyi mtatakaswa na dhambi zenu zote mbele za BWANA.
Mambo ya Walawi 16:30.



101

Sasa, Kitabu cha Waebrania kinalifanya hili kuwa wazi  ya kwamba hekalu  la kidunia na huduma yake lilikuwa kielelezo cha hekalu la mbinguni ambapo Kristo Kuhani wetu Mkuu anapotusamehe dhambi zetu.




102

(Fungu: Waebrania 8:1,2)
Paulo anasema, ...tunaye kuhani mkuu wa namna hii, aliyeketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Ukuu mbinguni.



103

mhudumu wa patakatifu na wa ile hema ya kweli, ambayo Bwana aliiweka wala si mwanadamu.
Waebrania 8:1,2.



104

(Fungu: Waebrania 9:11, 12, 24)
Na tena: Lakini kama Kristo akiisha kuja, aliye kuhani mkuu......




105

....bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika Patakatifu,



106

akiisha kupata ukombozi wa  milele....



107

Kwa sababu Kristo
hakuingia katika patakatifu palipofanyika kwa mikono,

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri




108

ndio mfano wa patakatifu halisi; bali aliingia mbinguni hasa,




109

aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu........ Waebrania 9: 11, 12,24.
Kifo cha Kristo Kalvari kilitoa upatanisho wenye kafara ulio kamili kwa ajili ya dhambi zetu.



110

(Fungu: Waebrania 7:25)
....Aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye;



111

maana yu hai siku zote ili awaombee. Waebrania 7:25.
Madhabahu ya kweli au hekalu liko mbinguni.
Kila kitu kinachotokea hapa duniani ni mfano tu wa kile kinachotokea katika mpango wa wokovu.
Yesu ni Mwana-Kondoo anayekufa. Yesu ni kuhani anayeishi. Yesu ni Kuhani Wetu Mkuu.
Kama jinsi Kuhani Mkuu wa Israeli alivyoingia Mahali Patakatifu sana mara moja kwa mwaka, vivyo hivyo Yesu wakati wa mwisho aliingia Patakatifu Sana kutenda kazi yake ya hukumu.



112

(Fungu: Mathayo 10:32,33)
Katika hukumu, ni uhusiano wetu na mtizamo wetu kwa Kristo utakaoamua juu ya hatima yetu ya milele.
Kristo anatamani kutuokoa.
Anatenda kila awezacho ili kutuokoa. Anasema, Basi kila mtu atakayenikiri mbele ya watu,



113

nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni.

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri



114

Bali mtu yeyote atakayenikana
mbele ya watu, nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni.
Mathayo 10:32,33.


115

Je, unaona? Huhitaji kusimama mwenyewe kwenye hukumu!
Kama tukimkiri Kristo, atatukiri mbele za Baba yake. Kama sisi tu wa Kristo, Yeye ni Wakili wetu. Kupitia kwa Yesu tutasimama mbele za Mungu kana kwamba hatujawahi kutenda dhambi.


116

Taarifa zetu zitaonyesha tu maisha ya upendo ya Mwokozi wetu, na tunapata sifa kwa maisha yake yaliyo kamili. Kwa hiyo, rafiki yangu, hakuna la kuhofu juu ya Siku ya Hukumu kwa wale wanaompenda na kumfuata Yesu kwa mioyo yao yote na roho zao zote.
Kwani Yesu atawakilisha sifa ya damu yake mwenyewe iliyomwagika kufunika kila dhambi iliyoungamwa, maana Yohana aliandika:



117

(Fungu: 1 Yohana 1:7)
.....Na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote. 1 Yohana 1:7.



118

Tunaishi katika saa za mwisho za Dunia. Hukumu ya upelelezi imekuwa ikiendelea katika mahakama ya mbinguni tangu mwaka wa 1844.



119

Bila ya shaka hukumu ilianza na Habili, mwenye haki wa kwanza kufariki katika Sayari Dunia.

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri




120

(Fungu: 1 Petro 4:17)
Petro aliandika: Kwa maana wakati umefika kwa hukumu kuanza katika nyumba ya Mungu.
1 Petro 4:17.
Kwa maneno mengine, hukumu inaanza na wale wanaojiita watu wa Mungu.


121

Twaweza kupiga picha katika mawazo yetu siku ya Habili mahakamani.
Kesi yake inapotajwa mahakamani, Mungu anaona maisha ya Habili, na pale ipo taarifa ya ukubali wake wa mauti ya Mwana-Kondoo wa Mungu.


122

Mojawapo ya matendo ya mwisho ya Habili yaliyorekodiwa katika Biblia, ilikuwa ni ile kafara aliyoitoa, akionyesha imani yake kwa Mkombozi anayekuja.
Maisha ya Kristo yamewekwa katika taarifa badala ya yale yake.
Dhambi zake zimefunikwa zote kwa damu ya Kristo.


123

Waweza kuhakikishiwa ya kwamba  Yesu, Wakili wa Habili, aliinyoosha mikono yake iliyoogopa misumari na akasema:
Damu yangu, Baba, ililipa deni la Habili.
Na je huwezi tu kusikia wale malaika wengi wasiohesabika wakishangilia wakati Yesu akisema:
Tunza jina la Habili katika Kitabu cha Uzima!
Na jina lake bado liko pale!
Kama jinsi Kristo alivyoahidi:



124

(Fungu: Ufunuo 3:5)
Yeye ashindaye, atavikwa hivyo mavazi meupe,



125

wala sitalifuta kamwe jina lake katika kitabu cha uzima,

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri



126

nami nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu na mbele za malaika zake.
Ufunuo 3: 5.


127

Bila ya shaka pia, jina la Yuda limepata kuletwa mbele za mahakama ya mbinguni.
Yuda alikuwa mfuasi wa Kristo - alikuwa mmoja wa wanafunzi wake.
Hakuwa mbaya sana, lakini maisha yake hayakufikia kipimo cha heshima aliyoidai.
Hakumpenda Kristo kupita vyote!


128


Wakati fulani alikuwa akivutwa kwa Kristo, lakini udhaifu mmoja ulipelekea kwa mwingine hadi hatimaye alipomuuza Bwana wake kwa vipande thelathini vya fedha!
Kisha katika hali ya uchungu alijinyonga mwenyewe!


129

Yesu alimpenda Yuda. Hata aliinama na kuosha miguu ya Yuda iliyokuwa na vumbi usiku wa Pasaka ya Mwisho! Yesu alitegemea kugusa ule moyo wenye kiburi.
Alitaka aweze kusimama kando yake katika hukumu kama Wakili wake,


130

lakini Yuda aligeukia mbali.
Ni lazima limekuwa jambo la kusikitisha kiasi gani kwa Yesu kupitia jina la Yuda.
Haki yetu wenyewe haiwezi kutuokoa katika hukumu.
Sikiliza:




131

(Fungu: Isaya 64:6)
Kwa maana sisi sote tumekuwa
kama mtu aliye mchafu,na matendo yetu
yote ya haki yamekuwa kama
nguo iliyotiwa unajisi;..... Isaya 64:6.

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri


132

Wale tu ambao wameendelea kumfanya Kristo kuwa wa kwanza katika maisha yao waweza kuvaa vazi la haki la Kristo.
Bila hivyo, hakuna mtu atakayetetewa katika hukumu.
Hivyo jina la Yuda linafutwa toka katika Kitabu cha Uzima.


133

Huu ni wakati wa muhimu sana tunaoishi kwawo, Kama jinsi ilivyokuwa kwa Wana wa Israeli, tunahitaji kuchunguza takwimu za maisha yetu.
Tunahitaji kutunza ahadi yetu kwa Yesu, kwani ndiyo tu maandalizi pekee yawezekanayo kwa ajili ya kuitwa kwetu mahakamani.
Hivi karibuni rehema kwa ajili ya mwanadamu itafungwa na tamko litasikika:




134

(Fungu: Ufunuo 22:11)
Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu;...na mtakatifu na azidi kutakaswa.
Ufunuo 22:11.
Wakati huo, rehema na msamaha ambao Mungu ameutoa kwa mwanadamu kwa muda mrefu kiasi hicho vitaondolewa.
Maneno ya kusikitisha sana katika lugha ya kibinadamu yatakuwa ya wale ambao wametupilia mbali wokovu -- ambao hawajamkubali Kristo kama Mwokozi wao na Wakili wao.



135

(Fungu: Yeremia 8:20)
Watasema, Mavuno yamepita, wakati wa hari umekwisha, wala sisi hatukuokoka!
Yeremia 8:20.
Kisha Yesu anarejea Duniani, kwani tunasoma:



136

(Fungu: Ufunuo 22:12)
Tazama,  naja upesi, na ujira wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo.
Ufunuo 22:12.

# 9 - Kuikabili Hukumu kwa Ujasiri



137

Rafiki, Yesu anatamani kuwa Wakili katika hukumu! Anatamani uipokee kafara yake katika Kalvari. Anatamani wewe uungame dhambi zako kwake ili apate kuziondolea mbali.
Anatamani jina lako liandikwa katika Kitabu cha Uzima.
Yohana anaelezea juu ya wale watakaoingia na ambao hawataingia katika jiji takatifu:




138

(Fungu: Ufunuo 21:27)
Na ndani yake hakitaingia kamwe chochote kilicho kinyonge, wala yeye afanyaye machukizo na uongo,




139

bali wale walioandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo.
Ufunuo 21:27.




140

Je, ungependa kufungua moyo wako kwa Yesu sasa hivi? Je, ungependa kumuomba achukue toka katika maisha yako chochote ambacho chaweza kukuzuia usiingie katika ufalme wake? Katika hukumu Mungu hufunua kila kitu kwa ajili kutuhusu sisi.
Kila kitu hufunuliwa mbele za ulimwengu huu wote. Dhambi zetu zote hurekodiwa. Je, ungependa dhambi zako zifunikwe - zifunikwe na damu ya Yesu? Je, ungependa Kristo asimame na kusema, Ndiyo, huyu mwanamume, huyu mwanamke, ni wangu halisi. Nimewasamehe dhambi zao. Nimelifuta deni lao. Nimesamehe hatia yao. Dhambi zao zimefunikwa kwa damu yangu. Zifute toka kwenye taarifa milele. Yesu anasimama katika kiti cha enzi cha mbinguni. Anasimama pale katika hukumu kama Mwokozi wako. Hivi sasa! Je, utampatia maisha yako yote? Kwa nini usiinue mkono wako kuelekea mbinguni sasa hivi tunaposali na useme, Ndiyo, Bwana. Chukua maisha yangu. Ninataka kuwa wako.



1

Je, Hufanya Tofauti Kweli ?



2

Je, umetambua jinsi uhalifu unavyoinuka katika majiji duniani kote?
Unajionyesha katika namna za kushangaza.


3

Mtu mmoja aliyavamia makao makuu ya Polisi siku moja, akiwa ameghadhibika sana.
Mtu fulani alikuwa amevunja nyumbani kwake na kutoroka na vitu kadhaa vyenye thamani. Kama katika mpito tu hivi, mtu huyu alikuwa amepata mwonekano kidogo wa mwizi na alikuwa akidai ya kuwa askari polisi wafanye kitu juu ya hili.
Afisa wa polisi aliyekuwa akiwajibika alimuongoza hadi kwenye lundo la vitabu vyenye majina ya wahalifu. Alimsaidia mtu huyu kupitia picha za watu wenye taarifa za uhalifu, ili kuona kama angemtambua mwizi.


4

Ghafla yule afisa wa polisi akasema, ngoja kwanza. Akapiga kofi sehemu ya chini ya ukurasa na kutizama kwa uangalifu -- akatazama picha iliyokuwa kwenye kitabu cha wahalifu kisha akamtizama huyu mtu tena. Huyu ni wewe! Askari polisi alitamka kwa mkazo, Na inasema kuna hati iliyopo ya kukukamata!
Kama mambo yalivyoonekana, yule mwenye nyumba mwenye ghadhabu, aliyekuwa amevamia kituo cha polisi akidai haki, aliishia bila kupenda akijitambulisha yeye mwenyewe kama mhalifu aliyekuwa akitafutwa!



5

Uhalifu na ujeuri viko kila mahali, hata mahali usipoutegemea kuwepo. Upo mahali pa kazi, kwenye viwanda, vijijini mwetu, mijini na kwenye majiji.

10 – Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?



6

kwenye baadhi ya nchi maasi, mapinduzi na ujambazi ni mambo ya kawaida. Mitaa imekosa usalama. Mauaji, utekaji wa nyara, mabomu ya majasusi, ubaradhuli, ubakaji, wizi, 'wizi wa kalamu', na rushwa katika serikali vimejaza taarifa za kila siku katika nchi kote duniani.
Kwa nini uhalifu unaongezeka?
Ninini kilicho nyuma ya maongezeko yasiyo na kifani ya uvunjaji wa sheria?
Ni kitu gani ambacho kimetokea kwa dunia yetu?




7

Katika ulimwengu wa Magharibi na nchi nyingi zenye maendeleo duniani, kizazi kipya cha vijana kimeinuka - vijana wanaohoji, wasioamini na wenye kutoa changamoto.
Mungu anawaita watu wazima wawe vilelezo vya kufaa kuigwa kwa watoto wao. Watoto huiga tabia ya jamii inayowazunguka. Ni nani atakayekuwa kielelezo chao cha kiroho?



8

Akina Baba wanadanganya makazini mwao ama kwenye kodi, akina mama wanatafuta namna za kutoa mimba, na wazazi wote wa kiume na wa kike wanadanganyana.



9

Watoto wanayaona haya yote!
Na nyumba zilizovunjika huacha makovu mabaya sana!
Ni nani atakaye ingiza hisia juu ya tofauti kati ya haki na uovu kama wazazi hawatafanya hivyo na hawawezi kufanya hivyo?
Kwa hakika wazazi hawapaswi kuacha wajibu mkuu kiasi hicho kwa mashule!
Mashule mengi hayawezi kufundisha ama hata kuunga mkono maisha ya maadili. Kuna hisia fulani inayoonekana kutawala sasa ya kwamba tumekuwa kuliko viwango vya maadili ya Biblia!

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?



10

Hata baadhi ya makanisa hivi sasa yanafundisha hivyo Viwango vya Mungu vionyeshavyo haki na uovu havitumiki tena.



11

Wanasema, amri zake zimetanguliwa,



12

si za muhimu tena,



13

haziwezekani kutunza.



14

Matokeo yake, watu wengi wanatenda mambo yao tu - na jamii inavuna mavuno mengi ya ndoa zilizovunjika, watoto wasio dhibitika, na uhalifu usioweza kudhibitiwa.



15

(Fungu: Hosea 8:7)
Kwa maneno ya Hosea, nabii,
wanapanda upepo, nao watavuna tufani.


16

Lakini swali lazima liulizwe: Ni nani anayeamua kwamba jambo fulani ni sahihi ama siyo sahihi?
Je, siyo maamuzi ya maadili tu ya hata watu wema ambao mara kwa mara ni wapungufu nyakati fulani?
Kama hatuna kiwango cha jambo gani ni sahihi na lipi siyo sahihi ambacho hakitokani nasi wenyewe, twaweza kuhalalisha karibu kila kitu.

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?



17

(Fungu: Mithali 16:25)
Lakini Biblia inatukumbusha ya kwamba sisi si waamuzi wazuri wa kile kilichochema na kibaya: Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu; Lakini mwisho wake ni njia za mauti. Mithali 16:25.



18

(Fungu: 2 Timotheo 4:3,4)
Mtume Paulo alitabiri: Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe



19

watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti.




20

Nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo.
2 Timotheo 4:3,4.


21

Ndiyo, ni jambo la kusikitisha, tunagundua ya kwamba hatuupati uhuru kwa kutupilia mbali sheria! Ondoa viwango vya haki na uovu, na machafuko yatafuata mara.



22

Ukiviondoa vibao vyote vya alama za barabarani, kutakuwa na vurugu kwenye barabara ndogo na kuu.



23

Sheria ni nini?
Je, twaweza kujua kile kilicho sahihi na kisicho sahihi?

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?


24

Muda mrefu uliopita Mungu alitupatia kanuni ya jamii iliyo huru toka kwa uhalifu.
Na kama ingelikuwa ikifuatwa daima, uhalifu kamwe usingelikuwepo!
Kila mmoja angekuwa salama na mwenye furaha popote pale duniani.



25

(Fungu: Kutoka 20:2)
Wakati wana wa Israeli walipopiga kambi kando ya Mlima Sinai, Bwana alishuka kukutana nao na akasema,Mimi ni BWANA,
Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa.



26

Kwanza Mungu alijitambulisha Yeye Mwenyewe kama mkombozi wao toka utumwani.
Ndiye aliyefungua bahari ya Shamu mbele zao;
Ndiye aliyekuwa mlinzi wao.
Kwa maneno mengine, alikuwa akisema, Ninawajali. Mwaweza kuniamini.


27

Kisha akazitaja sheria zake za kimbingu ili mtu ajue namna ya kuishi kwa amani na usalama - ili ajue kile kilichokuwa chema na kile kilichokuwa kibaya.



28

Hebu tupitie kwa upesi orodha ya Amri Kumi alizozinena kileleni pa Mlima Sinai:
(Fungu: Amri 10 toka katika Kutoka 20)
Usiwe na miungu mingine ila mimi...



29


Usijifanyie sanamu ya kuchonga....usivisujudie........



30


Usilitaje bure jina la BWANA, Mungu wako,....

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?



31

Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, ...lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako.......



32

Waheshimu baba yako na mama yako.....



33

Usiue....



34

Usizini......




35

Usiibe.




36

Usimshuhudie jirani yako uongo.



37

Usitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako; wala mtumwa wake,



38

wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala chochote alicho nacho jirani yako. Kutoka 20:3 - 17.

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?



39

Watu wa Israeli waliposikiliza, walisisimka sana. Kama hayo ndiyo yaliyo kuwa mapenzi ya Mungu, walikuwa wamekusudia kuyatenda !


40

Lakini halafu, kwa kujua jinsi sisi wanadamu tulivyo wasahaulifu, Mungu aliandika Amri zote Kumi kwenye mbao mbili za mawe kwa kidole chake mwenyewe.



41

(Fungu: Kutoka 31:18)
Hapo BWANA alipokuwa amekwisha zungumza na Musa katika mlima wa Sinai,



42

akampa hizo mbao mbili za ushuhuda,



43

mbao mbili za mawe, zilizoandikwa kwa chanda cha Mungu.
Kutoka 31:18


44

Hata ingawa huu ulikuwa ni wakati wa kwanza kwa Mungu kutoa Sheria yake katika mfumo wa maandishi, ilikuwa imedumu tangu milele.

Muda mrefu kabla ya Sinai, au hata kabla ya Adamu na Hawa, kiwango cha milele, cha wema na uovu kilikuwa ndiyo msingi wa serikali ya kimbingu ya Mungu.


45

Kwa kweli, hata malaika walikuwa wakitawaliwa na amri za Mungu.
Walikuwa wamepewa uchaguzi wa ama kufuata sheria ya Mungu au kutoijali na kuiasi.

10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa  Haki na Isiyo Haki?


46

Shetani na malaika zake walichagua kufanya kitu chao wenyewe - kufanya sheria zao wenyewe.
Na uasi huu ulipelekea kufukuzwa kwao toka mbinguni.



47

(Fungu: Ufunuo 12:7-9)
Biblia yasema, Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake;



48

Nao hawakuwashinda,wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni.



49

Yule joka akatupwa, yule mkubwa,nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi  na Shetani, audanganyaye  ulimwengu wote;



50

akatupwa hata nchi,na malaika zake wakatupwa pamoja naye.
Ufunuo 12:7-9.
Lakini walikuwepo malaika waliochagua kumfuata Mungu na walisalia kuwa watii kwa sheria yake.




51

(Fungu: Zaburi 103:20)
Mhimidini BWANA enyi malaika zake,
Ninyi mlio hodari, mtendao neno lake.


52

Adamu na Hawa wallikuwa na ujuzi wa sheria ya Mungu ndani ya Edeni,  kwani walipata hisia ya aibu na hatia mara walipotenda dhambi.


53

Na wakati Kaini alipokuwa na hasira kwa sababu Mungu alikuwa ameikubali sadaka ya Habili  na kuikataa yake,  Bwana alimuuliza,

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa  Haki na Isiyo Haki?



54

(Fungu: Mwanzo 4:6,7)
...Kwa nini una ghadhabu? Na kwa nini uso wako umekunjamana?



55

Kama ukitenda vyema, hutapata  kibali? Usipotenda vyema  dhambi iko, inakuotea mlangoni. Mwanzo 4:6,7.
Sheria ya Mungu ilipasa itumike  wakati ule, kwani tunaambiwa,



56

(Fungu: Warumi 4:15)
......Maana pasipokuwapo sheria, hapana kosa. Warumi 4:15.




57

Kamusi ya  Chuo ya Webster's  New World inasema, Uasi ni ..kuvunja  sheria, wajibu, nk.; dhambi.


58

Ibrahimu alijua na alitii sheria ya Mungu  muda mrefu kabla ya sheria kutamkwa pale Sinai.



59

(Fungu: Mwanzo 26:5)
Mungu alisema angembariki Ibrahimu  na wazao wake, Kwa sababu Ibrahimu
alisikia sauti yangu,akayahifadhi maagizo yangu,na amri zangu,na hukumu zangu,na sheria zangu. Mwanzo 26:5.


60

Ni wazi, muda mrefu kabla ya Sinai, dhamiri ya Yusufu iliyokuwa na hisia kali ilimuongoza kulikabili jaribu la mke wa Potifa kwa kusema,

10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa  Haki na Isiyo Haki?

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?



61

(Fungu: Mwanzo 39:9)
.....Wala hakunizuilia kitu chochote ila wewe, kwa kuwa u mkewe.



62

Nifanyeje ubaya huu mkubwa nikamkose Mungu?
Mwanzo 39:9.


63

Yusufu alijua ya kwamba uzinzi ulikuwa dhambi; alijua kiwango cha Mungu cha wema na uovu.
Kwa msimamo kabisa alinuia kutoasi sheria takatifu ya Mungu!




64

Wana wa Israeli walikuwa wameelekezwa kumtumikia na kumtii Mungu, lakini wakati wa utekwa wao wa kikatili kule Misri, waliisahau sheria ya Mungu.


65

Baada ya kutoka Misri, majuma machache kabla hawajafika Sinai, Bwana alimkemea Musa kwa sababu wana wa Israeli walikuwa wanaivunja sheria yake kwa kujaribu kukusanya Mana siku ya Sabato:



66

(Fungu: Kutoka 16:28, 30)
BWANA akamwambiaMusa, 'Mtakataa kuyashika maagizo yangu na sheria zangu hata lini?'



67

Basi haowatu wakapumzika kwa siku ya saba. Kutoka 16:28,30.
Hivyo unaona, amri ya nne ilitambulika kabla ya Sinai.


68

Ndiyo, amri ya Mungu ni kiwango cha milele cha haki kwa ulimwengu wote.
Na kwa kweli, hivi inatushangaza ya kwamba Mungu anayo sheria inayotawala Ufalme Wake?

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?



69

(Fungu: 1 Wakorintho 14:33,40 HNKK)
Mtume Paulo aliandika: Maana Mungu
si Mungu wa fujo.....



70

Lakini yote yafanyike kwa heshima na kwa utaratibu.
1 Wakorintho 14:33,40.


71

Hakuna serikali yenye utaratibu iwezayo kuwepo bila sheria. Hakuna jamii yenye utulivu, furaha, na usalama iwezayo kuendelea hivyo bila sheria. Viumbe vya asili vyenyewe vina sheria; hata watoto hawawezi kucheza mchezo wowote bila sheria!




72

(Fungu: Warumi 2:13)
Biblia yasema, Kwa sababusio wale  waisikiao sheria
waliowenye haki mbele
za Mungu,  bali ni wale waitendao sheria
watakaohesabiwa haki,



73

,  bali ni wale waitendao  sheria  watakaohesabiwa haki,  Warumi 2:13.
Unaona, si tu muhimu kwetu  kuzijua amri za Mungu, lakini pia twapaswa kuitikia.



74

(Fungu: Yohana 14:15)
Yesu alisema,  Mkinipenda ,
mtazishika amri zangu.  Yohana 14:15.
Kwa kweli, Yesu, akinukuu toka kwa Agano la Kale,alielekeza  ya kwamba upendo ni msingi wa kutunza amri zote.



75

(Fungu: Mathayo 22:37-40)
.....Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote.

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?



76

Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza.



77

Kisha Yesu akasema, Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii,'Mpende jirani yako kama nafsi yako.'



78

Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii.
Mathayo 22:37-40.


79

Kama kweli tunampenda Mungu kwa mioyo yetu yote, kwa akili zetu zote na kwa roho zetu zote,




80

ni wazi ya kuwa tutauonyesha upendo huo kwa kutunza amri nne za kwanza:



81

Mungu atakuwa namba moja katika maisha yetu



82


Ibada yetu itakuwa kwa ajili yake mwenyewe



83

Tutaliheshimu na kulicha Jina Lake Takatifu

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?



84

Tutakuwa na shauku ya kutunza miadi yetu naye kila Sabato



85

Na kama kweli tunawapenda watu wenzetu kama tujipendavyo wenyewe, kwa hakika tuta



86

waheshimu na kuwastahi wazazi wetu



87

Tutathamini Uhai



88

Tutatunza maadili



89

Tutaheshimu mali  za wenzetu



90

Tutakuwa waaminifu  katika mahusiano yetu  kila mmoja na  mwingine



91

Hatutatamani kile ambacho ni mali ya mwingine

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?


92

Makadirio yanaonyesha ya kwamba zaidi ya sheria milioni 35 zimetengenezwa na wanadamu ili kushughulikia tabia.


93

Lakini katika Amri Kumi, Mungu aliandika kanuni za mwenendo ambazo kwa kweli hutawala mwenendo wote wa binadamu.
Mungu peke yake ndiye angeweza kuandika sheria timilifu kiasi hicho. Biblia yasema:



94

(Fungu: Zaburi 19:7)
Sheria ya BWANA ni kamilifu, Huiburudisha nafsi...
Zaburi 19:7,




95

(Fungu: Zaburi 19:11)
.....Katika kuzishika kuna thawabu kubwa.



96

Msomi wa Biblia aitwaye August Strong aliandika:Sheria ni nakala tu ya asili ya Mungu.



97

Leo tunasema, Amri Kumi nisura ya tabia ya Mungu - tabia isiyobadilika!


98

Unaona, badiliko lolote katika sheria ya Mungu lingeifanya iwe pungufu - isiwe kamilifu.
Kwa kuwa sheria kamilifu, haiwezi kubadilishwa.

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?



99


(Fungu: Luka 16:17 HNKK)
Huo ndiwo ukweli ambao Yesu aliuzungumzia aliposema:Lakini ni rahisi zaidi mbingu na dunia kupita, kuliko hata herufi moja ya Sheria kufutwa.


100

Lakini, wasema, Daima nimejisikia ya kwamba Amri Kumi zimeizuia furaha yangu - ni kama zimekuwa zikinikinga kama kwa kuniweka ndani ya ua.
Mungu hakuwa na mpango ya kwamba sheria yake iwe mzigo kwa mwanadamu au imzuie kupata furaha yake.


101

Kinyume chake, Mungu alikusudia ya kuwa iwe ukuta wa ulinzi unaotukinga toka katika huzuni na hatia.
Alikusudia ya kwamba sheria yake ihakikishe ya kuwa kila mtu anaupata uhuru na usalama kila mahali.



102

(Fungu: Kumbukumbu 5:29)
BWANA alisema, Laiti wangekuwa
na moyo kama huu ndani yaosikuzote, wa kunicha,na kushika amri zangu siku zote,



103

wapate kufanikiwa wao na watoto wao milele!
Kumbukumbu 5:29.


104

Kama jinsi tujengavyo kingo za barabara katika madaraja na barabara zilizo milimani ili kutulinda na hatari, Mungu alitupatia sheria yake ili kutulinda sisi na katika barabara ya maisha.



105

(Fungu: Warumi 3:20)
Lakini ipo sababu nyingine ya Mungu kumpa mwanadamu sheria yake:.......kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria.

10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?



106

(Fungu: Warumi7:7)
Na Paulo alisema,........singalitambua
dhambi ila kwa sheria;



107


Kwa kuwa singalijua kutamani, kama torati isingalisema, 'Usitamani.'
Warumi 7:7.


108

Kisa kinaelezwa juu ya binti mfalme ambaye alikuwa ameambiwa na kuaminishwa na raia wa ufalme ya kuwa hakuna aliyemzidi kwa urembo.
Hata hivyo, siku moja mfanyabiashara alikuja kwenye kijiji chake na kumuuzia kioo.
Alipojitizama katika kioo alichukizwa na muonekano wake na kuamua kukivunja kioo vipande vipande!


109

Sheria ya Mungu ni kama kioo, na tunapojiangalia, kama yule binti mfalme, twaweza tusipendezwe na kile tunachokiona,


110

lakini kuvunja sheria au kutoijali hakutabadili hali yetu.


111

Sheria inasonda dhambi yetu!
Ni mwongozo wa kutusaidia kuwa na furaha, kuishi maisha yasiyo na hatia kama tukifuata maelekezo yake yaliyo katika sheria yake.

# 10 – Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?



112

Sheria haiwezi kutupa nguvu kushinda dhambi au kuondoa hatia.
Hakuna kiasi cha wema tuwezacho kufanya wakati ujao kiwezacho kuondoa dhambi iliyotendwa wakati uliopita.
Sasa je, twawezaje kupata msamaha?
Twawezaje kuokolewa toka katika adhabu ya kuvunja sheria, ambayo ni mauti?




113

Katika malango yenyewe ya Bustani ya Edeni, Mungu aliweka kumbukumbu ionekanayo dhahiri ya kwamba kutotii huleta mauti - ama kwa asiyetii au kwa anayemwakilisha hata kama hana hatia.
Mwana-Kondoo alipaswa atolewe ili kuonyesha imani ya mdhambi katika mpango wa Mungu wa kumwokoa mwanadamu.




114

Hii ilikuwa njia ya Mungu ya kumsaidia Adamu kuelewa jinsi gani Mwana wa Mungu lazima afe ili kukidhi mahitaji ya sheria iliyovunjwa.
Kristo, Mwana - Kondoo wa Mungu, angechukua adhabu ya mwanadamu, na kuteseka kwa hata mauti yake.



115

Unaona, sheria isingeweza kumuokoa yeyote toka dhambini.




116

(Fungu: Wagalatia 3:21)
Mtume Paulo alisema,
.....kama ingalitolewa sheria iwezayo kuhuisha,




117

yakini hakiingalipatikana kwa sheria.
Wagalatia 3:21.
Siyo sheria iletayo msamaha na wokovu - ni neema ya Mungu!
Ni kwa kupitia kwa neema ya Kristo tu tunaweza kuupata uzima wa milele.

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?



118

(Fungu: Warumi 6:23)
Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti;
bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.
Warumi 6:23.
Wokovu hauwezi kupatikana kwa kutunza sheria:



119

(Fungu: Waefeso 2:8,9)
Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyohaikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu,



120

wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.
Waefeso 2:8,9.


121

Kama tuliokolewa kwa neema, je, tuko huru tena kuishi maisha ya ukaidi? KAMWE!



122

(Fungu: Warumi 6:1,2)
Paulo aliandika: Tusema nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi?



123

Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?
Warumi 6:1,2.
Wokovu unatolewa kwa wale wanaotaka kuokolewa toka dhambini na wanataka kuwa sehemu ya ufalme wa Mungu.



124

Wapo wale wanaoamini ya kuwa sheria ya Mungu ilitupiliwa mbali. Litafakari hilo kwa muda mfupi. Kama hakuna sheria, hakuna dhambi, kwa sababu dhambi ni uasi wa sheria.

# 10 – Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?



125

Kama hakuna sheria, hatuhitaji neema, kwa sababu neema ni rehema ya Mungu iliyopo kwa ajili yetu tunapokuwa tumevunja sheria ya Mungu.



126

Kama hatuhitaji neema, twaweza kutupilia mbali msalaba.



127

Kama hakuna hitaji la msalaba, ni wazi hatuhitaji Mwokozi.
Kama unatupilia mbali sheria, unatupilia mbali pia ...Dhambi, Neema, Msalaba, na Mwokozi. Ni jinsi gani basi tunamhitaji Mwokozi aliyekufa msalabani ili kutuokoa kwa neema Yake ili deni la dhambi lilipwe, kwa sababu tumevunja sheria yake. Hii ni injili. Neema haitupilii mbali sheria ya Mungu. Kwa neema ya Mungu tunatamani kutunza sheria ya Mungu.


128

Kama mfungwa anayesubiri kufa


129

anapokea msamaha na kuwekwa huru, je, hii ina maana sasa yuko huru kuishi maisha yasiyojali sheria?
Kufanya mambo yake tu? La hasha!


130

Kwa sababu alisamehewa, anapaswa kujisikia sasa kwa uzito kuliko wakati wowote uliopita wajibu wake wa kuziheshimu sheria za nchi.

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?



131

Muhimu zaidi, sheria ya Mungu inaonyesha dhambi na inatusaidia kuhisi hitaji la Mwokozi. Tunapomkubali Kristo kama Mwokozi wetu na Bwana, anatupatia msamaha na pia uwezo wa kuzitunza amri zake, kwani ameahidi:



132

(Fungu: Waebrania 8:10)
.....Nitaweka sheria zangu katika nia zao, Na katika mioyo yao nitaziandika;.....


133

Ni rahisi kutenda jambo upendalo kulitenda, sivyo? Na hilo ndilo ambalo Bwana aliwaahidi wale wanaochagua kumfuata.
Ataandika sheria yake katika mioyo yao ili wapende kuitunza.



134

Hiyo ndiyo njia pekee mwanadamu ataweza kumtii na kumfuata Mungu.
Ilikuwa kwa sababu ya upendo wake kwa Baba Yake ndiyo maana Kristo aliweza kuzitunza amri,



135

(Fungu: Yohana 15:10)
kwani alisema, ...kama vile mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake.
Yohana 15:10



136

(Fungu: Yohana 14:15)
Na Yesu anatuomba tuonyeshe upendo wetu kwake kwa kuzitunza Amri zake: Mkinipenda, mtazishika amri zangu.


137

Kielelezo kikuu kuliko vyote cha upendo na utii kwa mapenzi ya Mungu kilidhihirika wazi kabisa usiku mmoja wenye baridi, tena giza chini ya mzeituni mkuukuu katika bustani.
Akiwa na matone ya damu yakidondoka toka usoni pake, Mwana wa Mungu alisali,

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?



138

(Fungu: Mathayo 26:39)
...Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke; walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe....
Mathayo 26:39.
Hatima ya jamii ya mwanadamu ilikuwa ikining'inia katika mizani - dunia yenye hatia ilikuwa iokolewe ama ipotee.


139

Je, huyu Mgalilaya angeweka pembeni tamaa yote ya kuishi na ridhaa ya kibinadamu pembeni na kufa Kalvari?
Angeweza kupangusa jasho toka kipajini kwake na kusema, Acha mdhambi ataabikie matokeo ya dhambi zake mwenyewe.


140


Au angebeba msalaba kwa ajili yetu.
Alipofanya uchaguzi ule alikufa kwa ajili yetu.
Alimwaga damu yake. Alikufa mauti yaliyokuwa yetu ili tupate kuishi milele pamoja naye.


141

Kwa sababu Kristo alilipa gharama kwa ajili ya dhambi zetu, twaweza kupokea msamaha kupitia kwa kafara yake sasa hivi.


142

Msalaba wa kale katika kilima kilichoitwa Mlima Kalvari ni kumbukumbu ya milele ya gharama ambayo Mungu alikuwa tayari kuilipa ili kuridhisha dai la sheria iliyovunjwa na kumwokoa mwanadamu aliye na hatia.


143


Kama sheria ya Mungu ingetanguliwa au kubadilishwa, Yesu asingehitaji kufa.
Kalvari isingelikuwa muhimu.

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?



144

Mungu asingeweza kupuuzia dhambi za mtu mwenye hatia!



145

Asingeweza kuibadili sheria yake.


146

Hivyo mtu mwenye dhambi alimhitaji Mwokozi.
Na Mungu ashukuriwe kwa upendo wake kwa kukubali kumtoa Mwana wake wa pekee ili afe kama badala yetu!



147

(Fungu: Yohana 3:16)
Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee,




148

ili kila amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.
Yohana 3:16.



149

Kitabu cha Ufunuo kinaeleza namna ya wtu walio tayari kumpokea Yesu ajapo mara ya pili na kwenda naye nyumbani pamoja naye ili kuutumia umilele katika lile Jiji la Mbinguni.



150

(Fungu: Ufunuo 14:12)
Mungu anasema hili kuwahusu:
Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu.
Ufunuo 14:12.

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?



151

(Fungu: Ufunuo 14:14)
kwenye fungu la 14, Mungu anasema,Kisha nikaona, na tazama, wingu jeupe, na juu ya wingu hilo ameketi mmoja, mfano wa Mwanadamu,



152

mwenye taji ya dhahabu juu ya kichwa chake, na katika mkono wake mundu mkali.
Haya ni maelezo ya Bwana ajapo kuvuna dunia.


153

Katika unabii mkuu ambao Yesu alimpatia Yohana katika kitabu cha Ufunuo kuhusu historia ya kanisa, anasema ya kwamba masalio wa sehemu ya kweli ya mwisho ya kanisa la Mungu hapa duniani inaelezwa hivi:



154

(Fungu: Ufunuo 12:17)
Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia,



155

wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu;...
Ufunuo 12:17.


156

Hapo umeipata ipo katika kitabu cha mwisho cha Biblia!

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?


157

Watu wa Mungu wanampenda Muumbaji wao na Mwokozi wao sana kiasi ambacho wanataka kutenda yote ambayo anawaomba ama anatamani wakitende.
Wanataka waonyeshe upendo wao kwake kwa kutenda mapenzi yake.
Wanatambua ya kwamba mapenzi yake yamo katika Amri zake.
Wanamuitikia Yeye kwa utii ambaye alitenda kiasi kikubwa kiasi hicho ili kuwaokoa toka dhambini.
Hali akiwa amenyoosha mikono Yesu anaita, Njoo! Angali akituita!
Anataka kutupatia uwezo wa kuishi kwa ajili yake.



158

(Fungu: Ufunuo 22:17)
Anataka kutuosha dhambi zetu.
Sauti yake inayosihi bado inaita, ....Na Roho na Bibi-arusi wasema, Njoo! Naye asikiaye na aseme, Njoo! Naye mwenye kiu na aje; na yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure. Ufunuo 22:17.


159

Mhubiri alitembelea nyumba moja katika moja ya viunga vya jiji kubwa. Mama wa nyumba alikuwa mkarimu lakini akiwa na msimamo wake: Sivutiwi na Biblia au Ukristo - hata kidogo, alisema, lakini kama mtajali kiasi cha kuja tena jioni moja, mtamkuta mume wangu anavutiwa sana kujifunza zaidi juu ya hiyo. Ningependa sana ninyi mrejee ili mkutane naye. Mhubiri alirejea siku moja ya Jumamosi jioni. Kwa sababu haikuwa siku ya kazi, mume wa mwanamke huyu alikuwa amedumisha ile desturi ya kutumia muda wa mchana akicheza kamari na rafiki zake hotelini. Alikuwa katika hali ya kujihisi kuzungumza sana, lakini akiwa na msukumo wa yule roho amfanyaye mtu kuzungumza zaidi sana hali akiwa amesema machache sana.
Ninayo Biblia, alisema. Lazima uione Biblia yangu. Mama aliiweka kwenye sanduku nilipoondoka nyumbani ili nikaoe. Biblia yangu iko wapi, mpenzi? Msako mkali wa muda mrefu ili kuipata Biblia uliishia katika kupatikana kwa kijitabu cha sala. Hakuipata Biblia kabisa.


160

Lakini ulevi wa pombe halikuwa tatizo pekee kwake. Kamari ilikuwa ikimuangamiza, na alikuwa pia mvutaji wa sigara mfululizo. Haya, pamoja na tabia zingine, zilikuwa zimepanua mwanya sana kati yake na mkewe. Alikuwa ameshafungasha mifuko yake, tayari kuondoka nyumbani.
Walikuwa katika mpango wa kuachana. Mambo yalikuwa katika sura mbaya. Lakini tamaa kubwa kwa ajili ya jambo fulani lililo bora zaidi ilikuwa ndani ya moyo wa mtu yule. Hata kinywaji chenye nguvu hakikuweza kuizamisha. Mhubiri alifanya miadi kukutana naye tena Jumatatu jioni, na wakati huu, mfuatano wa mafundisho ya Biblia ya kila juma ukaanza.

# 10 - Ni Kitu Gani Kilichotokea kwa Haki na Isiyo Haki?


161

Juma baada ya juma, masomo toka kwa Neno la Mungu yalipowakilishwa, mwito wa msalaba ukaanza kazi yake. Kristo, kwa Roho wake, alikuwa akienda sasa katika nyumba nyingine yenye uhutaji. Ilikuwa jioni ya ajabu wakati yule mtu aliposema, Sharti ukae muda mrefu zaidi kidogo usiku huu. Mke wangu ataenda kupumzika sasa. Je, wewe na mimi hatuwezi kuwa na gumzo kidogo pamoja, sisi wanaume?


162

Kisha, kwa uwazi, alifungua kwa mhubiri kisa cha kusikitisha cha maisha yaliyoanza vyema. Alikuwa amezaliwa katika nyumba ya Kikristo yenye nguvu, lakini alikubali misukumo ya ujana ikamtawala. Mwanampotevu mwingine alikuwa amekwenda katika barabara, katika mashimo yaliyo na kina yaliyomuongoza tu hadi katika nchi ile ya mbali. Kanisa lilisahaulika mara, Biblia ikapuuzwa. Kristo alitajwa tu katika viapo vya kipuuzi.

Lakini ninachotaka kujua, mhubiri, ni - hivi umenifanyia nini mimi? Sijatumia kinywaji wala sijacheza kamari kwa muda wa majuma manne sasa. Wala sijaapa au kutumia jina la Mungu bure kwa muda huu wote. Kisha hali akitupa kwa mahali pa kukokea moto nusu ya sigara iliyovutwa, aliendelea. Sigara zangu zimekosa ladha kwangu. Ninajua niko mbioni kuacha.

Lakini lipo jambo la kushangaza zaidi ya yote hayo. Mke wangu ameifungua mizigo yake. Alilifanya hilo majuma matatu yaliyopita sasa.

Asubuhi ya leo alinifuata hadi kwenye lango na, kwa mara ya kwanza baada ya miaka mingi, alinibusu akiniaga.

Ndiyo alifanya hivyo! Nilishangaa, mhubiri, na nilishangaa zaidi alipotabasamu huku akiniangalia na kusema, 'Ninampenda Jack mpya.'

Sasa, ni kitu gani kimetokea kwangu? Nina hakika kina uhusiano na mafundisho yetu ya Biblia ya Jumatatu jioni.


163

Mhubiri akasema,Sijafanya chochote peke yangu, lakini ninaamini ya kwamba Biblia yaweza kueleza yote hayo. Kisha, akifungua katika 2 Wakorintho 5:17, alianza kusoma: Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya.
Polepole Jack mpya alisoma fungu mwenyewe. Kiumbe kipya - Jack mpya! Hivyo ndivyo ulivyo! Jack mpya! Na kama ungelinifahamu mimi, mhubiri, hivyo ndivyo nilivyo kabisa usiku wa leo.
Ndiyo, marafiki, Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu wa mbinguni, na yeye pekee anazo nguvu za kubadili wanaume na wanawake.
Huyu Yesu anataka kubadili maisha yako pia. Anataka kukupatia neema na uwezo wa kutunza sheria yake. Waweza kujihisi mdhaifu lakini Yesu ana nguvu. Haidhuru umetenda nini wakati uliopita, Yesu atakusamehe na kukutakasa. Atakupatia nguvu zake ili uweze kuishi maisha mapya. Usiruhusu chochote kikurudishe nyuma. Yesu anakuita. Anakuita urejee nyumbani. Je, ungependa kupiga magoti kwa utulivu na kusema, Bwana, ndiyo, nakuja. Sahau juu ya mkutano wa watu. Mfikirie Yesu peke yake unapopiga magoti. Sema, ndiyo, Yesu, ninakuja. Ninakuja sasa hivi.
Hebu tuombe.

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi

11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi



1

Jinsi ya Kuridhisha Tamaa Yako Ya Ndani.


2

Ipo hadithi ya mwanabaiolojia, Thomas Huxley, aliyekuwa amewasili katika jiji akiwa amechelewa hali akitarajiwa kutoa mhadhara. Alirukia gari ndogo ya abiria, ambayo wakati huo ilikuwa ni gari ya kukokotwa kwa farasi, na kisha akapaza sauti yake kwa mwendeshaji, Kasi sana!


3

Mwendeshaji akavuta kamba sawa sawa kwa utii na gari likawa likienda likirukaruka katika mitaa kwa kasi sana. Huxley aliyeshikwa na kihoro aliketi kitini pake kwa sekunde moja, huku akiridhika vikubwa, kisha ghafla akasimama kwa kugutuka. Akaita, Sikia, sikia unajua ninakotaka kwenda?
La, mheshimiwa, Mwendeshaji alijibu, Lakini naendesha kwa kasi kadiri niwezavyo.


4

Watu wengi kiasi cha kushangaza wapo kwenye kasi siku hizi. Kuna mengi yanayoendelea katika maisha yao. Daima wanakwenda mahali fulani kwa kasi. Lakini ukweli ni kwamba, wengi sana kwa kweli hawajui wanakokwenda; hawajui wapi maisha yao yanakoelekea.


5

Ni kwa sababu hii Mungu anatoa wito Wake wa mwisho katika kitabu cha mwisho cha Biblia, Ufunuo. Katika sura ya 14, fungu la 7, mtume Yohana anaita ulimwengu unaosubiri kuja kwa Yesu katika maneno haya......



6

(Fungu: Ufunuo 14:7)
....Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja;

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi



7

Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji.
Ufunuo 14:7.
Lakini kama unayo ramani ya mji wako na unajaribu kuifuata ili kupata mahali, na ramani yako haiko sahihi, inafanya tofauti kubwa!


8

Msujudie nani? Msujudieni Yeye aliyezifanya mbingu na nchi. Msujudieni Muumbaji wa kila kitu. Mungu anatualika tupunguze mwendo ili tutafakari juu ya mahali tuendapo.
Tunapoelewa ya kwamba tuliumbwa na Mungu, inatupatia hisia ya kutambua kwa nini tupo hapa na tunakwenda wapi.



9

Lakini leo, watu wamesahau ya kwamba Mungu ni Muumbaji wa ulimwengu, ulimwengu wetu, na kila kitu na kila aliyemo ndani yake.
Baadhi ya watu husema waweza kuiamini Biblia bila mashaka yoyote kabisa. Wengine husema huwezi. Ni nani aliye sahihi?



10

Leo, mamilioni wanafikiri tunatokana na uibukaji tu. Baada ya miaka mabilioni tulikuwa toka kwa chembe hai moja moja hadi kuwa wanyama wa baharini kisha kuwa wanyama wa nchi kavu hadi kuwa wanadamu.
Wanafikiri kila kitu kilitokea kwa nasibu tu au kwa ajali tusiyoielewa sawasawa.


11

Lakini je, wajua ya kwamba Mungu alitupatia ishara ya kazi Yake kama Muumbaji wetu?
Alitupatia kitu ambacho kingetukumbusha kila juma ya kwamba alituumba, dunia yetu au ulimwengu?
Kama Biblia ni ya kweli, uzima wako wote wa milele unategemea kama unaiamini na kuikubali. Kile unachokiamini kuhusu Biblia kinafanya tofauti yote katika yale unayoamini juu ya Mungu.

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi



12

Kwa kweli, alitupatia huu ukumbusho wa kila juma pale pale mwisho wa juma la  Uumbaji.
Lakini karibia dunia nzima imesahau huo ukumbusho ni nini.



13

Na bila ya ukumbusho huo, wengi wamesahau ya kwamba Mungu ndiye aliyeuumba ulimwengu.
Hivyo katika wakati wetu tunatuma watu kwenda mwezini  kutafuta vidokezi vionyeshavyo jinsi gani dunia yetu ilianza.


14

Tunazama mbali katika anga kwa kutumia darubini zenye nguvu,  tukitafuta vidokezo vionyeshavyo jinsi gani ulimwengu ulianza.
Hivyo hebu tuangalie kitabu hiki kikuu-Biblia-kiitwacho pia Neno la Mungu-na tuone kama twaweza kupata kithibitisho kionyeshacho kama ni kweli au la-kama yaweza kuaminiwa au la.


15

Kwa nini jitihada yote hii na gharama-shauku kali hivi ya nini? Kwa sababu tunahitaji majibu kwa maswali yetu yaliyo makubwa zaidi. Je, tupo wenyewe katika ulimwengu? Tulifikaje hapa? Kwa nini tupo hapa? Na tunakwenda wapi? Hivyo utafiti unaendelea. Bado pamoja na hayo yote, majibu yapo hapa hapa mbele yetu. Lakini sisi ni dunia ambayo imesahau-hatukumbuki tena tulikotokea!



16

Kwa ulimwengu ambao umesahau, Mungu anasema, Kumbuka-kumbuka ya kwamba Mimi ndiye Muumbaji wako. Na ili kukusaidia kukumbuka, nimekupa  dalili - ishara!



17


Katika wakati huu wa historia uibukaji unapofundisha ya kwamba sisi ni matokeo ya nasibu, Mungu anasema,
Hukuibuka-Nilikuumba wewe!

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi




18

Lakini baadhi waweza uliza, Ni ishara gani hii au alama inayotukumbusha ya kwamba Mungu alituumba?
Je, unakumbuka tulipojifunza juu ya kile Mungu alichoumba kila siku ya juma la Uumbaji?




19

(Fungu: Zaburi 33:8,9)
Uumbaji ulikuwa wa kushangaza! Aliufanyaje-na tena kwa haraka kiasi hicho? Biblia inatoa jibu: Nchi yote na imwogope BWANA, Wote wakaao duniani na wamche.




20

(Sabato) Maana Yeye alisema, ikawa; Na Yeye aliamuru, ikasimama.
Zaburi 33:8,9



21

Hatuwezi kuelewa ni vipi, lakini Mungu aliweza kuvifanya vitu vyote vikawepo kwa Neno Lake. Neno la Mungu, liwe limenenwa, limeandikwa katika Biblia linauwezo wa kuumba na lina nguvu!
Makubaliano haya yanaweza tu kuelezewa na utambuzi ya kwamba Mungu alitoa Kitabu hiki kwetu ili aweze kuwasiliana nasi mapenzi yake.




22

(Fungu: Mwanzo 2:1)
Basi mbingu na nchi zikamalizika, na jeshi lake lote.
Mwanzo 2:1.



23

Katika siku sita Muumbaji aliufanya ulimwengu ukawepo, akauvisha vichaka na miti, maua na mito.



24

Alileta mwanga wa jua na machweo ya kuvutia na mwezi unaopendeza kuangalia wakati wa usiku.

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi


25

Lakini bora kuliko yote, Aliumba watu wawili wakamilifu. Ni heshima y a ajabu kiasi gani! Kuumbwa katika sura ya Muumbaji! Waliumbwa kuwa watawala juu ya dunia na vyote vilivyokuwamo



26

(Fungu: Mwanzo 1:27)
Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba.
Mwanzo 1:27.


27

Lakini, Mungu alikuwa hajamaliza bado! Alikuwa na jambo moja zaidi alilotaka kulitenda. Angalia kwa makini kile Biblia inachokisema kilitokea siku iliyofuata-siku ya saba ya uumbaji:




28

(Fungu: Mwanzo 2:2-4)
Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya;



29

akastarehe siku y a saba , akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya.




30

Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kuifanya.




31

Hivyo ndivyo vizazi vya mbingu na nchi zilipoumbwa.
Mwanzo 2:2-4.


32

Mungu pekee aweza kufanya kitu kuwa kitakatifu, na Biblia yasema Aliitakasa siku ya saba.

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi



33

Kutakasa kitu fulani ni kukiweka pekee kwa matumizi matakatifu.
Mungu aliiweka Sabato pembeni ya siku zingine zote.
Iliwekwa pembeni kama takatifu - ikiwa imetakaswa kikamilifu kwa ajili yake.
Wapo baadhi ya watu ambao wanashangaa - siku inafanya tofauti gani? Labda kielelezo hiki kitasaidia.


34

Kwenye harusi mwanamke mmoja hutakaswa kwa ajili ya mwanamume mmoja. Hebu tuseme ni siku yako ya harusi. Umesisimka sana. Umeitazamia siku hii kwa muda fulani.


35

Hebu tuseme yule mkeo mtarajiwa anao dada sita. Wakati wa sherehe ya harusi mwanamke mmoja anaunganishwa na mwanamume mmoja. Anawekwa pembeni. Yeye hapo si tena mmoja kati ya saba. Anatakaswa. Anawekwa wakfu kwa mumewe katika ndoa.


36

Habari gani kama baada ya ndoa, mmoja kati ya dada za mkeo akisema, Kwani kuna tofauti gani? Mmoja kati ya saba anafaa. Yeyote kati ya dada saba ni sawa tu kama mwingine.
Ungesemaje? Je, kuna tofauti?


37

Je, habari gani wewe Mama, inaleta tofauti yoyote kwa bibi harusi?
Hakika!
Kama mume, ungesema, Bibi harusi wangu alichaguliwa, akatakaswa, akawekwa pembeni, wakfu kwa ajili yangu!
Hivyo Mungu alichukua siku ya kawaida, yenye masaa 24 - siku ya saba - aliichagua, akaitakasa, akaiweka pembeni, wakfu kwa ajili yake Mwenyewe.
Sabato imebarikiwa, ni siku ambayo imetakaswa.
Kufuatana na neno la Mungu, si siku yoyote bali siku ya saba.

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi



38

(Fungu: Marko 2:27,28)
Basi, Yesu akawaambia, Sabato iliwekwa kwa ajili ya binadamu na si binadamu kwa ajili ya Sabato! Basi, Mwana wa Adamu ni Bwana hata wa Sabato pia.



39

Kwa hiyo, Mwana wa Adamu ni Bwana pia wa Sabato. Marko 2:27,28.


40

Mungu alitupatia Sabato ili kwamba tuwe na muda wa kukumbuka ya kwamba hatukuibuka tu. Mungu alimuumba na vyote vinginevyo katika ulimwengu wa ajabu kwa siku sita!
Huu ulipaswa kuwa wakati mtakatifu ambapo binadamu na Muumbaji wake wangefanya upya maagano yao ya upendo na ibada pamoja kila juma.
Kila juma, binadamu alipaswa kukumbuka ya kwamba Mungu aliumba mbingu na nchi kwa siku sita na kupumzika siku ya saba.


41

Mungu alimuomba mwanadamu akumbuke wakati aliandika kwa kidole chake mwenyewe ile sheria. Amri ya nne iko katikati ya ile Sheria takatifu ya Mungu
Alimwambia mwanadamu akumbuke siku hii, kwani katika siku sita alikuwa ameumba nchi, bahari, na chemchemi za maji.



42

Kama Sabato ingekuwa imetunzwa wakati wote kama kumbukumbu ya Uumbaji, kusingekuwa na muumini wa uibukaji, mpagani, au asiyeamini leo. Wangekuwa wamekumbushwa kila juma juu ya mizizi yao na uhusiano wao na Muumbaji wao!
Dhambi ilipoendelea kuongezeka juu ya nchi, mwanadamu alisahau alipotokea na kwa nini alikuwa hapa na alikuwa akielekea wapi.
Wakati hili lilipotokea, alisahau pia jinsi gani apaswa kuishi.

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi



43

Ulipofika wakati wa Musa, watu wa Israeli walikuwa wamekaribia kusahau kabisa juu ya Mungu wao. Walikuwa wamezamia katika kuabudu miungu iliyotengenezwa na mwanadamu!



44

Mungu kwa muujiza aliwaokoa toka kwa adui zao na kuwaongoza kupitia katika jangwa katika njia ya kwenda kwenye Nchi ya Ahadi. Katika jangwa, alitenda mambo mawili ili kuwaonyesha kile alichotaka wakifanye kihusianacho na Sabato ya siku ya saba aliyokuwa amewaumbia katika juma la kwanza la historia ya dunia hii.



45

Kwanza, Mungu aliwakumbusha ya kwamba aliwajali na kwamba aliwaongoza toka Misri.
Wasingeweza kubeba chakula cha kutosha.
Mara walianza kunung'unika kwa sababu walikuwa wameishiwa.
Hawakuonekana kushukuru miujiza yote na wema ambao Mungu aliwaonyesha, lakini Mungu mwenye upendo alitoa chakula kwa ajili yao!



46

(Fungu: Kutoka 16:4,5)
Ndipo Bwana akamwambia Musa, Tazama, mimi nitawanyeshea ninyi mvua ya mkate kutoka mbinguni;



47

Na hao watu watatoka nje na kuokota kila siku sehemu ya siku;



48

ili nipate kuwajaribu, kwamba watakwenda katika sheria yangu, ama sivyo.
Kutoka 16:4
Mkate unaonenwa hapa unafahamika zaidi kama mana.

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi





49

Kisha itakuwa siku ya sita, ya kwamba watayaandaa hayo watakayoyaleta ndani,




50

nayo yatakuwa ni mara mbili kuliko wayaokotayo kila siku.
Kutoka 16:5




51

(Fungu: Kutoka 16:6)
Musa na Haruni wakawaambia wana wote wa Israeli,



52

Jioni ndipo mtakapojua ya kuwa BWANA amewaleta kutoka nchi ya Misri.
Kutoka 16:6




53

Mana ilikuja usiku umande ulipotanda. Asubuhi baada ya umande kupotea mana ilikuwa ikiifunika nchi.
Watu walitoka na kuikusanya masaa ya mapema asubuhi na ilipofikia adhuhuri mana iliyokuwa imesalia ilitoweka.
Lakini subiri-tambua kilichotokea katika siku ya sita ya juma:



54

(Fungu: Kutoka 16:21,22)
Basi wakaokota asubuhi baada ya asubuhi, kila mtu kama ulaji wake ulivyokuwa;



55

Na jua lilipokuwa kali, iliyeyuka.

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi



56

Basi ikawa siku ya sita wakaokota kile chakula sehemu maradufu, kila mtu pishi mbili;



57

Na wazee wote wa mkutano wakaenda na kumwambia Musa.



58

(Fungu: Kutoka 16:23)
Ndilo neno alilonena BWANA kesho ni starehe takatifu, Sabato takatifu kwa BWANA;



59

Okeni mtakachooka, na kutokosa mtakachotokosa; na hicho kitakachosalia jiwekeeni kilindwe hata asubuhi.
Kutoka 16:21- 23.



60

(Fungu: Kutoka 16:25,26)
Kuhusu siku ya saba: Musa akasema, Haya, kuleni hiki leo; kwa kuwa leo ni Sabato ya BWANA; leo hamtakiona nje barani.



61

Siku sita mtaokota; lakini siku ya saba ni Sabato, siku hiyo hakitapatikana.'
Mafungu 25, 26.


62

Watu wengi walitenda kama Mungu alivyoamuru, lakini baadhi ya watu walitoka siku ya Sabato ili kukusanya mana.
Tazama alichokisema Mungu juu ya hilo!



63

(Fungu: Kutoka 16:28-30)
BWANA akamwambia Musa, 'Mtakataa kuyashika maagizo yangu na sheria zangu hata lini?

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi



64

Angalieni, kwa kuwa BWANA amewapa ninyi hiyo Sabato, kwa sababu hii huwapa siku ya sita chakula cha siku mbili;



65

Kaeni kila mtu mahali pake, mtu awaye yote asiondoke mahali pake kwa siku ya saba.'



66

Basi hao watu wakapumzika kwa siku ya saba. Kutoka 16:28-30.


67

Sabato ilisimikwa wakati wa uumbaji na iliadhimishwa na watu wa Mungu kabla hawajafika Sinai, mahali Mungu alipowapatia Amri Kumi.


68

Katika mwezi wa tatu wa safari ya Kutoka Misri, Mungu aliwaleta watu kwa Mlima Sinai, na pale akatokea kwa Musa na kumpa ujumbe ili aupeleke kwa watu:



69

(Fungu: Kutoka 19:5,6)
Sasa basi ikiwa mtaitii sauti yangu kweli kweli, na kulishika agano langu,



70

hapo ndipo mtakapokuwa tunu kwangu kuliko makabila yote ya watu; maana dunia yote pia ni mali yangu.



71

nanyi mtakuwa kwangu ufalme wa amani, na taifa takatifu.

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi



72

Hayo ndiyo maneno utakayowaambia wana wa Israeli.
Kutoka 19:5,6.


73

Mungu alikuwa ametoa zawadi ya neema kubwa kwa watu wake.
Kama wangetii  Sheria zake na amri, wangekuwa watu wa pekee na taifa takatifu! Moja ya zile amri ilitolewa ili kuhakikisha ya kwamba watu wake hawasahau kamwe uhusiano wao na Muumbaji. Kwa kweli, inaanza kwa neno 'kumbuka'.



74

(Fungu: Kutoka 20:8-11)
Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote;




75

lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yoyote,




76

wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala



77

mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana kwa siku sita BWANA alifanya



78

mbingu, na nchi, na bahari, na  vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba;

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi



79

Kwa hiyo BWANA  akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa. Kutoka 20:8-11.



80

Sabato ipo katikati, ama ni kiini, cha zile kanuni kumi.
Siku ya Sabato ni kumbukumbu ya uumbaji.
Ni ya zamani kama dunia yenyewe!
Mungu anaahidi watu wake  baraka nyingi kama wakimtii na kukumbuka siku yake ya uumbaji.



81

Kama ukiugeuza mguu wako usihalifu sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu wangu; ukiita sabato siku ya furaha,



82

na siku takatifu ya BWANA yenye heshima; ukiitukuza, kwa kutokuzifanya njia zako mwenyewe,



83

wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe,



84

ndipo utakapojifurahisha  katika BWANA....
Isaya 58:13,14
Kama mtu angeikumbuka siku ya kumbukumbu, matatizo mengi anayoyakabili leo - Mungu kusahauliwa, maisha yasiyo na maana, tatizo la kujijua mwelekeo - yote yangetatuliwa. Kusingelikuwa na waumini wa uibukaji!



85

Lakini inasikitisha  kusema, Watu wa Mungu walisahau. Walisahau kumuabudu  Yeye katika siku yake  takatifu na,

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi


86

haikuchukua muda walianza kuabudu miungu wa vijiti na mawe.
Walipoteza mwonekano wa mizizi yao!


87

Kulikuwa na uamsho wa utunzaji wa Sabato wakati katika karne kadhaa wakati manabii wa Mungu walipoita watu wamrudie Mungu Muumbaji.
Isaya alisisitiza ya kwamba Mungu kamwe hakukusudia kuifunga Sabato kwa Wayahudi pekee.


88

Sabato ilisimikwa kabla ya taifa la Kiyahudi kuwepo. Mungu hakuzuia mibaraka ya namna hiyo kwa taifa moja pekee.



89

(Fungu: Isaya 56:6,7)
Anaalika kila mmoja, kila mahali kukumbuka  na kuitunza Sabato pamoja naye. Kila aishikaye Sabato ........




90

Nitawaleta hao nao hata mlima wangu mtakatifu, na kuwafurahisha katika nyumba yangu ya sala;




91

...Kwa maana nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa mataifa yote.
Isaya 56:6,7.



92

Hakuna mahali katika Biblia ambapo siku ya sabato huitwa Sabato ya Wayahudi.
Yesu aliiweka wazi ya kwamba ni siku kwa ajili ya wanadamu wote wakati aliposema,



93

(Fungu: Marko 2:27)
Sabato iliwekwa kwa ajili ya binadamu na si binadamu kwa ajili ya Sabato!

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi



94

(Fungu: Kutoka 20:10)
Na Mungu akasema, ..Siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako...
Kutoka 20:10.



95

(Fungu: Mathayo 12:8)
Yesu alisema pia ya kwamba Yeye ni
Bwana wa Sabato. (Mathayo 12:8) kwa sababu ndiye aliyeiumba.



96

(Fungu: Ufunuo 1:10)
Ndiyo maana Yohana wa Ufunuo aliiita Siku ya Bwana.
Ufunuo 1:10.
Sabato ni zaidi ya kumbukumbu ya uumbaji na Muumbaji.
Ni ishara kati ya Mungu na mwanadamu.



97

(Fungu: Ezekieli 20:20)
Zitakaseni Sabato zangu; zitakuwa ishara kati ya mimi na ninyi,



98

mpate kujua ya kuwa mimi ndimi BWANA, Mungu wenu. Ezekieli 20:20.
Yeye aliyefanya Sabato kuwa takatifu wakati wa juma la uumbaji ndiye huyo huyo afanyaye wadhambi kuwa watakatifu.
Muumbaji wetu ndiye pia Mwokozi wetu!



99

(Fungu: Ezekieli 20:12)
Tena naliwapa Sabato zangu, ziwe ishara kati ya mimi na wao,



100

wapate kujua ya kuwa mimi, BWANA, ndimi niwatakasaye.
Ezekieli 20:12.

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi



101

Sabato iliwekwa kabla dhambi haijaingia hapa Duniani, na pia itaendelea kusherehekewa baada ya dhambi kuondolewa toka Duniani.



102

(Fungu: Isaya 66:22,23)
'Kama vile mbingu mpya na nchi mpya , nitakazofanya, zitakavyokaa mbele zangu,' asema BWANA,



103

ndivyo uzao wenu na jina lenu litakavyokaa.



104

Na itakuwa, mwezi mpya hata mwezi mpya, na sabato hata sabato,



105

wanadamu wote watakuja kuabudu mbele zangu, asema BWANA.
Isaya 66:22,23.



106

Milele zote, watu wa Mungu watasherehekea Sabato kwa kumheshimu Yeye kama Muumbaji na Mwokozi. Kama Sabato ilisherehekewa kabla dhambi haijaingia Duniani, na itasherehekewa wakati dunia itakapofanywa upya, je haileti maana kusema ni muhimu watu wa Mungu waisherehekee sasa?


107

Kama tunayo maswali yoyote kuhusu Mungu na Sabato, twaweza kuangalia jinsi Yesu alivyoshughulikia swala hilo.

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi


108

Luka anatuambia kile Yesu alichokitenda siku ya Sabato:




109

(Fungu: Luka 4:16)
Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa;




110

na siku ya sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake, akasimama ili asome.
Luka 4:16.
Biblia yasema kwamba hiyo ilikuwa desturi ya Yesu!



111

Kamusi ya kiingereza ya Webster inasema,
Sabato;



112

siku ya saba ya juma (Jumamosi).
- Webster's New World Dictionary, toleo la chuo la pili.




113

Kama siku ingekuwa imebadilishwa au kusahauliwa kati ya Adamu na Musa, Mungu angeirekebisha wakati alipoandika Amri Kumi pale Sinai.



114

Kama siku ingekuwa imepotea kati ya Musa na Yesu, Kristo kwa hakika angeirekebisha rekodi sawa sawa.



115

Kama siku ingekuwa imebadilishwa wakati wa uhai wa wanafunzi wangekuwa wameandika bayana juu ya hilo.

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi



116

Na kwa kweli Wayahudi, ambao hutunza kwa makini sana rekodi ya wakati, bado huabudu katika siku ya saba, au Sabato.



117

Kitambulisho cha siku ya kupumzika hakikuwa swali hata kidogo wakati wa maisha ya Yesu hapa Duniani. Pambano lilitokea tu juu ya jinsi gani alivyoitunza. Ma-Rabi walikuwa wameharibu uadhimishaji wa Sabato kwa kuweka masharti magumu na ya kutesa. Yesu alijaribu kuondoa masharti yaliyowekwa na mwanadamu na kuonyesha maana ya utunzaji wa Sabato.


118

Walipomshitaki Yesu kwa kuvunja Sabato kwa sababu aliponya watu siku hiyo , Aliwajibu,



119

(Fungu: Mathayo 12:12)
...Ni halali kutenda mema siku ya Sabato.
Mathayo 12:12.



120

Biblia yasema kuwa Yesu aliponya na kuhudumia, Sabato ni kwa ajili ya kutufanya kuwa wakamilifu, kutuweka huru toka kwa hatia, ubaguzi, na uchoyo, na kutupatia amani mawazoni;
Ni kwa ajili ya kuturejesha sisi kwa sura ya Mungu na kutuelekeza kwa Muumbaji wetu!
Hii ndiyo kazi aliyokuja kuifanya Yesu, na ndiyo kazi waliyofanya wanafunzi baada ya kuondoka kwake.



121

Maana ya utunzaji wa Sabato ililelezwa na wafuasi wa Yesu wakati wa kifo chake.
Katika maafa haya, marafiki wa Yesu walipumzika kulingana na amri ya Mungu, wakiiacha kazi ya kuutia mwili mafuta hadi baada ya masaa ya Sabato.

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi




122

(Fungu: Luka 23:54-56)
Na siku ile ilikuwa siku ya Maandalio, na sabato ikaanza kuingia.



123

Na wale wanawake waliokuja naye toka Galilaya walifuata, wakaliona kaburi, na jinsi mwili wake ulivyowekwa.



124

Wakarudi, wakafanya tayari manukato na marhamu. Na siku ya sabato walistarehe kama ilivyoamriwa. Luka 23:54-56.



125

Siku kabla ya Sabato, tegemeo lao kwa Kristo lilikuwa limevunjwa vunjwa.
Walishuhudia akifa kifo cha kikatili msalabani.
Ndoto zao na matumaini yao ziliishia katika giza la kaburi.
Walitaka kuupaka mafuta mwili wake uliokufa.




126

(Fungu: Luka 24:1 HNKK)
....Jumapili, alfajiri na mapema, wale wanawake walikwenda kaburini wakichukua yale manukato waliyotayarisha.
Luka 24:1



127

Hebu tuangalie kwa mtizamo mwingine matukio ya siku zile tatu zisizosahaulika.



128

1. Ijumaa: Yesu alikufa; wanawake wakaandaa marhamu na manukato.

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi



129

2.Jumamosi (siku ya Sabato): Yesu alipumzika kaburini; Wafuasi wake walipumzika.



130

3. Jumapili (siku ya kwanza ya juma): Yesu alifufuka toka kwa wafu! Wanawake walikuja kutia mwili wa Yesu mafuta.
Hakuna mashaka juu ya siku gani ilikuwa ya Sabato wakati wa kifo cha Yesu.



131

(Fungu: Yohana 19:30)
Yesu alining'inia msalabani siku ya maandalio na kulia,
...Imekwisha!....
Yohana 19:30.



132

Kazi yake ya ukombozi ilikuwa imekamilika!
Alipumzika ndani ya kaburi siku ya Sabato




133

na akafufuka siku ya Jumapili, siku ya kwanza ya juma.
Hata katika mauti Yesu aliitunza Sabato;
Alipumzika kaburini siku ya Sabato.
Tusimamapo karibu na msalaba, tunapata hisia ya kwamba siku yoyote kati ya siku saba haiwezi kufaa!
Kwani kucheza na Sabato ingekuwa ni kucheza na uumbaji, na Sinai, na Kalvari yenyewe!


134


Ndiyo, inadhuru ni siku gani kati ya saba tunayoisherehekea.
Mwandishi mkristo aliyeitwa George Vandeman aliandika:



135

Twawezaje kuwaona wafuasi wake wakikataa kunajisi masaa matakatifu hata kwa kitendo chao cha kutaka kuonyesha upendo,

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi



136

twawezaje kumuona Yeye akifa katika msalaba kwa sababu sheria isingeweza kumridhia hata kujiokoa maisha yake Yeye mwenyewe-



137

twawezaje kusimama katika miali ya nuru ya Kalvari na kusema haidhuru?
-Siku ya Kukumbuka, uk. 40.



138

Muumbaji alisema Kumbuka, bado wengi sana wanasahau! Lakini hilo halikuwa kusudi la Mungu. Yesu alitegemea kwamba Wakristo wangetunza Sabato wakati wote.



139

(Fungu: Mathayo 24:20)
Ombeni ili kukimbia kwenu kusiwe siku za baridi au siku ya Sabato!
Mathayo 24:20.



140

Yesu alitegemea kwamba Wakristo mwaka 70 B.K., wakati Yerusalemi ilipoangamizwa, wangekuwa bado wanaitunza Sabato!



141

(Fungu: Matendo 17:1,2)
Agano Jipya linayo taarifa kwamba wafuasi wa Yesu waliitunza Sabato baada ya ufufuo:
Wakafika Thesalonike, ambapo palikuwa na sinagogi la Wayahudi:



142

Na Paulo, kama ilivyokuwa desturi yake, akaingia mle walimo, akahojiana nao kwa maneno ya maandiko Sabato tatu,
Matendo 17:1,2.
Katika Sabato nyingine wakati Paulo alipokuwa akihubiri, baadhi ya Wamataifa walikuja na ombi:

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi



143

(Fungu: Matendo 13:42,44)
....(wamataifa) wakawasihi wawaambie maneno haya sabato ya pili.




144

Hata sabato ya pili, watu wengi, karibu mji wote, wakakusanyika walisikie neno la Mungu.
Matendo 13:42, 44.



145

Kwa kweli, kitabu cha Matendo kinazo taarifa za mikutano 84 ambayo Paulo aliiendesha siku za Sabato.



146

Sabato inakwenda kama uzi wa dhahabu tokea Mwanzo hadi kitabu cha Ufunuo, kinachowaeleza wale ambao wamejiandaa kukutana na Yesu ajapo mara ya Pili!




147

(Fungu: Ufunuo 14:12)
Hapa ndipo penye subira ya watakatifu: hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu.
Ufunuo 14:12.



148

(Fungu: Yohana 14:15)
Yesu alisema,
Mkinipenda mtazishika amri zangu.
(Yohana 14:15)
na moja ya amri hizo inatuambia
ikumbuke siku ya Sabato


149

Kama tukimwabudu Mungu Muumbaji wetu katika Sabato ya siku ya saba kila juma, hatutasahau kamwe tulipotokea au aliyetuumba pamoja na ulimwengu unaotuzunguka.

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi



150

Kama tukiitunza Sabato kila juma, hatutahitaji kushangaa ya kwamba sisi ni nani - wana na binti za Mungu, Mfalme wa ulimwengu!


151

Hatutahitaji kushangaa kamwe jinsi gani tulifika hapa - tupo hapa kwa sababu Mungu alitutaka, kwa sababu alituumba.


152

Yesu huyo huyo anayekuomba kukumbuka ananyoosha mikono yake kwako leo - mikono ambayo ilipata kupigiliwa kwenye msalaba wa Kalvari kwa ajili ya dhambi zetu-na anaita kwa upole, Nifuate.



153

Je,utamfuata Muumbaji wako sasa?
Je, utaitii amri yake na kuikumbuka siku ya Sabato aliyoiumba kwa ajili yako?
Je, utamwabudu Yeye kila juma kuanzia sasa na kuendelea wakati Sabato ifikapo kila siku ya saba?
Je, utafuata mfano wa Yesu na mitume katika kumwabudu Muumbaji wako katika Sabato ya siku ya saba?

# 11 - Kuumbwa kwa Ajili ya Kitu Bora Zaidi


154

Sabato si swala tu la siku gani tunayoabudu rafiki. Ni swala la kumfuata Yesu njia yote. Ni swala la kusimama pamoja na Adamu na Hawa walipokuwa wakiabudu ndani ya Edeni katika Sabato ya kwanza.
Ni swala la kutii amri ya Mungu pamoja na Musa wakati Mungu aliposema, Ikumbuke siku ya Sabato uitakase.
Ni swala la kuabudu katika siku moja pamoja na Isaya, Yeremia, Danieli na mashujaa wote wa imani wa Agano la Kale.
Ni swala la kumtukuza Mungu kila Sabato kama Muumbaji wa vyote pamoja na Petro, Yakobo na Yohana.
Ni swala la kuwa sehemu ya watu wa Mungu wa wakati wa mwisho, ambao kulingana na Ufunuo, wanazitunza amri.
Je, ungependa kusema, Ndiyo, Yesu, Nitasimama pamoja nawe. Nitakupa nafasi ya kwanza. Nitakufuata njia yote.
Kama hii ndiyo tamaa yako, inua mkono wako tunapoomba.

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo



1

Usiruhusu Litokee Kwako.


2

Hadithi za kubuni hukubalika kama ukweli hasa kama zimekuwa zikinenwa kwa muda mrefu. Chukua habari ya buibui. Takribani mwaka wa 350 K.K., mwana falsafa mkuu wa Kiyunani Aristotle alimuainisha buibui kama mwenye miguu sita.

Na kwa karne zilizofuata 20 kila mmoja aliamini buibui alikuwa na miguu sita. Hakuna aliyejali kuhesabu. Hata hivyo, ni nani angediriki kumpa changamoto Aristotle mkuu?

Naam, punde akaja Lamarck, mwanabaiolojia na mchunguzi wa viumbe hai. Kwa uangalifu alihesabu miguu ya buibui. Na unadhani miguu mingapi aliyohesabu? Nane kwa hakika!

Habari isiyo ya kweli iliyokuwa imefundishwa kwa karne kadhaa iliharibiwa kwa sababu Lamarck alijali kuhesabu

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo


3

Je, yawezekana ya kwamba fundisho la uongo la kidini limejipenyeza ndani ya kanisa la Kikristo? Je, yawezekana tunashughulika na jambo ambalo ni zaidi ya mjadala wa buibui mwenye miguu sita - nane hapa?
Mamilioni ya watu wanaabudu katika siku ya kwanza ya juma wakiamini ya kwamba ni Sabato ya Biblia. Katika mjadala wetu uliopita, tuligundua ya kwamba siku ya saba ya juma, Jumamosi, ni Sabato ya kweli ya Mungu. Kama jinsi ambavyo vitabu kwa miaka 2,000 vilivyofundisha kwa makosa ya kwamba buibui ana miguu sita, vivyo hivyo mamilioni wamekubali uongo kuhusu Sabato.
Sababu yako ya kuhudhuria mikutano hii ya mafundisho ya Biblia ni kwa sababu moyo wako unautamani ukweli. Unataka kujua kwa hakika kile neno la Mungu linachokisema. Huna shauku na kile viongozi wa kidini wanachokifundisha. Unahitaji kujua kile Mungu anachokisema. Hebu tufanye mapitio ya kile tulichojifunza katika mkutano wetu uliopita.



4

Tumejifunza ya kwamba Mungu ametupatia siku maalum kila juma - siku ya Sabato - ambayo katika hiyo tunamwabudu na kukumbuka kazi Yake kama Muumbaji wetu.
Tulijifunza ya kwamba siku ya Sabato siyo siku yoyote tu - bali ni siku ya saba ya juma.
Na tulijifunza ya kwamba Sabato itaendelea kutunzwa baada ya dunia hii kufikia mwisho na tukiwa mbinguni pamoja na Muumbaji wetu.


5

Lakini kama tunavyotazama dunia, tunaona ya kwamba watu wengi - wengi zaidi kwa kweli - hawamuabudu Mungu siku ya saba.


6

Wengi hata hawamwabudu Mungu wa Biblia, kwa kweli, wanakuwa tu na miungu mingine.

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo



7

Lakini kwa wale wanaomwabudu Mungu wa Biblia, hata wengi wa wale wanaomwabudu Yeye katika siku nyingine kando ya ile aliyoiweka pembeni kama siku Yake takatifu.
Kwa nini hilo lipo?
Je, Mungu aliibadilisha siku?
Je, yupo aliyeibadilisha siku ?
Kwa  nini watu wengi kiasi hicho wanaadhimisha siku nyingine, kama Jumapili, kama siku ya Mungu, badala ya Sabato ya siku ya saba?


8

Tumejifunza ya kwamba Biblia inatuambia ya kwamba katika sheria Yake, Mungu alitupatia sisi sote ishara - ishara ya pekee sana:



9

(Fungu: Ezekieli 20:12, 20)
Tena naliwapa sabato zangu, ziwe ishara kati ya mimi na wao,



10

wapate kujua ya kuwa mimi,  BWANA, ndimi niwatakasaye....



11

Zitakaseni sabato zangu: zipate kuwa ishara kati ya mimi na ninyi,



12

mpate kujua ya kuwa mimi ndimi BWANA, Mungu wenu.
Ezekieli 20:12,20.

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo



13

Biblia,  tangu mwanzo hadi mwisho, inashuhudia ukweli ya kwamba  Mungu ameiweka siku ya Sabato na ya kwamba siku ya Sabato ni siku ya saba ya juma.
Na hakuna mahali katika Biblia ambapo Mungu anaonyesha ya kwamba amebadilisha siku ile ya kuabudu na ya pumziko- ile ishara kati yake Yeye mwenyewe na watu Wake.



14

Hebu tupitie kidogo yale ambayo tumeyaona katika jumbe hizi, kwa kujifunza Neno la Mungu.
Wakati Mungu alipomaliza kuumba Sayari Dunia na mwanadamu, aliiumba Sabato.



15

kama kumbukumbu ya Uumbaji wake katika siku ya saba ya juma la kwanza na katika historia yote.


16

Wakati Mungu alipoiandika sheria yake pale Mlimani Sinai, aliweka katika moyo kabisa wa hizo amri Sabato.



17

Hii amri ilikuwa daima pale ili kumkumbusha mwanadamu ya kwamba hakutokea tu  na kuwepo.



18

Sababu anayoitoa imfanyayo kuomba mwanadamu kuitunza siku ya saba ni kwamba aliiumba dunia kwa siku sita



19

na kupumzika katika siku ya saba.
Kuhusu amri zake, Mungu, kupitia kwa Musa, aliwaambia watu ya kwamba hawakupaswa kupunguza wala kuongeza katika hizo.

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo



20

(Fungu: Kumbukumbu 4:2)
Msiliongeze neno niwaamurulo wala msilipunguze,



21

mpate kuzishika amri za BWANA,Mungu wenu niwaamuruzo.
Kumbukumbu 4:2. Mungu pia aliwaambia,



22

(Fungu: Zaburi 89:34)
Mimi sitalihalifu agano langu, Sitalibadili neno lililotoka midomoni mwangu.


23

Yesu mwenyewe alionyesha dhamira yake ya kuitukuza Sheria aliyoitoa Mlimani Sinai. Aliwaambia watu katika hotuba yake katika Mlima ya kwamba hakuja kuiweka pembeni Sheria ya Mungu bali kuitimiliza!



24

(Fungu: Mathayo 5:17 - 19)
Tambua maneno haya:
Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kuitangua, bali kutimiliza.



25

Kwa maana, amin, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka,



26

yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie.



27

Basi mtu yeyote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo,

12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo



28

ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni..... Mathayo 5:17 - 19.
Wakati Mungu alipotoa Amri Kumi kwa watu wake, aliweka wazi pia ya kwamba hakuna mtu anayeruhusiwa kufanya marekebisho au kubadili maelekezo yaliyotoka katika kinywa chake kitakatifu.


29

Yesu mwenyewe alieleza kwa mfano wake ya kwamba alitaka kuheshimu siku ambayo Yeye na Baba Yake waliitakasa katika juma la kwanza la historia ya dunia hii.



30

(Fungu: Luka 4:16)
Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na siku ya sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake,



31

Alikwenda kwenye sinagogi siku ya Sabato na akasimama kusoma.
Luka 4:16.


32

Wakati viongozi wa kidini walipowashitaki wanafunzi wa Yesu kwa sababu ya kuivunja Sabato, Yesu alisema alikuwa pia Bwana wa siku hiyo.



33

(Fungu: Marko 2:27,28)
Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya sabato.



34

(Nani Alibadili Sabato) Basi Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa sabato pia.
Marko 2:27,28.

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo


35

Si tu kwamba Yesu aliiheshimu siku ya Sabato, bali pia aliwaomba wanafunzi wake wasali ili waweze kuitunza siku yake takatifu mbeleni sana – siku za usoni.



36

(Fungu: Mathayo 24:20)
Tunaliona ombi hili katika Mathayo 24:20 ; Ombeni ili kukimbia kwenu kusiwe siku za baridi au siku ya Sabato!


37

Hapa Yesu alikuwa akinena juu ya kukimbia kwa wafuasi wake toka Yerusalemi kabla tu ya



38

kuangamizwa kwake katika mwaka wa 70 B.K.kulikofanywa na Warumi.


39

Aliposulubishwa alitegemea kwamba wafuasi wake wangeendelea kuiheshimu Sabato.



40

Wayahudi Waorthodoxi wamekuwa wakiabudu katika siku ya saba tangu wakati wa Kutoka, zaidi ya miaka 3,500 iliyopita.
Popote walipo duniani, hutambua Jumamosi, siku ya saba ya juma, kama siku ambayo Mungu aliiweka pembeni kwa ajili ya ibada.


41

Hata kama Biblia ingekuwa chanzo chetu pekee cha taarifa, bado tungeweza kutambua siku ipi ni siku ya saba, au Sabato. Tunapoangalia taarifa ya kusulubiwa kwa Yesu, Kitabu cha Luka kinafupisha matukio ya mwisho ule wa juma.
Baada ya Kristo kufa msalabani siku ya Ijumaa, Biblia inatoa wazo:

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo



42

(Fungu: Luka 23:54-56; 24:1)
Na siku ile ilikuwa siku ya Maandalio, na sabato ikaanza kuingia.



43

Na wale wanawake waliokuja naye toka Galilaya walifuata, wakaliona kaburi, na jinsi mwili wake ulivyowekwa.




44

Wakarudi, wakafanya tayari manukato na marhamu. Na siku ya sabato walistarehe kama ilivyoamriwa.



45

(Luka 24:1 HNKK)
Jumapili, alfajiri na mapema, wale wanawake walikwenda kaburini wakichukua yale manukato waliyotayarisha.



46

walikwenda kaburini, wakiyaleta manukato waliyoweka tayari.
Luka 23:54-56; 24:1.


47

Sehemu kubwa ya ulimwengu wa Kikristo unasherehekea kile kiitwacho Ijumaa Kuu kama kumbukumbu ya mauti ya Kristo. Wanasherehekea Jumapili ya Pasaka kama kumbukumbu ya Ufufuo wa Kristo.



48

Biblia inatuambia ya kwamba siku iliyo katikati ni ya Sabato, kama ilivyoamriwa.

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo



49

Hata ingawa Luka aliandika maneno hayo miaka mingi baada ya msalaba, bado aliitaja Jumapili kama siku ya kwanza ya juma,
Na bado aliiita siku ya saba Sabato.
Taarifa ya Kibiblia inatofautisha wazi kabisa siku hizi mbili.


50

Hakika, mitume waliendelea kuabudu na kuhubiri katika Sabato ya siku ya saba kwa miaka mingi baada ya msalaba.



51

(Fungu: Matendo 13:14,42,44)
Biblia yasema juu ya Paulo na wenzake walipotembelea Antiokia kuwa:
....wakaingia katika sinagogi siku ya sabato, wakaketi.



52

Matendo 13:42. Baadaye, ..Walipokuwa wakitoka,



53

wakawasihi wawaambie maneno haya sabato ya pili.



54

Hata sabato ya pili, watu wengi, karibu mji wote, wakakusanyika walisikie neno la Mungu. Matendo 13:44.
Ilikuwa desturi ya Paulo kuabudu katika sinagogi kila Sabato:

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo




55

(Fungu: Matendo 18:4)
Akatoa hoja zake katika sinagogi kila sabato,akajaribu kuwavuta Wayahudi na Wayunani. Matendo 18:4
Kutokana na dondoo hizi za Biblia, mtu aweza kuona kwa urahisi ya kwamba hakuna kithibitisho ya kwamba Kristo au wanafunzi wake waliibadili siku ya ibada.
Hakuna taarifa katika Biblia inayoamuru badiliko la namna hiyo!


56

Hakuna kati ya waandishi wa Agano Jipya aliyeeleza juu ya mabadiliko yoyote ya siku ya Sabato! Ingekuwa makala inayoongoza katika Sehemu ya Agano Jipya  ya Biblia kama badiliko la namna hiyo lingetokea!



57

(Fungu: Zaburi 89:34)
Mungu alisema, Mimi sitalihalifu  agano langu, Sitalibadili neno lililotoka midomoni mwangu. Zaburi 89:34.
Mungu hajaibadili sheria yake na hakuna hata mmoja aliye na haki ya kubadili Sheria ya Mungu! Wasomi tokea makundi mbalimbali yatunzayo siku ya Jumapili wanalitambua hili.



58


Kadinali wa Kikatoliki James Gibbons aliwahi kuandika:
Waweza kusoma Biblia tokea Mwanzo hadi Ufunuo, na hutapata mstari mmoja unaotoa mamlaka ya utakaso wa siku ya Jumapili.



59

Maandiko yanasisitiza uadhimishaji wa Jumamosi.

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo



60

Clovis G. Chappell, Mmethodist, anatoa maneno kama hayo asemapo, Sababu ya kuadhimisha siku ya kwanza badala ya siku ya saba haina msingi katika amri yoyote.




61

Mtu aweza kuchunguza Maandiko bure kwa ajili ya kupata ushuhuda wa kubadilishwa toka siku ya saba hadi ya kwanza.
- Kanuni Kumi za Maisha. Uk.61.



62

Hakuna taarifa yoyote ya Kibiblia kwamba Kristo au wanafunzi wake walitunza siku nyingine yoyote au walielekeza wengine kufanya hivyo!
Sasa je, Utunzaji wa siku ya Jumapili ulianzaje? Waweza kuuliza.



63

Tunajifunza toka kwa Socrates Scholasticus, mwana historia wa karne ya tano: Karibia makanisa yote katika dunia nzima yanasherehekea siri takatifu [ Meza ya Bwana ] katika Sabato ya kila juma,



64

na bado Wakristo wa Aleksandria na wa Rumi, kwa sababu ya taarifa za mapokeo ya kale, wamekoma kutenda hivi.
- Historia ya Makanisa, kama ilivyonukuliwa na C.B. Haynes, Kutoka Sabato Hadi Jumapili, Uk. 35.



65

Wanahistoria wengine wameandika taarifa ya kwamba vikundi vingi vya makanisa vilikuwa vikiiadhimisha Sabato ya siku ya saba wakati wa Zama za Kati, na mazoea hayo yamewekwa vizuri na Wakristo katika nyaraka za kisasa katika ulimwengu mzima.



66

Wana historia wengi wa kanisa wanaweka bayana mabadilliko ya siku yaliyokuja polepole wakati fulani kati ya mwaka 70 B.K. na 135, tarehe ambapo maasi makuu yaliyotokea mara mbili yalizimwa na Warumi.

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo



67

Chuki ya Warumi iliyokuwa ikiongezeka dhidi ya Wayahudi iliungana na kuhitilafiana kati ya Wayahudi na Wakristo, na kuongeza kuwepo kwa fasihi iliyoupinga U-yahudi, ambayo baadaye, ilileteleza fikira za kuupinga U-yahudi katika Himaya yote ya Kirumi.
Wakristo wakawa na tahadhari zaidi na swala la kuhusianishwa na Wayahudi.
Kwa sababu utunzaji wa Sabato ulionekana kuwafanya wahusianishwe na Wayahudi, Wakristo wengi walianza kupunguza masharti yake.



68

Dalili za muhimu zinaonyesha ya kwamba uadhimishaji wa Jumapili ulianza wakati huohuo pamoja n Jumapili y a Pasaka,



69

kama jaribio la kuhakikishia mamlaka ya Kirumi utofauti kati ya Ukristo na U-yahudi.
Ibid. (Kitabu hicho hicho), Uk. 237.


70

Ukiwa na hili mawazoni, ni rahisi kuona jinsi Wakristo walioishi katika jiji la Ufalme wa Kirumi walivyoongoza njia katika kujitenga wao wenyewe na utunzaji wa Sabato.
Walikuwa katikati mahali ambapo uadui ulikuwa na nguvu zaidi!



71

Inaeleweka zaidi hasa  kwamba waliweza kuaibikia utunzaji wa Sabato, uliodharauliwa zaidi na Warumi, katika pia mtizamo huu ya kwamba kanisa la Kirumi lilikuwa zaidi na uwingi wa Wamataifa, ambao walikuwa waongofu tokea upagani.



72

(Fungu: Warumi 11:13)
Inapendeza kutambua jinsi Paulo alivyolitaja kanisa katika Rumi: Lakini nasema na ninyi, mlio watu wa Mataifa...
Warumi 11:13.

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo


73

Wakristo hawa, ambao walikuwa wameongoka hivi karibuni kutokea uapagani, hawakuwa wameimarika vema katika utunzaji wa Sabato kama Wayahudi Wakristo, ambao daima walizoea kutunza Sabato.



74

Lakini kwa nini Jumapili ilichaguliwa na wala siyo siku nyingine yoyote ya juma?
Hilo ni swali zuri!
Wapagani katika Ufalme wa Kirumi walikuwa waabudu mungu jua kwa miaka mingi, wakiisherehekea Jumapili kama siku ya jua.




75

Wafalme wa Kirumi walikuwa hata wamejiwakilisha wao wenyewe kama miungu jua, wakiweka mihuri ya nembo za jua katika sarafu zao na majengo na wakidai ibada toka kwa waliowatawala.
Baadhi ya wanathiolojia huamini ya kwamba kanisa lilipata faida katika kupatana na upagani.
Kwa kukubali desturi chache za kipagani, wapagani wangeongoka katika Ukristo kwa urahisi na kujisikia huru.
Ingesaidia pia ufalme kwa kuunganisha raia wake katika dini moja kuu.




76

Kwa karne kadhaa Jumapili ilisherehekewa, siyo kama siku takatifu, bali kama sikukuu.
Halafu siku zote mbili zikatunzwa kama siku takatifu.



77

Tunasoma yafuatayo kutoka katiba za Kitume, sura ya 23.
Wakristo hawakuwa peke yao ambao walikuwa wazembe na polepole wakalegea katika imani yao.



78

Mmomonyoko wa usafi wa kanisa la Mitume ulisimama imara na dhahiri, lakini wakati kizazi cha pili na cha tatu cha Wakristo kilipokuja,



79

tunaona kithibisho cha kuridhiana na upagani pamoja na uasi.



80

Huku kusererreka  na kuingia katika maridhiano haya kulikaziwa na sheria ya kwanza ya kiserikali ya Jumapili iliyopitishwa na Mfalme wa Kirumi Konstantine tarehe 7 Machi, 321 B.K.



81

Wakati akiwa bado mpagani, aliifanya sheria: Katika siku ya kuheshimiwa ya Jua hebu wakuu  na  watu wakaao kwenye majiji na miji wapumzike, hebu karakana zote zifungwe.



82

Mashambani, hata hivyo, watu walio katika kilimo wanaweza kuendelea kwa uhuru na kulingana na sheria waendelee tu na shughuli zao.
Historia ya Kanisa la Kikristo, Tol. 1902, Gom.3, uk, 380.



83

Hatua iliyofuata katika kufanya utunzaji wa Jumapili kuwa sehemu ya muhimu katika Ukristo ilichukuliwa na Kanisa la Kirumi katika Baraza la Laudikia. Lilifanya sheria ya kwanza ya kidini kuhusu utunzaji wa Jumapili.



84

Katika mwaka wa 325, Sylvester, Askofu wa Kirumi alibadili cheo cha siku ya kwanza na kuiita 'Siku ya Bwana.'
- Historia Ecclesiastica, uk 739.
Katika Baraza jingine la Laudikia, lililofanyika mwaka 364, sheria ifuatayo iliwekwa:



85

Wakristo  hawatafanya Kiyahudi [kutunza Sabato] na kukaa bila kazi siku ya Jumamosi,... bali watafanya kazi katika siku hiyo;


# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo






86


lakini siku ya Bwana wataiheshimu kwa namna ya pekee, na, kwa kuwa Wakristo, kama itawezekana,




87

hawatafanya kazi katika siku hiyo.

- Historia ya Mabaraza ya Kanisa, gombo la 2, uk. 316.



88

Hata pamoja na hili, Wakristo bado walikuwa wakiiadhimisha Sabato katika karne ya sita, kwani Papa Gregory alishutumu




89

Kama manabii wa Mpinga-Kristo wale waliokaza kusema kazi haipaswi kufanywa siku ya saba.
- Sheria ya Jumapili, imenukuliwa katika C.B. Haynes, Toka Sabato Hadi Jumapili, uk. 43.




90

Kumbuka ya kwamba Biblia haikupatikana kwa kila mmoja wakati ule kama ilivyo sasa.
Mafundisho yalipitishwa kwa kauli za midomo hadi kufikia kiasi kwamba walei hawakuweza kutofautisha kwa urahisi kati ya Maandiko na mapokeo.



91

Hadi watu walipojua kwa hakika ukweli kama ulivyofundishwa na Kristo na wanafunzi wake.
Karne zilipita,



92

na Matengenezo ya Kiprotenstanti yakaja, yakihoji kanuni nyingi na mapokeo ambayo yalikuwa yamesimamishwa badala ya mafundisho ya Neno la Mungu.

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo



93


Kilio cha matengenezo kilikuwa, Biblia na Biblia yenyewe kama kanuni yetu ya imani.


94

Wengi kama Huss na Jerome, walilipa kwa ajili ya uaminifu wao kwa Biblia kwa kuchomwa katika miti iliyoandaliwa kwa makusudi hayo!


95

Hata hivyo, baada ya karne ya sita, ukweli wa Sabato ulikuwa kana kwamba umelala, ukijificha chini ya karne za mapokeo.
Wachache walijifunza kwa karibu kuona kama Maandiko yalifundisha nini.
Walikubali yale yaliyokuwa yamepokelewa toka kwa vizazi vilivyowatangulia, bila kuhoji kama ulikuwa ukweli ama habari za kubuni.


96

Wakati fulani watu hukubali mambo bila kuhoji. Kwa karne nyingi watu wengi waliamini ya kwamba dunia ilikuwa kiini cha ulimwengu. Waliamini ya kwamba jua na sayari zote viliizunguka dunia.
Copernicus (Kopanikas) aliyetumia uhuru wake wa kuwaza aliipinga imani hii isiyo sahihi.
Alitamka, Jua, siyo dunia, ndilo lililo kiini cha ulimwengu. Je, wajua ni nani waliompinga zaidi? Viongozi wa Kanisa -- waalimu wa dini. Walipaza sauti, Huwezi kubadili mbingu za Mungu.
Kwa vyovyote, Copernicus hakuwa akibadili mbingu za Mungu. Alikuwa akifunua tu mapokeo makongwe ambayo hayakuwa na msingi wowote wa kisayansi. Copernicus alikuwa akifunua ukweli.
Kwa kuamini jambo fulani kwa muda mrefu hakulifanyi kuwa la kweli.
Sabato ilibadilishwaje? Sikiliza kauli zifuatazo za kushangaza za waandishi wa Kikatoliki ambao kanisa lao liliongoza njia ya mabadiliko toka Sabato hadi Jumapili.

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo




97

Kanisa la Kikatoliki kwa zaidi ya miaka elfu moja kabla ya kuwepo kwa U-Protestanti, kwa uwezo wa utume wake wa Kimbingu,



98

lilibadili siku toka Jumamosi hadi Jumapili.
- Sabato ya Kikristo, uk.16.




99

Toka katika Katekisimu ya Muongofu, tunasoma:



100

Swali: Siku ya Sabato ni ipi?




101

Jibu: Jumamosi ni siku ya Sabato.



102

Swali: Kwanini tunaiadhimisha Jumapili badala ya Jumamosi?



103

Jibu: .....kwa sababu Kanisa la Kikatoliki lilihamisha utukufu toka Jumamosi hadi Jumapili.
Badiliko hili lilifanywa na Baraza la Laudikia mwaka 336 B.K.

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo


104

Kwa nini, unahoji, Kanisa Katoliki, kwa uhuru wake lenyewe na kujiamulia lenyewe, lilisimika badiliko hili? Jibu lipo, kwa sehemu, katika ukweli juu ya jinsi Kanisa la Kikatoliki lilivyoweka mamlaka katika mapokeo.


105

Mojawapo ya mada muhimu zilizotofautisha Waprotestanti na Wakatholiki nyakati za awali za Matengenezo ni hii ya mamlaka ya mapokeo kanisani.
Wakati Martin Luther alipotamka ya kwamba ilikuwa lazima afuate Biblia na Biblia pekee, alipingana na taasisi nyingi za Kanisa Katoliki ambazo zilikuwa na misingi yake yote katika mapokeo.




106

Kwa kweli, Baraza la Trent liliitishwa ili kuamua msimamo gani halisi kanisa Katoliki lilipaswa kuchukua katika swala la mapokeo na hasa jinsi linavyohusianishwa na Biblia.
Swala hili liliamuliwa hatimaye.
Tazama muhtasari wa hotuba uliotolewa uliogeuza upepo, kama ambavyo imerekodiwa na H.H. Holtzman:



107

Hatimaye, katika ufunguzi wa mwisho wa tarehe kumi na nane Januari, 1562, kusita kwote kuliwekwa pembeni:



108

Askofu Mkuu wa Reggio alitoa hotuba ambayo kwayo alitamka wazi ya kwamba mapokeo yalikuwa juu ya Maandiko.
- Kanuni na Mapokeo, uk. 263.
Biblia haiungi mkono wazo kwamba mapokeo ni msingi wa mafundisho ya kanisa.


109

Je, unakumbuka swali Yesu alilouliza viongozi wa kidini wa wakati wake?

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo





110

(Fungu: Mathayo 15:3,9)
Aliuliza, Mbona ninyi nanyi huihalifu amri ya Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu?




111

Kisha akaongeza, Nao waniabudu bure, Wakifundisha mafundisho Yaliyo maagizo ya wanadamu.
Mathayo 15:3,9.




112

Je unaiona hoja ?
Je, utamfuata Kristo na Biblia - au mapokeo ya mwanadamu?
Si tu swala la siku na nambari.
Ni swala la mabwana!
Huo ndio majadala hakika!
Je, Yesu Kristo ni Bwana wako- au ni mapokeo tu ya mifumo mingine?



113

Tume tazama wasomi wanaoaminika kadhaa pamoja na taarifa za kihistoria. Lakini hapa ni baadhi ya kauli za kisasa juu ya kubadilishwa kwa Sabato.



114


Tunaikuta kauli hii: Lilikuwa Kanisa la Kikatoliki lililoamua ya kwamba Jumapili iwe siku ya ibada kwa Wakristo ili kuuheshimu ufufuo.
- Karl Keating, Ukatoliki na Uanzilishi, 1988, uk. 38.



115


Kauli nyingine itakayokusababisha utulie na kufikiri inatoka kwa gazeti la Sentinel la Mtakatifu Catherine la Kanisa Katoliki, Mei 21, 1995. Lilisema,
Pengine jambo la kijasiri kuliko yote, badiliko la kimapinduzi kuliko yote ambayo Kanisa limepata kufanya, lilitokea katika karne ya kwanza. Siku takatifu,

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo



116

Sabato, ilibadilishwa tokea  Jumamosi hadi Jumapili ....siyo kutokana na maelekezo yoyote yaliyo katika Maandiko, bali kutokana na Kanisa lenyewe kuhisi uwezo wake lenyewe......



117

Watu wanaodhani ya kwamba maandiko yanapaswa kuwa mamlaka pekee wanapaswa kwa uamuzi wa maana kabisa kuwa Waadventista wa Sabato, na kuitunza Sabato takatifu.




118

Katika unabii wa Danieli 7, Mungu alifunua kwa Danieli ya kwamba pembe ndogo ya Danieli 7:21,25, ilikuwa inakwenda



119

(Fungu: Danieli 7:25)
kubadili nyakati na sheria.
NI UNABII WA MAANA KIASI GANI HUU!
Hapa kuna utabiri ulio wazi kabisa ya kwamba mamlaka ua kidini ya duniani ingejaribu kubadili sheria ya Mungu.
Kuna amri moja tu  kati ya  kumi inenayo juu ya wakati - amri ya Sabato.


120

Kanisa la Kirumi lilifikiria kutenda hili, lakini Mungu ni yule yule bado leo kama alivyokuwa alipoumba mbingu na nchi na hajabadilisha kile alichokiweka katika Edeni.
Kwa kweli, unabii unaalika kila mmoja popote pale kumwabudu Muumbaji,  kwa sababu Yeye ndiye atakaye hukumu wanadamu.


121

Unabii unatolewa ili kuita nje  watu watakaokuwa tayari kumpokea Yesu wakati atakaporudi katika utukufu.
Watu watakaoitikia na kuwa tayari wanaelezwa kwa namna hii,

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo



122

(Fungu: Ufunuo 14:12)
Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu.
Ufunuo 14:12


123

Hili halihitaji maelezo ya kwamba wale walio na imani ya Yesu, watatunza amri zake kutokana tu na moyo wa  upendo walio nao kwa Mungu.



124

Ndiyo, Mungu anatuomba sisi TUMKUMBUKE  Yeye kama Muumbaji wetu kwa kutunza Siku yake takatifu.
Kutenda kama anavyotuomba inamaanisha ya kwamba tunaonyesha  utii wetu kwake.
Wakati mtu atunzapo Sabato iliyofanywa na mwanadamu, anatii mapokeo ya mwanadamu.
Tunapogundua mapenzi ya Mungu, ni furaha yetu kuyafuata.
Mungu analo la kusema juu ya mapokeo ya mwanadamu:



125

(Fungu: Marko 7:6,7)
...Watu hawa huniheshimu kwa midomo, ila mioyo yao iko mbali nami;



126

Nao waniabudu bure, Wakifundisha mafundisho Yaliyo maagizo ya wanadamu.
Marko 7:6,7.



127

(Fungu: Marko 7:9 HNKK)
Na tena, .....Ninyi mnajua kuepa kwa ujanja sheria ya Mungu kwa ajili ya kufuata mapokeo yenu!
Marko 7:9.

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo



128

(Fungu: Marko 7:6)
Yesu alisema, Mioyo yao iko mbali nami.
Unaona, ni swala la moyo .
Swala la upendo.



129

(Fungu: 1 Yohana 5:3)
Biblia yasema, Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito.
1 Yohana 5:3.



130

Yesu, alipokuwa akifundisha siku moja, aliwaambia wasikilizaji wake ya kwamba si kila mtu atakaye kwenda mbinguni.
Alisema utaujua mti kwa matunda yake, yakiwa mema au mabaya.



131

(Fungu: Mathayo 7:21)
Kisha akasema, Si kila mtu aniambiaye, 'Bwana, Bwana,' atakayeingia katika ufalme wa mbinguni,



132

bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Mathayo 7:21.


133

Hilo liko wazi kabisa. Mungu anawajua walio wake kwa kutizama tunda la maisha yao.
siyo tu wale wasemao ya kuwa ni wa Mungu, bali wale ambao hutenda kile alichowaambia wakitende.
Ni wale watu watakaokaribishwa katika ufalme wa Mungu.


134

Kama unampenda, utamruhusu awe ndiye anayeendesha maisha yako ili upate kutenda mapenzi yake. Tunapotunza Sabato, hatutunzi tu amri ya Mungu kwetu, bali pia tunafungua maisha yetu kwa mibaraka ya ajabu.

# 12 - Mamilioni Wamedanganywa na Uongo



135

Tunapotumia siku ile maalumu kila juma tukimkumbuka Muumbaji wetu na tukimwendea, tunafikia hatua ya kumjua sana na kwa ubora zaidi. Maisha yetu yamejazwa na shughuli nyingi sana siku hizil
Kila mmoja anaonekana kuwa katika kukimbia. Kuna mengi sana ya kufanya - na kuna wakati mchache sana wa kuyatenda yote!


136

Katikati ya huku kutimka kote na msongo na haraka, Mungu anatualika tutoke kidogo kwa siku moja na tupumzike.
Anatualika tutumie muda pamoja naye- tukimwabudu, tukinena naye, tukimsikiliza anenapo nasi kupitia katika Neno lake, Biblia.
Ni upendeleo mzuri ulioje - kutumia siku nzima kila juma tukifikiri na kuwasiliana na Yule aliyetuumba!


137

Hebu nilifanye swala kuwa wazi zaidi kwako, rafiki. Upande mmoja tunao ukweli wakati upande mwingine tunayo mapokeo.
Upande mmoja tunayo Biblia na mwingine, mafundisho ya wanadamu.
Upande mmoja tunayo amri ya Mungu, wakati huo upande mwingine tunayo mafundisho ya watu.
Upande mmoja tunayo Sabato wakati upande mwingine tunayo Jumapili.
Siyo swala la siku - ni swala la mabwana.
Siyo swala la kumtii Mungu - ni swala la kumfuata Yesu.
Je, ungependa kufanya uamuzi wa kuyatoa maisha yako kufuata ukweli wa Mungu badala ya kukubali mapokeo yaliyotengenezwa na mwanadamu? Kwa nini usimwambie Yesu ya kwamba utamfuata Yeye njia yote tunaposali.

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?



1

Mbingu, Kuzimu, au Hakuna chochote?


2

Mwaka wa 1956 Congo Ubelgiji (sasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo), ilinaswa katika mtego mbaya wa vita vya wenyewe kwa wenyewe. Hospitali ya Daktari Paul Carlson ilichukuliwa na majeshi ya waasi. Waajiriwa wengi wa hospitali waliuawa. Inasikitisha, kuwa Dk. Carlson alikuwa mmoja wao. Wakati mwili wake ulipokutwa siku chache baada ya mauaji ya kikatili, kulikuwa na Agano Jipya ndani ya mfuko wa koti lake. Katika kurasa zake, daktari alikuwa ameandika tarehe.
Ilikuwa siku moja tu kabla hajauawa, na aliandika neno moja kwa kalamu yake, amani.
Amani usoni pa mazingira mabaya kuliko yote. Amani katika kuikabili mauti. Ni nini kilichompa Dk. Paul Carlson amani ya namna hiyo?


3

Je, yawezekana kwetu kuwa na amani ya ajabu kiasi hiki wakati tunapokabiliana na mauti? Ni kitu gani kiwezacho kutuzuia tusisambaratike wakati mauti inapotufikia?
Yapo maswali mengi yaliyo magumu kuyajibu yahusuyo mauti. Ni kitu gani hasa kinachotokea wakati mtu anapokufa? Je, ni mbingu? Au mauti? Au hakuna chochote? Unajua kile ambacho hutokea kwa mwili halisi, lakini yu wapi mtu aliyekuwa ndani ya huo?
Watu wanapokufa, je, wanakoma kabisa kuwepo ama huendelea kuishi mahali fulani?


4

Maumivu ya mauti huchoma kiasi ambacho tunataka kuamini kabisa ya kwamba LAZIMA kuna namna ambayo wale tunaowapenda hawaendi kabisa -- na kwamba kama tukitafuta tu kidogo, tutapata njia ya kunena nao bado.

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?


5

Kwa msisitizo kabisa, sauti husikika zikituhakikishia ya kwamba haya yote ni ya kweli na yanawezekana. Hebu kwa mfano mfikirie huyu James Van Praagh. Kitabu chake 'Kunena na Mbinguni': Ujumbe wa wa Uzima Baada ya Mauti, kiliinuka na kuwa katika kilele cha orodha ya vitabu vilivyouzika zaidi baada ya kuonekana akihojiwa katika Larry King Show (CNN).



6

Mioyo yetu inalia kwa kutaka kujua ukweli halisi juu ya mauti ili iwe na amani tunapolikabili kaburi.



7

Je, Mungu analo la kusema juu ya somo hili?
Je, Biblia inalo lolote la kusema juu ya inavyokuwa tunapokufa?
Jibu ni la mkazo NDIYO!


8

Na jibu linapatikana katika ufufuo wa Yesu Kristo.


9

Baada ya Yesu kufa msalabani, rafiki zake waliuweka mwili wake, kama isemavyo Biblia, katika Kaburi la Yusufu.


10

Gavana wa Kirumi Pilato alituma ulinzi, na askari zake waliziba jiwe lililofunika mdomo wa kaburi kwa muhuri wa Kirumi.
Sasa hakuna ambaye angechukua mwili wake.
Hakuna yeyote, isipokuwa Baba ya Kristo.


11

Mapema Jumapili asubuhi wakati ikiwa bado giza, malaika aliyeng'aa alishuka toka mbinguni, akalivingirisha jiwe lililofunika mlango wa kaburi, na kumuita Kristo atoke.

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?


12

Mwokozi aliyefufuka alitoka akiwa katika ushindi kamili  juu ya mauti -- Mshindi Mkuu.
Askari walibwagwa chini wakawa kama wafu kwa utukufu wa malaika.



13

Kisa cha ufufuo wa Kristo kilikuwa ni kichocheo chenye nguvu kwa kanisa la awali la Kikristo -- kwani pia Warumi hawakuwa na tumaini lolote baada ya kaburi.
Yote waliyojua ilikuwa kwamba kaburi ni shimo refu, lenye giza  ambalo hakuna  aliyeweza kuwa na tumaini la kutoka tena akiwa hai kama alizikwa humo.
Sasa Wakristo walikuwa na ujumbe wenye tumaini la kweli zaidi.
Kaburi halikuwa mwisho wa yote.
Wale waliokufa katika Kristo siku moja wangeishi tena!


14

Makaburi yaliyoko chini ya Jiji la Rumi yanaonyesha tofauti kati ya mauti ya wapagani katika nyakati zile za kale - na ile ya Wakristo.
Tambua  maandishi yaliyoko katika makaburi ya wale waliokufa katika upagani usio na matumaini.


15

Tena na tena maneno haya yameandikwa yenye huzuni: Kwaheri milele --au, Kwa heri kwa umilele.
Kisha tambua maandishi yaliyoko katika makaburi ya Wakristo:


16

Kwa heri hadi tutakapokutana tena -- au, Usiku mwema hadi asubuhi.
Makaburi yao yaliandikwa yakionyesha matumaini na ujasiri, kwa kutizamia mbele katika siku ya ufufuo.



17

(Fungu: Ufunuo 1:18)
na aliye hai; nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele.

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?



18

Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu.
Ufunuo 1:18
Hakuna tumaini kwa ajili ya wakati ujao baada ya mauti kama Mkristo hajui kile alicho nacho Mungu kwa ajili yake.


19

Sura ya kumi na tano ya 1 Wakorintho ni makala kuu ya Paulo juu ya mauti na ufufuo.
Anataja wazi ya kwamba kama hakuna ufufuo, basi hakuna tumaini la wakati ujao kwa Mkristo.



20

(Fungu: 1 Wakorintho 15:16-18)
Tambua alichosema:
Maana kama wafu hawafufuliwi, Kristo naye hakufufuka.



21

Na kama Kristo hakufufuka, imani yenu
ni bure; mngalimo katika dhambi zenu!



22

Na hapo wao waliolala katika Kristo wamepotea.
1 Wakorintho 15:16-18.


23

Lakini kuelewa kwanini anasema alishosema, tuanpaswa kuelewa kile ambacho Biblia inafundisha kuhusu mauti yenyewe.

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?


24

Wakati Mungu alipomuumba mwanadamu, kamwe halikuwa kusudi lake kwamba yeyote apate kufa. Baada ya Mungu kumuumba Adamu, alitizama alichikifanya, na Biblia inatuambia katika Mwanzo 1:32 ya kwamba kila kitu kilikuwa chema sana! Hapakuwa na mauti, maradhi, au huzuni katika Sayari Dunia kabla na baada ya kuanguka kwa Hawa. Pengine waweza kukumbuka kile Mungu alichomwambia mwanadamu:



25

(Fungu: Mwanzo 2:16,17)
BWANA Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema, 'Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula;




26

walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile,




27

kwa maana siku utakayokula matunda ya mti huo utakufa hakika,'
Mwanzo 2:16, 17.


28

Sura inayofuata ya kisa hiki siyo ya furaha sana. Kisa cha kusikitisha kimerekodiwa kwa ajili yetu katika Kitabu cha Mwanzo, sura ya 3.


29

Mwovu, akimtumia joka kama wakala wake, alimtokea Hawa na kumjaribu ili asimtii Mungu na kula matunda ya mti uliopigwa marufuku.
Wakati Hawa alipoeleza ya kwamba Mungu alikuwa amemwambia asile matunda ya mti ule asije akafa,

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?



30

(Fungu: Mwanzo 3:4)
Joka alisema, .....Hakika hamtakufa.
(Fungu la 4)
Huu ni uwongo wa kwanza uliorekodiwa katika Biblia juu ya mauti!
Hawa alichagua kumwamini mwovu na kula matunda ya mti wa mema na mabaya.


31

Mungu alilazimika kuwatenganisha Adamu na Hawa toka kwa Mti wa Uzima, kwa sababu:



32

(Fungu: Mwanzo 3:22,23)
......Basi, huyu mtu amekuwa kama mmoja
wetu, kwa kujua mema na mabaya;



33

na sasa asije akanyoosha mkono wake
akatwaa matunda ya mti wa uzima, akala, akaishi milele.




34

Kwa hiyo BWANA Mungu,akamtoa katika bustani ya Edeni



35

ailime ardhi ambayo katika hiyo alitwaliwa.
Mwanzo 3:22,23.


36

Kifo kilikuja kwa wanadamu kwa sababu alikuwa ametenganishwa na Mungu, chanzo cha maisha na pia alitenganishwa na Mti wa Uzima.

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?



37

(Fungu: Mwanzo 3:18,19)
Mungu alimwambia Adamu wakati huu:
.............Nawe utakula mboga za kondeni.



38

Kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi,



39

kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi. Mwanzo 3:18,19


40

Hapa ndipo ulipo ufunguo wa kuelewa mauti ninini na kile Mungu anachokusudia kukitenda ili kutuokoa kutoka katikka utengano tulio nao naye.


41

Biblia yasema ya kwamba mwanadamu angerejea mavumbini ambapo alitwaliwa.
Tambua jinsi Mungu alivyomuumba Adamu:



42

(Fungu: Mwanzo 2:7)
BWANA Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi,



43

akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai.
Mwanzo 2:7.

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?




44

Mungu alichukua vitu vya asili vya nchi na kuutengeneza mwili kwa ajili ya mwanadamu. Wakati alipomaliza kuuumba mwili kwa ajili ya mwanadamu, alikuwa tu na mwili usio na uhai -- mwili tu.
Kuna kilicho hitajika zaidi ili kumfanya awe kiumbe hai.
Biblia yasema hapa ya kwamba Mungu alimpulizia katika pua zake Adamu pumzi ya uhai -- na mtu akawa nafsi hai.




45

Twaweza kutengeneza mlinganyo wa namna hii:
Mwili + Pumzi ya Uhai = Nafsi Hai




46

Au kwa swala la mauti, twaweza kuandika;
Mtu hai - Pumzi ya Uhai = Maiti.




47

(Fungu: Mhubiri 12:7)
Hilo ndilo alilolisema mwenye hekima katika Mhubiri: Nayo mavumbi kuirudia nchi kama yalivyokuwa, nayo roho kumrudia Mungu aliyeitoa. Mhubiri 12:7.




48

Hili ndilo ambalo limekaziwa pia katika Kitabu cha Ayubu - Kitabu cha kwanza kuandikwa kati ya Vitabu vya Biblia -- hiki ndicho kisemacho juu ya mauti.




49

(Fungu: Ayubu 27:3)
(Kwa kuwa uhai wangu ukali ndani yangu,
na roho ya Mungu i katika pua yangu;)
Ayubu 27:3.
Tambua ya kwamba Biblia yasema, Kwa kuwa roho ya Mungu ikali katika pua yangu.

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?


50

Hicho ndicho Mungu alichokiweka katika pua ya mwanadamu  hapo alipomuumba.




51

(Fungu: Zaburi 146:3,4)
Hebu tuweke mtizamo wetu katika fungu jingine:
Msiwatumainie  wakuu, Wala
binadamu ambaye hakuna  wokovu  kwake.



52

Pumzi yake hutoka, huurudia udongo wake,
Siku hiyo mawazo yake yapotea.
Zaburi 146:3,4.


53

Mfalme Daudi anaufunua ukweli juu ya mauti anaposema ya kwamba pumzi huuacha mwili na kuirudia ardhi. Mtu anakufa.



54

(Fungu: Mhubiri 9:5,6)
Hili linapatana na lile alisemalo Sulemani:
Kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba  watakufa;
lakini wafu hawajui lolote, wala hawana  ijara tena;



55

maana  kumbukumbu lao limesahauliwa.



56

Mapenzi yao na machukio yao, na husuda yao, imepotea....
Mhubiri 9:5,6.

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?




57

Hajui chochote!
Hakuna!
Hakuna chochote!
Hii inapelekana na kile alichokisema mtunga Zaburi, ya kwamba wafu hawapo mbinguni wakimtukuza Mungu.
Hivyo wako wapi sasa? Lazima uulize.




58

(Fungu: Zaburi 115:17)
Daudi analiweka wazi: Siyo wafu  wamsifuo BWANA, wala wao  washukao  kwenye kimya.
Zaburi 115:17.



59

(Fungu: Ayubu 14: 10, 12,13)
Lakini mwanadamu hufa, huifariki dunia;
Naam mwanadamu hutoa roho, naye yupo wapi?




60

Ni vivyo mwanadamu hulala chini,asiinuke;
Hata wakati wa mbingu kutokuwako  tena,




61

hawataamka, wala kuamshwa usingizini.



62

Laiti  ungenificha  kuzimuni, ukanilinda
kwa siri,  hata ghadhabu zako zitakapopita,



63

na kuniandikia  muda ulioamuriwa, na kunikumbuka!
Ayubu 14:10,12,13.

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?



64

Hapa tunalo hili toka kwa Neno pekee la Mungu ya kwamba mwanadamu hufa na kulala chini katika kaburi na hainuki  hadi siku ya ufufuo.
Tambua anavyolifafanua hili:



65

(Fungu: Ayubu 14:14,15)
Mtu akifa, je, atakuwa hai tena? Mimi ningengoja siku zote za vita  vyangu, hata kufunguliwa  kwangu kunifikie.



66

Wewe ungeniita, nami  ningekujibu.....
Ayubu 14:14,15.



67

(Fungu: Ayubu 17:13)
Tambua jinsi Ayubu anavyotuambia: Nikitazamia kuzimu kuwa
nyumba yangu; Nikitandika  malazi yangu gizani;
Ayubu 17:13



68

Tambua pia ya kwamba Ayubu alitumia neno usingizi katika kuzungumzia juu ya mauti.
Ndilo jambo hilo hilo waandishi wengine wa Biblia wanalisema.



69

(Fungu: Zaburi 13:3)
Daudi aliandika: Ee BWANA, Mungu wangu, uangalie, uniitikie; uyatie nuru macho yangu, nisije nikalala  usingizi wa mauti.
Zaburi 13:3.
Daudi aliogopa  kulala usingizi wa mauti-- alitaka kuishi!

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?



70

(Fungu: Danieli 12:2)
Danieli anaeleza juu ya wafu ambao watafufuliwa:Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele,wengine aibu na kudharauliwa milele.
Danieli 12:2.


71

Moja ya kweli zinazofariji katika Neno la Mungu ni kwamba wakati mtu anapokufa, mtu huyo hupumzika kimya, asisumbuliwe na matatizo ya maisha hadi mwito wa Mpaji wa Uzima.
Je, inashangaza ya kwamba Biblia inafananisha mauti na usingizi?


72

Nabii Nathani alimwambia Mfalme Daudi kile kitakachotokea kwake wakati wake wa kufa ukifika.



73

(Fungu: 2 Samweli 7:12)
Nawe siku zako zitakapotimia, ukalala na baba zako,
2 Samweli 7:12.


74

Yesu mwenyewe aliita mauti usingizi.
Alitumia neno hilo hilo katika kueleza juu ya kifo cha rafiki yake mpendwa, Lazaro.
Hebu tuangalie jinsi Yesu na washirika wake wa karibu walivyozungumza juu ya kifo.
Kulikuwa na nyumba katika Bethania ambayo Yesu mara kwa mara aliitembelea - nyumba ya Lazaro, Mariamu, na Martha.



75

(Fungu: Yohana 11:5)
Biblia yasema,Naye Yesu alimpenda Martha, na umbu lake (dada yake), na Lazaro. Yohana 11:5

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?


76

Siku moja wakati Yesu na wanafunzi wake walipokuwa kando kando ya mto Yordani, alipokea ujumbe wa muhimu toka kwa rafiki zake watatu waliokuwa Bethania  ya kwamba Lazaro alikuwa mgonjwa sana, lakini Yesu akakaa pale alipokuwa siku zingine mbili.




77

(Fungu: Yohana 11:11,12,14,15)
Kisha, baada ya hayo, akawaambia, Rafiki yetu, Lazaro, amelala; lakini ninakwenda nipate kumwamsha.



78

Basi wale wanafunzi wakamwambia, 'Bwana, ikiwa amelala, atapona.'



79

Basi hapo Yesu akawaambia waziwazi, Lazaro amekufa;



80

Nami nafurahi kwa ajili yenu kwamba sikuwako huko, ili mpate kuamini; lakini na twendeni kwake.'
Yohana 11:11-15


81

Wakaelekea Bethania mahali ambapo familia ilikuwa ikiishi.
Walipolikaribia jiji, Martha alikuja kuwalaki akikimbia.



82

(Fungu: Yohana 11:21,23,24)
Alipokutana na Yesu, alisema, Basi Martha akamwambia  Yesu,  'Bwana, kama ungalikuwapo hapa, ndugu yangu hangalikufa.'
Yohana 11:21.
Bila ya shaka alikuwa sahihi juu ya hilo!
Lakini, Yesu alikuwa na mpango.

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?



83

Alisema, Ndugu yako atafufuka.
Sasa tazama kwa uangalifu jibu la Martha:



84

Martha akamwambia, Najua ya kuwa atafufuka katika ufufuo siku ya mwisho.
Yohana 11:23-24.
Martha alimhakikishia Yesu ya kwamba alitegemea kumuona Lazaro katika ufufuo mwisho wa dunia.



85

Hata hivyo, Yesu alikuwa anakaribia kuonyesha kabla ya wakati wake lile tukio la siku ya mwisho leo.



86

(Fungu: Yohana 11:25)
Kisha Yesu akasema wazi wazi: ...Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi.
Yohana 11:25.



87

Yesu alipofika kwenye kaburi la Lazaro, Yohana anatuambia



88

(Fungu: Yohana 11:35)
Ya kwamba Yesu akalia machozi!
Hakuwa akilia kwa ajili ya Lazaro rafiki yake.
Alijua alikuwa akienda kumfufua awe hai tena.


89

Alikuwa akilia kwa sababu ya huzuni iliyokuwa ikipitiwa na hii familia na marafiki na kwa ajili ya wote wale ambao katika vizazi vyote wanahuzunuka na kuomboleza wanapopotelewa na wapendwa wao.

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?


90

Yesu aliomba kuwa jiwe lile lililoziba



91

kaburi liondolewe.



92

(Fungu: Yohana 11:39)
Akijihisi kuhusika na ombi la Yesu, Martha alipinga:....Bwana, ananuka sasa; maana amekuwa maiti siku nne.
Yohana 11:39.
Ndiyo, Yesu alichelewa kwenda zake Bethania kwa siku nne. Huku kuchelewa kungefanya bila wasiwasi nafasi ya kutosha ya ukweli wa Lazaro kuwa mfu.


93

Lakini jiwe lilikuwa limevingirishwa mbali, na Yesu akapaza sauti yake, LAZARO, NJOO HUKU NJE!


94

Mtu mmoja amesema ilikuwa ni vyema ya kwamba Yesu alitamka jina mahususi kwamba alinena kwa Lazaro; vinginevyo, kila kaburi kwenye Sayari Dunia lingefunuka!


95

Ilikuwa siku ya maana kiasi gani kwa marafiki watatu wa Bethania!
Ilikuwa shangwe na furaha kiasi gani!
Marafiki, hii ilikuwa ni siku ya kusisimua pale Bethania,

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?


96

lakini ilikuwa kionyesho kidogo tu  cha utukufu na msisimko utakaotokea wakati  Yesu akija tena na makaburi ya marafiki zake wote  ambao watakuwa walimkubali Yeye kama Mwokozi yatakapofunguka-- na watakapoamka ili kumlaki angani!
Huu ni ujumbe wa faraja  ambao mtume Paulo alishiriki na Wakristo wa awali:



97

(Fungu: 1 Wathesalonike 4:13,16)
Lakini, ndugu, hatutaki msijue habari zao walio lala mauti,



98

msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini.
1 Wathesalonike 4:13.
Paulo anatuambia kile ambacho Yesu atakitenda wakati ajapo mara ya pili:



99

Kwa sababu  Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na  mwaliko, na sauti ya malaika mkuu,



100

na parapanda  ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza.
1 Wathesalonike 4:16.


101

Paulo anaeleza wazi kwa undani matukio yatakayotokea  wakati Yesu ajapo:



102

(Fungu: 1Wakorintho 15:51-55)
Angalieni, nawaambia ninyi siri; hatutalala sote,  lakini  tutabadilika,

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?



103

kwa dakika moja, kufumba na kufumbua,
wakati wa parapanda ya mwisho;



104

Maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa,
wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika.
1 Wakorintho 15:51, 52.
Kisha Paulo anatuambia jinsi tutakavyobadilishwa:



105

Maana sharti huu uharibikao uvae kutokuharibika,
nao huu wa kufa uvae
kutokufa.



106

Basi huu uharibikao utakapovaa
kutokuharibika, na huu wa kufa utakapovaa
kutokufa,



107

hapo ndipo litakapokuwa lile neno lililoandikwa,
'Mauti imemezwa kwa kushinda.'




108

.....Ku wapi Ewe Mauti kushinda kwako?
1 Wakorintho 15:53-55.


109

Yesu aliwaambia wanafunzi ya kwamba wote
wangefufuliwa toka kaburini.



110

(Fungu: Yohana 5:28,29)
Msistaajabie maneno hayo, kwa maana
saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini
wataisikia sauti yake

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?



111

Nao watatoka;wale waliofanya
mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda
kwa ufufuo wa hukumu,



112

na wale waliotenda kwa ufufuo wa hukumu.
Yohana 5:28,29.



113

Fikiria kwa muda mfupi: Kama watu wangelikuwa wanakwenda mbinguni au jehanamu wakifa, kwa nini basi kuwepo na hitaji la ufufuo wa ama wenye haki au wasio haki?
Kwa nini basi Yesu atoe kauli hii ajapo mara ya pili?



114

(Fungu: Ufunuo 22:12)
Tazama, naja upesi, na ujira wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo.
Ufunuo 22:12.


115

Inaonekana kuwa wazi kabisa!
Wakati watu wanapokufa, wanalala usingizi, wanapumzika toka katika taabu zao na shida zao hadi Yesu anapokuja.


116

Anakuja kwa ajili ya nani?
Anakuja ili kuwafufua na kuunganika na wale ambao wameikubali kafara yake iliyotolewa kwa niaba yao.
Yesu pia anakuja kuwakaribisha wale ambao wamekuwa wafuasi wake waaminifu wakati huo.
Hebu tega sikio tu kwa habari hii njema!



117

(Fungu: 1 Wathesalonike 4:17)
Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja na Bwana milele.

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?



118

na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.
1 Wathesalonike 4:17.


119

Tumeona ya kwamba waliookolewa wote watakuwa na miili itakayokuwa na utukufu kama Yesu, na watapokea kule kutokufa (uzima wa milele) ili wapate kuwa na Bwana milele.


120

Mtu aweza kuuliza, Habari gani juu ya yule mwizi msalabani?


121

Hebu na tuone kile Biblia inachokifundisha juu ya yule mwizi na ahadi ambayo Yesu alimpatia.
Yesu alisulubishwa kati ya wevi wawili ili kwamba wale wanaomsulubisha wapate kumtambua kama mwenye chembe chembe za uhalifu.



122

Kitabu cha Marko kinasema ya kwamba mwanzoni, wevi wote wawili walimdhihaki Yesu na kusema kama kweli alikuwa na uwezo, basi angelijiokoa Yeye mwenyewe na wao. Kisha mmoja wa wale wezi akatubu na kuulilia wokovu.



123

(Fungu: Luka 23:42,43)
Kisha akasema, Ee Yesu, nikumbuke utakapoingia katika ufalme wako.



124

Yesu akamwambia, 'Amin, nakuambia, leo hivi, utakuwa pamoja nami peponi.'
Luka 23:42,43.

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?


125

Hebu tuitazame ile ahadi tena. Ndiyo, rafiki! Leo, sasa hivi, wewe pia waweza kuwa na uhakika huo . Katika Kristo kunao huo uhakika.


126

Hata ingawa Kristo angekufa katika siku ile, na angelala kaburini  hadi siku ya Jumapili alfajiri, Yesu alitoa uhakika wa kutoka kaburini.



127

(Fungu: Luka 23:43)
Uhakika wa ajabu kiasi gani kwa mwivi aliyekuwa katika kufa! Wakati hakukuwa na matumaini kwa ajili yake. Wakati ambapo yote yaliyoonekana ni giza lililotisha roho yake, Yesu aliweza kumuahidi tumaini hata baada  ya kaburi.
Yesu alimuahidi mwizi katika saa ile ile, Leo ninakwambia, au sasa hivi ninakwambia, 'utakuwa pamoja nami Paradiso.'



128

Baadhi ya watu hudhania ya kwamba Yesu alimuahidi mwizi ya kwamba angeenda Paradiso mara moja. Lakini Yesu mwenyewe hakuenda Paradiso mara moja alipofariki.


129

Biblia inatuambia  ya kwamba alikufa siku ile, Ijumaa, na alizikwa katika kaburi lililoazimwa.


130

Siku ya Jumapili asubuhi, Yesu alimtokea Mariamu, na alitaka kumuabudu, lakini alimzuia kwa sababu alikuwa bado hajaenda mbinguni. Sikiliza kwa alilosema:

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?



131

(Fungu:Yohana 20:17)
...Sijapaa kwenda kwa Baba....
Hii ilikuwa Jumapili asubuhi, na alisema hajapaa kwenda kwa Baba yake! Yohana 20:17.
Yesu hakuwa Paradiso siku ya Ijumaa!


132

Biblia inatuambia pia ya kwamba mwizi hakuwa Paradiso siku ya Ijumaa pia.



133

(Fungu: Yohana 19:31-33)
Kwa sababu ni Maandalio, miili isikae juu ya msalaba siku ya sabato,




134

(maana sabato ile ilikuwa siku kubwa), walimwomba Pilato miguu yao ivunjwe, wakaondolewe. Yohana 19:31



135

Basi askari wakaenda, wakamvunja miguu wa kwanza, na wa pili, aliyesulubiwa pamoja naye.



136

Lakini walipomjia Yesu na
kuona ya kuwa amekwisha kufa,
hawakumvunja miguu. Yohana 19:31-33


137

Hapa tunaona ya kwamba walivunja miguu ya wevi ili wasiweze kutoroka,

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?


138

lakini wawakuvunja miguu ya Yesu kwani alikuwa ameshakufa siku hii ya Ijumaa.
Hivyo, Kristo wala mwizi hakuna aliyekuwako Paradiso siku ya Ijumaa.


139

Yesu alilipa gharama kwa ajili ya ukombozi wetu na kurejeshwa kwetu.


140

Zawadi kuu kuliko zote ambayo Mungu aweza kuitoa kwa mwanadamu ni uzima wa milele, ushindi juu ya mauti!
Karama zingine zote hazina maana kama hiyo haipo!
Na ni yako ikiwa tu utaiomba!


141

Uamuzi wako ni uamuzi mkuu kuliko wote uwezao kuufanya; wakati wako wa milele ujao unategemea sana hilo!



142

Hii karama yenye thamani kubwa sana ya uzima wa milele imeahidiwa kwa kila mmoja anayemkubali Kristo kama Mwokozi wake na Bwana.
Na bei? Ni moyo tu uliokabidhiwa.
Moyo uliotakaswa na kubadilishwa.
Moyo uliokuwa na kiburi na ubinafsi ufanywao upya chini ya msalaba.
Kristo alifanya yote yawezekane pale Kalvari.
Angefanya lipi zaidi?


143

Na uzima wa milele waweza kuwa wako kama unautaka kikamilifu.

# 13 - Kitu Gani Kinatokea Unapokufa?


144

Kwa sababu yu hai,
tunalo tumaini lenye utukufu--tumaini lipitalo kaburi!


145

Jioni moja mfululizo wa mikutano ulikuwa ukiendelea katika mji mmoja mdogo katika sehemu ya mashariki ya Marekani. Kijana mmoja alitanga na kuingia katika mikutano hii akiwa mwenye huzuni nyingi.


146

Ukumbi wa mikutano ulikuwa karibu tu na makaburi. Kabla ya kuingia ukumbini mahali mikutano ilipokuwa ikifanyikia, huyu kijana alitembea polepole katika yale makaburi. alihoji maana ya uhai.
Alitamani msamaha na amani mawazoni.
Alipokuwa akiwaza juu ya mauti, alihitaji zaidi ya yote uhakika wa uzima wa milele.


147

Kichwa cha somo la Biblia jioni ile kilikuwa Tumaini Baada ya Kaburi. Kijana huyu aliketi katikati ya mkutano akisikiliza kwa makini.
Usiku ule ule alitoa maisha yake kwa Kristo.
Usiku ule ule alimkubali Kristo aliyekufa kwa ajili yake na kufufuka toka kwa wafu ili kumpa uzima wa milele.
Usiku ule ule maisha ake yote yalibadilishwa na huyu Kristo aliye hai.
Usiku ule ule amani iliiijaza roho yake.
Usiku ule ule tumaini jipya lilichipuka katika moyo wake.


148

Waweza kuwa na amani hii - tumaini hili -uhakika huu wa uzima wa milele - maisha baada ya kaburi. Kama unataka uhakika huu, je waweza kusimama sasa hivi tunaposali?

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi




1

Je, Walio Hai Waweza Kunena na Wafu?



2

Watu wanapokufa, je, hurudi katika mfumo wa roho na kuwatembelea wale walio hai bado?
Je, roho za wafu zaweza kurejea na kunena na walio hai?
Katika mauti, je, ni mwili tu unaokufa wakati roho ikiendelea kuishi?



3

Je, wanaoamini mizimu na wataalamu wa mambo ya roho na mawakala wa mizimu na wapashaji habari wa mizimu wanapotuambia ya kwamba watatupa mawasiliano na roho za wapendwa wetu waliopotea katika mauti wapo sahihi?




4

Na je, roho za watu waliokufa zaweza kutawala watu walio hai, kwa kutumia miili yao, sauti zao, mawazo yao, kutenda na kunena?




5

Tunachokizungumzia sasa hivi ni moja ya matatizo mazito kabisa ambayo yeyote kati yetu anaweza kukutana nayo.



6

Na ni muhimu kiasi kwamba kwa kweli yaweza kuitwa maswala ya uzima au mauti.
Uzima wetu wa milele unawekwa hatarini.
Hivyo ni lazima tuwe na hakika kuhusu jambo hili.
Twawezaje kujua kwa hakika kama uzoefu tulio nao ni wa kweli na hakika - ama ni uongo na hatari?




7


Jibu ni lile lililoko katika Biblia, Yesu anatupatia ukweli!

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi



8

Yesu ni rafiki yetu. Yeye anaelewa kile tunachokipitia tunapokuwa tumepoteza mpendwa wetu katika bonde la mauti.
Yeye huguswa  na huzuni yetu. Amewahi kuwa hapo.
Hivyo tutarejea kwa Yesu ili kugundua kile ambacho amekisema juu ya mauti, ufufuo na uzima wa milele.
Kama Yesu alisema, nitaweka maisha yangu kwa imani katika hilo.
Hilo linatatua tatizo lote. Je, twaweza kukubaliana katika hilo?



9

Je, una shukurani kwa ajili ya Yesu?
Yeye huguswa na huzuni yako.




10

(Fungu: Yohana 11:35)
Katika mazishi ya rafiki yake, Biblia yasema ya kwamba Yesu akalia machozi. (John 11:35 )
Amewahi kuwa katika bonde la uvuli wa mauti yeye mwenyewe.





11

(Fungu: Ufunuo 1:17,18)
.....Usiogope; mimi ni wa kwanza na wa mwisho.




12

Na aliye hai; nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na  milele.




13

Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu.
Ufunuo 1:17,18.
Lililo zaidi, Yesu ni Mpaji wa Uzima.
Amekuja ili tupate kuwa na uzima tele sasa.

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi



14

(Fungu: Yohana 10:10)
....mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.
Yohana 10:10
Anaahidi kurejeshwa kwa uzima milele.



15

(Fungu: Yohana 11:25)
Yesu akamwambia, 'Mimi ndimi huo ufufuo na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi.'
Yohana 11:25
Yesu ni Bingwa wa Uhai.
Anajua juu ya uhai zaidi ya yeyote katika ulimwengu, kwa sababu Aliumba uhai katika sayari hii.



16

(Fungu: Yohana 1:1,3)
Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.



17

Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika.
Yohana 1:1,3.



18

(Fungu: Wakolosai 1:16)
Kwa kuwa katika Yeye vitu vyote viliumbwa,
.......vitu vyote viliumbwa kwa njia yake na kwa ajili yake.
Wakolosai 1:16.


19

Ni muhimu tunapofikia katika mada hii kupitia kile ambacho tumejifunza hadi sasa katika mfululizo wa masomo haya.
Yesu alilifanya hili kuwa wazi kabisa ya kwamba kifo siyo uzima, wala si muendelezo wa uhai katika mfumo mwingine.

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi



20

(Fungu: Yohana 11:11)
Kuhusiana na rafiki yake aliyekuwa amefariki, Yesu alisema, ....Rafiki yetu, Lazaro, amelala... Yohana 11:11.
Alikuwa akinena juu ya mtu aliyekuwa amefariki. Tazama jinsi Yesu anavyoeleza juu ya mauti: Usingizi. Ndiyo namna iliyo ya karibu zaidi ya kufananisha mauti katika Biblia.



21

(Fungu: Yohana 11:14)
Ili wanafunzi wake wasishindwe kumuelewa, Yesu alisema kwa uwazi kabisa, Lazaro amekufa. Yohana 11:14.
Lazaro hakuwa hai mahali fulani katika mfumo mwingine.


22

Alikuwa amekufa, na mwili wake ulikuwa katika kaburi. Yesu alifundisha zaidi waziwazi ya kwamba hakuna uhai  baada ya kifo hadi ufufuo, na alibainisha wazi kabisa ya kwamba ufufuo uko wakati wa usoni kabisa.



23

(Fungu: Yohana 6:40)
Kwa kuwa mapenzi yake Baba yangu ni haya, ya kwamba kila amtazamaye Mwana na kumwamini Yeye,



24

awe na uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho.
Yohana 6:40


25

Mioyo yetu imestuliwa kwa jinsi ambavyo tumejifunza juu ya kurudi kwa Yesu mara ya pili. Kuja kwake ni dhahiri, na kunaweka nuru kubwa katika somo la uzima na mauti.
Kwa nini anarejea?


# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi





26

(Fungu: Yohana 14:1-3)
Msifadhaike  mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi.




27

Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali.



28

Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu;




29

ili nilipo mimi, nanyi muwepo.
Yohana 14:1-3



30

Yesu yeye mwenyewe alielezea tukio la muhimu:



31

(Fungu: Mathayo 24:30,31)
Ndipo itakapoonekana ishara yake Mwana wa Adamu mbinguni; ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboleza,



32

nao watamwona
Mwana wa Adamu
akija juu ya mawingu
ya mbinguni pamoja
na  nguvu na
utukufu mwingi.

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi



33

Naye atawatuma malaika zake pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watawakusanya wateule  wake toka pepo nne,



34


toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu. Mathayo 24:30,31


35

Kwa nini tarumbeta? Kwa nini malaika?



36

Ili kuwaamsha wateule toka katika usingizi wa mauti na kuwakusanya ili kuwachukua mbinguni -- mahali ambapo Yesu amepaandaa kwa ajili ya wale wampendao. Kuja kwa Bwana kunaelezwa kwa undani usio na makosa:




37

(Fungu: 1 Wathesalonike 4: 13-18)
Lakini, ndugu, hatutaki msijue habari zao walio lala mauti, msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini,



38


msije mkahuzunika kama  na wengine wasio na matumaini.



39


Sisi tunaamini kwamba Yesu alikufa, akafufuka; na hivyo sisi tunaamini kwamba Mungu atawaleta pamoja na Yesu wale wote waliofariki wakiwa wanamwamini. (1 Wathesalonike 4:14 HNKK)

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi




40

Hili tunalowaambieni ni fundisho la Bwana; sisi tulio hai, ambao tutakuwa tumebaki, wakati Bwana atakapokuja, hakika hatutawatangulia wale waliokwisha fariki dunia.
(1 Wathesalonike 4:15 HNKK)



41

wakati Bwana atakapokuja,
hakika hatutawatangulia
wale waliokwisha fariki dunia.




42

Maana patatolewa amri, sauti ya malaika mkuu, sauti ya tarumbeta ya Mungu, Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni.




43

Ndipo wale waliokufa wakiwa wanamwamini Kristo watafufuliwa kwanza.




44

Kisha sisi tulio hai wakati huo tutakusanywa pamoja nao katika mawingu kumlaki Bwana hewani.



45

Na hivyo tutakuwa daima pamoja na Bwana.
(1 Wathesalonike 4:17 HNKK)



46

Basi, farijianeni kwa maneno haya.
1 Wathesalonike 4: 13 - 18



47

Tambua, tafadhali, kweli tatu muhimu zilizotajwa hapa:

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi



48

1. Hii ni kulingana na Neno la Mungu Mwenyewe. Hili ndilo Yesu mwenyewe alifundisha na kwa hivyo anatatua tatizo kwa ajili yetu.



49

2. Wakristo watakaookutwa wakiwa hai wakati Yesu akirudi wananyakuliwa juu pamoja na wale ambao wamefufuliwa toka katika mauti wakati wa kuja kwa Kristo mara ya pili.
Walio hai hawatawatangulia wale walio lala katika Yesu, na wala watu waliokufa hawatangulii mmoja mmoja wanapokufa.



50

3. Usingizi ni neno lililotumiwa na Yesu na Paulo kuelezea mauti kabla ya ufufuo: Waliolala katika Yeye [Yesu].
Yesu analiweka bayana na wazi kabisa ya kwamba mauti si uhai ambapo watu huwa na fahamu. Hakuna fahamu katika mauti. Ufahamu ni sehemu ya muhimu ya mawazo, na katika mauti mawazo hukoma kufanya kazi.



51

(Fungu: Mhubiri 9:5)
Kwa hili Biblia inaliweka wazi kabisa: Kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba watakufa; lakini wafu hawajui neno lolote,..........
Mhubiri 9:5



52

Je, wafu wanajua kiasi gani? Hakuna.
Haiwezekani basi kwa wafu kuwasiliana na walio hai.
Imani hii ya kwamba mtu huishi mara anapokufa inatoka wapi basi?



53

(Fungu: Ayubu 7:9,10)
Biblia hufundisha hali ya kutojua lo lote ya mtu awapo amekufa, Ayubu alisema wazi kabisa, Kama vile wingu likomavyo na kutoweka, Ni vivyo huyo ashukaye kuzimuni hatazuka tena kabisa.

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi



54

Hatarudi tena nyumbani kwake, wala mahali pake hapatamjua tena. Ayubu 7:10



55

Imani hii hutoka kwa Shetani mwenyewe. Katika Bustani ya Edeni, alimdanganya Hawa na kumsababisha yeye, na mumewe, kupoteza nyumba yao ya bustannini na hatimaye uhai wenyewe. Shetani alipata mbinu ya kumtumia nyoka ili kumnasa Hawa na kunena kupitia kwa huyo -nyoka. Yeye ni mdanganyifu mkuu.



56

(Fungu: Mwanzo 3:4)
Aliamini uongo wa Shetani: ....Hakika hamtakufa. Mwanzo 3:4.



57

(Fungu: Mwanzo 2:17)
Hii ilikuwa namna ya kupinga moja kwa moja kweli ya Mungu: ...Utakufa hakika. Mwanzo 2:17. Swala lipo hapa : Tumuamini nani?



58

Muamini mizimu husema (na hili hurudiwa rudiwa na maelfu ya wataalamu wa mizimu - watambuzi wa roho - pote duniani), Yawezekana kuwasiliana  na wapendwa wetu waliotuacha.
Je, hii ni sahihi? Je, yawezekana? La.


59

Kutokana na mafundisho ya Yesu, tunajua kabisa ya kwamba walio hai hawawezi kuwasiliana na walio kufa. Kwa nini haiwezekani? Wafu hawajui neno lolote.
Wanalala usingizi wa kutojitambua wa mauti.
Waweza kuuliza -- na kwa namna fulani kama unayo mawasiliano na roho hizi--

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi



60

Kama wafu hawana fahamu,
hawa 'roho' ni nani wanaowasiliana
na walio hai?


61

Biblia inaweka wazi kabisa ya kwamba hawa ni nani.




62

Kisha nikaona pepo wabaya watatu walio kama vyura,




63

wakitoka kinywani mwa yule joka, kinywani mwa yule mnyama, na kinywani mwa yule nabii wa uongo.



64

Hawa ndio roho za pepo wafanyao miujiza. Ndio wanaokwenda kwa wafalme wa ulimwengu wote



65

na kuwakusanya pamoja kwa ajili ya vita kuu Siku ile ya Mungu Mwenye Uwezo.
Ufunuo 16:13,14


66

Biblia inafunua zaidi juu ya siyo tu ya kwamba hawa ni nani bali pia wanakotokea:



67

(Ufunuo 12:7-9)
Kisha kukazuka vita mbinguni: Mikaeli na malaika wake walipigana na hilo joka, nalo likawashambulia pamoja na malaika wake. (Ufunuo 12:7 HNKK)

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi



68

Lakini joka hilo halikuweza kuwashinda,  na hatimaye hapakuwa tena na nafasi mbinguni kwa ajili yake na malaika wake.



69

Basi, joka hilo kuu likatupwa nje. Joka hilo ndiye yule nyoka wa kale ambaye huitwa pia Ibilisi au Shetani. Ndiye anayeudanganya ulimwengu wote.



70

Naam, alitupwa duniani, na malaika wake wote pamoja naye. (Ufunuo 12:7-9)


71

Hawa ni malaika walioanguka! Marafiki, Muwe Macho!  Ni jambo la hatari kuliko yote uwezalo kulifanya kuwa na uhusiano wo wote na roho. Kusudi pekee, ninarudia, kusudi lao la pekee ni kukudanganya  wewe na kukugeuza uwe mbali na Yesu na kukusabisha wewe upoteze uzima wako wa milele.


72

Linapaswa kufanya nywele zako zisimame, litetemeshe hata uti wako wa ubongo, na kukusabisha uweke umbali kati yako na roho. Kama unaamini ya kwamba wafu wako hai, umefungua mlango wa kudanganywa hadi kupotea, kwa sababu bado hujaona lo lote!


73

Mungu katika Neno lake amehukumu  moja kwa moja  mambo umizimu na kupiga marufuku jaribio lo lote la mwanadamu kuwasiliana na wafu. Tambua onyo ambalo Mungu alilitoa kwa watu wake kuhusu kumuona au kumtafuta mtu anayejaribu kunena na roho zijulikanazo.

14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi




74

(Fungu: Mambo ya Walawi 19:31)
Msiwaendee wenye pepo, wala wachawi; msiwafatute; ili kutiwa unajisi na wao;



75

Mimi ndimi BWANA, Mungu wenu.




76

(Fungu: Kumbukumbu la torati 18:10-12)
Kabla wana wa Israeli hawajaingia Kaanani, walionywa vikali, Asionekane kati kwako mtu ......mchawi,



77

au mwenye kubashiri au msihiri au apandishaye pepo au mchawi au mtu aombaye wafu.



78

Kwa maana mtu atendaye hayo ni chukizo kwa BWANA..... Kumbukumbu 18:10-12, Mungu anajua ya kwamba watu wanao wasiliana na roho za namna hiyo watasababisha watu wake kupotoka na kwa hivyo aliwaambia hivi:



79

(Fungu: Kutoka 22:18)
Usimwache mwanamke mchawi kuishi.


80

Uzoefu wa Mfalme Sauli katika kukutana kwake na mchawi unaeleleza juu ya upumbavu wa kujaribu kunena kwa wafu.



81

(Fungu: 1 Wakorintho 10:13)
Basi Sauli alikufa kwa sababu ya kosa lake alilomkosa BWANA ......

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi



82

na tena kwa kutaka shauri kwa mwenye pepo wa utambuzi , aulize kwake. 1 Mambo ya Nyakati 10:13


83

Shetani mwenyewe atajaribu kumuiga Yesu mwenyewe.



84

(Fungu: 2 Wakorintho 11:14 HNKK)
Wala si ajabu, maana hata Shetani mwenyewe hujisingizia kuwa malaika wa mwanga!


85

Je, umepata kushangaa jinsi gani mtu aweza kunena na mtu ambaye anafanana, anazungumza, anatenda kama mtu waliyekuwa wanamfahamu kabla ya kufa kwake?
Biblia yasema ni kwa sababu ya Shetani (na malaika zake) uigaji.


86

Wanaweza kumuiga mtu ye yote ambaye amepata kuishi. Inatisha kabisa kufikiri ya kwamba watu wazuri waweza kudanganywa hivyo na kuvutwa na kukumbatiwa na Shetani, hali wakidhani ya kwamba wanafurahia faraja ya kuwa na wenzi wao waliopotea katika mauti!


87

Lakini maandiko haya yanafunua kitu fulani ambacho ni kibaya zaidi: Shetani mwenyewe atatafuta kumuigiliza Yesu.
Je, waweza kufikiria jinsi umati wa watu utakavyodanganywa kwa sababu hawajui kweli ya kuja kwa mara ya pili kwa Yesu?
Je, hili hushangaza hata kidogo ya kwamba Yesu alitoa onyo kali kiasi hicho juu ya swala hili hili?

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi



88

(Fungu: Mathayo 24:4,5)
Yesu akawajibu, Jihadharini msije mkadanganywa na mtu




89

Maana wengi watatokea na kulitumia jina langu wakisema: Mimi ndiye Kristo,
nao watawapotosha watu wengi. (Mathayo 24:4,5
Hili swala ni zito sana kiasi kwamba


90

Yesu alirudia onyo lile lile katika hotuba yake:



91

Basi, mtu akiwaambieni siku hizo: Kristo yuko hapa au'Yuko pale,' msimsadiki. (Mathayo 24:23 HNKK)




92

Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza,




93

kama yamkini, hata walio wateule.



94

Sikilizeni, nimekwisha kuwaonya kabla ya wakati.
Mathayo 24:23-25 (HNKK)



95

Lakini mtu aweza kusema - au waweza kujua mtu asemaye, Nimemuona mpendwa aliyetuacha akiwa hai.

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi



96

Mwingine pia aweza kusisitiza, Nimezungumza na mume wangu.



97

Na mwingine; Nilipoteza mtoto wangu katika shambulio la kigaidi (kama New York), lakini ninamtembelea na kunena naye, yeye ni faraja kubwa kwangu. Je, Yesu alisemaje?
Ya kwamba wafu wamelala -- na kwamba roho zingewadanganya wengi yamkini hata walio wateule. Mamilioni watadanganywa.
Kwa nini? Kwa sababu wanategemea zaidi hisia zao, na uzoefu wao badala ya Neno la Mungu.


98

Kwa nini wateule hawadanganywi?
Kwa sababu wanamwamini Yesu.
Wanaliamini Neno la hakika la Mungu badala ya hisia zao wenyewe, tashwishi zao, na uzoefu wao.



99

Swala ni hili:



100

Je, tutaukubali ukweli wa Mungu,



101

au tutauamini uongo wa Sheatani?

14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi


102


Ni wale tu ambao wamejiwekea ngome ya maneno ya Biblia katika mawazo yao watakaoweza kusimama dhidi ya upepo wa kutisha wa udanganyifu ambao tayari unaigharikisha dunia.
Tunahitaji kujua mambo haya na kuyaamini tukiwa na nia imara, na tusiruhusu uzoefu wowote, hisia , au mwonekano utuyumbishe toka katika kweli.


103

Pengine umeshangaa juu ya uzoefu wa karibia na mauti, ambao kwa huo watu ambao wametamkwa kuwa wamekufa wamefanikiwa kuishi tena


104

na taarifa ya kwamba walijikuta wakizungukazunguka katika chumba cha hospitali wakitizama miili yao wenyewe--


105

au ya kwamba waliona nuru angavu na Yesu au malaika akawaitwa waje. Baadhi hata wanatoa taarifa ya kuwaona wapendwa wao toka sehemu ya pili ya mauti.
Ni kwa kutumia Neno la Mungu tu ndivyo twaweza kutambua uongo na kuwa salama dhidi ya udangayifu.



106

Kusema, Kuona ni kuamini -Nitaamini nitakapoona kwa macho yangu mwenyewe, ni njia ya hakika ya kudanganyika.


107

Twaweza kufanya uamuzi wa makosa makubwa kama tunaweka msingi katika hisia, au matashi yetu, au uzoefu wetu-- badala ya Neno la Mungu, Biblia. Zipo tu imani nyingi sana ambazo zinadumu kuhusu mauti katika dunia nzima.

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi



108


Chukua hii imani ya mtu kutokea tena kama kiumbe kwa mara nyingine kwa mfano. Mamilioni huamini ya kwamba mtu anapokufa, huzaliwa tena katika mfumo mwingine, na bila kujua ni upi. Inawezekana kabisa anaweza kuwa kama mnyama, kama vile ng'ombe, panya, au nyoka.


109

Au aweza kuwa kama mtu mwingine, akiwa na uwezekano wa kuwa tajiri, au mfalme, au fukara au maskini au ombaomba, au kipofu au kiziwi, au mlemavu, au akiwa na maumivu na ugonjwa wa kudhoofisha.



110

Wahindu hufundisha ya kwamba kuna Gurudumu la Uhai ambalo huzunguka wakati wote, na ya kwamba wakati mtu anapokufa, huzaliwa tena -- na ya kwamba kuna marudio yasiyoisha ya hili katika dunia.
Watu wengi wamenaswa katika hili bila ya kujua falsafa iliyo nyuma ya hili. Katika imani hii, hakuna hali ya kujitawala ya mtu binafsi, na hakuna uchaguzi, na hakuna maamuzi ya kufanya.




111

Lengo si maisha yaliyo na hali ya mtu kujitambua tena mwenye utu, uchaguzi, furaha na urafiki, Badala yake, mtu hatimaye hufikia Nirvana --



112

Hali ya amani ya kutokuwepo, bila  utu, bila ufahamu, bila ujuzi, na bila kumbukumbu,



113

hakuna wewe kama nafsi huru, wala hakuna uwezo wa kuwaza na kupenda na kuhisi na kuwa na hali ya kuhisi furaha.

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi



114

Nafsi inakuwa imemezwa katika ulimwengu kama tone la maji limezwavyo katika bahari, katika hali ya kupoteza utambulisho kabisa.




115

Ubudha hufanana na huo.
Hata hivyo, Buddha alifundisha ya kwamba ungeweza kutoka katika hili Gurudumu la Uhai mwishoni mwa maisha haya --ya kwamba hukuhitaji kupitia katika mizunguko hii isiyoisha ya kuzaliwa tena kama ungekuwa na 'karma' iliyo sahihi.



116

Kwa njia ya hali kujitawala nia kusiko na utambuzi kamili, fundisho linaendelea, mtu anaweza kufikia katika hatua fulani katika maisha ambapo kunakuwa na kikomo kabisa cha tamaa au hisia.




117

Wakati hali hii ya mawazo na mwili inapofikiwa, anaweza kwenda wakati wa kufa moja kwa moja hadi kwa Nirvana, ambapo anakuwa amefyonzwa katika ulimwengu kama kichembe chembe kidogo sana kati ya zingine.




118

Pamoja na hizi dini kubwa, ipo pia imani ya kwamba wema na uovu ni mamlaka zinazolingana na zitadumu hata katika umilele wote.




119

Kisiwani cha Bali katika Indonesia, mtu aweza kushuhudia dansi ya Barong.



120

Barong, wakiwa wamevalia vazi ambalo huonekana kama yai kubwa lililochemshwa, hukabili watu sita wenye silaha ya kris -ambayo ni kama jambia kali lililojipinda kama mundu. Wanakuwa wametumia kileo fulani kilichopo katika mazingira yao.

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi


121

Wa Barong husonga mbele kuwakabili, nao husonga nyuma kama wanaoepuka shari. Hupiga yowe na kugeuka, kisha watu humkimbiza, hali wakikata hewa wakijaribu kumkata.


122

Barong husimama  na kugeuka kuwakabili watu hawa. Nao husimama. Anasonga hatua moja, nao hurudi nyuma hatua moja.

Hili hurudiwa, nyuma na mbele, tena na tena, hadi watu sita hupigwa na bumbuwazi kiasi cha kushindwa kujitawala katika mchezo. Siyo jambo la ajabu kwa mmoja au zaidi kutupa kris yake na kumkata mmoja wa watizamaji kwa makosa. Katika hatua hii,  wanaume wa kijiji huja nyuma ya wale watu, na kupigana nao mieleka hadi wawaangushe chini na kuwamwagia maji wakiwa katika hali ya kudhoofika.

Hatimaye, hutingisha vichwa vyao kana kwamba wanatoka katika kuzimia, huamka na kutembea kuelekea kwenye vibanda vyao, wakati huo Barong huenda zake katika mwelekeo tofauti,

Hilo lina maana gani? Ni sherehe za kidini ambapo watu hutenda kulingana na imani zao.

Barong humwakilisha Mungu, na watu hawa sita huwakilisha uovu. Kulingana na imani ya kihindu, kuna pambano la milele kati ya wema na uovu. Hakuna anayepata ushindi -daima hutoka sawasawa.



123

Msingi wake u katika kauli hiii  ya kwamba historia ni mzunguko --ya kwamba inadumu katika kujirudia yenyewe bila kukoma, ya kwamba historia haiendi popote.

Hakuna Mungu wa milele wa Upendo ambaye hatimaye atabwaga chini uovu na kuleta haki na amani katika dunia yote.

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi



124

Ninashukuru sana  kwa ajili ya Yesu, Ufufuo na Uzima, je, sivyo hata wewe?
Ni tumaini zuri kiasi gani analotupa!
Uovu hautashinda daima. Historia siyo tu mzunguko; inaelekea mahali fulani. Historia inelekea katika wakati ambapo Mungu ataumba nchi mpya kwa ajili ya watu halisi pasipo dhambi, maradhi, vita, upungufu wa chakula, matatizo au mauti.



125

(Fungu: Ufunuo 21:1-4)
Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita,



126

wala hapana bahari tena.



127

Nikaona mji mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka kwa Mungu mbinguni.




128

Ulikuwa umetayarishwa vizuri kama bibi arusi aliyepambwa tayari kukutana na mumewe. (Ufunuo 21:2 HNKK)



129

Kisha nikasikia sauti kubwa kutoka katika kiti cha enzi ikisema, Tazama! Mungu amefanya makao yake kati ya watu.



130

Atakaa kati yao, nao watakuwa watu wake, naye atakuwa Mungu wao.  (Ufunuo 21:3 HNKK)

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi



131

Yeye atayafuta machozi yao yote; maana hakutakuwako tena na kifo, wala uchungu, wala kilio, wala maumivu



132

wala maumivu hayatakuwapo tena, kwa maana mambo ya kale yamekwisha kupita.
Ufunuo 21:1-4


133

Je, huwezi kumchagua Yesu sasa na kuzaliwa upya? Siyo baada ya mauti utakapokuwa umechelewa sana. Siyo kupitia kwa marudio rudio yasiyoisha ya kuwepo tena kwa namna nyingine ya kiumbe katika mifumo mbalimbaliya maisha kwa miaka mamilioni. Lakini sasa, leo!




134

(Fungu: 1 Petro 1:3,4)
Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo,




135

ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili ili tupate tumaini lenye uzima



136

kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu,



137

tupate na urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka,

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi



138

uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu.
1 Petro 1:3,4


139

Waweza kuwa na maisha milele.
Huo ndiwo uhakika ambao Mungu anakuhitaji uwe nao leo.



140

Na, ushahidi wenyewe ndio huu: Mungu alitupatia uzima wa milele, na uzima huo uko kwa Bwana.



141

Yeyote, aliye na Mwana wa Mungu anao uzima huo; asiye na Mwana wa Mungu, hana uzima. (1 Yohana 5:11,12)
Tunajuaje? Twawezaje kuwa na uhakika? Neno la Mungu linalifanya swala hili kuwa wazi kabisa:



142

(Fungu: 1 Yohana 5:13)
Nawaandikieni mpate kujua kwamba mnao uzima wa milele ninyi mnaoamini kwa jina la Mwana wa Mungu.,



143

ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele.......
1 Yohana 5:13
Swali ambalo kila mmoja apaswa kulijibu ni: Je, ninaye Yesu?
Waweza kuwa naye wakati huu huu.



144

(Fungu: Ufunuo 3:20)
Anasema,Tazama, nasimama mlangoni[wa moyo wako], nabisha;

# 14 - Sauti Toka Mbali Zaidi ya Kaburi




145

mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango,



146

nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami.
Ufunuo 3:20


147

Hebu fungua tu mlango wa moyo wako sasa hivi, na umkaribishe ndani.

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma



1

Jinsi ya Kupata Afya Kamili


2


Ikiwa imekaa katika kilele cha genge litizamalo zumaradi ya maji ya buluu ya Mediterranian (Shamu) ni nyumba ya Kireno ya watawa.
Mandhari yanashangaza.
Sura ya mahali pale ni ya ajabu.
Lakini kuna tatizo moja.
Njia moja pekee ya kufikia juu katika genge lile ilikuwa ni ya njia ya kikapu kilichosukwa kwa matete kisha kikafungwa kwa kamba na kikapandishwa juu na mtawa mwenye umri mkubwa.


3

Siku moja kiongozi wa msafara wa utalii na mgeni wake waliondoka toka kwa nyumba hii.
Walipotoka tu na kuingia kwenye kile kikapu walishushwa taratibu na huyu mtawa, kamba ikayumba na kwenda juu ya miamba iliyoning'inia chini.
Katika mshtuko mtalii aliuliza, Je, ni mara ngapi wanabadilisha kamba hii?


4

Usiwe na wasiwasi, kiongozi alijibu katika sauti yenye kuthibitisha, kila mara moja inapokatika, tunaweka mpya.


5

Kama tu katika kisa hiki, maelfu ya watu wanajiweka mazingira yasiyo tabirika kuhusu afya.
Wanasubiri hadi afya zao zinapovunjika, kama ile kamba, kisha katika hali ya kutowaza sawasawa hung'ang'ania katika fundo la mwisho la afya.Afya iliyovunjika siyo rahisi kuweka nyingine badala yake kama kamba iliyovunjika!Afya siyo swala la nafasi, ni swala la uchaguzi--wa kutii sheria za asili.

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma



6

Rafiki, je waweza kumudu kuwa na afya mbovu? Watu hutumia mabilioni ya dola kila mwaka kwa ajili ya huduma ya tiba. Maradhi ni jambo lenye gharama zaidi katika dunia ambalo watu hutumia fedha yao kwa ajili yake!
Ina thamani gani basi kuwa mzima?
Muulize mtu anayeugua sarakani au mtu anayesumbuliwa na maradhi ya UKIMWI.



7

Uliza wazazi wa mtoto anayeugua sarakani ya damu ( leukemia ) au mzee ambaye ameathiriwa na baridi yabisi (arthritis).
Watakwambia ya kwamba afya njema inazidi thamani iwezayo kukadiriwa-- ya kwamba ni mbaraka ambao hatushukuru kiasi cha kutosha kuwa nao hadi tuwe tumeupoteza!





8

Je, thamani ya mwaka mmoja wa maisha -- au hata siku moja -- ni kiasi gani?
Malkia Elizabeth I anasemwa kuwa alilia katika kitanda ambapo mauti yalimkuta,
Vyote nilivyo navyo kwa wasaa mmoja tu wa maisha!
Lakini hauwezi kununuliwa kwa fedha.
Je, unatambua, hata hivyo, ya kuwa waweza kuvuna zaidi na kuwa na maisha bora zaidi kwa miongozo mizuri iliyo rahisi, inayoeleweka ya afya?




9

Dk. Breslow wa UCLA (Chuo Kikuu cha California, Los Angeles) alifanya utafiti katika kipindi cha miaka tisa.
Alihoji watu 7,000 maswali saba yahusianayo na mazoea ya kiafya na kisha akachunguza wagonjwa hawa, akilinganisha wale waliofuata mazoea mazuri ya afya na wale ambao hawakufanya hivyo.




10

Hapa ni maswali saba aliyouliza:

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma



11

1. Je, unavuta sigara?
2. Je, unakunywa vileo, na kama ndivyo, kiasi gani?
3. Je, kwa kawaida unafanya mazoezi?



12


4. Je, unalala masaa mangapi kila usiku?
5. Je, una uzito gani?
6. Je, kwa kawaida unakula kifungua kinywa ?
7. Je, una kawaida ya kula kula kati ya milo?

Wale waliofuata mazoea mazuri ya kiafya kwa uaminifu yahusianayo na haya maswali saba waliishi wastani wa miaka 11.5 zaidi ya wale ambao hawakufanya hivyo.



13

Ungetoa nini kwa ajili ya ongezeko la miaka 11.5 katika maisha yako?
Kile unachoelezwa sasa hivi katika ujumbe huu kinaweza kuongeza vizuri sana miaka katika maisha yako-- miaka yenye furaha na afya.
Je, wadhani itakuwa ni jambo la thamani kwako kusikiliza vyema?
Linakuja kama jambo la kushangaza kwa watu wengi ya kwamba Mungu anajihusisha na afya na furaha yetu hapa tulipo wakati huu .



14

(Fungu: 3 Yohana 1:2)
Mpenzi wangu, nakutakia mafanikio mema ya kila aina; nakutakia afya njema ya mwili kama ulivyo nayo rohoni. (3 Yohana 1:2 HNKK)



15

(Fungu: Yohana 10:10)
Yesu alisema, ...Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.
Yohana 10:10.


16

Yesu anatutaka tuwe na maisha ya furaha, ya shangwe, ya afya. Anatutaka tuishi maisha katika ukamilifu wake!

15 - Irejeshe Saa Nyuma

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma


17

Je, yawezekana kujua jinsi ya kuwa na afya njema?
Ndiyo yawezekana!
Wengi hawajui ya kuwa katika Biblia, Mungu ametoa kanuni muhimu na miongozo ihusuyo maisha yenye afya.



18

Kwa miongo mingi mtindo wa maisha ya Wayahudi wa Orthodox umekuwa ukiwavutia sana watafiti wa mambo ya tiba.
Tatizo la kufisha la sarakani kwao liko pungufu sana zaidi ya wengine, na wanaonekana kutokuwa na mwelekeo wa kuwa na maradhi mengine ya kutisha.
Je, Wayahudi  wanayo namna ya asili inayowafanya wawe huru toka kwa haya maradhi yanayoua, ambayo yanawapiga chini wengine?


19

Inapendeza kutambua ya kwamba Wayahudi waanzapo kula kile wengine wanaowazunguka wanachokula, kasi yao ya kupata sarakani, na ya maradhi mengine pia, ni sawa sawa na ile ya watu wengine.
Imegunduliwa ya kwamba siri ya yote imo katika mazoea yao (taratibu) ya  kiafya, lishe, na mtindo wa maisha.



20

Wakati Mungu alipowatoa wana wa Israeli toka Misri, aliwakumbusha juu ya kanuni muhimu sana na masharti yahusuyo maisha yenye afya.

Baada ya kutoa muhtasari wa mpango wake juu ya afya njema, alitoa ahadi ya pekee kabisa kwa wale ambao wangelifuata maelekezo yake.



21

(Fungu: Kutoka 15:26)
Alisema: ....Kwamba  utaisikiza kwa   bidii sauti ya BWANA, Mungu  wako, na kuyafanya yaliyoelekea mbele  zake,

# 15 - IREJESHE SAA NYUMA



22

na kutega sikio usikie maagizo  yake, na kuzishika amri zake,



23

mimi sitatia juu yako maradhi  yo yote niliyowatia Wamisri; kwa kuwa Mimi ndimi BWANA nikuponyaye.
Kutoka 15: 26.
Alisema pia,



24

(Fungu: Kutoka 23:25)
Nanyi mtamtumikia BWANA, Mungu wenu, naye atakibarikia chakula chako, na maji yako;



25

nami nitakuondolea ugonjwa kati yako.
Kutoka 23:25.
Je, unaona umuhimu wa hili?
Kama tukifuata maelekezo ya Bwana, madhara ya maradhi yanayotukabili mara kwa mara yanaweza kurudishwa nyuma!
Hiyo ni habari isiyoweza kuelezeka thamani yake!


26

Akitoa maoni juu ya utimilifu wa ahadi hii, mtunga zaburi anatuambia,



27

(Fungu: Zaburi 105:37)
Katika kabila zao asiwepo mwenye kukwaa.
Zaburi 105:37.
Naam wasema, pengine Wamisri hawakuwa na maradhi kama yale tuliyonayo leo.  Umekosea!

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma


28

Kundi la mabingwa toka pote duniani walikusanyika mwaka wa 1975 kwa makusudi halisi ya uchunguzi wa maiti zilizotunzwa kwa madawa za ki Misri katika jumba la makumbusho la Shule ya Tiba ya Manchester (Uingereza).
Hawa wamiani walionekana kuwa waliishi kama miaka ya 1900 K.K.



29

Ugunduzi ulikuwa wa kushangaza. Wamisri wa kale waliugua maradhi yaliyo ya kawaida kwa mtu wa kisasa:



30

maradhi ya moyo,
sarakani,
maradhi ya mishipa ya damu,
baridi yabisi,



31

homa ya manjano,
pepo punda,
uti wa mgongo na mengine.


32

Ingawa Misri ilikuwa ni kituo cha elimu na tamaduni za dunia wakati wa maisha ya Musa, ujuzi wake wa tiba na uganga ulikuwa unafanana kwa kiasi kikubwa na ule wa mganga wa kienyeji wa Afrika leo!


33

Katika mwaka wa 1552 K.K., muda mfupi kabla ya kuzaliwa kwa Musa, kitabu kinachofahamika sana cha tiba kiliandikwa kule Misri kiitwacho Papyrus Ebers.
Kitabu hiki kinaorodhesha idadi kubwa ya uganga au madawa kwa ajili ya kundi la magonjwa,maambukizo, na ajali, ambazo chache tu ndizo labda ungelipenda kutumia!

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma


34

Kwa ajili ya kipande chembamba kilichopenya ndani sana (kwenye ngozi), kinashauri upachue kwa damu ya mnyoo na kinyesi cha farasi katika jeraha.
Si ajabu  pepo punda iliongezeka kiasi hicho!
Ukiwa umeumwa na nyoka: kunywa maji yaliyomwagwa kwa mungu-sanamu.


35

Ukiwa na kipara? Chua katika upaa na mafuta yaliyotengenezwa kwa kwato za farasi, tende zinazochanua, na visigino vya mbwa vilivyochemshwa katika mafuta.


36

Biblia inatuambia ya kwamba Musa alielimishwa katika hekima ya Wamisri(Matendo 7:22).
Maandishi yake yamejaza maelekezo yahusuyo usafi, kutengwa kwa mgonjwa ili kuepuka maambukizo, usafi wa mtu binafsi, na lishe, lakini hata mara moja hakueleza  juu ya madawa haya kuorodheshwa katika Papyrus Ebers.
Je, Musa alipata wapi  hizi kanuni za afya au miongozo?
Kutoka kwa Mungu!


37

Ukoma na maafa yafahamikayo kama Black Death na yalikuwa ni mapigo ya kutisha zaidi yaliyowahi kuwepo katika Zama za Kati.


38

Kanuni za afya, zilizotolewa na Mungu na kufundishwa na Musa baada ya Kutoka Misri, zilisaidia katika kuzuia hii misiba mikuu.
Mamilioni ya maisha ya watu kama madaktari waliwageukia viongozi wa makanisa kwa ajili ya msaada wakati wa mapigo haya.



39

George Rosen aliandika: Uongozi ulichukuliwa na kanisa,  wakati wauguzi wakiwa wameshindwa kufanya lolote.

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma



40

Kanisa lilichukua dhana ya maambukizo kama kanuni inayoongoza iliyopo katika Agano la Kale...



41

Dhana hii na matokeo yake yaliyo dhahiri vinaelezwa kwa uwazi kabisa katika Kitabu cha Mambo ya Walawi.
- George Rosen, M.D., Historia ya Afya ya Umma, uk. 63-65.


42


Ni aibu kubwa kiasi gani ya kwamba watu milioni 60 walikufa katika mapigo haya wakati kanuni za Biblia za afya ya umma zilikuwepo wakati wote


43

Mungu aliisanii miili yetu.
Anajua jinsi tuwezavyo kuepuka magonjwa na kuitunza miili yetu katika utendaji ulio bora sana!
Mungu alimpatia mwanadamu mwili wa pekee wenye uwezekano wa kuwa mambo mengi sana.
Una sehemu nyingi zilizo nyeti.


44

Mungu alitutengeneza, na anajua wazi kabisa kilicho muhimu ili kututunza afya zetu na katika utendaji wa hali ya juu zaidi.


45

Kijana alinunua gari jipya linalong'aa ambalo kwa ajili yake alikuwa amedunduliza fedha kwa miaka mingi.


46

Alipewa kijitabu cha maelekezo toka kwa mtengenezaji ambacho kilimwambia wazi namna ya kulitunza gari lake jipya katika njia iliyo bora zaidi, kulifanya litembee katika hali ya ubora zaidi kwa miaka mingi.

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma


47

Hili lilikuwa ni gari aghali, na ungefikiri mwenye gari mpya angelisoma haidhuru maelekezo juu ya namna ya kuitunza.
Lakini hakufanya hivyo.
Jambo pekee ambalo aliliwazia lilikuwa ni jinsi gani angeliweza kufikia maili 60 kwa saa kwa sekunde chache tu.
Alipenda kulifanya liende kwa kasi kadiri alivyoweza, kisha akakanyaga breki ili aone lingesimama kwa haraka kiasi gani.
Alipenda kusikia mlio wa tairi.


48

Hakuangalia mafuta wala maji wala pumzi katika tairi - hili lilikuwa likimsumbua na kwake lilikuwa linachukuwa muda mrefu sana.
Hakuweza kupoteza muda wake wa thamani katika mambo madogo madogo hivyo.
Alipenda tu kuwa nyuma ya usukani, akiendesha alipopenda kwenda -- hasa zile sehemu ambapo watu wengi wangelimuona akiendesha kwa kasi akiwa ndani ya gari yake iliyong'aa.


49

Waweza kuhisi sehemu inayosalia ya kisa hiki.
Ndiyo, gari halikudumu kwa muda mrefu kabla ya kuhitaji ukarabati wa gharama kubwa.
Je, tunafanya vivyo hivyo na mwili huu wa ajabu Mungu aliotupatia?
Ni hakika tunataka kufuata maelekezo yake!


50

Safari moja tu ya kwenda hospitali yaweza kufuta akiba yetu ya maisha yote.

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma



51

Ni dhahiri basi ni jambo la thamani kwetu kurejea bustanini Edeni, kurejea katika Uuumbaji, na kugundua baadhi ya mambo ambayo Mungu alimwambia Adamu na Hawa ambayo yanajenga afya njema.
Lishe yenye Afya
Kabla dhambi haijaingia, Mungu alimpatia Adamu na Hawa lishe kamili ili kuwatunza na kujenga afya zao.




52

(Fungu: Mwanzo 1:29)
Mungu akasema, Tazama, nimewapa kila mche utoao mbegu, ulio juu ya uso wa nchi yote pia,




53

na kila mti, ambao matunda yake yana mbegu; vitakuwa ndivyo chakula chenu;
Mwanzo 1:29.



54

Katika lugha ya kisasa tungelisema walipewa matunda, nafaka, na namna za njugu.



55

Hiki kilikuwa chakula chao.
Mungu aliwapatia Mti wa Uzima, ambao ulikuwa badala ya lishe yao kwa namna iliyo hakiki ujana wa milele na afya.
Baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi, Mungu aliwatenganisha na Mti wa Uzima na kuongeza mboga kwa lishe yao.

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma



56

(Fungu: Mwanzo 3:18)
....Nawe utakula mboga za kondeni.
Mwanzo 3:18.
Hizi, pamoja na matunda, nafaka, na njugu, vilikuwa lishe ya jumla ya mwanadamu hadi wakati wa Gharika Kuu.
Je, kilikuwa chakula cha kutosha? Ndiyo, hakika!Tafakari juu ya watu waliokuwa katika mpango wa asili wa Mungu wa lishe waliishi hadi kufikia umri wa miaka mamia.



57

(Fungu: Mwanzo 5:27)
Mtu aliyepata kuishi umri mkubwa kuliko wote hapa duniani alikuwa Methusela: Siku zote za Methusela ni miaka mia kenda na sitini na kenda, akafa.
Mwanzo 5:27.


58

Baada ya Gharika, urefu wa maisha ya mwanadamu ulipunguzwa kiasi kikubwa.
Mwana wa Nuhu, Shemu, aliishi miaka 600;
mjukuu wake aliishi miaka 239;
kitukuu chake miaka 175.
Ilipofikia wakati wa Mfalme Daudi, urefu wa maisha ya mwanadamu ulikuwa umeshuka hadi kufikia miaka 70!
Na huo ni upungufu mkubwa, je, usingelisema hivyo?


59

Uhai wa mimea hapa duniani ulikuwa umezuiwa sana na Gharika Kuu.
Akiba ya chakula ya Nuhu ilikuwa imekwisha baada ya familia yake kuishi katika safina kwa zaidi ya mwaka mmoja. Mungu alikuwa hajaruhusu hadi hapo kwamba mtu ale wanyama kama hatua ya wakati wa hatari.
Si mimea yote wala wanyama wote ambao walistahili kuwa chakula kizuri.
Mungu alitoa miongozo kwa ajili ya chakula iliyofikirika kuwa mizuri kwa mtu kula.

15 - Irejeshe Saa Nyuma

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma


60

Tofauti ilifanywa kati ya wanyama safi na wasio safi. Mungu alitoa pia maelekezo kwa Nuhu wanyama gani waingie safinani naye na kiasi na wangapi wa kila aina:




61

(Fungu: Mwanzo 7:2)
Katika wanyama wote walio safi ujitwalie saba saba, mume na mke.



62

na katika wanyama wasio safi wawili wawili
mume na mke.
Mwanzo 7:2


63

Inaonekana ya kwamba Nuhu alijua wanyama wa namna gani ambao Mungu aliwahesabu kuwa safi au wasiosafi.


64

Baadaye, Mungu alipowaleta Wana wa Israeli kutoka utumwani Misri, alipatia Israeli kanuni za lishe ili kuwalinda afya zao na kuwapa maisha marefu. Mungu aliwatambua wanyama ya kwamba wapi walikuwa safi na wapi hawakuwa safi kwa chakula:



65

(Fungu: Kumbukumbu la Torati 14:6)
na kila mnyama aliyepasuliwa ukwato,



66

ukapasuka ukwato wake zikawa mbili, naye ni mnyama mwenye kucheua akatafuna tena, katika wanyama wote,
Kumbukumbu 14:6.
Tambua muongozo ulio rahisi sana kukumbuka:
Mambo mawili tu: 1) Kwato zilizogawanyika, na
2) Mwenye Kucheua na kutafuna tena.

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma



67

Wanyama wachache kati wanyama wanaofahamika walio safi kulingana na mafungu 4-6:
madume ya ng'ombe, kondoo,kulungu, mbuzi, mbuzi mwitu, swala, na ng'ombe.




68

Wanyama wasio safi ambao sasa wanatumika kama chakula kwa kawaida, kulingana na mafungu 7 na la 8 yangehusisha ngamia, sungura, nguruwe, na mbweha.
Unakumbuka miongozo miwili?
Kama mnyama ana kwato zilizogawanyika na anacheua na kutafuna tena, huyo ni salama kwa chakula. Ni muhimu kukumbuka ya kwamba kwa sababu baadhi hutafuna walichocheua wakati hawana kwato zilizogawanyika.


69

Kwa mfano, nguruwe, ana kwato zilizogawanyika, na hali hacheui na kutafuna tena, yeye si safi.
Biblia ina maelekezo ya moja kwa moja kuhusu nguruwe:



70

(Fungu: Mambo ya Walawi 11:7,8)
Na nguruwe, kwa sababu yeye anazo kwato, ni mwenye miguu iliyopasuka kati, lakini hacheui, yeye ni najisi kwenu.



71

Msiile nyama yao, wala msiiguse mizoga yao; hao ni najisi kwenu.
Mambo ya Walawi 11:7,8.
Wengi wa wanyama ambao Mungu aliwaorodhesha kama wasio safi wako katika kundi la 'wafagiaji.'
Mungu hakuzuia kitu chochote kilicho kizuri wakati alipotoa miongozo hii.
Anajua ni wapi walio na afya na ni wapi wawezao kusababisha magonjwa ama maradhi.




72

(Fungu: Zaburi 84:11)
....Hatawanyima chema hao waendao kwa ukamilifu.
Zaburi 84:11.


# 15 - Irejeshe Saa Nyuma


73

Nguruwe ni mfagiaji.
Chakula, takataka zikiwemo, kikiliwa na nguruwe hugeuka na kuwa chakula katika muda wa masaa.
Ng'ombe, kwa upande mwingine, anawo mfumo wenye sehemu nyingi wa usagaji wa chakula.
Inachukua masaa 48 kwa chakula chake kugeuzwa na kuwa sehemu ya mwili.
Anawo pia mfumo wenye sehemu nyingi wa uondoshaji wa visivyohitajika miwilini, anaondoa sehemu nyingine zisizo safi toka katika mfumo mzima ndani ya mwili.


74

Nyama ya nguruwe mara kwa mara huathiriwa na trichina larvae, au minyoo.
Wakati mtu anapokula nguruwe iliyoathirika, utando mgumu unaoifunika larva huyeyuka.
Mnyoo ufahamikao kama trichina hujichimbia katika kuta za utumbo na kuzaliana.


75

Minyoo hii huingia katika mishipa ya damu na hubebwa hadi kufikia sehemu zingine za mwili.
Trichinosis yaweza kuwa ugonjwa wa kufisha, ikitegemea idadi ya minyoo iliyoliwa.
Mara kwa mara ugonjwa huu hukosewa na kufikirika kuwa baridi yabisi au tatizo dogo tu la uchafu kwenye chakula.


76

Uchunguzi wa maiti pia umeonyesha ya kwamba wengi wa wamiani kati ya watu walioishi siku za Musa walikuwa wameathiriwa na minyoo ya trichina!
Mungu ajua kwa ubora zaidi -- liache hilo!
Mungu alitoa pia maelekezo juu ya samaki:



77

(Fungu: Kumbukumbu la Torati 14:9,10)
Mtakula hawa katika wote walio majini; kila kilicho na mapezi na magamba mtakula.

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma



78

Na kila  kisicho na mapezi na magamba msile; ni  najisi kwenu.
Kumbukumbu la Torati 14:9,10.




79

Hilo li wazi kabisa, na hebu tambua tena ya kwamba kuna miongozo miwili inayorahisisha kukumbuka:



80

1) Wana mapezi, na



81

2) wana magamba.
Je, waweza kufikiria juu ya vyakula vya baharini ambavyo huliwa kuzunguka dunia nzima  ambavyo havina mapezi wala magamba?


82

Dk. Bruce Hallsted, wa Chuo Kikuu cha Loma Linda, aliombwa na serikali kufanya utafiti kwa ajili ya jeshi ili kujua ni aina gani ya samaki walikuwa salama kwa ajili ya watu kula na  samaki gani walikuwa na sumu.


83

Watumishi wa umma wameharibikiwa na mashua ama wamekwama katika maeneo  pweke na wanahitaji kujua  aina gani ya samaki wana sumu na aina gani wanaweza kula ili kuendelea kuishi. Wakati kazi yote hii ilipomalizika, Dk. Hallsted alihitimisha ya kwamba kanuni rahisi kutumia kwa ajili ya jeshi na wapiganaji wa majini ni ile ile ambayo Mungu aliwapatia Wana wa Israeli yapata kama miaka 3,500 iliyopita:

15 - Irejeshe Saa Nyuma

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma




84

(Fungu: Kumbukumbu la Torati 14:9)
Mtakula hawa katika wote walio majini; kila kilicho na mapezi na magamba mtakula; Mungu alijua kwa nini waliumbwa na kwa nini twaweza kula  au kutokula vitu fulani.



85

Vipi kuhusu ndege, waweza kuuliza.
Biblia inatoa maelekezo haya yaliyo muhimu:




86

(Fungu: Kumbukumbu 14:11, 12)
Mna ruhusa kula katika nyuni wote walio safi.





87

Lakini hawa msiwale:......
Fungu la 11,12.




88

Mungu anaendelea kuwaorodhesha:
tai, furukombe, kipungu;kengewa,  kozi,  mwewe, kunguru, mbuni, kirukanjia,  dudumizi, kipanga, bundi,  mumbi, bundi mkubwa, mwari, nderi, mnandi, membe, koikoi, hudihudi na popo kwa aina zake.




89

(Fungu: Kumbukumbu la Torati 14:19)
Kisha Mungu akasema, Na wadudu wote watambaao wenye mabawa ni najisi kwenu; msiwale.
Fungu la 19.




90

(Fungu: Mambo ya Walawi 3:17)
Mungu alitoa maelekezo zaidi: Neno hili litakuwa amri  ya daima, katika vizazi vyenu vyote, ndani ya nyumba zenu zote:




91

hamtakula mafuta wala damu kabisa.
Mambo ya Walawi 3:17.




92

Wayahudi wa Orthodoxy wangaliwakifuata maelekezo haya hadi leo. Wanapochinja mnyama, humning'iniza juu chini ili damu idondoke yote. Kisha mnyama hukatwa katwa na kulowekwa katika maji yenye chumvi ili kuondoa damu yote iliyosalia.



93

Mafuta hukatiliwa mbali na hayaliwi.
Kwa miaka mingi watu walidhani ya kwamba hii amri ikatazayo ulaji wa mafuta na damu ilikuwa tu ni moja ya zile zilizohusu sherehe za ibada zilizokuwa na makatazo fulani toka kwa Mungu.



94

Hata hivyo, utafiti wa kisasa unaithibitisha hekima ionekanayo katika amri ya Mungu.



95

Sasa tunajua ya kwamba damu inabeba uchafu ndani yake, vijidudu, virusi na taka za mwili.
Maradhi mengi hupitishwa kwa njia ya damu.



96

Tunajua pia ya kwamba mafuta mazito kabisa kama yale yapatikanayo katika vyakula vitokanavyo na maziwa na nyama husababisha muongezeko wa kiwango cha cholestrol katika damu -- jambo muhimu katika ugonjwa wa mishipa ya damu na moyo.
Maradhi mengi kiasi gani yangekwepwa kama mtu angemtegemea Muumbaji wake katika kuamua juu ya kile kilicho cha muhimu kwa kula!

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma


97

Mazoezi kwa ajili ya Afya
Biblia yasema ya kwamba baada ya Mungu kumuumba Adamu na Hawa, aliwapatia kazi ya kufanya -- shughuli ya maana na itoayo mazoezi:



98

(Fungu: Mwanzo 2:15)
BWANA Mungu akamtwaa huyo mtu, akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza. Mwanzo 2:15.


99

Mazoezi huulinda mwili usipate maradhi mengi! Mwili usioshughulika huchakaa.


100

Mazoezi huimarisha misuli na mishipa ya damu.


101

Mapafu hutenda kazi kwa ufanisi zaidi, na kuiwezesha kuchuja hewa kwa wingi zaidi kwa jitihada kidogo.


102

Moyo una kuwa na ufanisi zaidi, ukisukuma damu zaidi katika kila pigo. Nguvu (Nishati) --itengenezayo oxygen huchukuliwa hadi kwenye tishu, ambazo huimarisha hali ya jumla ya mwili.
Baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi, Mungu aliongeza kazi na zaidi sana kazi ihitajiyo nguvu za mwili.

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma



103

(Fungu: Mwanzo 3:19)
Mungu alisema, Kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi......
Mwanzo 3:19.
Alisema pia ya kwamba ardhi ingelaaniwa kwamba kungekuwa na miiba na michongoma na kwamba kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako. Fungu la 17, 18.


104

Mungu alijua ya kwamba mwanadamu alihitaji kufanya mazoezi na kwamba aliyahitaji si tu kwa ajili ya mwili wake, lakini ili kumzuia asiingie kwenye matatizo.
Mtu mmoja alisema, Uvivu ni karakana ya mwovu.



105

(Fungu: Kutoka 20:9)
Mungu alisema, Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote, Kutoka 20:9.
Kama kila mmoja angelifanya kazi siku sita kwa juma, pengine wangelikuwa wachovu mno kiasi cha kutoweza kuingia matatizoni!



106

Miili yenu ni Hekalu la Roho Mtakatifu.
Umuhimu wa kuijali miili yetu waweza kueleweka pale tu tunapoelewa jinsi ilivyo muhimu kwa Mungu.



107

(Fungu: 1 Wakorintho 6:19,20)
Mtume Paulo alisema,Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu,



108

mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe;

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma



109

maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu.
1 Wakorintho 6:19,20.


110

Mwanadamu ni mali ya Mungu kwa uumbaji na tena kwa ukombozi.
Gharama ambayo Mungu aliilipa kwa ajili yetu ilikuwa kafara ya Mwanae wa pekee katika Kalvari.
Kwa sababu mwanadamu amekombolewa kwa gharama kubwa kiasi hicho, anapaswa amtukuze Mungu kwa kila alitendalo.



111

(Fungu: 1 Wakorintho 10:31)
Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo
neno lolote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu.
1 Wakorintho 10:31
Kila mtu ambaye anampenda Mungu kweli atakuwa mwangalifu na ataepuka jambo lolote ambalo litaharibu au kuchafua mwili wake.



112

(Fungu: 1 Wakorintho 3:17)
Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo.



113

Kwa maana hekaulu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi.
1 Wakorintho 3:17.
Pengine unashangaa ni kwa njia gani mtu huuharibu mwili wake.
Paulo anaorodhesha mambo kadhaa tunayotakiwa kuyaepuka:



114

(Fungu: 1 Wakorintho 6:9,10)
...Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti,

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma



115

wala wevi, wala watamanio, wala walevi, .....
1 Wakorintho 6:9,10.
Biblia inaorodhesha uasherati na upotofu kama mazoea yanayochafua mwili.
Inaorodhesha pia ulevi.



116

(Fungu: Mithali 20:1)
Sulemani aliandika: Mvinyo hudhihaki,
kileo huleta ugomvi; Na akosaye kwa vitu hivyo hana hekima.
Mithali 20:1.



117

(Fungu: Mithali 23:31-33)
Na tena: Usiitazame mvinyo iwapo ni nyekundu;
iitiapo bilauri rangi yake, ishukapo taratibu;



118

Mwisho wake huuma kama nyoka; huchoma kama fira.



119

Macho yako yataona mambo mageni;
na moyo wako utatoa yaliyopotoka.
Mithali 23:31-33.


120

Vileo ni moja ya matatizo makuu ya kiafya duniani. Zaidi ya nusu ya ajali za magari zaweza kuhusiana moja kwa moja na dereva au mtembea kwa miguu ambaye anaongozwa na.....


121

Kati ya zaidi ya nusu ya wauaji wote, ama muuaji mwenyewe au aliyeuawa, au wote wawili, wamekuwa katika kunywa!

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma


122

Kileo kinaharibu uwezo wa mwili wa kutumia vitamini, na sukari iliyo ndani ya vileo( kama ile iliyo katika vinywaji baridi vingi) hupunguza uwezo wa mwili wa kupambana na maambukizo.


123

Mtumiaji wa vileo hufanya ini lake liwe nene; uwezekano wa kufa kwa ugonjwa wa cirrhosis ya ini unakuwa mkubwa zaidi. Urefu wa maisha ya watu hupunguzwa kwa kiasi cha miaka 12.
Na kulingana na takwimu za hivi karibuni sana, mmoja kati ya watu kumi achukuaye kinywaji cha kwanza anakuwa mlevi.


124

Utafiti wa hivi karibuni unaonyesha ya kwamba chembe hai nyingi za ubongo hufa wakati wowote alcohol inapoingizwa katika mishipa ya damu na hivyo unywaji huendelea


125

na akina mama wanakuwa na idadi kubwa zaidi ya watoto wao kuzaliwa wakiwa na mapungufu katika miili yao ukilinganisha na wale wa wasio kunywa.
Lakini kwa Wakristo, matumizi ya vinywaji vyenye alcohol huwa hata na madhara makubwa zaidi.


126

Wakristo wanapaswa kuwa na uwezo wa kutumia kikamilifu mawazo yao ili kukwepa majaribu ya Shetani.
Hawawezi kuendelea katika kuharibu maamuzi yao katika akili au kupoteza uwezo wa kutofautisha haki na makosa!


127

Yesu alikataa kinywaji cha kupumbaza kilichotolewa kwake msalabani na askari kama njia ya kuua maumivu.

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma


128

Hata ingawa Yesu alitaabika kwa maumivu ya kutisha, hakuweza kupokea chochote ambacho kingeweka kiwingu katika mawazo yake, hadi katika hatua ya kifo chake.


129

Idadi kubwa tu ya mazoea mengine huharibu afya njema kwa uhakika.
Wavutaji wana uwezekano wa asilimia elfu wa kufa kwa sarakani ya mapafu zaidi ya wasiovuta.
Na sarakani siyo tu muuaji anayetumiwa na tumbaku.
Nafasi ya mvutaji kufa kwa ugonjwa wa moyo ni asilimia 103 kwa ukubwa kuliko wale ambao hawajapata kuwa na mazoea ya uvutaji.



130


Emphysema huua zaidi ya watu 55,000 kila mwaka!
Nikotini pia husababisha mishipa ya damu kusinyaa.


131

Muunganiko kati ya kujengeka kwa mafuta na kusinyaa kwa mshipa mkuu wa damu huzuia mishipa ya damu kusambaza damu ya kutosha kwa moyo, sehemu mbalimbali za mwili, na viungo vingine.
Katika hatua hii ni kiasi cha kupata tu kijibonge kidogo cha damu iliyoganda kikishikwa katika mishipa ya damu kusababisha moyo kusimama ghafula ama kiharusi.


132

Mtu mvutaji pia anakuwa shabaha kuu ya tatizo la udhaifu wa kizee kwa sababu ya kupungua kwa oxygen kwenye ubongo.


133

Wanawake wavutao wakati wakiwa na mimba huharibu mishipa ya damu ya watoto wao.
Vifo vya watoto wanaozaliwa huwa vinakuwa ni asilimia 27 zaidi kwa wale wakina mama wavutao.

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma


134

Uvutaji wa Sigara ulichangia kwa vifo vya watu 500,000 katika Amerika peke yake mwaka jana.



135

(Fungu: Kutoka 20:13)
Mungu alisema, Usiue. Kutoka 20:13. Watu wangapi wanajiua wenyewe kwa vitu wanavyokula, wanavyokunywa, na wanavyovuta?


136

Mmoja amewahi kusema ya kwamba silaha za kujiua zinazozoeleka zaidi ni visu, uma na vijiko. Pengine tunaweza kuongeza vikombe na chupa!



137

Caffeine, dawa iliyopo
katika kahawa, imewekwa katika viwango katika vitabu vya muhimu kama kichocheo na sumu.



138

Chai na vinywaji vya cola pia vinayo hiyo caffeine. Vinywaji vyote hivi sasa vinaunganishwa na maradhi ya moyo, matatizo ya neva, na sarakani ya tumbo.


139

Kama mtu fulani unayemfahamu angekuwa anakimbia na kuingia katika chumba kingine ili kujichoma sindano yenye kiasi fulani cha caffeine kwenye mishipa yake kila baada ya masaa machache, ungemuita mlevi.
Bado watu wangapi wanatenda jambo hilo hilo kwa kutumia kahawa na vinywaji vya cola.



140


Toba ya kweli humaanisha kuepuka matumizi ya chochote kinachoharibu, na kutumia kwa kiasi kile kilichochema.

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma




141

Watu wengi hula kuliko kiasi vile vilivyo vyema!
Hili hupelekea katika tatizo lingine la kiafya lililo kubwa kwa watu katika sehemu nyingi za dunia.




142

Mtu fulani amekadiria ya kwamba kila nusu kilo ya mafuta katika mwili huhitaji kiasi kingine cha kama theluthi mbili ya maili cha mishipa mipya ya damu.



143


Na moyo lazima usukume damu hata kwa huu mfumo zaidi wa mishipa.
-- Harold Shryock, M.D. Afya Yako na Wewe, Gomb. la 1, uk. 395.


144

Moyo, figo, ini, na mapafu vya watu wenye uzito kuliko kiasi kinachotakiwa vinakuwa na kazi kuliko uwezo wake.
Watu wenye uzito kuliko kiasi hutaabishwa na maradhi kumi na sita zaidi ya wenzao walio wembamba.


145

Mungu anatutaka tuwe waangalifu wa miili yetu ili tupate kufurahia maisha katika ubora wake kabisa sasa.
Anatutaka tuwajibike, tuwe na maadili, watu wenye furaha.
Anatutaka tuwe na uhai tele.
Urefu wa maisha yetu na afya katika maisha yetu hutegemea sana jinsi tunavyofuata maelekezo yake.


146

Pumziko na Starehe
Yesu aliamini katika likizo na kutoka nje ya shinikizo la shughuli.
Baada ya siku ngumu na umati wa watu, Yesu aliwaambia wanafunzi wake,

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma



147

(Fungu: Marko 6:31)
Njoni ninyi peke yenu kwa faragha, mahali pasipokuwa na watu, mkapumzike kidogo.
Marko 6:31.
Yesu anataka tuwe na ulinganifu katika kazi kwa kuwa pia na pumziko na starehe.



148

Hii ndiyo sababu akatupatia Sabato.
Mungu anajua ya kwamba tunahitaji kusahau matatizo yetu na kazi zetu na kutumia muda naye.


149

Wakati wako ukiwa mbali na shughuli nyingi waweza usiwe jangwani, ingawa hapo paweza kuwa sehemu nzuri ya kupumzika katika nyakati fulani za mwaka.

Waweza kupendelea sehemu za mashambani katika milima mahali ambapo miti mirefu na maziwa yenye kina yaweza kutuliza moyo wenye mashaka.


150

Lolote liwalo lile, unahitaji kutafuta mahali palipo mbali na umati wa watu na majiji yenye kelele na barabara zake.
Kama utakuwa na wakati mzuri kidogo, hilo ni bora zaidi!


151

Ndiyo, Mungu anakuhutaji wewe uwe na mbingu ndogo hapa, na uwe tayari kuishi katika dunia iliyofanywa upya, mahali ambapo maradhi yote yanayoipiga dunia yetu yatakuwa yamefutika milele.


152

Hilo naliona kuwa zuri kwangu, wasema. Ninahitaji kuwa pale, lakini nina mazoea fulani ambayo siwezi kuyashinda.
Kuna habari njema leo.
Mungu hakutarajii wewe kutenda hilo peke yako.

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma



153

(Fungu: Yohana 15:5)
Kwa kweli, Yesu asema, Pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote.
Yohana 15:5.
Kwa nguvu zetu wenyewe, hatuwezi kushinda mazoea mabaya.
Mwokozi wetu yu pale pale, akitamani kutusaidia!
Paulo alijua siri.



154

(Fungu: Wafilipi 4:13)
Alisema, Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.
Wafilipi 4:13.


155


Mwanamke mmoja alihudhuria mikutano kama huu jioni moja.
Wakati mchungaji alipozungumza naye, alinena juu ya kurejea kwa familia ya Mungu.
Macho yake yaling'aa alipojibu, Ningependa, lakini siwezi. Ninavuta.
Akamuita kwa jina na kuuliza, Je, unaamini ya kwamba Yesu anataka uwe na ushindi juu ya haya mazoea?
OO ndiyo, Ninaamini. Lakini siwezi. Mimi ni mdhaifu sana.
Akasema, Je, naweza kukusomea fungu la Biblia?
Akafungua Biblia yake katika 1 Yohana 5:14, Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawa sawa na mapenzi yake: atusikia.
Sasa, Mariamu, je, unawo ujjasiri ya kwamba waweza kuacha uvutaji sigara? Aliuliza.
La. Yule mwanamke alijibu.
Vema, akasema mchungaji, kwa sababu Biblia yasema,' Huu ndio ujasiri tulio nao kwake.' Hivyo ujasiri u wapi?
Yule mwanamke akajibu, Kwake.

# 15 - Irejeshe Saa Nyuma



156

Akalisoma fungu kwa mara nyingine akaongeza. Kama tukiomba chochote kulingana na mapenzi yake, isipokuwa uvutaji wa sigara, yeye hutusikia. Huku akimgeukia Mariamu aliuliza, Je, niandike hivyo katika Biblia yako? Je, naweza kuishika Biblia yako na kuiandika hiyo kauli hapo?
La, la,  alisema, Sitaki kugeuza chochote katika Biblia.
Akasema, Je, hii ni kulingana na mapenzi ya Mungu ya kwamba uache kuvuta sigara?
Ndiyo, ndivyo ilivyo, alijibu.
Sasa, je, waweza kumuomba Kristo kwa ujasiri kwa ajili ya uwezo aliouahidi?
Oo ndiyo, alijibu, Nina imani naweza.
Ninalo swali moja zaidi,
Ni lini utapokea nguvu hii ya kukuwezesha kuacha kuvuta sigara? Je, itakuwa katika kipindi cha juma moja, mwezi mmoja,  miezi mitatu? Ni lini utapokea uwezo huu?
Ndipo akafungua Biblia yake katika Yohana 1:12 na kusoma,
Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu Kumpokea Yesu ni kupokea nguvu au uwezo, aliendelea.
Sasa, usiku wa leo tumeona ya kwamba waweza kuwa na ujasiri katika Yesu. Tumeona ya kwamba chochote tuombacho kulingana na mapenzi yake, atatupatia.
Na tunajua ni mapenzi yake kwamba wewe uache kuvuta sigara. Tumeona pia ya kwamba unapompokea,  utapokea uwezo.


157

Kwa msaada wake waweza kuishi maisha yaliyo kamili, yenye afya, yenye furaha hapa na wakati huu, na kufurahia uzima wa milele katika nchi mpya. Mwelekee Yesu --Yeye anakuelekea wewe!

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya




1

Waweza Kuanza Tena



2

Mwezi wa Machi,  mwaka 1992, muinjilisti mkristo alikuwa na mfululizo wa mikutano ya kiinjilisti katika ukumbi wa Kremlin kule Moscow.
Baada ya moja ya mikutano, aliketi katika ofisi yake ndogo, wakati mlango ulipofunguliwa wazi ghafula.


3

Kijana aliyeonekana kuwa mkakamavu akiwa na ndevu zisizo chanwa na mwonekano usio nadhifu alivamia chumba.
Akiamini ya kuwa huyu alikuwa akienda kumvamia, muinjilisti alipiga hatua nyuma. Mkalimani wa Kirusi akakaa kati yao.
Mara ile huyu mtu alianza kurusha mikono hewani huku akiongea kwa jazba kwa Kirusi.
Huyu mkalimani akaeleza ya kwamba huyu mtu alikuwa  mmoja kati ya wahalifu waliokithiri wa Moscow.
Alikuwa ameingia na kutoka gerezani mara ishirini na nane.
Hali akiwa amejazwa  na hatia na kukata tamaa juu ya wakati ujao, alitamani kupata amani.
Muinjilisti alisoma kwa utulivu kabisa 1Yohana 1:9 Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.
Alimueleza huyu mtu aliyefadhaika kisa cha yule mwivi msalabani aliyepata msamaha.
Alimhakikishia, Yesu ni Mwokozi yule yule leo. Anatoa msamaha. Anatoa ukombozi. Anatoa wokovu. Uchukue! Shangilia katika huo ! Mtukuze Mungu kwa huo!
Huku machozi yakimtiririka usoni pake, kijana huyu wa Kirusi  mwenye hatia  alipiga magoti na kupokea msamaha wa Mungu.

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya


4

Mwaka mmoja hivi baadaye muinjilisti alitembelea Moscow. Alipomsifu Mungu pamoja na kundi la waumini katika kanisa jipya lililopangwa karibuni, alitambua huyu aliyekuwa mhalifu akiimba katikati ya kwaya.


5

Uso wa huyu mhalifu wa zamani ulionyesha amani mpya ya ndani. Huyu mtu aling'aa tu kwa furaha. Alikuwa amemkubali Kristo. Mafundisho ya Biblia yalikuwa yamebadili maisha yake, na alimfuata Yesu katika ubatizo wa Biblia.

Ubatizo wa Biblia ni kielelezo cha maisha yaliyobadilishwa na neema ya Mungu. Ubatizo hutoa ushuhuda wa mwanzo wa maisha mapya katika Yesu Kristo.

Ubatizo hunena juu ya maisha yaliyo badilishwa. Moja ya vielelezo vyenye nguvu sana vya mabadiliko ya kushangaza ambayo Kristo aweza kuyafanya katika maisha ni kisa cha Sauli ambaye baadaye alikuwa Paulo.


6

Ingawa Sauli alikuwa raia wa Kirumi kwa kuzaliwa,na alielimishwa na waalimu bora zaidi katika Yerusalemi, Sauli alikuwa mtu wenye bidii sana katika dini ya Kiyahudi, na alitambulika kama mtetezi aliyekubuhu wa imani yao.


7

Sauli - ambaye jina lake baadaye lilibadilishwa na kuwa Paulo baada ya kuongoka kwake-- yeye mwenyewe anaeleza alichokitenda ili kuwamaliza Wakristo.



8

(Fungu: Matendo 22:4,5)
Nikawaudhi.....hata kuwaua, nikawafunga,  nikawatia gerezani, wanaume na wanawake.....

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya




9

nikaenda Dameski, ili niwalete wale waliokuwa huko hata Yerusalemu, hali wamefungwa ili waadhibiwe. Matendo 22:4,5.



10

Alipokuwa njiani mwake kwenda Dameski, nuru ng'avu ilitokea mbinguni na kumpiga hata chini.



11

(Fungu: Matendo 22:7,8)
Alisikia sauti, ikisema, ...Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?




12

naye akajibu, Wewe u nani, Bwana? Na sauti ikajibu,




13

Mimi ni Yesu Mnazareti, ambaye wewe unaniudhi. Matendo 22:7,8.




14

(Fungu: Matendo 22:10)
Huyu Farisayo mwenye kiburi alimuuliza Bwana kwa unyenyekevu, 'Nifanye nini, Bwana?' Bwana akaniambia..., 'Simama, uingie Dameski,



15

na huko utaambiwa habari za mambo yote yaliyoamriwa uyafanye.'
Matendo 22:10.


16

Sauli alipigwa upofu na nuru kali hata ikabidi aongozwe hadi kwenye nyumba ndani ya Dameski.

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya


17

Kwa siku tatu Sauli alikuwa na muda wa kuwaza taabu na mateso aliyokuwa amewasababishia watu wa Mungu, na pia juu ya nyakati ambazo alikuwa ameapa ya kwamba Yesu hakuwa Masihi na ya kwamba Wafuasi wake walikuwa tu wazushi waliodanganyika.
Katika kushuhudia dhidi ya watu wa Mungu na katika kuwashitaki kwa kuwasingizia, alikuwa amemshitaki na hata kushuhudia dhidi ya Mwokozi wa Ulimwengu!
Ni taabu kiasi gani katika moyo wake, aliyoipata kutokana na utambuzi huu.
Sauli alikuwa na wasaa kurekebisha mambo yake na Bwana wake.


18

Aliketi katika giza totoro kwa siku tatu, kisha Mungu alimtuma nabii kwake aliyeitwa Anania.
Kisha Anania akamwambia Sauli,



19

(Fungu: Matendo 22:13-15)
'Ndugu yangu Sauli, uone.' Nikamwinulia macho yangu saa ile ile.



20

Akasema, Mungu wa baba zetu amekuchagua wewe upate kujua mapenzi yake,



21

na kumwona yule Mwenye haki, na kuisikia sauti itokayo katika kinywa chake.

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya



22

Kwa maana utakuwa shahidi wake kwa watu wote, wa mambo hayo uliyoyaona na kuyasikia.' Matendo 22: 13-15.
Kisha, ili Sauli asonge mbele katika maisha yake na kufunga mlango kwa yale ya wakati uliopita,




23

(Fungu: Matendo 22:16)
Anania akamwambia Sauli, Basi sasa, unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshe dhambi zako,



24


ukiliitia jina lake.
Matendo 22:16.


25

Hii ndiyo njia ambayo kwayo Sauli alikuwa aunganishwe na Bwana wake milele.
Ubatizo ulikuwa mlango wa kuingilia katika maisha mapya kwa Sauli. Sauli alihitaji kuoshwa na kuwa safi toka kwa mambo ya kutisha aliyokuwa ameyatenda katika jina la dini.
Alihitaji kusafishwa. Alijua alihitaji neema ya Mungu ya ajabu na wokovu na msamaha.


26

Wakati alipobatizwa alijua ya kwamba Mungu alikuwa amemsamehe.
Na Paulo mtesaji angekuwa Paulo, mtauwa kwa ajili ya Yesu maisha yake yote!


27

Je, umewahi kutamani ungeanza upya tena na makosa yote ya wakati uliopita yangeoshwa kabisa?

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya



28

Mungu alijua ya kwamba tulihitaji sote uzoefu kama huo, hivyo akaweka ubatizo kama ishara ili tuunganishwe naye kuanzia wakati huo na kuendelea: mwanzo mpya - maisha mapya ndani ya Yesu.
Ni kipi ambacho kwa uzuri zaidi kingewakilisha kufa katika dhambi na mwanzo wa maisha mapya kuliko ubatizo kwa kuzamisha - kwa kuzamishwa ndani ya maji?


29

Ubatizo wa Kikristo ulikuwa na mwanzo wake kwa Yohana Mbatizaji, nabii ambaye hakuwa mtanashati aliyetokea katika jangwa la Yudea akihubiri kwa ujasiri juu ya toba.
Njia zote zilizoongoza kwenda Mto Yordani zilikuwa zimefurikiwa na watu wakienda kumsikiliza.



30

(Fungu: Mathayo 3:5,6)
Biblia yasema, Ndipo walipomuendea Yerusalemu, na Uyahudi wote, na nchi zote za kando kando ya Yordani;




31

Naye akawabatiza katika mto wa Yordani, huku wakiziungama dhambi zao.
Mathayo 3:5,6.


32

Akifunga mlango kwa karakana yake ya useremala na kumpungia mama yake kwa mkono wa kwaheri, Yesu pia alielekea Yordani.
Wakati Yohana alipomuona Yesu, alimtambua na akasimamisha hubiri lake.



33

(Fungu: Yohana 1:29)
Huku akielekeza wasikilizaji wake kwa Yesu, Yohana alisema, ....Tazama! Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu.
Yohana 1:29.

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya


34

Yohana alitambua Mwana-Kondoo wa kweli wa kafara ambaye alikuwa afe kwa ajili ya dhambi za wote ambao wangeikubali kafara yake.
Wakati Yesu alipoomba kubatizwa, Yohana alisita.



35

(Fungu: Mathayo 3:14)
Alisema, Mimi nahitaji kubatizwa na wewe. Mathayo 3:14.




36

(Fungu: Mathayo 3:15)
Lakini Yesu alisisitiza,....Kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Fungu la 15.
Yohana alitambua ya kwamba Yesu hakuwa na dhambi yoyote ya kuungama.
Na Yesu kwa kweli hakuhitaji kueleleza imani yake katika ufufuo wake mwenyewe!



37

Yesu aliomba abatizwe kwa sababu alitaka kuwa sawa na mwanadamu mwingine yeyote.
Alitaka kuacha mfano ulio mkamilifu kwa ajili yetu kuufuata.
Hivyo Yohana akamzamisha Yesu  ndani ya Mto Yordani,  kwani hii ndiyo maana ya neno ubatizo.



38

(Fungu: Mathayo 3:16,17)
Biblia yasema, Naye Yesu alipokwisha kubatizwa, mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia,



39

akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake;
Mathayo 3:16.

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya



40

na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye.' Mathayo 3:16,17
Katika mbawa za hua, Mungu alituma Upendo wake na maneno ya kumtia moyo Yesu, lakini  alifanya jambo jingie zaidi.


41

Yesu alipokuwa akitembea toka ndani ya maji na kusimama nguo zikidondosha matone ya maji katika kingo zenye tope za Yordani,  Mungu alimtambulisha hadharani kama Mwanae-Mtiwa Mafuta.
Ubatizo wa Kristo uliashiria mwanzo wa huduma yake ya hadhara. Petro alisema,



42

(Fungu: Matendo 10:38)
.......Mungu ali..mtia mafuta (Yesu wa Nazareti) kwa Roho Mtakatifu na nguvu...



43

naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya  wote walioonewa na Ibilisi; kwa maana Mungu alikuwa pamoja naye.
Matendo 10:38.
Yesu mwenyewe hakubatiza, lakini Biblia inayo taarifa ya wanafunzi wake wakifanya hivyo:



44

(Fungu: Yohana 4: 1,2)
..Mafarisayo wamesikia ya kwamba , Yesu anafanya wanafunzi wengi kuliko Yohana,



45

(lakini Yesu mwenyewe hakubatiza, bali wanafunzi wake,)
Yohana 4: 1, 2.
Na tazama amri ya mwisho ya Kristo iliyorekodiwa kabla tu hajaenda mbinguni:

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya



46

(Fungu: Mathayo 28:19,20)
Enendeni basi, mkawafanye watu wa mataifa yote wawe wanafunzi wangu; mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu:



47

Na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.......
Mathayo 28:19,20.


48

Pengine unajiuliza kuwa ni aina gani ya ubatizo wafuasi wa Yesu waliyoufanya baada ya kurudi zake mbinguni.
Bila ya shaka walifuata mfano wa Yesu, kwani walikuwa wanafunzi wake.



49

(Fungu: Waefeso 4:5)
Paulo, mmoja wa wafuasi wa Yesu aliyekuwa na bidii sana, anasema ya kwamba kuna Bwana mmoja, imani moja na ubatizo mmoja
Waefeso 4:5.



50

Taarifa makini kabisa moja tu ya ubatizo baada ya msalaba imerekodiwa katika Kitabu cha Matendo - ubatizo ulioendeshwa na Filipo, muinjilisti.


51

Filipo alipokuwa akitembea kwenye barabara ya vumbi kuelekea Gaza, alimuona mhazini wa Kushi (Ethiopia) wa Malkia Kandake, aliyekuwa na mamlaka ya hazina yote. Alikuwa amekuja Yerusalemu kuabudu.


52

Sasa alikuwa safarini kurejea nyumbani, akisafiri katika gari la farasi huku akisoma katika gombo. Filipo alimkimbilia huyu mtu na kumuuliza

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya



53

(Fungu: Matendo 8:30,31)
...Je, Yamekuelea haya unayosoma? Yule mhazini akajibu kwa haraka,



54

Nitawezaje kuelewa,
mtu asiponiongoza?



55

Akamsihi Filipo apande na kuketi pamoja naye. Filipo akatizama akaona ya kuwa mtu huyu alikuwa akisoma Isaya, sura ya 53.
Huyu Mkushi akamkaribisha Filipo ili amulezee. Sura ilikuwa ikieleza juu ya maisha ya Yesu na kwa undani ilieleza juu ya kusulubishwa kwa Masihi.



56

(Fungu: Matendo 8:35)
Biblia yasema, Filipo....akianzia kwa andiko lilo hilo, akamhubiri habari njema za Yesu.
Matendo 8:35.


57

Lilikuwa fundisho la Biblia zuri kiasi gani, wakiendelea kurushwa rushwa katika lile gari la farasi!
Filipo hakueleza tu juu ya Yesu, bali ni wazi alieleza umuhimu wa ubatizo, kwani Biblia yasema ya kuwa walipofika katika dimbwi la maji, Mkushi alimwambia Filipo,



58

(Fungu: Matendo 8: 36,37 HNKK)
Mahali hapa pana maji; je,kuna chochote cha kunizuia nisibatizwe? Matendo 8:36.



59

Filipo akasema, Kama unaamini kwa moyo wako wote unaweza kubatizwa.

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya



60

Yule Mkushi akasema, Naam, ninaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.
Fungu la 37.



61

(Fungu: Matendo 8: 38)
Basi, huyo ofisa akaamuru lile gari lisimame; na wote wawili, Filipo na huyo ofisa wakashuka majini, naye Filipo akambatiza.
Matendo 8:38.
Filipo akamzamisha mhazini wa Kikushi ndani ya maji, kama jinsi Yohana alivyomzamisha Kristo wakati alipobatizwa.



62

(Fungu: Matendo 8: 39)
Kisha walipopanda kutoka majini, Roho wa Bwana akamnyakua Filipo,



63

.....basi alikwenda zake  akifurahi.
Matendo 8:39


64

Hilo ndilo linalotokea tunapozika maisha ya kale ya dhambi  na kuanza maisha mapya katika Kristo. Wazi kabisa, kuzamisha ilikuwa ni aina ya ubatizo uliotumiwa na kanisa la Kikristo la awali.



65

Kwa kweli, hakuna kielelezo chochote katika Agano Jipya cha aina nyingine yoyote ya ubatizo. Hapa ipo picha ya dimbwi la kubatizia katika kanisa la  karne ya kwanza  kule Filipi.Wanahistoria wa awali wa kanisa na utafiti wa wanaakiolojia


66

wote huonyesha ya kwamba uzamisha ilikuwa aina ya ubatizo hadi kufikia karne za kumi na mbili na tatu.

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya



67

Kadinali James Gibbons aliandika:Kwa karne kadhaa baada ya kuanzishwa kwa
Ukristo ubatizo kwa kawaida ulifanywa kwa njia ya kuzamisha;



68

lakini tangu karne ya kumi na mbili mazoea ya kubatiza kwa kunyunyiza yametawala kanisa Katoliki.



69

Kwani namna hii hufanyika bila usumbufu kama ilivyo ile ya kuzamisha......



70

...Kanisa linatumia busara yake katika kuchagua namna isiyo na usumbufu kuliko zote, kulingana na manzili ya wakati na mahali.
-Imani ya Baba Zetu, Tol. la 94, uk.277.



71

Watalii wengi leo wanalitembelea kanisa la Mt. Yohana, lililopo katika magofu ya jiji la kibiblia la Efeso kule Uturuki. Kanisa hili lilijengwa kama kumbukumbu kwa ajili ya mwanafunzi Yohana. Jambo la kuvutia zaidi ni kisima cha kubatizia, hali kikiwa mviringo kwa umbo, kama futi kumi na mbili za upana na futi nne za kina, kina ngazi ziendazo chini hadi kwenye maji ya ubatizo yaliyo sehemu mbili.



72

Watu wengi wamesikia juu ya kinara cha kale cha kengele kilicho mbele ya Kanisa kuu la Pisa, nchini Italia, ambacho kinafahamika zaidi kama Kinara Kilichoinama cha Pisa.


73

Pamoja na Kanisa kuu na kinara kilichoinama ni kisima cha kubatizia, jengo kubwa la mviringo


74

linalozinga kisima ambacho ni futi kama ishirini toka upande mmoja hadi mwingine na futi nne za kina ambacho kilijengwa katika karne ya kumi na nne.
Miaka elfu moja na mia tatu iliyopita baada ya kupaa kwa Kristo, namna ya ubatizo bado ilikuwa kwa namna ya kuzamisha!



75

Kuna dazani za makanisa ya aina hii yenye visima vya kubatizia kama hivi katika Ulaya. Sitini na sita vinapatikana katika Ulaya pekee, ambavyo ujenzi wake unaonekana kuwa wa kati ya karne ya nne na ya kumi na nne.



76

Lakini huduma ya ubatizo ina umuhimu kiasi gani?



77

Je, kweli ni muhimu kubatizwa?




78

(Fungu: Yohana 3:5)
Yesu akajibu, 'Amin, amin nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho,'



79

hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.' Yohana 3:5


80

Yesu anaelekeza hapa ya kwamba kuzaliwa kwa maji, ikimaanisha ubatizo kama tutakavyoona baadaye, ni muhimu ili mtu aingie mbinguni.

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya


81

Kristo hakuitoa hii kauli ya muhimu mara moja tu. Tazama ya kwamba anasema kwa umuhimu kabisa jambo hilo hilo  katika Marko 16:16:



82

Anayeamini na kubatizwa ataokolewa; asiyeamini atahukumiwa.(Marko 16:16 HNKK). Hatua ya kwanza katika kujiandaa na ubatizo wa Biblia ni kuamini ya kwamba Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zako na ni Mowokozi wako na Bwana.


83

Filipo anasisitiza hitaji hili la imani iliyo kamili katika Kristo kwa huyu Mkushi.
Wakati Mkushi alipomuuliza Filipo kama angebatizwa, Filipo alisema,



84

.......Kama unaamini kwa moyo wako wote unaweza kubatizwa..... Matendo 8:37.



85

(Fungu: Mathayo 28:19)
Yesu aliwapatia wanafunzi wake hatua ya pili, Enendeni....mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza. Mathayo 28:19.
Kufundisha kunatangulia ubatizo.



86

(Fungu: Mathayo 28:20)
Yesu alisema atakaye kubatizwa anapaswa kufundishwa ..kuyashika yote niliyowaamuru ninyi......
Mathayo 28:20.


87

Kwa maneno mengine, mtu anayejiandaa kwa ajili ya huduma takatifu ya ubatizo anahitaji kuelewa mafundisho ya Yesu na kuyakubali. Lakini, inahitajika zaidi ya ujuzi wa mafundisho.

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya



88

(Fungu: Mathayo 28:19)
Basi, enendeni,mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi,mkiwabatiza kwa jina
la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; Mathayo 28:19
Lazima kuwe na kujitoa kwa maisha ya mtu kwa Kristo. Wakati mtu aunganikapo na Yesu, anakuwa na asili ya kuishi kama Kristo.
Hataki kukubali kufanya jambo lolote ambalo Yesu asingekubali kulifanya!


89

Hatua ya tatu ni toba. Petro alisema,



90

(Fungu: Matendo 3:19)
Basi, tubuni mkamrudie Mungu ili afute dhambi zenu........
Matendo 3:19. Toba humaanisha mtu kuhuzunikia dhambi zake kwa ndani kabisa na kuziacha.


91

Hili laweza kutokea tu kwa moyo ambao umekuwa Kalvari - moyo  ambao umeguswa  na kulainishwa na kafara iliyotolewa kwenye msalaba  ili kutuokoa toka dhambini.



92

Hebu tufanye muhtasari wa hatua hizi katika kujiandaa na ubatizo;



93

1. Kabla ya ubatizo mtu sharti amkubali Yesu kama Mwokozi na Bwana.

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya



94

2. Kabla ya ubatizo, mtu sharti aelewe mafundisho ya Yesu na awe tayari kumfuata Yeye.



95

3. Anapaswa aungame dhambi zake zote  na kutubu.


96

Pengine umekuwa ukitamani nyakati fulani kubadilisha maisha yako ili yawe bora zaidi - lakini hujajua tu ni vipi inaweza kufanya hivyo.
Kwa kufuata hizi hatua tatu katika kujiandaa na ubatizo, waweza kuwa mtu mpya-tokea ndani hadi nje.
Kwa nguvu ya Mungu, waweza kubadilishwa, kuzaliwa upya, na kuongoka.


97

Wakati fulani watu huuliza, Ninapobatizwa, Je, ninakuwa sehemu ya kanisa? Au huwa ninabatizwa tu katika Yesu?
Biblia inafundisha ya kwamba ubatizo katika Kristo ni ubatizo wa kuingia katika mwili wake, kanisa.
Wakati umati ulipobatizwa siku  ya Pentekoste, Biblia inatamka,



98

(Fungu: Matendo 2:41, 42)
Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu.



99

Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika,



100

na katika kuumega mkate na kusali. (Matendo 2:41,42)
Fungu li wazi. Tunapobatizwa, hatuwi wajane wa kiroho. Hatuachwi peke yetu. Watu waliobatizwa katika Matendo walidumu katika fundisho la mitume na katika ushirika.
Walikuwa sehemu ya kanisa la Mungu lililoamini Biblia.



101

(Fungu: 1 Wakorintho 12:13)
1 Wakorintho 12:13 inasema: ....Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja. .. Fungu la 28 linabainisha kabisa ya kwamba mwili huu ni kanisa.
Wakati wanaume na wanawake wanapomkubali Yesu na kutoa maisha yao kumfuata, wanatamani kuabudu na waumini wenzao. Mioyo yao inawaka ndani yao kuwa sehemu ya kanisa linalozishika amri za Kristo.



102

(Fungu: Mathayo 28:19,20)
Hii ndiyo sababu Yesu alisema katika Mathayo 28:19,20:
Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu;



103

na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi;........


104

Usiku wa leo Yesu anakuita utoe maisha yako kwake. Anakuita ili uwe sehemu ya watu wake wanaoiamini Biblia, na kuzishika amri zake. Anakupatia mwaliko ule ule aliompatia Paulo:

16 - KUWA NA MWANZO MPYA

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya



105

Sasa basi, ya nini kukawia zaidi? Simama ubatizwe na uondolewe dhambi zako kwa kuliungama jina lake. (Matendo 22:16 HNKK).


106

Jioni moja kiongozi mmoja wa Kiyahudi aliyeitwa Nikodemu alimjia Yesu.
Hakutaka marafiki zake wajue ya kwamba alikuwa akimpenda Yesu.



107

(Fungu: Yohana 3:2)
Alimsifu Yesu kwa kumwambia, Rabi, twajua ya kuwa u mwalimu, umetoka kwa Mungu:



108

kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye.
Yohana 3:2.
Yesu aliweza kusoma moyo wa mtu huyu, hivyo akaenda moja kwa moja kwa mada husika na kumuonyesha Nikodemu alicho hitaji.



109

(Fungu: Yohana 3:3)
Yesu akajibu, akamwambia, 'Amin, amin, nakwambia,



110

Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu.
Yohana 3:3.



111

(Fungu: Yohana 3:4)
Nikodemu alishangaa, kisha akamwuliza Yesu, Awezaje mtu kuzaliwa, akiwa mzee?

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya



112

Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa?'  Yohana 3:4



113

(Fungu: Yohana 3:5)
Yesu akamfafanulia ya kwamba alikuwa akinena juu ya kuzaliwa kiroho, aliposema, Amin, amin, nakwambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho,



114

hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.
Yohana 3:5.
Hapa Yesu ananena juu ya kuzaliwa kiroho ambako kunashuhudiwa kwa njia ya ubatizo.
Maelezo hapa yanamaanisha ukweli ya kwamba mtu ataoshwa kwa maji ya ubatizo.


115

Bila ya shaka Nikodemo, Farisayo aliyejisikia, alitegemea kuingia kwa ufalme wa Mungu kwa heshima ya yeye kuwa mzaliwa asilia, mcha Mungu wa Kiyahudi.


116

Hata hivyo,  Yesu aliliweka wazi ya kwamba chochote kilicho pungufu ya badiliko kamili la maisha kwa uwezo wa Roho Mtakatifu - kama linavyoelelezwa katika ubatizo - hakikuwa cha kufaa.


117

Hii ndiyo njia ya mtu kuweka muhuri katika ukubali wake wa kafara iliyotolewa na Baba kupitia kwa utekelezaji wa Mwana.


118

Huu ndiwo mwanzo wa maisha mapya katika Kristo.

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya



119

(Fungu: Mathayo 3:17)
Kwenye ubatizo wa Kristo, sauti ya Mungu ilisikika, ikisema Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye.
Mathayo 3:17.



120

Ilikuwa wakati huu, ambapo Roho Mtakatifu katika umbo la huwa alimtia mafuta Yesu, ndipo alipokuwa Mtiwa Mafuta au Masihi au Kristo.


121

Tukio hili liliashiria mwanzo wa huduma ya hadhara ya Yesu Kristo.
Kama hivyo, ndivyo ubatizo wa muumini unavyoashiria mwanzo wa maisha mapya pamoja na Kristo Mwokozi wake.
Tukio hili pia huashiria ushuhuda wa hadharani wa muumini kwa ubatizo wake ya kwamba ameunganishwa na Kristo, ya kwamba amemvaa Kristo.




122

(Fungu: Wagalatia 3:27)
Wagalatia 3:27 inasema, Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.



123

Ubatizo, kwake yeye ambaye amemkubali Kristo kama kafara yake, huonyesha imani yake katika mambo makuu matatu ya kafara ya Kristo.



124


(Fungu: Warumi 6:3,4)
Paulo alisema, Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake?
Warumi 6:3

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya




125

Kisha anaendelea katika kuelekeza hatua inayofuata ambayo Mkristo anaichukua katika huduma hii: Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake. Fungu 4.
Lakini kuna sehemu ya tatu kwa tendo hili la imani.



126

(Fungu: Warumi 6:4)
Kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba,




127

vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Fungu la 4.
Umeupata hapo. Mtu akibatizwa amezaliwa kwa Roho na kwa maji!



128

Tunaeleleza  hadharani imani yetu katika mauti, mazishi  na ufufuo wa Yesu Kristo.



129

(Fungu: Warumi 6:11)
Kisha Paulo anatuambia, Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi, na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu Bwana wetu.
Sasa je, waweza kuona kwa nini hii ni sehemu nzuri sana katika maisha ya Kikristo?


130

Ni kama ilivyo sherehe ya Harusi kwa waliochumbiana.
Huu ni wasaa wao wa kushuhudia hadharani ya kwamba wameunganishwa pamoja katika maisha yao yote.



131

(Fungu: Waefeso 4:5)
Biblia inatuambia ya kwamba tunaye, Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja. Waefeso 4:5.
Na bado katika kanisa, inaelekea kuna njia nyingi sana za ubatizo ambazo zinafanyika.

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya


132

Baadhi wananyunyiza, baadhi wanamwagia maji, na wengine  huzamisha. Yawezekanaje kuwa na ubatizo mmoja, wakati kuna kuchanganyikiwa juu ya  njia iliyo sahihi?




133

Tunapaswa tu kuuliza, Je, Yesu alifanya nini?



134

Tunaona ya kuwa Biblia yasema ya kwamba Yohana alikuwa akibatiza katika mto wa Yordani.
Wakati Yesu alipobatizwa, alipanda kutoka majini.
Alibatizwa kwa kuzamishwa.



135

Kwa kweli, Hiyo ndiyo maana ya neno la Kiyahudi baptizo.
Lina maana ya kudumbukiza ndani ya maji au kufunika kabisa kwa maji.
Hii ndiyo njia pekee ya  ubatizo inayowakilisha mauti,  mazishi na ufufuo wa Kristo.


136

Wakati fulani Paulo na mtenda kazi mwenzake Sila walikwenda Filipi kwa mwaliko wa mtu wa Makedonia ambaye Paulo alikuwa amemwona katika ndoto.


137

Waliamka kiasi kwamba watu wenye ghasia waliwashambulia, hata maisha yao yakawa hatarini. Halaiki hii ya watu ilipasua mavazi ya hawa watu wawili, na wenye mamlaka wakaruhusu wapigwe.


138

Waliamka kiasi kwamba watu wenye ghasia waliwashambulia, hata maisha yao yakawa hatarini. Halaiki hii ya watu ilipasua mavazi ya hawa watu wawili, na wenye mamlaka wakaruhusu wapigwe.

# 16 - KUWA NA MWANZO MPYA


139

Walipelekwa gerezani, ambapo askari magereza aliagizwa kuwaweka katika kifungo chenye ulinzi mkali zaidi na kuhakikisha ya kwamba hawatoroki.


140

Usiku wa manane, Paulo na Sila walikuwa wakiimba na kusali, mara ghafula tetemeko likatingisha kuta za gereza - ghafula, malango ya gereza yakafunguka na minyororo ya kila mmoja ikafunguka. Mlinzi wa gereza - yule askari- akaja akikimbia, na, alipoona malango yakiwa wazi alidhani ya kwamba wafungwa wote walikuwa wamekimbia.



141

Alikuwa katika hatua ya kuchukua jambia ili ajiue - akiwa na hakika kabisa ya kwamba angeuawa kwa kuwaruhusu wafungwa watoroke.



142

Lakini Paulo akaita kwa sauti kubwa: Usijidhuru mwenyewe kwa maana sisi sote tuko hapa. (Matendo 16:28 HNKK).


143

Maskini askari magereza aliogopa!- Paulo na Sila- walikuwa wameteswa mikononi mwake huyu mlinzi, bado hawakumchukia na wala hawakutaka kulipiza kisasi. Huyu mlinzi akajua ya kwamba hawakuwa na hatia. Alikimbia akapata taa, kisha akaenda kwenye kichumba chao, hali akianguka katika miguu yao akiomba msamaha.



144

(Fungu: Matendo 16:30,31)
Halafu aliwaongoza nje, akawauliza, Waheshimiwa, nifanye nini nipate kuokoka?




145

Hivyo watu wa Mungu wawili wakajibu, Mwamini Bwana Yesu nawe utaokolewa pamoja na jamaa yako yote.

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya



146

Mlinzi akawachukua Paulo na Sila hadi nyumbani kwake na kuwaosha miguu yao iliyokuwa ikitoa damu pamoja na migongo yao.



147

(Fungu: Matendo 16:33)
Yule askari aliwachukua saa ileile ya usiku akawasafisha majeraha yao, kisha yeye na jamaa yake wakabatizwa papo hapo.



148

kisha yeye na jamaa yake wakabatizwa papo hapo.
Matendo 16:33


149

Marafiki, kama ulikuwa hujaelewa maana na umuhimu wa ubatizo kabla, au kama hujawa na wasaa  wa kumfuata Yesu katika huduma yake takatifu ya ubatizo kwa njia ya kuzamisha, swali lilo hilo na mwaliko unakujia kama ambavyo  Anania alimwuliza Sauli:



150

(Fungu: Matendo 22:16)
Sasa basi, ya nini kukawia zaidi? Simama ubatizwe na uondolewe dhambi zako......
Matendo 22:16.

# 16 - Kuwa na Mwanzo Mpya



151

Wakati Yesu alipobatizwa, sauti toka mbinguni ilisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye. Nawe pia, uingiapo katika maji ya ubatizo, Bwana wetu atanena kwa moyo wako akisema, Wewe u mwanangu mpendwa wangu. Wewe u binti yangu mpendwa wangu. Ninapendezwa nawe. Furaha kuu ya maisha kuliko zote ipo katika kujua ya kwamba unampendeza Mungu. Wakati unapobatizwa, utakuwa na hisia ya ajabu ya kwamba u wa Mungu. U mwana wa Mungu. Kwa namna fulani, ubatizo ni kama harusi. Kabla ya ndoa bibi harusi na bwana harusi ni wapenzi. Ndoa ni ahadi ya hadhara mbele za jamaa na marafiki. Ubatizo uko kama hivyo. Ubatizo hauumbi upendo kwa Mungu ndani ya mioyo yetu.
Sababu ya sisi kutaka kubatizwa ni hii: tumeshampenda tayari.
Ubatizo ni ushuhuda wa hadhara mbele za jamaa zetu na marafiki na kanisa ya kwamba tumo katika mapenzi na tumejitoa kwa Yesu Kristo.
Tufanyapo hili agano la hadhara, maisha yetu ya zamani yanazikwa kwa mfano huu ndani ya maji kwa njia ya ubatizo, na tunainuka kuishi maisha mapya katika Kristo.
Maisha ya kale yamepita - yamezikwa - yasitusumbue tena. Mungu anaahidi kutupatia uwezo wa Roho wake Mtakatifu ili kutuwezesha kuishi maisha ya Kikristo. Watu wengine husita. Wanajizuia. Hawadhani wapo tayari. Ubatizo haumaanishi ya kwamba wewe u mkamilifu. Una maana wewe umejitoa (au umeweka agano).

Yesu anakuita leo ufuate nyayo zake hadi katika kaburi la maji la ubatizo. Anakupa msamaha, uhuru kutoka katika hatia yako yote ya wakati uliopita na uwezo wa kuishi maisha mapya kwa uwezo wa Roho wake Mtakatifu.
Je, utasema ndiyo kwa Yesu sasa hivi? Kama unapenda kumfuata Yesu njia yote katika ubatizo wa Biblia, nataka utembee uje mbele katika ukumbi

huu ili nipate kuomba kwa namna ya pekee kwa ajili yako.
Nawaalika wote msimame kwa ajili ya ombi sasa. Kabla sijaomba, kama wataka kusema, Ndiyo, Yesu, nataka kubatizwa, tembea sasa hivi uje hapa mbele na usimame mbele za madhabahu haya uinamishe kichwa chako, ili nipate kuomba kwa ajili yako. Usisite. Njoo.... sasa hivi, nami nitasali.

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia



1

Udanganyifu Mkuu Kuliko Wote  Duniani




2

Mojawapo kati ya ulaghai mkuu uliopata kurekodiwa ulifanyika miaka ya mwishoni ya  1960. David Stein, kijana stadi wa Kifaransa,  alichora picha zaidi ya 400 alizoziiga tu toka kwa Wachoraji (wasanii) wakuu wa zamani-akawa:
Picasso bandia, Chagall bandia, Renoir bandia, na Van Gogh kati ya wengine.
Aliweka sahihi za majina halisi ya hawa wasanii waliojulikana  katika picha hizi kuu na kuzitoa kana kwamba ni halisi. Zilikuwa ni matoleo ya udanganyifu.
Zilionekana halisi kiasi kwamba, zilitajwa kuwa halisi!



3

Hadi leo, picha za kugushi 110 tu ndizo zimetambulika na kurejeshwa. Stein alikamatwa mwaka 1972 na kutumikia kifungo katika vipindi viwili ; kimoja kule katika gereza la  Sing Sing,  Paris, Ufaransa.
Aliachiliwa mwaka 1980. Wakati akiwa gerezani Stein alibadilika moyo wake na akaamua kuchora picha zenye sahihi yake  yeye mwenyewe.



4

Leo yeye ni msanii mshuhuri na mhadhiri katika vyuo mbalimbali duniani. Na unafikiri anatoa mihadhara juu ya nini zaidi? Kile akijuacho zaidi - Jinsi ya Kugundua Bandia.
Itabidi ukubali, Stein kwa namna fulani alieleleza ya kwamba si rahisi daima kutambua bandia - hata kwa walio mabingwa!
Lakini, mahiri kama alivyokuwa katika utapeli, waweza kusema alikuwa tu  'mtoto wa kuja' (toka mashambani), kama ukimlinganisha na

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia




5

babu yao wote -Shetani! Mwovu anasimama mwenyewe bila ya kiwango chake hasa unapokuja kwa ulaghai, udanganyifu, na utengenezaji wa bandia. Kwa kweli, Shetani hatendi kazi zake waziwazi. Anatenda kupitia kwa watu wengine, mamlaka zingine na mawakala.
Kama angelikuwa adui wa wazi wa Mungu na kweli yake kungekuwa na hatari pungufu kwa Wakristo kudanganywa.
Hivyo hutenda kazi zake kwa kujificha, wakati mwingine akijivisha sura  na vazi la dini-


6

kwa ustadi kabisa akichanganya ukweli na uongo ili kuvuta watu mbali zaidi na ibada ya kweli ya Mungu. Hii imekuwa tamaa iwakayo sana  ndani yake kwa maelfu ya miaka.


7

Mungu hatuachi katika mikono hatari ya huyu mdanganyifu mkuu, bali ametuonya katika Biblia hata juu ya udanganyifu mkuu kuliko wote utakao kuwepo mwishoni mwa wakati.


8

Biblia yasema, Danieli mwenyewe alikuwa na ndoto ya wanyama waliokuwa wakiinuka toka baharini.



9

(Fungu: Danieli 7:2,3)
.........Naliona katika maono yangu wakati wa usiku; Danieli aliandika, na tazama, hizo pepo nne za mbinguni
zilizuma kwa  nguvu juu ya  bahari kubwa.



10

Ndipo  wanyama wakubwa wanne wakatoka baharini, wote wa  namna mbalimbali. Danieli 7:2,3.

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia


11

Wanyama wakitokea baharini?
Hii ina maana gani?



12

Hebu tuiruhusu Biblia itupatie ufunguo wa kufungua huu unabii wenye kutumia mifano. Kwanza, katika ndoto hii, yapo maji.



13

(Fungu: Ufunuo 17:15)
Ufunuo 17:15 yasema...Yale maji uliyoyaona, ......ni jamaa(=watu) na makutano na mataifa na lugha.
Katika sura hiyo hiyo, Mungu anamwambia Danieli kile ambacho wanyama hawa wanawakilisha:




14

(Fungu: Danieli 7:17,23)
Wanyama hao wakubwa walio wanne ni wafalme wanne watakaotokea duniani.



15

....mnyama wa nne atakuwa ni ufalme wa nne juu ya dunia...... Danieli 7:17,23
Neno la Mungu linataja wazi ya kwamba mnyama anawakilisha mfalme au ufalme.


16

Wanyama watokeao kwenye maeneo yenye idadi kubwa ya watu yalikuwa yawakilishe mataifa fulani ambayo yangelitokea hapo mbeleni.
Tambua jinsi anavyoyafafanua katika Danieli 7:3.



17

(Fungu: Danieli 7:3)
Ndipo wanyama wakubwa wanne wakatoka baharini, wote wa namna mbalimbali.

17 - Namna ya Kugundua Bandia

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia



18

(Fungu: Danieli 7:4)
Kwanza alikuwa kama simba, naye alikuwa na mabawa ya tai......
Danieli 7:4



19

(Fungu: Danieli 7:5)
Na tazama, mnyama mwingine, wa pili, kama dubu, naye aliiniliwa upande mmoja,



20

na mifupa mitatu ya mbavu ilikuwamo kinywani mwake katika meno yake.....
Danieli 7:5



21

(Fungu: Danieli 7:6)
Kisha nikatizama, na kumbe! Mnyama mwingine, kama chui, naye juu ya mgongo wake alikuwa na mabawa manne kama ya ndege....
Danieli 7:6




22

(Fungu: Danieli 7:7)
Baadaye nikaona katika njozi ya usiku, na tazama, mnyama wa nne, mwenye kutisha, mwenye nguvu, mwenye uwezo mwingi.



23

naye alikuwa na meno ya chuma, makubwa sana; alikula na kuvunja vipande vipande, na kuyakanyaga mabaki kwa miguu yake.



24

na umbo lake lilikuwa mbali kabisa na wale wa kwanza, naye alikuwa na pembe kumi.
Danieli 7:7.

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia


25

Bustani ya wanyama ya ajabu kiasi gani! Utaon ya kwamba kila mmoja kati ya wanyama hawa hakuwa mnyama wa kawaida.
Wote wanazo tabia fulani zisizo za kawaida zinazotusaidia kuelewa njozi.


26

Danieli alipoendelea kuitafakari njozi ya wanyama wanne, lazima alikumbuka njozi ya Mfalme Nebukadneza -- ndoto ya mtu mkubwa aliyetengenezwa kwa madini mbalimbali. Katika ndoto zote mbili, vielelezo vilivyotumika viliwakilisha falme nne za ulimwengu wa kale,



27

kuanzia Babeli, ufalme wa Wamedi na Waajemi, ufalme wa Wayunani, ufalme wa Kirumi,


28

na kuishia katika kuja kwa Yesu na kuthibitishwa kwa ufalme wake wa milele.


29

Hebu turudi nyuma na tutazame kila moja ya wanyama hawa au mataifa wanapoinuka toka kwa eneo lenye watu la dunia:



30

(Fungu: Danieli 7:4)
Wa kwanza alikuwa kama simba, naye alikuwa na mabawa ya tai; nikatazama, hata mabawa yake yakafutuka manyoya,



31

akainuliwa katika nchi, akasimamishwa juu kwa miguu miwili kama mwanadamu; naye akapewa moyo wa mwanadamu. Danieli 7:4

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia




32

Kitu gani kingewakilisha Babeli kwa uzuri zaidi, ufalme wa kwanza wa dunia ( uliowakilishwa na kichwa cha dhahabu katika sanamu refu), zaidi ya simba - mfalme wa wanyama?


33

Wababeli wa kale wenyewe je, walitumia simba kuwakilisha ufalme wao?
Wana akiolojia waligundua katika mabaki ya Babeli kielelezo hiki cha simba mwenye mbawa za tai.


34

Kama jinsi simba afahamikavyo kwa nguvu zake na ushindi wake, ushindi wa kijeshi wa Mfalme Nebukadneza ulizidi wote.
Kasi ambayo kwayo Babeli ilipata uwezo wake na kusambaza utawala wake inawakilishwa kwa usahihi kabisa kwa mbawa za tai.
Tambua jinsi Mungu anavyotumia kielelezo hicho hicho cha simba kuiwakilisha Babeli:



35

(Fungu: Yeremia 4:7)
Simba ametoka katika kichaka chake, ndiye aangamizaye mataifa; ameanza kushika njia,



36

ametoka katika nchi mahali pake; ili aifanye nchi yako kuwa ukiwa... Yeremia 4:7.


37

Mfalme mwenye kiburi, na majivuno wa Babeli aliutafakari ufalme wake kama utakaodumu milele.
Yaonekana wazi ya kwamba hakulipa nafasi wazo la taifa jingine kuitawala dunia.
Aliandika katika matofali ya majengo, Na udumu milele.

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia



38

Mwezi wa Oktoba  tarehe 13, 539 K.K., ufalme wa Babeli (uliowakilishwa na kichwa cha dhahabu katika sanamu la madini na simba mwenye mbawa za tai katika ndoto ya Danieli) uliufikia mwisho ambao haukuwa na utukufu.



39

Ufalme  au himaya iliyowakilishwa na mnyama wa pili - dubu - hauwezi kuwa mwingine isipokuwa taifa lililokuwa likishinda la Wamedi - Waajemi, ufalme huo huo uliowakilishwa na mikono na kifua cha fedha katika sanamu kubwa la mtu  la madini. Danieli alipomwangalia yule dubu katika ndoto, alisema,



40

(Fungu: Danieli 7:5)
.......Naye aliinuliwa upande mmoja, na mifupa mitatu ya mbavu ilikuwamo kinywani mwake katika meno yake......
Danieli 7:5.


41

Danieli alisema ya kwamba dubu alikuwa na mifupa mitatu katika kinywa chake kati ya meno yake, lakini Biblia haielezi maana yake.



42

Hata hivyo, wasomi wengi  wanaamini ya kwamba mifupa mitatu iliwakilisha



43

Lydia, Babeli na Misri - maeneo makuu matatu yaliyoliwa na majeshi ya Wamedi na Waajemi.



44

Ufalme wa Kiajemi ulitawala kwa karne mbili, lakini  licha ya kuwa utawala mkali na wenye nguvu, Mungu alimfunulia Danieli katika ndoto ya kwamba mnyama mwingine, au ufalme, ungeinuka:

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia



45

(Fungu: Danieli 7:6)
na kumbe! Mnyama mwingine; kama chui, naye juu ya mgongo
wake alikuwa na mabawa manne kama ya ndege;



46

mnyama huyo alikuwa na vichwa vinne; akapewa mamlaka. Danieli 7:6.


47

Kama jinsi mwendo wa pole wa dubu usivyopatana kabisa na kasi ya juu ya chui, ndivyo ilivyokuwa kwa majeshi ya Kiajemi yalivyoshindwa kujitetea yenyewe dhidi ya mwendo wa kasi wa Aleksanda Mkuu.



48

Katika ndoto ya kinabii ya Nebukadneza, tumbo la shaba na mapaja (au kiuno isemavyo Biblia ya kiswahili) ya sanamu viliwakilisha ufalme wa tatu wa dunia wa Uyunani, na vivyo ndivyo ilivyo kwa chui katika ndoto ya Danieli.


49

mabawa manne huwakilisha kasi ya juu ya ushindi wa Aleksanda.
Alimshinda Dario wa III wa Uajemi katika pambano la Arbela mwaka wa 331 K.K., na hivyo kuwa katika kipindi cha pungufu ya miaka 12 mtawala wa himaya pana zaidi kuliko zote ambazo dunia ilipata kufahamu.
Vichwa vinne vya chui viliwakilisha migawanyo minne ya Uyunani.



50

(Fungu: Danieli 8:22)
....falme nne zitasimama kutoka katika taifa lile,.....
Danieli 8:22.

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia


51

Historia inatuambia ya kwamba Ufalme wa Kiyunani uligawanyika katika sehemu nne.
Aleksanda alikufa katika umri wa miaka thelathini na mbili, miaka saba tu baada ya ushindi wake wa Arbela.
Hata kabla hajazikwa, pambano kwa ajili ya mamlaka lilianza, kwanza kati ya jamaa zake na halafu kati ya viongozi wake wa kijeshi.
Hatimaye, majenerali wanne wa Aleksanda walipata utawala wa ile milki.



52

Sasa mnyama chui, au Uyunani alikuwa na vichwa vinne!
Cassander, Lysimachus Ptolemy, na Seleucus.



53

Watu wengi hupata shida katika kuelekeza kichwa kimoja katika mwelekeo ulio sahihi.
Je, unafikiri ingekuaje kama ungekuwa navyo vinne? Fujo!
Kila kichwa kikijitahidi kuwa cha kwanza!
Kwa hakika hivyo ndivyo ilivyotokea kwa Milki ya Kiyunani, majenerali wanne wa Aleksanda walikuwa wachoyo na wenye tamaa ya cheo, watu waliotaka kutawala ufalme.



54

Kila mmoja alinoa jambia dhidi ya mwenzie
na ufalme ukaanguka katika tatizo la mashindano.
Aleksanda Mkuu, uk. 494.



55

Vurugu na mashindano yaliendelea kati ya sehemu nne za milki hadi hatimaye,Mwezi wa Juni 22, 168 K.K., katika pambano la Pydna,
Ufalme wa Aleksanda Mkuu uliangamia, miaka 144 baada ya kifo chake.-
Historia ya Rumi, kitabu cha 3, sura ya 10.

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia


56

Lakini vipi juu ya mnyama wa nne mkatili ambaye Danieli alisema angeinuka na kutawala baada ya Ufalme wa Kirumi?


57

Malaika alimwambia Danieli ya kwamba huu ufalme wa nne ungekuwa tofauti na zile falme zingine. Mnyama awakilishaye ufalme huu angekuwa na nguvu zaidi kuliko kawaida, na alikuwa na meno makubwa  ambayo yaliangamiza mawindo yake. Hapa imewekwa picha ya mamlaka ya kikatili na ya ubaya.


58

Maelezo mazuri zaidi ya kuinuka kwa Ufalme wa Kirumi hayawezi kupatikana.


59

Rumi ilikuwa korofi na isiyo na huruma kuliko falme zote zilizotangulia.
Waliweza hata kuangamiza mataifa mazima  au kuuza watu wao kuwa watumwa.



60

Huyu mnyama wa kutisha alikuwa na meno ya chuma, wakati yule mnyama wa nne aliyekuwa katika  mfumo wa yale madini aliwakilishwa kwa miguu ya chuma.
Danieli alivutiwa na huyu mnyama wa kutisha, na hasa zile pembe zake kumi.



61

(Fungu: Danieli 7:8)
Alisema, Nikaziangalia sana pembe
zake, na tazama, pembe nyingine ikazuka kati yao, nayo ilikuwa  ndogo,



62

ambayo mbele yake  pembe tatu katika zile za kwanza zaikang'olewa kabisa; .... Danieli 7:8.

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia




63

(Fungu: Danieli 7:24)
Malaika alimwambia Danieli ya kwamba, Na habari za zile pembe kumi, katika ufalme huo wataondoka wafalme kumi... Danieli 7:24.



64

Bila wasiwasi mawazo ya Danieli yalirudishwa nyuma kwa lile sanamu kubwa la madini lililokuwa na miguu ya chuma na udongo, ikiwakilisha migawanyiko ya Ufalme wa Kirumi.



65

Mwaka wa 476 BK makabila ya kishenzi ya kaskazini ya Ulaya yalikuwa yameangamiza kwa ukubwa Ufalme wa Kirumi. Saba kati ya falme hizi (mataifa) bado yako Ulaya leo.


66

Lakini jambo liliompendeza Danieli zaidi lilikuwa ile pembe ndogo iliyojisukuma yenyewe kwenda juu kati ya pembe kumi, ikizing'oa pembe tatu katika pambano lake la kupata ukuu.



67

(Fungu: Danieli 7:8)
Danieli alitambua ya kwamba ...katika pembe hiyo mlikuwa na macho kama macho
ya mwanadamu, na kinywa kilichokuwa kikinena maneno makuu. Danieli 7:8.


68

Hii pembe ndogo ilimtia wasiwasi Danieli.



69

(Fungu: Danieli 7:15)
Aliandika, Basi, mimi Danieli, roho yangu ilihuzunika mwilini mwangu, na hayo maono ya kichwa changu yakanifadhaisha. Danieli 7:15.


70

Kwa nini maelezo haya ya hii pembe ndogo yamsababishe Danieli kuwaza kiasi hiki?

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia



71

(Fungu: Danieli 7: 21,25)
Kwa sababu ... na pembe iyo hiyo ilifanya vita na watakatifu, ikawashinda.



72

Naye atanena maneno kinyume chake Aliye juu,



73

naye atawadhoofisha watakatifu wake
Aliye juu; naye ataazimu kubadili majira na sheria:



74

nao watatiwa mikononi mwake kwa wakati,
na nyakati mbili na nusu wakati.
Danieli 7:21,25.


75

Danieli alitambua ya kwamba huu utabiri haukuwa tu juu ya historia ya kidunia, lakini ya kwamba ulikuwa na uhusiano na watu wa Mungu.


76

Pembe hii ndogo ilifanya vita dhidi ya watakatifu wa Mungu na kwa kweli ilishinda dhidi yao kwa kipindi fulani.
Ni wazi, ilikuwa iwe ni mamlaka yenye chuki, itesayo --- mamlaka au wakala atumiwaye na Shetani ili kufanya vita dhidi ya Mungu, watu wake, na kweli yake.



77

(Fungu: Danieli 7:28)
Danieli alisema, .......fikira zangu zilinifadhaisha,

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia



78

na uso wangu ulinibadilika; lakini naliliweka jambo hilo moyoni mwangu.
Danieli 7:28,



79

Ni nani huyu aliye pembe ndogo?




80

Hebu na tuchunguze maelezo ya Biblia juu ya hii pembe ndogo na kuona taarifa ya kihistoria iliyopo juu ya utimilifu wake.
Danieli alieleza juu ya mnyama wa nne, ama ufalme wa nne wa dunia wa Rumi, kama




81

(Fungu: Danieli 7:7)
... mwenye kutisha, mwenye nguvu, mwenye uwezo mwingi...... naye alikuwa na pembe kumi.
Danieli 7:7.



82

(Fungu: Danieli 7:24)
Danieli 7: 24 inatuambia ya kwamba pembe kumi ziliwakilisha ' wafalme kumi watakaoinuka.'


83

Badala ya ufalme mwingine wa dunia kutokea katika sura ya kihistoria baada ya kuanguka kwa ile ya nne, unabii ulitabiri ya kwamba kungekuwa na mgawanyiko wa Ufalme wa Kirumi, matokeo yake yakiwa ni falme ndogo ndogo kumi.
Historia inatuhakikishia juu ya ile sehemu ya unabii wa Danieli.

17 - Namna ya Kugundua Bandia

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia


84

Wanahistoria wanatuambia ya kwamba mgawanyiko wa Rumi ulimalizika mwaka wa 476 B.K.
Kulingana na mwana  historia wa Kiingereza, Edward Elliot, katika kitabu chake Horae Apocalyptiae, makabila yafuatayo ya kishenzi yaliipelekesha Milki ya Kirumi tokea  351 B.K. hadi 476 B.K.



85

Orodha ifuatayo inatupatia majina ya majina ya makabila ya  Kijerumani  na yale ya  leo yanayotokana nayo:
Alamanni  --------- Wajerumani
Burgundian -------Waswisi
Franks    -----------Wafaransa
Lombards ---------Waitalia
Saxons   ----------- Waingereza
Suevi    -------------Wareno
Visigoths ----------Wahispania
Heruli  -------------- Walimalizika
Ostrogoths --------Walimalizika
Vandals-------------Walimalizika


86

Hizi ndizo pembe kumi za mnyama wa nne ambazo Danieli aliziona.
Na kulingana na unabii, pembe ndogo ilikuwa iinuke na kuwa mamlaka kuu baada ya pembe kumi, au migawanyiko ya Ufalme wa Kirumi.



87

(Fungu: Danieli 7:24)
Na habari za zile pembe kumi, katika ufalme huo wataondoka wafalme kumi;



88

na mwingine ataondoka baada ya hao;.....
naye atawashusha wafalme watatu.
Danieli 7:24.

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia



89

Mwaka wa 493 B.K., Heruli walifikia hatima yao kwa msaada pia wa Mfalme Zeno.




90

Mfalme mwingine, Justinian, aliwafutilia mbali Wavandal katika mwaka wa 534 B.K.
na kisha akavunja nguvu ya WaOstrogoth mwaka wa 538 B.K.



91

Hivyo, pembe tatu za unabii wa Danieli zikang'olewa kabisa, hili likifanya kuinuka kwa kanisa la Kirumi kuwa hakika.



92

Ilikuwa wakati huu ambapo Justinian alitoa tamko la kumsimika askofu, au papa, wa Rumi kama kiongozi wa kidini wa Rumi Magharibi.
Danieli pia alitabiri ya kwamba pembe ndogo ingekuwa tofauti na falme zingine:



93

(Fungu: Danieli 7:24)
....Naye atakuwa mbali na hao wa kwanza.... Danieli 7:24. Je, huyu mnyama alikuwa tofauti? Hakika alikuwa hivyo!


94

Falme zingine zilikuwa mamlaka za kisiasa, lakini pembe ndogo ilikuwa kanisa lililotawala mamlaka ya kisiasa.


95

kidole cha kinabii kingeonekana kusonda bila makosa kwa Kanisa la Kirumi la Zama za Kati kama pembe ndogo ya Danieli 7, kama jinsi Wanamatengenezo wa Kiprotestanti walivyodai.
Danieli alitoa tabia nyingine inayotambulisha hii pembe ndogo:

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia



96

(Fungu: Danieli 7: 21)
Nikatazama, na pembe iyo hiyo ilifanya vita na watakatifu, ikawashinda;
Danieli 7:21.



97

(Fungu: Danieli 7:25)
Alisema pia ya kwamba mamlaka hii inge ...wadhoofisha watakatifu ..... Fungu 25.


98

Je, kanisa la Zama za Kati lilijihusisha na utesaji? Kwa bahati mbaya, Ndiyo!
Mabaraza makuu ya kuwahukumisha watu, vita vitakatifu vya kidini, Wahaguenoti, Wawaldensia, Waalbigense, Miaka Thelathini ya Vita, mateso ya kutumia vifaa kama vitanda, magereza yaliyokuwa chini ya ngome,


99

miali ya moto toka kwa wafia dini waliochomwa katika mti - yote haya kihistoria yanahusiana na kanisa nyakati za zama za giza - wakati wa ukuu wake.
Lakini tunaona ya kwamba kuna tabia nyingine ya muhimu sana inayoitambulisha hii pembe ndogo.



100

(Fungu: Danieli 7:25)
Unabii ulitabiri ya kwamba haya mamlaka yange ........azimu kubadili majira na sheria;...... Danieli 7:25.
Je, mamlaka ya upapa katika Zama za Kati yalijaribu kubadili sheria ya kimbingu ya Mungu?


101

Ndiyo, inadai ilibadili Sabato, ikijenga misingi yake katika mapokeo, ikabadili toka Jumamosi kwenda Jumapili.




102

Tabia ya mwisho tutakayojifunza inaeleza ni wakati gani haya mamlaka yatakuwa na ukuu na urefu wa muda ambao itawatesa watakatifu wa Mungu:




103

(Fungu: Danieli 7: 25)
.....Nao watatiwa mikononi mwake kwa
wakati, na nyakati mbili na nusu wakati. Danieli 7:25. Hapa tunapata mifano zaidi ya Kibiblia.




104

Neno wakati huwakilisha mwaka mmoja na neno nyakati huwakilisha miaka miwili, au siku za kinabii 720.
Nusu wakati ingewakilisha nusu mwaka, au siku 180. Tunapoongeza wakati (siku 360), nyakati (siku 720), na nusu wakati (siku 180), tunafikia jumla ya siku za kinabii 1,260, au miaka.




105

(Fungu: Ezekieli 4:6)
Kulingana na Ezekieli, siku ya kinabii inawakilisha mwaka mmoja. ...siku moja
kwa mwaka mmoja, nimekuagizia. Ezekieli 4:6.
Mamlaka ya pembe ndogo ilikuwa iwe na nguvu kwa miaka 1,260!
Historia inahakikisha juu ya usahihi wa kipindi hiki cha wakati.




106

Waostrogoth, kabila la mwisho kati ya makabila kumi yaliyopinga kanisa la Kirumi, liliangushwa katika mwaka wa 538 B.K., likiacha kanisa la Kirumi likiwa huru kuendeleza mamlaka yake ya kisiasa na ya kikanisa.




107

Miaka 1,260 kamili baadaye, katika mwaka wa 1798, mamlaka ya kisiasa ya Kanisa la Kirumi yalivunjwa na jenerali wa Napolioni, Berthia.

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia


108

Kama ambavyo tumejifunza katika unabii wa Danieli 7 na pembe ndogo iliyoinuka katika kichwa cha mnyama wa nne, tumegundua tabia zifuatazo zihakikishazo kuwa mamlaka hii ni ya namna gani. Hebu tutizame dondoo hizi.


109

1. Pembe hii ndogo ingeinuka katikati ya Ulaya Magharibi kati ya falme kumi ambazo zilikuwa zimepanda wakati Rumi ilipovunjika. Danieli 7:8.



110

2. Katika kuinuka kwake katika mamlaka, pembe ndogo iliing'oa falme tatu kati ya zile falme za zilizotangulia. Hizi falme tatu zilikuwa ni Heruli, Ostrogoth, na Wavandali. Haya mataifa matatu yalikuwa yakifuata mafundisho ya Arius na yakikataa kumkubali papa kama kiongozi wa kanisa. Danieli 7:8


111

3. Unabii unasema ya kwamba hii Pembe Ndogo ingeinuka kati ya pembe zingine baada ya kuimarishwa. Danieli 7:20. Hii ina maanisha ya kwamba ufalme huu ungeanza baada ya mwaka wa 476 B.K.


112

4. Mamlaka haya yangekuwa tofauti na falme zingine. Ulikuwa ufalme wa kisiasa na wa kidini hapo kwa wakati mmoja. Danieli 7:24.


113

(Fungu: Danieli 7: 21,25)
5. Pembe ndogo ingetesa au kuwadhoofisha watakatifu. Nikatazama, na pembe iyo hiyo ilifanya vita na watakatifu, ikawashinda; Danieli 7: 21,25.

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia


114

(Fungu: Danieli 7:25)
6. Hii mamlaka ingeli azimu kubadili majira na sheria; Kwa maneno mengine kanisa hili lingejifikiria lenyewe kuwa na uwezo wa kubadili nyakati za Mungu na Amri zake. Danieli 7:25.




115

(Fungu: Danieli 7:25)
7. Unabii unaonyesha ya kwamba mamlaka hii ingetawala kwa ukuu kwa kipindi cha miaka 1260. Kwani Biblia yasema: nao watatiwa mikononi mwake kwa wakati, na nyakati mbili, na nusu wakati. Danieli 7:25.


116

Waweza kuona kwa unabii huu ya kwamba kuna mamlaka moja tu katika dunia iliyoinuka katika wakati sahihi mahali sahihi ili kutimiliza dondoo zote hizi. Hili ni kanisa la Kirumi.


117

Sasa, hebu tukimbie mbele zaidi hadi katika kilele cha unabii mkuu wa Danieli, kwani una mwisho wa kufurahisha sana kwa watu wa Mungu.


118

Katika njozi, kama jinsi Danieli alivyoshuhudia mamlaka duniani zikipambana ili kuupata ukuu zaidi ya zingine katika mambo ya kisiasa na kidini,


119

mtizamo wake kwa ghafula ulihamishwa toka duniani hadi mbinguni.



120

(Fungu: Danieli 7:9, 10)
Nikatazama hata viti vikawekwa, na mmoja aliye mzee wa siku ameketi;

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia



121

Mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa chake kama sufu safi.



122

kiti chake cha  enzi kilikuwa  miali ya moto
na gurudumu zake  moto uwakao;



123

Mto kama wa moto ukatoka ukapita mbele zake;



124

maelfu elfu  wakamtumikia;



125

na elfu kumi mara elfu kumi wakasimama mbele zake; hukumu ikawekwa na vitabu vikafunuliwa. Danieli 7:9,10.


126

Danieli alimuona Mungu Baba, hapa akiitwa Mzee wa Siku, akija na kuketi katika kiti cha enzi cha utukufu.



127

(Fungu: Danieli 7:22)
Tambua jinsi Danieli alielezavyo tukio hili:Hata akaja huyo mzee wa siku.... Danieli7:22.
Sasa mahakama iko tayari kwa ajili ya hukumu kuanza

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia



128

(Fungu: Danieli 7:10)
....hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa. Danieli 7:10.
Danieli alionyeshwa hukumu ya mbinguni, Mungu akihukumu mamlaka ya pembe ndogo iliyofanya vita dhidi ya watakatifu.
Danieli pia aliona matokeo ya hukumu hii:



129

(Fungu: Danieli 7:26)
Lakini hukumu
itawekwa, nao watamwondolea mamlaka
yake,



130

kuipoteza na kuiangamiza, hata milele.
Danieli 7:26.


131

Kisha Danieli akaona kitu fulani cha pekee sana, kizuri sana, kikitokea baada ya Baba kuketi na hukumu kuwa tayari kuanza:



132

(Fungu:Danieli 7:13)
Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbingu,



133

akamkaribia huyo mzee wa siku, wakamleta karibu naye. Danieli 7:13.


134

Ni nani huyu mheshimiwa aitwaye mwana wa mtu aliyewakilishwa mbele za Hakimu wa Milele?

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia



135

Yesu alilitumia jina hili kwa ajili yake mwenyewe kwa zaidi ya mara arobaini katika Agano Jipya. Kwa wanafunzi wake walioshangaa,



136

(Fungu: Mathayo 17:22,23)
Alisema, ....Mwana wa Adamu anakwenda kutiwa katika mikono ya watu:



137

Nao watamwua, na siku ya tatu atafufuka....
Mathayo 17:22,23.
Kwa swala la Yuda, mwanafunzi msaliti, Yesu aliuliza,



138

(Fungu: Luka 22:48)
.....Wamsaliti Mwana wa Adamu kwa kumbusu?.....Wamsaliti Mwana wa Adamu kwa kumbusu? Luka 22:48.
Lakini kauli ya muhimu zaidi ilielekezwa kwa kuhani mkuu aliyekuwa ameketi katika hukumu kwa kesi ya Kristo:



139

(Fungu: Mathayo 26:64)
....Tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu,



140

akija juu ya mawingu ya mbinguni. Mathayo 26:64.
Hapa Yesu bila ya kukosea anajitambulisha Yeye binafsi kama Mwana wa Mtu ambaye Danieli alimwona katika njozi -- Yeye aliyekuja katika mawingu ya mbinguni.

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia



141

Kristo anakuja kwenye hukumu kuwakilisha wadhambi wote ambao wamemkubali Yeye kama Wakili na Mpatanishi.
Kama wakili wetu katika mahakama, kamwe hajashindwa kesi!
Fungu lasema ya kuwa vitabu vilifunguliwa.



142

(Fungu: Danieli 7:10)
....hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa.
Danieli 7:10, sehemu ya mwisho.


143

Vitabu vitakuwa na kila tendo katika maisha yetu kama ni maovu ama mema.
Ipo taarifa pia ya nafasi  ambazo Mungu ametupatia na jinsi ambavyo tumeitikia kwa nafasi hizo alizotupatia.


144

Kama tumemkubali Kristo kama Mwokozi wetu na Bwana, pale kesi yetu ijapo mbele za Mungu, Kristo anasimama mbele na kutangaza ya kwamba Yeye ni Mwokozi wetu na ya kwamba Mauti yake imeondoa kila dhambi tuliyopata kuitenda!


145

Katika siku ile kulingana na taarifa za mbinguni, maisha yake yasiyo na dhambi huchukua nafasi ya maisha yenye dhambi tuliyoyaishi, na jambo moja tu ambalo Baba analiona anapotizama katika taarifa zetu ni maisha yasiyo na dhambi ya Kristo ambayo yamewekwa badala ya yetu katika taarifa zetu.


146

Tutakuwa na uzima wa milele, siyo kwa sababu ya kile tulichokitenda, lakini kwa sababu ya kile alichokitenda Kristo kwa ajili yetu msalabani.
Pengine Danieli alipendezwa sana hivyo katika swala la Pembe Ndogo na kile kitakachotokea kwayo kiasi cha kurukia mbele na kutoa kisa kamili cha kazi yake, ambacho kwa hakika huchukua nafasi baada ya hukumu ya upelelezi,

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia


147

wakati mambo ya dunia hii yakiwa yametizamwa kwa karibu na uamuzi kufanyika juu ya wale watakao kuwa sehemu ya ufalme wa milele wa Mungu. Ufalme ulikabidhiwa kwa Kristo na mamlaka yake:



148

(Fungu: Danieli 7:14)
Naye akapewa  mamlaka, na utukufu, na ufalme,



149

ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wamtumikie:



150

mamlaka yake  ni mamlaka ya  milele, ambayo hayatapita kamwe,



151

na ufalme wake ni ufalme usioweza kuangamizwa.
Danieli 7:14.
Danieli anaendelea na habari nzuri zaidi juu ya ufalme huu:



152

(Fungu: Danieli 7:27)
....Na ufalme, na mamlaka... watapewa watu wa watakatifu wake  Aliye juu.......
Danieli 7:27.
Watu wa Mungu, watakatifu wake, watakuwa warithi pamoja na Kristo katika kuchukua ufalme  ule wa milele:



153

(Fungu: Danieli 7:18)
.....Lakini watakatifu  wake Aliye juu wataupokea ufalme, na kuumiliki huo ufalme milele, naam hata milele na milele. Danieli 7:18.

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia


154

Sehemu hii ya unabii inapelekana na lile jiwe katika ndoto ya Nebukadneza lililochongwa bila kutumia mikono ya mtu na kulipiga sanamu miguuni na kuwa




155

(Fungu: Danieli 2:35)
.....milima mikubwa, likaijaza dunia yote. Danieli 2:35.
Katika sehemu hizi mbili za kinabii zinazolandana---ndoto ya Nebukadneza ya sanamu kubwa na


156


ndoto ya Danieli ya wanyama -- Mungu aliiweka kwa muhtasari historia ya dunia tokea wakati wa Babeli ya kale hadi siku kuu wakati Yesu atakapokuja kuuweka ufalme wake wa milele wa upendo na haki.


157

Sisi leo tunaishi pale chini kabisa katika nyayo zenye mchanganyiko wa chuma na udongo.
Wakati unaisha kwa dunia hii na wakaaji wake!
Huu ndiwo ujumbe Mungu anaojaribu kushirikiana na kila mmoja wetu kwa njia ya unabii wake huu Mkuu.


158

Ni njia ya kushangaza kiasi gani ya kutabiri karne nyingi zijazo za historia ya ulimwengu katika sura mbili tu za Biblia!
Na ukija kulifikiria, je ndoto iliyotolewa kwa Danieli usiku ule wakati mrefu hivi uliopita kule Babeli haikuwa kielelezo kizuri zaidi cha upendo wa Mungu na kuhusika kwake na watu hapa duniani?


159

Unaona, Yerusalemu ilikuwa katika uharibifu.
Watu wa Mungu, Israeli, walikuwa utumwani kule Babeli.
Mambo yalionekana kutisha.
Lakini Mungu, katika njia hii isiyo ya kawaida, alikuwa akimwambia Danieli, Bado ninawatawala.

# 17 - Namna ya Kugundua Bandia



160

Wafalme watakuja na kwenda.
Milki zitainuka na kuanguka, lakini sijasahau watoto wangu duniani au mpango wangu kwa ajili yao. Siku moja kila kitu kitakuwa sawa. Na rafiki, wafalme na falme zimekuja na kwanda.
Jumbe za kinabii pacha za sanamu na mnyama zimekaribia kufikia utimilifu wao wa ujumla. Yesu anakuja upesi kutekeleza hukumu na kurejesha mamlaka iliyopotezwa na Adamu na Hawa muda mrefu uliopita.


161

Anataka watoto wake wote katika Sayari Dunia kuwa sehemu ya ufalme ule, kuwa tayari kwa ajili ya wakati ule wa utukufu wakati Mwokozi wetu atakaporejea!
Kwani katika siku ile ya utukufu tutamwona - Mwokozi wetu na Bwana!

# 18 - KUWEKEWA MUHURI MILELE





1

Jinsi ya kuepuka kupokea Alama ya Mnyama


2

Ilikuwa siku ya furaha, siku kuu, siku iliyosababisha sherehe ya pekee pamoja na gwaride na bendi ya kifalme.
Mfalme Nebukadneza alikuwa amesisimuka.


3

Alikuwa amealika waheshimiwa toka sehemu zote za falme ya Babeli waje.
Ilikuwa siku aliyoitizamia kwa shauku kubwa-- na pia siku ambayo kamwe asingeliisahau siku zote za maisha yake.


4

Wakati fulani uliopita, mfalme alikuwa amepata kuona ndoto ya ngeni.
Alikuwa ameona sanamu kuu ya madini mbalimbali.


5

Hakuweza kukumbuka kwamba ilikuwa ikihusu nini, kwa hiyo Danieli aliweza kumfunulia si tu maana yake bali pia ndoto yenyewe.
Nebukadneza hakuweza kuwaza lolote jingine!


6

Hata hivyo, yeye alikuwa ndiye kichwa cha dhahabu! Ufalme wake ulisimama bila kupingwa duniani. Na sasa kila mmoja angeliweza kuona kielelezo dhahiri cha jinsi Babeli ilivyokuwa hasa --jinsi alivyokuwa mkuu kwa kweli!


7

Alikuwa mkaidi na akaamuru watumishi wake watengeneze sanamu la dhahabu tupu.

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele



8

Sanamu lilikuwa dhahabu tupu, si kichwa tu, bali pia mwili wote.
Kila mmoja alishangazwa na mng'ao wa uzuri wa hii sanamu ya ajabu. Ilikuwa namna ya mfalme ya kuihakikishia dunia ya kwamba ufalme wake ungedumu milele.


9

Katika siku hii maelfu ya waheshimiwa sana wa himaya ya mfalme walikutanika ili kushuhudia kuzinduliwa kwa sanamu ya mfalme ya dhahabu.


10

Ghafula kukawa na ukimya wenye mshindo katika umati uliokuwa mkubwa. Tarumbeta zililia, na msemaji wa mfalme akatangaza kwa sauti kubwa,



11

(Fungu: Danieli 3:4-6)
Danieli 3:4-6
.....Enyi watu wa kabila zote, na taifa, na lugha, mmeamriwa hivi,



12

wakati mtakapoisikia sauti ya panda, na filimbi, na kinubi, na zeze, na santuri na zomari,



13

na namna zote za ngoma, lazima kuanguka na kuiabudu sanamu ya dhahabu



14

mfalme Nebukadneza aliyoisimamisha;



15

na kila mtu asiyeanguka na kuabudu



16

atatupwa saa iyo hiyo katika tanuru ya moto uwakao.
Danieli 3:4-6


17

muziki ukapigwa.
Watu wote wakaanguka chini na kuabudu sanamu.
Naam - karibia watu wote.


18

Katikati ya makutano yaliyosujudu walisimama Shadraka, Meshaki, na Abednego -- Waebrania watatu waliokataa kutomtii Mungu kwa kuinamia na kuiabudu sanamu.
Mara neno likamfikia Mfalme.




19

Akiwa na hasira kwa sababu ya kujua ya kwamba yupo ambaye amediriki kuiasi amri yake kali, Nebukadneza aliamuru ya kwamba waasi waletwe mbele zake.



20

Mfalme alipowatazama hawa Waebrania watatu, aliwatambua mara moja. Walikuwa vijana wasio wa kawaida wenye maarifa mengi na talanta nyingi.



21

Aliwahi kuwapatia majukumu mengi wakati uliopita, ambayo walikuwa wameyatekeleza kwa uaminifu na ustadi. Hali akijihisi kuwa mwema kwao kwa namna fulani, aliamua kuwapatia nafasi nyingine.
Akiwaita kila mmoja wao kwa majina, mfalme alisema,

18 - KUWEKEWA MUHURI MILELE

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele



22

(Fungu: Danieli 3:15)
Basi sasa, mkiwa tayari wakati mtakapoisikia sauti ya ..... na namna zote  za ngoma,



23

na kuanguka na kuisujudia sanamu niliyoisimamisha, ni vema; bali msipoisujudia,



24

mtatupwa saa iyo hiyo katika tanuru  iwakayo moto; Danieli 3:15.
Mara mfalme alipotoa tamko, ilimpasa alitetee la sivyo angepoteza heshima yake mbele za watu wote.


25


Shadraka, Meshaki, na Abednego waliweza kuona miali ya moto toka katika tanuru kubwa.
Kusingekuwa na wasiwasi wowote juu ya makusudio ya mfalme.


26

Je, wangefanya nini? Je, wewe ungefanya nini?
Je, wangeiasi amri dhahiri ya Mungu?
Ah, ingelikuwa rahisi sana kujitetea kibinadamu  ya kwamba isingedhuru sana  kwa mara moja tu kuiinamia sanamu katika mazingira kama haya.
Hata hivyo, maisha yao yalikuwa hatarini!
Je, isingekuwa muhimu kuonyesha heshima kwa mfalme?


27

Ni wazi ya kwamba mawazo ya namna hiyo hayakuwa ndani yao, kwani walikuwa wamefundishwa amri za Mungu tangu utoto, na mojawapo ya hizo ilisema,



28

(Fungu: Kutoka 20:4,5)
Usijifanyie  sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu chochote....

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele



29

Usivisujudie wala kuvitumikia;....
Kutoka 20:4,5.
Kwa utulivu na bila kusita wakatoa jibu:



30

(Fungu: Danieli 3:16-18)
.....Ee Nebukadneza, hamna haja kukujibu katika neno hili.



31

Kama ni hivyo, Mungu wetu tunayemtumikia aweza kutuokoa na tanuru ile iwakayo moto;



32

naye atatuokoa na mkono wako, Ee mfalme.




33

Bali kama si hivyo, ujue, Ee mfalme, ya kuwa sisi hatukubali kuitumikia miungu yako,



34

wala kuisujudia hiyo sanamu ya dhahabu uliyoisimamisha.
Danieli 3:16-18.
Sehemu ya kisa inayosalia inasisimua.
Mfalme alighadhibika na kuamuru ya kwamba tanuru lichochewe mara saba zaidi ya kawaida.


35

Kisha Mfalme akaamuru ya kwamba Shadraka, Meshaki, na Abednego wafungwe na kutupwa katika tanuru la moto.
Moto ulikuwa mkali sana kiasi ambacho wale askari waliowatupa vijana watatu kwenye tanuru walianguka na kufa.

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele


36

Ghafula, mfalme alikuwa miguuni pake akikimbia kuelekea kwenye lango la tanuru, huku akiwapigia kelele washauri wake ya kwamba aliwaona watu wanne wakitembea katikati ya miali ya moto na ya kwamba yule mmoja alionekana kama Mwana wa Mungu!


37

Bwana wetu aliingia katika tanuru la moto. Alikuwa pamoja na wale Waebrania watatu katika miali ya moto. Yeye ni mkombozi mkuu.


38

Nebukadneza aliamuru Waebrania hawa watoke nje ya tanuru, na kwa mshangao wa kila mmoja, hawa watatu walitoka nje bila hata unywele mmoja kuungua au hata harufu ya moshi katika mavazi yao! Ile sanamu kuu ya dhahabu ikasahaulika.
Kichwa cha habari cha tukio kuu la leo, na kwa miaka mingi iliyokuwa mbele , lazima kilikuwa juu ya kisa cha ajabu cha wale vijana watatu.


39

Mungu wao walikuwa amewaokoa toka katika miali ya moto! Ulikuwa ushuhuda wa ajabu kiasi gani wa upendo wa Mungu kwa wafuasi wake waaminifu!
Je, yawezekana kuwa wakati fulani ujao, kutakuwa na atakaye tuamuru jinsi ya kuabudu.
Je, yawezekana ya kwamba kama hawa vijana watatu Waebrania twaweza kukabili adhabu ya mauti juu ya swala la ibada.


40

Naam, wasema, Nina furaha hakuna anayetuamuru jinsi ya kuabudu!
Hiyo ingekuwa vibaya sana! Kukabili mauti kama hukuabudu kwa namna ambayo mtu fulani amekuamuru.


41

Je, wajua ya kwamba kulingana na unabii wa Biblia, changamoto kuu kuliko zote katika historia iko mbele yetu? na kiini cha swala zima kitakuwa ni ibada?

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele



42

Kama Waebrania watatu, kila mmoja aishie wakati wa saa za mwisho za dunia  atakabiliwa na uchaguzi kama huo?
Uchaguzi ambao utatia muhuri hatima yao milele!


43

Nebukadneza, kiongozi mwenye uwezo sana wa Babeli alisimika sanamu ili kila mmoja aiinamie.
Swala halisi lilikuwa ni ibada.
Amri ya pili inayokataza ibada ya sanamu ilikuwa ni jaribu la utii kati ya ibada ya Mungu wa kweli na ibada ya miungu ya uongo.
Tanuru lilichochewa  mara saba na kuwa na joto zaidi ya jinsi lilivyokuwa hapo awali.
Wakati wa taabu kuu kuliko wakati taabu nyingine yoyote.  Adhabu kwa ajili ya kutotii katika muungano huu wa kanisa-serikali ni mauti.




44

Onyo nyeti kabisa lililopaswa kutolewa kwa wakazi wa dunia hii limerekodiwa katika Kitabu cha Ufunuo.
Ni wazi Mungu anauona ujumbe huu kuwa wa muhimu sana, kwani Alisema:



45

(Fungu: Ufunuo 13:9)
Mtu akiwa  na sikio na  asikie.
Ufunuo 13:9.
Sharti tuusikilize ujumbe huu wa muhimu sana!



46

(Fungu: Ufunuo 14:9,10)
.....Mtu awaye yote akimsujudu huyo  mnyama na sanamu  yake, na kuipokea  chapa katika
kipaji cha uso wake, au katika mkono  wake,



47

yeye naye  atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele



48

iliyotengenezwa , pasipo kuchanganywa
na maji, katika kikombe cha hasira yake;



49

naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele
ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo.
Ufunuo 14:9,10.


50

Kila mmoja apaswa kujifunza unabii huu kwa uangalifu ili apate kuwa na uhakika wa kutoshirikiana na mnyama au alama yake.


51

Kulingana na unabii wa Biblia, mwishoni kabisa mwa wakati, wakazi wa dunia watagawanyika katika makundi mawili:
wale wanaomtii Mungu na kuzitii Amri zake, na wale wanaomwabudu mnyama na kupokea alama yake.




52

Shinikizo kubwa sana litawekwa kwa wale watakaokataa kuabudu mnyama au kupokea alama yake.
Itakuwa changamoto nzito kama wakati Waebrania watatu waliposimama mbele za Nebukadneza.



53

(Fungu: Ufunuo 13:16,17)
Naye awafanya wote, wadogo kwa wakubwa,na matajiri kwa maskini,na walio huru kwa watumwa, watiwe chapakatika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao,



54

tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake.
Ufunuo 13:16,17.

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele


55

Hatimaye, tamko litapitishwa litakalowahukumu kifo wale watakaokataa kumwabudu mnyama na sanamu yake.



56

(Fungu: Ufunuo 13:15)
Kuhusu mnyama wa pili wa Ufunuo, Biblia yasema:
Akapewa kutia pumzikatika ile sanamu ya mnyama, hata ile sanamu ya mnyama inene



57

na kuwafanya hao
wote wasioisujudu sanamu ya mnyama wauawe.
Ufunuo 13:15.


58


Mtu anasema, Kama usipomuabudu mnyama, hatutanunua kitu chochote toka kwako au kukuuzia chochote, tena hatimaye tutakuua.


59

Mungu asema, Kama ukimwabudu mnyama, utapokea mvinyo ya ghadhabu ya Mungu.


60

Kila mtu duniani atakabiliwa na uamuzi mgumu sana ambao hawajapata kuufanya.
Ni hukumu gani hii ya Mungu itakayomwagwa kwa waovu?
Ufunuo inalo jibu:



61

(Fungu: Ufunuo 15:1)
Kisha nikaona ishara nyingine katika mbingu,
iliyo kubwa, na  ya ajabu;



62

malaika saba wenye mapigo saba ya mwisho;
maana katika  hayo ghadhabu  ya Mungu imetimia.
Ufunuo 15:1.


# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele


63

Matatu kati ya mapigo saba ya mwisho yataelekezwa maalum kabisa kwa ajili ya mnyama na wale wanaomwabudu. Ni dhahiri ya kwamba Mungu hataruhusu hukumu zake ziwajie watu bila kuwaonya.


64

Hilo ndilo la kushangaza sana juu ya Mungu! Kamwe hatamimina mapigo kwa wanadamu bila kwanza kumpatia kila mmoja nafasi ya kujua kuwa alama ya mnyama ni nini na jinsi ya kuepuka kuipokea.


65

Hali akitoa ujumbe wake wa mwisho wa maonyo, Mungu anatoa ufunguo wa kuufungua unabii, ili tupate kuelewa maana yake.
Hakuna anayepaswa kuikabili changamoto ijayo bila kujiandaa. Ni muhimu sana kwetu kujua haya mamlaka ya mnyama ni yapi na kujifunza namna ya tuwezavyo kukwepa kupokea alama yake.



66

Hebu na tufungue unabii uliopo katika Kitabu cha Ufunuo, na kisha tusome juu ya mamlaka haya ya mnyama.



67

(Fungu: Ufunuo 13:1-8)
Mwanafunzi Yohana aliandika: Kisha nikaona mnyama akitoka katika bahari,



68

mwenye pembe kumi, na vichwa saba, na juu ya pembe zake ana vilemba kumi,



69

na juu ya vichwa vyake majina ya makufuru.

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele



70

Na yule mnyama
niliyemwona alikuwa mfano wa chui, na miguu yake ilikuwa mfano wa chui, na miguu yake ilikuwa kama miguu ya dubu,



71

na kinywa chake kama kinywa cha simba.



72

yule joka akampa nguvu zake na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi.
Ufunuo 13:1,2.



73

Nikaona kimoja cha vichwa vyake kama kwamba kimetiwa jeraha la mauti,



74

na pigo lake la mauti likapona. Dunia yote ikamstaajabia mnyama yule.



75

Wakamsujudu yule joka kwa sababu alimpa huyo mnyama uwezo wake;



76

nao wakamsujudu yule mnyama, wakisema, 'Ni nani afananaye na mnyama huyu?'



77

Tena ni nani awezaye kufanya vita naye?'

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele



78

Naye akapewa
kinywa cha kunena maneno makuu, ya makufuru,



79

Akapewa  uwezo wa kufanya kazi yake miezi arobaini na miwili.
Ufunuo 13:3-5.



80

Akafunua kinywa chake amtukane Mungu, na kulitukana jina lake,



81

na maskani yake, nao wakaao mbinguni.



82

Tena akapewa  kufanya vita na watakatifu na kuwashinda.



83

akapewa uwezo juu ya kila kabila na jamaa
na lugha na taifa.



84

Na watu wote wakaao juu ya  nchi watamsujudu, kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu



85

katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo,
aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia.
Ufunuo 13:6-8.

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele


86

Tunahitaji kuuangalia unabii huu dondoo baada ya nyingine. Hapa tena Mungu anatumia mifano ya kinabii kuelezea utaratibu wa maonyo yake kwa ulimwengu.


87

Na mnyama anawakilisha nini?
Danieli 7 ilitufundisha ya kwamba mnyama anawakilisha falme au mamlaka zinazotawala.
Hapa katika Ufunuo, tunaona picha ya jambo lisilo la kushangaza--mnyama mwenye sehemu nyingi kama mkusanyiko wa wanyama wote wanne aliowaona Danieli!
Hujapata kuona mnyama kama yule!
Mapitio ya wanyama wanne wa Danieli yatatuelekeza na kutusaidia sisi kuelewa uwezo wa mnyama tunayejifunza habari yake.



88

Je, simba aliwakilisha nini? Ndiyo, Babeli!




89

Dubu? Sawa tena: Umedi na Uajemi.



90

Na vipi habari ya chui? Uyunani, ndiyo.



91

Na mnyama wa kutisha mwenye pembe kumi? Mnakumbuka vema!  Ndiyo, aliwakilisha Ufalme wa Kirumi.

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele


92

Mnyama wa Ufunuo 13 ni mamlaka yanayokuja baada ya falme hizi kuu nne za dunia.
Tunaona sasa jambo la kushangaza: mamlaka moja tu duniani ina tabia zote zilizotajwa katika unabii huu.
Maandiko na historia ya kidunia inaweka utambulisho kuwa dhahiri.
Akinena juu ya  mnyama, Yohana aliandika,



93

(Fungu: Ufunuo 13:2)
...yule joka  akampa nguvu  zake na kiti chake cha enzi na  uwezo mwingi. Ufunuo 13:2.
Tunaona ya kwamba joka anamwakilisha Shetani, kwani Biblia yasema,



94

(Fungu: Ufunuo 12:7-9)
Kulikuwa  na vita mbinguni.......



95

Yule joka akatupwa yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na  Shetani, audanganyaye ulimwengu wote.....
Ufunuo 12:7-9.


96

Kwa kawaida, Shetani kamwe haingii katika pambano hali akionekana wazi wazi umbo lake.
Hutenda kazi, hali akijigeuza, kwa kichinichini, kupitia kwa mawakala wengine, mamlaka, na watu.
Ufunuo hutoa picha ya pambano kubwa kati ya Shetani na kanisa:



97

(Fungu: Ufunuo 12:3-5)
Ikaonekana ishara  nyingine mbinguni; na tazama, joka kubwa jekundu,

# 18 - KUWEKEWA MUHURI MILELE



98

alikuwa na vichwa saba na pembe kumi, na juu ya vichwa vyake vilemba saba.



99

....Na yule joka
akasimama mbele ya yule mwanamke aliye tayari kuzaa,



100

ili azaapo, amle mtoto wake.



101

Naye akazaa
mtoto mwanamume, yeye atakayewachunga mataifa kwa fimbo ya chuma.



102

Na mtoto wake akanyakuliwa hata kwa Mungu, na kwa kiti chake cha enzi. Ufunuo 12:3-5.


103

Ni nani huyu mtoto- mwanamume?
Jibu ni Yesu Kristo!
Aliye nyuma ya vitendo hivi ni joka, au Shetani, aonekanaye akitenda kazi zake kwa juhudi sana kupitia kwa mamlaka ya kidunia.
Hilo ndio jambo halisi lililotukia.
Je, mwovu alikuwa akitenda kazi kupitia kwa taifa gani wakati wa kuzaliwa kwa Kristo?



104

Tuendeleapo kufungua kurasa za historia ya kidunia, tunagundua ya kwamba Rumi ya kipagani, chini ya Kaisari, alikuwa akitawala wakati wa kuzaliwa kwa Kristo.

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele


105

Herode Mkuu  alitoa tamko ya kwamba watoto wote wa kiume ndani ya Bethlehemu, hadi katika umri wa miaka miwili, wauawe katika jitihada za kumuua Yesu wakati alipozaliwa.


106

Liwali wa Kirumi, Pontio Pilato, alimhukumu Kristo kifo.


107

Askari wa Kirumi walimpigilia misumari msalabani, na muhuri wa Kirumi ulilinda  mlango wa kaburi. Shetani alitenda kazi kupitia kwa Rumi ya kipagani ili kumuangamiza Kristo.


108

Na Yesu alifufuka na kupaa kwenda Mbinguni kama jinsi unabii uonyeshavyo utabiri.
Je, hili linakupa wewe ujasiri katika unabii wa Biblia?


109

Unabii pia unaonyesha ya kwamba mamlaka hii ya Rumi ya kipagani, inge



110

(Fungu: Ufunuo 13:2)
kumpa nguvu zake, kiti chake, na  uwezo mwingi yule mnyama.
Je, Rumi ya kipagani iliutimiza huu unabii?
Na kama ni hivyo, alipewa nani?


111

Kwa karne nyingi, kanisa la Kirumi lilitumia waraka ulioitwa Zawadi ya Konstantine  ili kuthibitisha haki yake  kwa jiji la Rumi.  Waraka huu, ambao baadaye ulithibitishwa kuwa wa kughushi, uliwapatia dai la haki ya kanisa  kutawala Rumi ya Magharibi, kwa namna zote - kisiasa na kidini.
Waraka huu ulikuwa ndiwo msingi wa kuthibitishia uwezo wao kama ufalme,  papa akiwa mfalme.

# 18 - KUWEKEWA MUHURI MILELE



112

Mwaka wa 300 B.K., Konstantine alihamisha makao yake makuu kwenda Byzantium na akabadili jina la jiji kuwa Konstantinopo kama heshima kwake mwenyewe.


113

Wakati Konstantine alipoondoka alikabidhi kiti chake kwa askofu wa Rumi.
Askofu wa Rumi akawa kiongozi wa kanisa, wakati huo huo akiwa mfalme kwenye kiti cha enzi.
Matokeo yake yalikuwa ni muunganiko wa kanisa na serikali, kanisa likitawala juu ya serikali.


114

Jiji la Vatikan lipo katikati ya Rumi, jiji lililokuwa kiti cha enzi cha Ufalme wa Rumi.


115

Kanisa la Kirumi linaendelea pale hadi leo, siyo tu kama mamlaka ya kidini lakini pia kama mamlaka ya kisiasa. karibu kila taifa duniani hutuma mabalozi Vatikani.


116

Ni muhimu sana kuweka mawazoni ya kwamba unabii hunena juu ya shirika, ama mfumo fulani wa kithiolojia. Hausondi watu mmoja mmoja!


117

Kuna watu wengi sana waaminifu wanaomwabudu Mungu lakini bado hawajui kile unachojifunza leo kutoka katika unabii wa Biblia juu ya mamlaka hii.


118

Utafiti wa ndani  unaoonyesha alama hizi za mamlaka ya mnyama katika Ufunuo 13 unaonyesha wazi ya kwamba ni mamlaka iyo hiyo inayowakilishwa na pembe ndogo ya Danieli 7, tuliyoitafakari muda uliopita.

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele



119

Nabii Yohana alisema mamlaka hii ya mnyama ingelikuwa na alama inayoitambulisha wazi na kwamba ingejaribu kuilazimisha kwa kila mtu katika dunia!




120

(Fungu: Ufunuo 13:16,17)
Naye awafanya wote,wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na
walio huru kwa watumwa, watiwe chapa
katika mkono wao wa kuume; au katika vipaji vya nyuso zao.



121

tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani jina la mnyama yule , au hesabu ya jina lake. Ufunuo 13:16,17.


122

Kulingana na Neno la Mungu, alama hii lazima iwe alama ya uasi au kutotii serikali ya Mungu. Biblia inaelezea wazi kundi lingine ambalo halitapokea alama ya mnyama.



123

(Fungu: Ufunuo 14:12)
Hapa ndipo penye subira ya watakatifu,
hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu.
Ufunuo 14:12.



124

Kwa hakika kabisa, swala kuu ambalo dunia hii inaelekea kwalo litajikita katika kiini cha utii wa amri za Mungu!
Kundi moja la watu linapokea alama ya mnyama, wakati lingine linakuwa tiifu na la kweli kwa Mungu kwa kutunza Amri zake zote na kuitunza imani ya Yesu.



125

Watu wa Mungu pia watapokea alama, lakini itakuwa alama ya Mungu, muhuri wa Mungu.

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele



126

Utawekwa katika vipaji vya nyuso za wafuasi wake.



127

(Fungu: Ufunuo 7:2,3)
Nikaona malaika mwingine, akipanda
kutoka maawio ya jua, mwenye muhuri ya Mungu
aliye hai;



128

akawapigia kelele kwa sauti kuu wale malaika wanne waliopewa kuidhuru nchi na bahari,



129

akisema, 'Msiidhuru nchi, wala bahari, wala miti,



130

hata tutakapokwisha kuwatia muhuri watumwa wa Mungu wetu juu ya vipaji vya nyuso zao.'
Ufunuo 7:2,3.



131

Ninataka muhuri huo, je wewe?
Hakuna kilicho muhimu zaidi ya hicho.
Shindano la mwisho la historia ya dunia liko katika muhuri wa Mungu au alama ya mnyama. Ni kati ya ishara ya Mungu na ishara iliyo bandia.
Tunapogundua muhuri wa Mungu, au alama, itakuwa rahisi kugundua alama bandia ambayo mamlaka ya mnyama yataishinikiza.
Mungu anatuambia kwamba alama yake au muhuri wake ni nini:

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele



132

(Fungu: Ezekieli 20:12)
Tena naliwapa sabato zangu, ziwe ishara kati ya mimi  na wao.....
Ezekieli 20:12.



133

(Fungu: Kutoka 31:13)
Tena, Mungu anasema,Kisha, nena  wewe na wana wa  Israeli, na  kuwaambia: 'Hakika mtazishika sabato zangu,



134

kwa kuwa  ni ishara kati ya mimi na  ninyi katika vizazi vyenu vyote;



135

ili mpate kujua ya kuwa  mimi ndimi  BWANA niwatakasaye ninyi.
Kutoka 31:13.



136

Mungu alisema ya kwamba Sabato ni ishara au alama yake ya mamlaka.
Je, mamlaka ya mnyama inasema ishara yake ya mamlaka ni ipi?



137

Kauli ifuatayo imechukuliwa kutoka katika Katekism ya Kikatoliki:
SWALI: Wawezaje kuthibitisha ya kwamba kanisa linao uwezo wa kuamuru kuwepo kwa sherehe na siku takatifu?



138

JIBU: Kwa kitendo halisi cha kubadili Sabato kwenda Jumapili, ambacho wa Protestanti wanakikubali na kwa  sababu hiyo



139

wanajipinga wenyewe kwa kutunza kwa uhalisi Jumapili na kuvunja vunja sherehe nyingi zingine zilizoamuriwa na kanisa  lilo hilo.

# 18 - KUWEKEWA MUHURI MILELE




140

SWALI: Je, unayo njia nyingine ya kuthibitisha ya kwamba kanisa linao uwezo wa kusimika amri zihusuzo sikukuu?




141

JIBU: Kama lisingelikuwa na uwezo huo lisingelikuwa limebandika utunzaji wa Jumapili, siku ya kwanza ya juma,





142

badala ya utunzaji wa Jumamosi, siku ya saba, badiliko ambalo halina mamlaka yoyote ya maandiko.
- Muhtasari wa Mafundisho ya Kikristo, Henry Tuberville, uk. 58.




143

Jumapili ni alama ya mamlaka ya kidini ya kanisa la Kirumi, kulingana na historia yake lenyewe. Linakubali wazi ya kwamba lilibadili siku ya ibada toka Jumamosi kwenda Jumapili, na zaidi ya hapo,




144

linasema tendo hili ni ....alama ya uwezo wake wa kikanisa na mamlaka.(Barua toka kwa C.F. Thomas, Askofu Mshauri wa Kadinali Gibbons, Oktoba 28, 1895.)
Kanisa la Kirumi linatoa changamoto kwa Waprotestanti kuonyesha kwa nini wameihalifu siku ya Mungu na kugeuka toka kwa




145

Sabato ya Biblia kufuata siku iliyowekwa na




146

desturi na mapokeo,
na kanisa la Rumi.

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele



147

(Fungu: Danieli 7:25)
Danieli alitabiri ya kuwa hii mamlaka ya mnyama inge ........azimu kubadili majira
na sheria......
Danieli 7:25.




148

(Fungu: Danieli 8:12)
Alitabiri pia ya kwamba mamlaka hii inge...angusha kweli hata chini; ikatenda
ilivyopenda, ikafanikiwa.
Danieli 8:12



149

Yohana alitabiri ya kwamba Shetani atajaribu kulazimisha kila mmoja kupokea alama ya mnyama:



150

(Fungu: Ufunuo 13:16,17)
Naye awafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao,




151

tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile,
yaani jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake.
Ufunuo 13:16,17.


152


Ili mamlaka hii itimize unabii huu wote, itajaribu kwa kutumia uwezo wa serikali za kiraia ili kushinikiza alama yake ya mamlaka wakati wa mwisho kwa kila mtu.
Tazama jinsi Mungu anavyoitambua mamlaka hii:



153

(Fungu: Ufunuo 13:18)
Hapa ndipo penye hekima. Yeye aliye na akili, na aihesabu hesabu ya mnyama huyo; maana ni hesabu ya kibinadamu.

# 18 - KUWEKEWA MUHURI MILELE



154

Na hesabu yake ni mia sita, sitini na sita.
(666).
Ufunuo 13:18.


155

Je hesabu ya mnyama ina maana gani, waweza kuhoji. Watu wengi wameuliza swali hilo.


156

Tutaliruhusu kanisa Katoliki lijibu. Kilatini ni lugha rasmi ya Kanisa Katoliki. Papa, katika thiolojia ya Kikatoliki, anasimama badala ya kanisa zima.



157

Mojawapo ya vyeo vya papa inatajwa kuwa Vicarius Filii Dei
Aliye badala ya Mwana wa Mungu



158

Wakatholiki wanashikilia ya kwamba kanisa, ambalo ni jamii ionekanayo dhahiri, lazima iwe na kiongozi aonekanaye dhahiri.



159

Utaona ya kwamba thamani ya kihesabu ya herufi za Kilatini ni rahisi kuifanyia hesabu
Vicarius Filii Dei
Vicarius 5, 1, 100, 0, 0, 1, 5, 0, = 112
Filii 0, 1, 50, 1, 1 = 53
Dei 500, 0, 1 = 501
= 666
Hii ni alama nyingine iliyo wazi kabisa inayotambulisha kanisa la Rumi kuwa ni mamlaka ya mnyama ya Ufunuo 13.

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele


160

Tunaweza kuhitimisha nini kutokana na majifunzo ya unabii katika Neno la Mungu?
Twaweza kuona kwamba wakati unakuja na kwamba hauko mbali, wakati kila mmoja atakapoamrishwa kutunza siku ya kwanza ya juma katika kuhalifu moja kwa moja amri ya Mungu!



161

Maelekezo ya hivi karibuni yaliyopewa kichwa: Barua ya Kitume, Dies Domini, ya Baba Mtakatifu, Yohana Paulo II, kwa Maaskofu, Mapadre, na Waaminifu wa Kanisa, katika kutunza Siku ya Bwana kama Takatifu, imetumwa kwa viongozi wa kanisa likiwaasa kukazia utunzaji wa Jumapili kama wakati wa pumziko na ibada.
Je, yawezekana kwamba hii barua yenye makusudi mema inaweka jukwaa zuri kwa ajili ya kuunga mkono uadhimishaji wa Jumapili badala ya Sabato ya Biblia?


162

Inaendelea kiasi cha kupendekeza washughulike katika mwelekeo wa kupata sheria ya kiserikali ili kuifanya iwe halisi. Je, hilo halionekani ya kuwa si geni?

Kama jinsi tu unabii usemavyo!


163

Swali ambalo wengi waweza kuuliza ni kwamba, Je, kuna yeyote mwenye alama ya mnyama hivi sasa?
La, bado, hakuna hata mtu mmoja mwenye alama ya mnyama sasa.
Mungu anao wafuasi wa kweli katika kila kanisa.

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele



164

Wakati alama ya mnyama itakaposhinikizwa kwa njia ya sheria ya kiserikali, kila mtu hapo itampasa achague kati ya utii kwa Mungu kwa kutunza Sabato kulingana na amri ya Mungu--

au utii kwa mnyama kwa kutunza siku iliyobandikwa na mamlaka ya mwanadamu.
Kisha, tena ni wakati huo, ndipo yeyote awezapo kupokea alama ya mnyama!
Kwa kila roho kutakuwepo na jaribio la muhimu: Je, nitamtii Mungu ama nitamtii mwanadamu?
Siyo tu swala la siku.
Ni swala la mabwana!



165

(Fungu: Warumi 6:16)
Paulo aliandika:Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii,



166

mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti,



167

au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki? Warumi 6:16.



168

Wakati mzito utamkabili kila mkaaji wa Dunia hivi karibuni.
Hakuna atakayekuwa na uwezo wa kununua au kuuza ambaye hana alama ya mnyama.

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele



169

Kinachotangulia ni katazo, kisha  tamko la kifo.
Na kwa wale wapokeao alama ya mnyama, mapigo saba ya mwisho.
Je, waona jinsi swala hili lilivyo muhimu?
Kwa nini ni swala la uzima au mauti?
Kwa nini ni muhimu hivyo kuwa tuchague sasa kumheshimu Mungu?




170

Ipo habari njema kwa wale wanaochagua kumheshimu Mungu na kupokea muhuri wake.





171

(Fungu: Isaya 33:16)
Wanaweza kushindwa kununua au kuuza, lakini Mungu anasema,  ....Atapewa chakula chake; maji yake  hayatakoma.
Isaya 33:16.





172

(Fungu: Zaburi 91:5-8)
Kuhusu mapigo yatakayomwagwa juu ya nchi,
Mungu anaahidi: Hutaogopa  hofu ya usiku,
Wala mshale  urukao mchana,





173

wala tauni  ipitayo gizani,wala uele uharibuo adhuhuri.




174


Ijapo watu elfu waanguka ubavuni pako.
Naam, kumi elfu mkono wako wa kuume!
Hata hivyo hautakukaribia wewe.




175


Ila kwa macho yako utatazama, Na kuyaona malipo ya wasio haki.
Zaburi 91:5-8
Na, kana kwamba bado unashangaa kile kitakachotokea, Biblia yasema,

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele




176

(Fungu: Zaburi 91:9-11)
Kwa sababu umemfanya Aliye juu kuwa makao yako,



177

Mabaya hayatakupata wewe, wala tauni haitaikaribia hema yako.




178

Kwa kuwa atakuagizia malaika zake wakulinde katika njia zako zote.
Zaburi 91:9-11.
Lakini Mungu anatoa ahadi ya ajabu kwa wale wanaochagua kumfuata:



179

(Fungu:Danieli 12:1)
Wakati huo Mikaeli atasimama, jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako;




180

Na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo.



181

Na wakati huo watu wako wataokolewa;
kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile.
Danieli 12:1.
Yohana alionyeshwa njozi ya wale walioupata ushindi juu ya mnyama:



182

(Fungu: Ufunuo 15:2)
Tena nikaona kitu kama mfano wa bahari ya kioo iliyochangamana na moto, na wale wenye kushinda, watokao kwa yule mnyama,

# 18 - Kuwekewa Muhuri Milele



183

na sanamu yake, na  kwa hesabu ya jina lake,



184

walikuwa  wamesimama kando-kando
ya hiyo bahari ya kioo, wenye vinubi vya Mungu. Ufunuo 15:2.
Hata sasa, Mungu anasihi wafuasi wake wa kweli watoke katika mifumo ya kidini bandia na wamfuate kikamilifu.



185

(Fungu: Ufunuo 18:4)
....Tokeni kwake enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake,



186

wala msipokee mapigo yake. Ufunuo 18:4.


187

Kuna gharama katika kuchagua kumfuata Mungu. Je, unakumbuka Waebrania watatu ambao kwa ujasiri, hata katika kuikabili mauti, na wala bila kuchelewa katika kutafuta sababu za kibinadamu, walichukua msimamo wa kumtii Mungu?


188

Mungu kupitia kwa Roho wake Mtakatifu amekuwa akinena nawe kupitia katika mikutano hii. Anafanya mwito wake wa mwisho kwa Dunia inayokufa ili iwe tayari kwa ajili ya Kuja kwa Mara ya Pili kwa Mwanae.
Anakuja kuwachukua nyumbani pamoja naye wale ambao wamechagua kumfuata njia yote. Je, wewe hutachukua uamuzi kama Waebrania watatu kusimama kwa ajili ya Mungu na kweli yake usiku wa leo?

# 19 - Wekezo Usiloweza Kupoteza



1

Jinsi ya Kuwa na Hakika Fedha Yako i Salama


2

Yesu alizungumza sana juu ya fedha.
Kati ya mifano yake 38, kumi na sita ilihusiana na jinsi ya kutumia fedha na mali.
Katika vitabu vya injili vinne vya Mathayo, Marko, Luka, na Yohana, katika namna ya kushangaza ya kila moja kati ya mafungu kumi, au mafungu 288 kwa ujumla, hushughulikia moja kwa moja swala la fedha na au mali.
Yapo takriban mafungu 500 katika Biblia yahusuyo maombi, mengine 500 yahusuyo imani, lakini kiasi cha kutisha cha mafungu 2,000 juu ya fedha na mali.
Fedha lazima liwe ni swala la muhimu sana kwa Mungu.
Hatuhitaji tuwe na fadhaa kuzihusu.
Anatuhitaji tumwamini ya kwamba atatupatia mahitaji yetu.


3

Watu wengi hutumia muda mwingi sana wakifadhaika juu ya matatizo ya fedha - jinsi gani ya kulipia vitu wanavyovitaka na wanavyovihitaji.
Wana fadhaa kuhusu wakati ujao pia.


4

Je, watakuwa na kiasi cha kuwatosha kuishi kwacho wakati wakistaafu?
Kitu gani kitatokea wakiwa wazee sana au wakiwa wagonjwa sana kiasi cha kutoweza kufanya kazi zaidi?
Watu wanatafuta kitu kilicho thabiti au cha kudumu.
Lakini twaweza kupata wapi usalama kwa ajili ya wakati uliopo na wakati ujao?

# 19 - Wekezo Usiloweza Kupoteza


5

Mungu kamwe hakukusudia  ya kwamba wewe na mimi tuwe na fadhaa kuhusu wakati uliopo au wakati ujao.
Kama tukimtegemea hatutahitaji kuwa na wasiwasi juu ya kile kitakachotokea kwetu.



6

(Fungu: Mathayo 6:31,32)
Msisumbuke, basi, mkisema, Tule nini? Au Tunywe nini? Au Tuvae nini?
Au, Tutakunywa nini? Au, Tutavaa nini?



7


.....Kwa  sababu Baba  yenu wa mbinguni anajua ya  kuwa mnahitaji hayo yote.
Mathayo 6:31,32.
Hebu na tuangalie mpango wa Mungu wa usalama kwa ajili yetu.


8


Yote hii ilianzia katika Bustani ya Edeni.


9

Sayari Dunia ilikuwa ndipo tu imetoka katika mikono ya Muumbaji katika uzuri wake wote na ukamilifu, utukutu kuliko maelezo.


10

Urembo wa Msanii Mkuu ulisalimia jicho katika kila mwelekeo.
Kucha kwa jua kuliko kuwa na urembo wa kushangaza kulilandana tu na urembo wa machweo ya jua.


11

Maziwa yenye utulivu yalilala kati ya vilima.

# 19 - Wekezo Usiloweza Kupoteza


12

Maua ya kupendeza ya kila rangi na mizabibu iliyokuwa ikichanua ilifurahisha hisia.


13

Miti ilikuwa ikining'inia kwa kuwa na mzigo wa matunda matamu ya kila aina.


14

Ndege waimbao walilijaza anga kwa nyimbo tamu. Wanyama katika majani mabichi walicheza na kuzurura bila hofu.
Chemchemi na maziwa vilikuwa hai vikiwa na samaki wazuri wenye rangi za kupendeza.
Paradiso ya namna gani tokea ncha moja hadi nyingine!


15

Ni kwa kiasi gani Adamu na Hawa lazima walikuwa wamefurahia dunia iliyokuwa kamilifu Mungu aliyokuwa amewatengenezea.



16

(Fungu: Mwanzo 2:8)
Lakini kulikuwa na zaidi! BWANA Mungu akapanda bustani........, akamweka ndani yake huyo mtu  aliyemfanya.
Mwanzo 2:8.


17

Hebu fikiria! Mahali fulani kati ya maajabu na uzuri wa dunia iliyozaliwa upya, Mungu alisanii  nyumba ya bustani kwa ajili ya Adamu na Hawa.

# 19 - Wekezo Usiloweza Kupoteza


18

Nyumba ya fahari kuliko zote Duniani haiwezi kulinganishwa na nyumba ya kwanza ya dunia iliyokuwa bustani.
Si tu kwamba Mungu aliwapatia nyumba ya kupendeza kwa ajili yao, lakini pia alielezea juu ya chakula cha ajabu alichokuwa amewapatia.



19

(Fungu: Mwanzo 1:29)
.....Tazama, nimewapa kila  mche utoao mbegu,ulio juu ya uso wa  nchi yote pia,




20

na kila mti  ambao matunda yake yana mbegu;  vitakuwa ndivyo  chakula chenu. Mwanzo 1:29.


21

Adamu na Hawa hawakuwa na kodi ya nyumba ya kulipa, wala hawakuwa na kodi ya kuwatia wasiwasi, wala hawakuwa na kufuli au funguo, hawakuwa na majambazi wala wezi, wala hospitali au maduka ya madawa.


22

Walifurahia afya kamili na ujana usioisha, kujitoa kikamilifu kila mmoja kwa mwingine, na upendo mkamilifu kwa Mungu.
Mungu alitaka washiriki mibaraka hii, hivyo akasema,



23

(Fungu: Mwanzo 1:28)
...Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi na kuitiisha... Mwanzo 1:28.



24

Sisi tu Mawakili wa Mali ya Mungu

# 19 - Wekezo Usiloweza Kupoteza



25

Ilikuwa ni mpango wa Mungu ya kwamba familia moja iliyo kubwa, yenye furaha na afya iishi katika Sayari Dunia/
Mungu alijua pia ya kwamba mwanadamu angepaswa kuwa na kazi ya kufanya, majukumu ambayo angefurahia kuyakamilisha.




26

(Fungu: Mwanzo 1:28)
Hivyo alimwambia Adamu na Hawa: ...Mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani,



27

na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi.



28

(Fungu: Mwanzo 2:15)
BWANA Mungu akamtwaa huyo mtu, akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na
kuitunza.
Mwanzo 1:28; 2:15.


29

Wakati kila kitu duniani ni mali ya Mungu,
Alimkabidhi mwanadamu uwakili wa dunia.
Mungu ndiye Mwenye, sisi ni mawakili, tunatunza mali ya Mungu.



30

(Fungu: Zaburi 24:1)
Biblia yasema, Nchi na vyote viijazavyo
ni mali ya BWANA, Dunia na wote wakaao ndani yake.
Zaburi 24:1.



31

(Fungu: Zaburi 50:10,11)
Na tena, Mungu anasema,Maana kila hayawani ni wangu, na makundi juu ya milima
elfu.

# 19 - Wekezo Usiloweza Kupoteza



32

Nawajua ndege wote wa milima,
na wanyama wote wa mashamba ni wangu.
Zaburi 50:10,11


33

Ni Mungu atupatiaye uwezo wa kupata fedha. Kwa kweli hatuna chochote kilicho mali yetu!
Kama Muumbaji wetu, Mungu analodai la mali yetu na maisha yetu.



34

(Fungu: Kumbukumbu la Torati 8:18)
Bali utamkumbuka BWANA Mungu wako, maana ndiye akupaye nguvu za kupata utajiri;




35

ili alifanye imara agano lake alilowapa
baba zako, kama hivi leo.
Kumbukumbu 8:18.




36

Kamusi ya "Webster's New World" inaeleza neno wakili kama Mtu atendaye kama msimamizi wa fedha na mali kwa ajili ya mwingine.
Leo mtu aingiapo katika uhusiano wa uwakili, anataka kujua mwenye mali anatarajia nini toka kwake.
Haya ndiyo maelewano ambayo Mungu alikuwa nayo na Adamu, kwani Biblia yasema,



37


(Fungu: Mwanzo 2:16,17)
........Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula;



38

Walakini mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile,

# 19 - WEKEZO USILOWEZA KUPOTEZA



39

kwa maana  siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa  hakika.
Mwanzo 2:16,17.



40

Mungu aliujaribu upendo wa mwanadamu na utii wake. Adamu na Hawa wangeweza kula toka katika miti mingine yote katika bustani, lakini hawakupaswa kula tunda toka kwa ule mti pekee. Kwa kumtii Mungu, wangeonyesha utambuzi wa Mwenye mali ambaye ni Yeye (Mungu).
Kama wangelikuwa mawakili waaminifu na kama wangelichagua kudumisha utii wao kwa Mungu, wangeliishi milele katika dunia iliyokuwa paradiso!
Adamu na Hawa walishindwa jaribu moja rahisi Mungu alilolihitaji toka kwao.
Walishindwa kuwa mawakili waaminifu, na walikuwa wamepoteza  kila kitu: nyumba yao ya bustani, kutokufa, upendo, furaha, usalama, dhamiri safi, na kutembea na kuzungumza uso kwa uso na Mungu!


41

Walianguka kutoka katika ufalme hadi utumwani.
Na nyuma ya yote hayo aliyekuwa na ridhaa ya ndani kabisa alikuwa Shetani, malaika muasi aliyetegemea kutawala dunia kikamilifu milele.


42

Hata hivyo, utawala wa Shetani ulivunjwa na kuingia kwa Kristo katika dunia karne kadhaa baadaye.


43

Mpango wa Shetani ulikuwa kumdanganya Mwana wa Mungu wa Mbinguni kwa urahisi kama alivyomdanganya  Adamu na Hawa.
Shetani alisubiri hadi Yesu alipokuwa amefunga kwa siku arobaini.

# 19 - Wekezo Usiloweza Kupoteza



44

(Fungu: Mathayo 4:8,9)
Kisha akamchukua hadi katika mlima mrefu mno, akamwonyesha falme zote za ulimwengu na fahari zake,



45

akamwonyesha milki zote za ulimwengu.....



46

Kisha akamwambia, Haya yote nitakupa, ukianguka kunisujudia. Mathayo 4:8,9.


47

Shetani alitegemea kumshawishi Yesu kwa kutumia falme za dunia hii, lakini hakufanikiwa. Vitu ambavyo Shetani aliahidi kumpatia Kristo havikuwa vyake na wala asingekuwa yeye avitoe!
Alikuwa ameiiba sayari kwa hila na udanganyifu. Na Yesu asingeweza kuuza uhusiano wake na Baba yake kwa ajili ya dunia nzima ya utajiri na iliyong'aa.


48

Hatimaye, hatima ya Shetani ilitiwa muhuri milele pale Kalvari.
Kwa mauti ya Kristo katika msalaba, Shetani alishindwa! Mauti ya Kristo ilifanya iwezekane kwa Sayari Dunia kufanywa upya tena.


49


Kila jinsi tulivyo na kila kitu tulicho nacho kimewezekana kwa sababu ya karama ya milele ya Kristo kwa familia ya mwanadamu.
Tumpende tusimpende, maisha yetu na vyote tulivyonavyo ni mali yake.



50

Yeye si tu Muumbaji wetu, Yeye ni Mkombozi wetu! Na kama Adamu na Hawa, sisi tu mawakili wa kile Mungu akiwekacho kwetu. Hivyo anahitaji nini kwetu?

# 19 - WEKEZO USILOWEZA KUPOTEZA



51

(Fungu: 1 Wakorintho 4:2)
Hapo tena inayohitajiwa katika mawakili, ndiyo mtu aonekane kuwa mwaminifu.
1 Wakorintho 4:2



52

Sisi tu mawakili wa karama ya Mungu ya Uhai
Karama iliyo kuu kuliko zote katika karama za Mungu ni Uhai wenyewe.
Mtume Paulo anatamka:



53

(Fungu: Matendo 17:24,25)
Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo....




54

......ndiye anayewapa wote uzima na pumzi na vitu vyote.
Matendo 17:24,25.


55

Uhai wetu unaanzia kwa Mungu, naye ndiye anayeutunza. Kila pigo la moyo, kila pumzi ya hewa, kila pigo la mshipa wa damu katika miili yetu ni karama toka kwa Mungu.



56

(Fungu: Warumi 12:1)
Paulo aliandika:Basi, ndugu zangu, nawasihi kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai,



57

takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana.
Warumi 12:1.
Kafara iliyo hai humaanisha kujitoa bila kubakiza chochote, au kujikabidhi kwa Kristo na uongozi wake katika maisha yetu.

# 19 - Wekezo Usiloweza Kupoteza



58

(Fungu: Matendo 10:38)
Kristo alizunguka huko na huko, akitenda kazi njema.. Matendo 10:38


59

Yeye ni kielelezo chetu; sisi tunapaswa kufuata kielelezo chake  cha huduma  isiyo na ubinafsi.



60

Sisi tu mawakili wa Wakati ambao Mungu natupatia
Sisi siyo tu mawakili wa fedha, lakini sisi tu mawakili wa wakati pia.
Mmoja aliwahi kusema ya kwamba muda ni kitu ambacho uhai umetengenezwa nacho.
Mtunga Zaburi alimuomba Mungu,



61

(Fungu: Zaburi 90:12)
Basi utujulishe kuzihesabu siku zetu, tujipatie moyo wa  hekima.
Zaburi 90:12.



62

Kupoteza wakati ni kupoteza maisha (uhai) --kuifuja ile talanta ambayo Mungu Mwenyewe ameitoa kwa kila mwanamume na mwanamke.
Kila mtu anayo idadi ile ile ya masaa kwa siku, idadi ile ile ya dakika katika masaa yale,
na atawajibika kwa chaguzi zilizofanyika kuyajaza.




63

Mungu anatutegemea ya kwamba tutatumia wakati kwa hekima katika ujumla wake. Anatutegemea pia tuweke pembeni wakati maalum, kipindi maalum - Sabato, siku ya saba ya juma, kama namna ya kudhihirisha imani yetu kwake kama Muumbaji wetu.

# 19 - Wekezo Usiloweza Kupoteza




64

Wakati muda wetu wote ni mali ya Mungu, Anatuomba ya kwamba Sabato ya siku ya saba iwekwe wakfu kwa ajili ya ushirika pamoja naye, tukitulia katika Neno lake na tukipata burudani kutoka katika ahadi zake.
Anatualika tuweke pembeni shinikizo la kazi za juma, kununua au kuuza na shughuli za kidunia, na kumkumbuka Yeye kama Muumbaji wetu na Mkombozi.



65

Sisi tu Mawakili wa Talanta Mungu anazotupatia. Naam, unahoji, Ni talanta zipi hasa ambazo tunawajibika kwazo kama mawakili wa Mungu? Sidhani ya kwamba ninazo talanta zozote.


66

Leo, talanta duniani humaanisha uwezo wa kuimba vizuri, kupiga chombo cha muziki, kuchora picha, kushona vazi, kuandika, au kupanga mambo.



67

Hizi ni talanta kwa kweli, lakini talanta ambazo Mungu alimaanisha haziishii katika hizi.
Kama mawakili wa Mungu, tunawajibika kwa kila kitu anachotupatia, ukiwemo uhai, wakati, uwezo, na mali.
Siku moja Mungu atatuuliza tuchague kuridhisha nia zetu na anasa au tubariki wengine!
Yesu alisema, Nifuate.
Aliishi maisha yasiyo ya kibinafsi.



68

(Fungu: Matendo 10:38)
Biblia yasema ya kuwa Yesu ndiye aliye...zunguka huko na huko, akitenda kazi njema.... Matendo 10:38. Wengi wetu tunaridhika tu kwa kwenda huko na huko.


69


Talanta zetu si za kutumia tu ili kupata sifa toka kwa watu au kupata tu ijara njema toka kwa Mungu. Tumeazimwa tu ili kuwabariki wengine.

# 19 - Wekezo Usiloweza Kupoteza



70

(Fungu: 1 Wakorintho 4:7)
Paulo aliandika: ....Nawe una nini usichokipokea?




71

Lakini iwapo ulipokea, wajisifia nini kana kwamba hukupokea?
1 Wakorintho 4:7.



72

Sisi tu Mawakili wa Fedha Mungu Anayotupatia



73

(Fungu: Mathayo 6:33)
Kama tukiutafuta ....kwanza ufalme wake, na haki yake
(Mathayo 6:33), tunagundua mibaraka ya Mungu inamiminwa juu yetu.



74

Na zaidi ya kutoa wakati wetu, tunapata katika Maandiko ya kwamba kujitoa kwa Mungu kunahusisha pia kumrudishia Yeye sehemu ya mibaraka ya mali halisi aliyotupatia.



75

Siku moja mpwa wa Ibrahimu; Lutu na familia yake walichukuliwa mateka na kabila adui toka nyumbani mwao Sodoma.
Wakati habari ilipomfikia Ibrahimu, alinuia kumuokoa Lutu pamoja na wengine. Alimuomba Mungu awe pamoja naye na ampatie mafanikio. Mungu alikuwa pamoja naye.
Lutu na familia yake waliokolewa pamoja na hazina za adui zikaletwa nyumbani.

# 19 - Wekezo Usiloweza Kupoteza



76

Wakati Ibrahimu alipokaribia Sodoma, mfalme alikuja kumpokea, akimsihi atunze kwa ajili yake mwenyewe hazina alizokuwa amezipata, arejeshe tu mateka.
Ibrahimu alikataa kuchukua chochote kwa ajili yake mwenyewe.
Melkizedeki, kuhani wa Mungu, akamletea Ibrahimu chakula na kumbariki.




77

(Fungu: Mwanzo 14:20)
Kisha Ibrahimu ....akampa fungu la kumi la vitu vyote.
Mwanzo 14:20.


78

Ibrahimu alitaka kuonyesha shukurani zake kwa msaada wa Mungu katika kufanikisha kuwaweka huru Lutu na wengine, akimtambua Mungu kama mwenye mali na mibaraka yake.


79

Miaka mia moja na ishirini baadaye, mjukuu wa Ibrahimu alionyesha shukrani yake kwa Mungu kwa njia iyo hiyo.
Wakati akimkimbia ndugu yake aliyekuwa na ghadhabu, Yakobo alijihisi mpweke hakika na tena mwenye hofu.
Kwa shauku kuu alitaka ulinzi wa Mungu, lakini alijihisi  mwenye hatia kwa kumnyang'anya ndugu yake,  Esau,  kiasi cha kuhofu ya kwamba Mungu alikuwa amemuacha na asingemsamehe.


80

Huku akiwa na hisia ya majuto makuu, Yakobo alikiri makosa yake kwa Mungu na kisha kwa uchovu akalala chini katika nchi na kupata usingizi.



81

(Fungu: Mwanzo 28:12,22)
Akaota ndoto; na tazama, ngazi imesimamishwa juu ya nchi, na ncha yake yafika hata mbinguni;

# 19 - Wekezo Usiloweza Kupoteza



82

Tena, tazama, malaika wa Mungu wanapanda, na kushuka juu yake.



83

Hali akiwa ameguswa kwa ndani kabisa, aliahidi kwa shukrani, ....Na katika kila utakalonipa hakika nitakutolea wewe sehemu ya kumi.
Fungu la 22.


84

Mfalme Daudi alijihisi vivyo hivyo alipoomba,



85

(Fungu: Zaburi 116:12)
Nimrudishie BWANA nini kwa ukarimu wake wote alionitendea? Zaburi 116:12.
Je, umepata kujiuliza ni jinsi gani umshukuru Mungu kwa sababu ya wema wake wa ajabu kwako -- kwa sababu ya karama ya uhai, familia, afya, mibaraka ya mali?
Je, wakati mwingine unajihoji kama ahsante inatosha?
Kanuni ya Biblia ya uwakili inatoa njia dhahiri ya kudhihirisha shukrani yetu kwa Mungu kwa Faida zote hizo.


86

Yakobo alisema angemrudishia Mungu sehemu ya kumi, au zaka, ya yote ambayo alikuwa apokee, kama jinsi babu yake, Ibrahimu alivyotenda.


87

Maelekezo ya kwanza kabisa kuandikwa yahusuyo zaka, au kurejesha sehemu ya kumi kwa Bwana, yanaonekana katika Kitabu cha Mambo ya Walawi.

# 19 - Wekezo Usiloweza Kupoteza



88

(Fungu: Mambo ya Walawi 27:30)
Tena zaka yote ya nchi, kama ni mbegu ya nchi, au kama ni matunda ya nchi, ni ya BWANA.



89

ni takatifu kwa BWANA.
Mambo ya Walawi 27:30.


90

Tunaporejesha zaka ya BWANA tunaendelea kwa kudumu kusimika ukweli ya kwamba Mungu ni Muumbaji na Chanzo cha kila mbaraka.
Na zaka inapaswa itumiweje?



91

(Fungu: Hesabu 18:21)
Kitabu cha Hesabu kinatoa maelezo yaliyo wazi: Na wana wa Lawi (watumishi katika huduma ya Mungu), nimewapa zaka yote katika Israeli kuwa urithi wao, badala ya huo utumishi wautumikao,



92

ni huo utumishi wa hema ya kukutania.
Hesabu 18:21.



93

Katika Biblia yote, tunaona ya kuwa zaka daima iliunga mkono kazi ya Mungu.



94

(Fungu: 1 Wakorintho 9:13,14)
Katika Agano Jipya, Paulo anaelezea, Hamjui ya kuwa wale wazifanyao kazi za hekaluni hula katika vitu vya hekalu,



95

na wale waihudumiayo madhabahu huwa na fungu lao katika vitu vya madhabahu?

# 19 - WEKEZO USILOWEZA KUPOTEZA



96

Na Bwana vivyo hivyo ameamuru kwamba wale waihubirio Injili wapate riziki kwa hiyo Injili.
1 Wakorintho 9:13,14.


97

Kristo alisifu mpango wa zaka na wakati uo huo aliwakemea waandishi na Mafarisayo kwa kuwa na mawazo mafupi kuhusu dini:




98

(Fungu: Mathayo 23:23)
...Kwa kuwa mnalipa zaka za mnaanaa na bizari na jira, lakini mmeacha mambo makuu ya sheria,



99

yaani, adili, na rehema, na imani; hayo imewapasa kuyafanya, wala yale mengine msiyaache.
Mathayo 23:23.


100

Pengine umekuwa ukijiuliza ni jinsi gani ungeweza kutoa sehemu ya kumi ya mapato yako kwa Bwana. Watu wengi wamejiuliza juu ya hilo!
Lakini tena kwa namna fulani walifanya uamuzi wa kutegemea uongozi na hekima ya Mungu na kurudisha zaka kwake.


101

Majuma kadhaa baadaye, watu hawa hawa kwa msisimko walishuhudia muujiza uliotokea katika maisha yao! Kwa namna fulani, tisa ya kumi ya mapato yao iliongezeka zaidi ya kumi ya kumi ilivyowahi kutokea kabla!
Hapa ndipo ilipo siri ya usalama wa kifedha!


102

Baadhi ya watu huuliza, Je, zaka siyo ya Wayahudi tu?
Kwa hao tunauliza, Je, mibaraka ya mbingni ni kwa ajili ya Wayahudi peke yao?

# 19 - Wekezo Usiloweza Kupoteza


103

Kulikuwa na Jim ambaye aliitoa kwa shida zaka kwa uaminifu toka katika hundi ipatikanayo kwa shida. Ilionekana vigumu mwanzoni, lakini baadaye alibarikiwa kwa biashara yake ambayo ilifanikiwa na kuleta usalama wa kifedha.


104

Sasa anampatia Mungu sifa kwa mafanikio yake ya kifedha na anapenda kutoa ili kuendeleza kazi ya Bwana.



105

Au mchukue Ed, kama mfano, ambaye alichukua hatua ya imani kwa kufunga biashara yake siku ya Sabato -- siku iliyo  na shughuli na mafanikio nyingi kuliko zote katika msimu -- anaishia kuzawadiwa kwa biashara iliyokua zaidi katika siku zingine sita za juma! Mungu ni mtunzaji wa ahadi!




106

Wakristo wa namna hiyo wamegundua kama hatua ya kwanza  mibaraka  iliyoahidiwa katika Malaki:



107

(Fungu: Malaki 3:10)
Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo,



108

asema BWANA wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni,



109

na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la.
Malaki 3:10.

# 19 - Wekezo Usiloweza Kupoteza



110

Bwana asema ya kwamba kumi ya kila kitu ni takatifu kwake.
Anatupatia sisi wasaa wa upendeleo wa kumrudishia Yeye ili apate kujaribu uwakili wetu, kuona kama tutaheshimu na kumtambua yeye kama Mwenye.



111

Kama tukikataa kutenda hivyo, kwa hakika tunamnyang'anya Mungu, kulingana na Biblia.



112

(Fungu: Malaki 3:8)
...Lakini ninyi mwasema, 'Tumekuibia kwa namna gani?' Mmeniibia zaka na dhabihu.
Malaki 3:8.


113

Wakati zaka, au moja ya kumi ya mapato yetu, ni mali ya Mungu, tunaalikwa kutoa kwa wingi, hata zaidi ya sehemu ambayo tayari ni moja kwa moja haki ya Mungu.

Pamoja na sadaka, hili linaachwa kuwa juu ya kila mmoja wetu kuamua kiasi gani ukarimu wetu unaweza kuwa.



114

(Fungu: Luka 6:38)
Hata hivyo, ipo baadhi ya miongozo katika Biblia. Yesu alisema, Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwa-sukwa hata kumwagika,....Luka 6:38.


115

Mpango wa Mungu wa kuendesha kazi yake hapa duniani kifedha, ni mrahisi na mzuri. Anaomba watu Wake kutoa toka mioyoni mwao, bila ya kuhofu mahitaji yao wenyewe, ambayo hatimaye yatakidhiwa kwa hali ya juu mbali kuliko matarajio yao.

# 19 - Wekezo Usiloweza Kupoteza



116

Pengine unafikiria, kama Mungu ni mwenye kila kitu, dhahabu, fedha, ng'ombe, ardhi na sisi, kwa nini anahitaji fedha yangu?
Mpango wa zaka ni mpango wa Mungu kwa ajili ya kuendeleza kazi  yake hapa Duniani.



117

Kamwe hakukusudia  ya kwamba kanisa liungwe mkono kifedha kutokana na bahati nasibu, michezo ya bingo, au nasibu ya namna yoyote!
Na je, si zaka ni namna ifaayo kwa ajili ya kuunga mkono huduma kifedha?



118

Kila mtu hutoa kulingana na jinsi apokeavyo.



119

Kama ukiwa na Shilingi elfu moja



120

unarudisha shilingi  mia moja kwa Mungu.



121

Kama ulipata mia moja,



122

unarudisha  shilingi kumi. Je, kuna mpango ambao ungekuwa wenye adili zaidi kuliko huo?

# 19 - Wekezo Usiloweza Kupoteza


123

Chochote tunachompatia Mungu, Yeye anatupatia zaidi. Daima tunapokea zaidi ya tunavyotoa. Tunaporejesha zaka kwa Mungu, tunaeleza shukurani yetu kwa kile alichotutendea, na tunapunguza hali ya kujijali nafsi na uchoyo.


124

Tunajihusisha zaidi na wengine. Na tunapoendelea kushiriki mibaraka yetu nao, tunakuwa katika upendo na huruma, huku tukiwa zaidi na zaidi kama Yesu.
Huo ni mpango wa Mungu kwa ukuaji wetu katika Kristo. Yesu alieleza visa vya ajabu ili kueleleza mafundisho yake.


125

Hapa ni moja ya vile vya kuvutia zaidi: mkulima shujaa mwenye bidii alifanya kazi sana na akawa na mazao ya kushangaza wakati wa mavuno.
Mavuno yalikuwa mengi sana kiasi ambacho ghala zake hazikuweza kuyahifadhi.
Zilikuwa tayari zinavunjika na mazao hayakuwa yameletwa ghalani yote bado.
Angelifanya nini? Hili lilikuwa swala lililomtia mashaka. Alikuwa akipambana katika kufanya uamuzi.
Je, atoe vilivyozidi kwa maskini?
Lakini vilikuwa mali yake.


126

Je, si yeye aliyepanga kwa uangalifu na kutumia hekima yake na utaalamu wa kilimo ili kufanya hili shamba kuwa la mafanikio kuliko yote katika bonde?
Akajishauri mwenyewe juu ya jambo la kutenda:



127

(Fungu:Luka 12:18 - 21)
...Nitafanya hivi: nitazivunja ghala zangu, nijenge nyingine kubwa zaidi, na humo nitaweka nafaka yangu yote na vitu vyangu.

# 19 - Wekezo Usiloweza Kupoteza



128

Kisha, nitajiambia, Ee nafsi yangu, una vitu vyema vingi ulivyojiwekea akiba kwa miaka mingi; pumzika basi, ule, unywe, ufurahi.
Luka 12:18,19.



129

Lakini Mungu akamwambia, 'Mpumbavu wewe, usiku wa leo wanataka roho
yako!



130

na vitu ulivyojiwekea tayari vitakuwa vya nani?'



131

Ndivyo alivyo mtu ajiwekeaye nafsi yake
akiba, asijitajirishe kwa Mungu.
Luka 12:20,21.


132

Mkulima tajiri hakutambua wapi mibaraka yake ilitokea.
Hakumtambua Muumbaji wake au wajibu wake kuwa wakili.
Aliwasahau kabisa maskini, yatima, wajane au wasio na makwao.
Alijifikiria yeye mwenyewe tu.
Mtu huyu alikuwa na tatizo la moyo.



133

(Fungu: Mathayo 6:21)
Yesu alisema, Kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako.
Mathayo 6:21.
Yesu alikuwa makini sana juu ya mtizamo wetu katika mali zetu, kwani kama havikutolewa kwa Yesu, vyaweza kutupeleka mbali na Mungu, na hata kuleta matokeo ya kupoteza uzima wa milele.

# 19 - Wekezo Usiloweza Kupoteza



134

(Fungu: Mathayo 16:26)
Alisema, Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake?.... Mathayo 16:26


135

Tatizo ambalo lipo na mwanadamu wa kisasa ni kwamba maisha yake yamekuwa na mambo mengi sana na ratiba yake imebana kiasi ambacho husahau au hapati wakati wa kukumbuka wapi mibaraka yake yote hii inatokea.



136

Anashindwa kukumbuka gharama ambayo ililipwa ili kumbkomboa toka katika dhambi.
Matokeo yake, hudharau swala la kumheshimu Mungu na muda wake, talanta, na hazina yake.
Kila mmoja wetu anahitaji kukumbushwa kila siku ya kwamba --



137

Vitu tuvipendavyo na kuvikumbatia kwa nguvu katika mioyo yetu



138

Vimeazimwa tu; si vyetu kabisa.



139

Yesu anaturuhusu tu tuvitumie ili kuangaza maisha yetu,



140

Hivyo tukumbushe, tukumbushe, mpendwa Bwana,
- Imenukuliwa toka kwa Dottie Rambo, Nikumbushe, Mpendwa Bwana

# 19 - Wekezo Usiloweza Kupoteza


141

Kila kitu tulichonacho ni karama toka kwa Mungu.
Maisha yetu ni karama toka kwa Mungu.
Afya yetu ni karama toka kwa Mungu.
Kila pumzi tuivutayo ni karama toka kwa Mungu.
Chakula tunachokula, mavazi tunayoyavaa, nyumba tunayoishi ndani yake ni karama zitokazo kwa Mungu.
Tunapomrudishia Mungu, tunasema, Ahsante, Bwana, kwa kile ulichonipatia.
Je, ungependa kusema, Bwana, ninataka nikuweke wa kwanza katika fedha zanguna katika kila eneo la maisha yangu?
Kama unapenda, je, waweza kunyosha mkono wako tunapoomba?

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli





1

Twaweza Kuipata Wapi Leo?



2

Kisa kinaelezwa cha kijana mmoja katika Uyunani ya kale aliyetaka kutafuta kweli.
Alimkabili mzee mmoja aliyefikirika kuwa mwenye hekima zaidi ya wote katika jiji.
Kijana huyu akamuuliza huyu mzee, Mzee Hekima e, niambie tafadhali, 'Nawezaje kuipata kweli?Je, waweza kuniongoza hadi ilipo?'
Mzee mwenye hekima akasimama akaanza kutembea. Kijana akafuata. Walitembea wakapita mitaa ya jiji na kufikia kwenye pwani ya bahari.
Huyu mzee akazidi kutembea kuingia kwenye maji. Walipofikia kina cha maji kwenye kiuno, huyu mzee akamwambia kijana aweke mikono yake kichwani pake mwenyewe. Huyu mzee akamtumbukiza kijana ndani ya maji.
Mara tatu kijana alitokeza huku akipambana kwa ajili ya kupata hewa. Mara tatu huyu mzee mwenye hekima alikisukuma kichwa cha kijana majini tena. Mara ya tatu, kijana alipiga yowe, Nilichohitaji tu ni kuupata ukweli! Mzee mwenye hekima akajibu, Kama ukiitamani kweli kama jinsi ulivyoitaka pumzi hii ya uhai, utaipata.
Mungu hazuii ukweli usitufikie. Nabii Yeremia anasema,




3

(Fungu: Yeremia 29:13)
Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote. Yeremia 29:13
Lakini baadhi ya watu wanatafuta katika sehemu zote zisizo sahihi.

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli


4

Imetajwa hii ya kwamba kila mmoja wetu huzaliwa na Ombwe lililotengenezwa kwa ajili ya Mungu ndani yetu.
Inaonekana tunazaliwa, na tamaa ya isiyoelezeka ya kitu fulani ambacho hatuna.
Kwa namna fulani katika akili zetu katika hali isiyotambulika vizuri, tunaelekea kutafuta kitu ambacho hatuwezi kukieleza -- lakini kitu ambacho tunakijua ya kwamba tunakitaka na kukihitaji!


5

Hivyo katika hali ya kujikinai na uchovu, tunatafuta kujaza utupu katika maisha yetu kwa fahari au sifa, bahati, madawa ya kulevya, vileo, mali na shughuli za starehe, na pamoja na yote haya tunaishia kugundua hata tukiwa tumeshinda na kupata tuzo hatuna ridhaa inayodumu.



6

Na sasa hivi au baadaye, uwezekano ni kwamba katika usiku wa upweke na kukosa usingizi, swali linalotusumbua la nabii wa kale linaleta mwangwi wake tokea zamani:



7

(Fungu: Isaya 55:2)
Kwani kutoa fedha kwa kitu
ambacho si chakula? Na mapato yenu kwa kitu kisichoshibisha?......... Isaya 55:2.
Yesu alielewa ridhaa ya kitambo tu ya kuwa na vitu.



8

(Fungu: Luka 12:15)
Alisema, .......uzima wa mtu haumo katika wingi wa vitu vyake alivyo navyo.
Luka 12:15.


9

Watu leo wanahisi hitaji la uwezo ulio mkubwa kuzidi wao wenyewe.
Hili si jipya hata kidogo.

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli


10

Tangu mwanadamu alipochagua kufuata njia yake katika Bustani ya Edeni, amekuwa na huu utupu usio wa kawaida ambao Mungu mwenyewe aweza kuujaza.


11

Mungu aliwaruhusu wana wa Israeli katika kutanga kwao jangwani wawe na njaa ili wapate kutambua hitaji lao la kuwa naye.
Mungu alinena na Wana wa Israeli kupitia kwa Musa, akisema,



12

(Fungu: Kumbukumbu la Torati 8:3)
Akakutweza, akakuacha uone njaa,




13

.....apate kukujulisha ya  kuwa mwanadamu haishi kwa mkate tu;



14

bali huishi kwa kila litokalo katika kinywa cha BWANA.
Kumbukumbu la Torati 8:3


15

Ni wazi Mungu huturuhusu tuhisi njaa ya ndani na kuchoka, ili tumfikie na tumruhusu Mungu aridhishe tamaa zetu.



16

Leo, tunaona tamaa kubwa katika namna mbalimbali za dini.
Pamoja na msisitizo mkubwa leo katika swala la muungano wa dini na msukumo wa kuvunja kuta za kimadhehebu, kuna majifunzo mengi zaidi na mawazo yahusuyo aina mbalimbali za dini na  za kanisa.

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli


17

Makanisa mapya yanaibuka kwa kasi zaidi katika dunia.
Kila moja linadai kuwa watu wa pekee wa Mungu likiwa na ujumbe wa kweli kwa ajili ya kila mtu duniani.
Bado hayo madai yanapotafakariwa itahakikishwa wazi ya kwamba  si madai yote yawezayo kuwa ya kweli.



18

Kila moja linadai kuwa Biblia ndiyo msingi wa imani yao, lakini mafundisho yao ni ya tofauti sana.


19

Yawezekanaje watu waaminifu kuchambua madai yote haya ya dini hizi na kujua kwa hakika kwamba kweli  ni  nini.
Je, Mungu kweli analo kundi la pekee katika Ukristo analolitambua kama kanisa lake leo?
Ni wazi hivyo, kwani Paulo aliandika:



20

(Fungu: Waefeso 4:4)
Mwili mmoja, na Roho mmoja,  kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu.



21

Bwana mmoja,  imani moja, ubatizo mmoja.



22

Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote.....
Waefeso 4:4-6

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli



23

(Fungu: 1 Timotheo 3:15)
Paulo aliandika kwa rafiki yake kijana, Timotheo, na kusema, ....upate kujua jinsi iwapasavyo watu kuenenda katika nyumba ya Mungu,



24

iliyo kanisa la Mungu  aliye hai, nguzo na msingi wa kweli.
1 Timotheo 3:15.
Paulo anataja wazi ya kwamba kanisa la Mungu leo ni nguzo na msingi wa kweli, lakini je, tunawezaje kugundua kanisa lipi linao ukweli.


25

Yapo madhehebu mengi sana, mapambano mengi sana,  kuchanganyikiwa kwingi sana katika jumuiya ya kidini.



26

Marafiki, kulingana na maandiko, Yesu kamwe hakukusudia ya kwamba kuwepo kuchanganyikiwa kwokwote, na ni wazi pia hakukusudia kuwepo madhehebu yote haya.
Kabla tu ya kusulubishwa, Yesu alisali:



27

(Fungu: Yohana 17:21)
Wote wawe na umoja,  kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako;



28

hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma.
Yohana 17:21.
Yesu alitaka ulimwengu uweze kutambua wafuasi wake kwa njia ya umoja wao na upendo.
Kristo hakutaka migawanyiko ya namna yoyote ndani  ya kanisa lake.

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli



29

(Fungu: 1 Wakorintho 12:25)
Kwa kweli, Paulo aliandika ya kwamba kusiwe na faraka (mgawanyiko) katika mwili.
1 Wakorintho 12:25.


30

Lakini Paulo alisema ya kwamba uasi ungekuja, na pamoja na huo, mgawanyiko!



31

(Fungu: Matendo 20:28 - 30)
Tunasoma:  Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo.........mpate kulilisha kanisa lake Mungu....



32

Najua mimi ya kuwa
baada ya kuondoka kwangu  mbwa mwitu wakali wataingia kwenu, wasilihurumie kundi.



33

Tena katika ninyi wenyewe
watainuka watu wakisema mapotovu,



34

wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao.
Matendo 20:28-30.


35

Tunapofungua kurasa za historia ya kanisa, tunagundua hili ndilo hakika lililotokea.
Waalimu wa uongo waliinuka, na baadhi wakapokea makosa yao na kuliacha kanisa.
Wengine wakachanganyikiwa. Wanafunzi wakavutwa mbali, na kukawa na kuanguka pole pole toka katika mafundisho ya Yesu.
Lakini hata kupitia katika yote hayo, bado Mungu amekuwa na kanisa lililosalia kuwa aminifu.

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli


36

Lakini baadhi ya watu husema, Yaweza kuchukua muda wa maisha yote kujifunza mafundisho ya kila dini ili kupata kuwa ni lipi ni kanisa la kweli la Mungu.
Lakini ipo njia rahisi.
Njia ya Mungu!


37


Mamlaka za kiserikali hutuambia ya kwamba ni rahisi sana kutofautisha kati ya noti ya fedha ya kweli na ile ya bandia. Unaona, wao hujifunza tabia ya ile note ya kweli kwa undani.


38


Wanajua wembamba na mpangilio wa vijinyuzi vidogo sana vitengenzavyo karatasi, wepesi au uzito wa rangi au wino, nembo na utaratibu halali wa nambari za fedha iliyo halisi na ya kweli. (elezea fedha)
Wanapoitizama noti, wanalinganisha upesi na zile sifa zitambulishazo fedha iliyo halali. Kama inapungukiwa sifa yoyote katika zile zilizo katika iliyo halali, basi inakuwa bandia.


39

Vivyo hivyo na kweli.


40

Hatuhitaji kujifunza mafundisho ya madhehebu yote kwa muda mrefu, kama tunajua tabia za kanisa la kweli la Mungu kama zilivyotajwa katika Biblia. Mungu hamuachi mwanadamu akisie kuwa ni ipi dini ya kufuata, kwani Mungu ametupatia kweli katika Neno lake:



41

(Fungu: Amosi 3:7)
Hakika Bwana  MUNGU
hatafanya  neno lolote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii  siri yake.
Amosi 3:7.

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli



42

Kitabu cha Ufunuo ni muhtasari wa unabii wote katika Biblia. Kinawapatia watu mtizamo wa pekee wa siku ya mwisho.
Hapa mchafuko wa uasi na dini uliopo katika siku za mwisho za historia ya Dunia unafunuliwa.
Ufunuo unatabiri juu ya pambano kati ya kanisa la Kristo na Shetani.
Sura ya 12 inatoa picha kama filamu ya historia ya kanisa tangu wakati wa Kristo hadi mwisho wa dunia:



43

(Fungu: Ufunuo 12:1,2)
Na ishara kuu ilionekana mbinguni; mwanamke aliyevikwa jua,




44

na mwezi ulikuwa chini ya miguu yake, na juu ya kichwa chake taji ya nyota kumi na mbili.



45

Naye alikuwa ana mimba, akilia, hali ana utungu na kuumwa katika kuzaa.
Ufunuo 12:1,2.


46

Hapa Mungu anaonyesha picha ya mwanamke aliye vaa mavazi meupe, aliyevishwa jua, akiwa amesimama katika mwezi hali amevaa taji yenye nyota 12 katika kichwa chake.
Je, hii ina maana gani?
Katika unabii wa Biblia, mwanamke safi anawakilisha watu wa Mungu -- kanisa lake.
Nabii Yeremia aliandika:

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli



47

(Fungu: Yeremia 6:2)
Binti Sayuni aliye mzuri, mwororo, nitamkatilia mbali. [Au: Nimemfananisha Binti Sayuni na mwanamke mtulivu na mwororo - kulingana na tafsiri ya Kiingereza].
Yeremia 6:2
Na Sayuni ni nani ? Kupitia kwa Isaya, Mungu alisema,



48

(Fungu: Isaya 51:16)
......Kuuambia Sayuni, 'Ninyi ni watu wangu.'
Isaya 51:16.
Tunapounganisha haya mafungu mawili, tunaona ya kuwa Mungu alitumia mwanamke muadilifu kuwakilisha kanisa lake la kweli.
Mtume Paulo anatumia msemo huo huo katika kulieleza kanisa la Wakorintho.



49

(Fungu: 2 Wakorintho 11: 2)
.....Kwa kuwa naliwaposea mume mmoja, ili nemletee Kristo bikira safi.
2 Wakorintho 11:2.



50

(Fungu: Ufunuo 17:3-5)
Hata hivyo, Yohana pia alionyeshwa mwanamke mwingine, ambaye alimueleza katika Ufunuo 17:......Nikaona mwanamke, ameketi juu ya mnyama mwekundu sana, mwenye kujaa majina ya makufuru......



51

Na mwanamke yule alikuwa
amevikwa nguo ya rangi ya zambarau, na nyekundu, imepambwa kwa dhahabu, na kito cha thamani, na lulu,



52

naye alikuwa na kikombe cha dhahabu mkononi mwake, kilichojawa na machukizo,
na machafu ya uasherati wake.

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli



53

Na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa,




54

SIRI , BABELI MKUU, MAMA WA MAKAHABA NA MACHUKIZO YA NCHI.
Ufunuo 17:3-5.


55

Lugha hii ya mifano inaeleza mwanamke asiye safi -- kanisa bandia. Kanisa lililoanguka limekuwa si aminifu kwa Kristo na limeiuza kweli ya Biblia. Yakobo alitumia maneno kama hayo katika kuelezea juu ya wale ambao wanayaacha mafundisho ya Mungu na kujiunga na dunia:



56

(Fungu: Yakobo 4:4)
Enyi wazinzi,
hamjui ya kwamba kwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu?......
Yakobo 4:4.



57

Kwa hiyo, mwanamke aliyeanguka, anawakilisha kanisa ongo, na mwanamke safi anawakilisha kanisa safi.
Hebu tutizame tena katika unabii wa mwanamke safi.
Mwanamke safi = Kanisa safi
Mwanamke muongo= Kanisa ongo.



58

(Fungu: Ufunuo 12:2,4)
Naye alikuwa ana mimba, akilia, hali ana utungu na kuumwa katika kuzaa...



59

Na yule joka akasimama mbele ya yule mwanamke aliye tayari kuzaa,

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli



60

ili azaapo amle mtoto wake.
Ufunuo 12:2,4.
Huyu joka  ni yupi ambaye alisimama mbele za mwanamke ili amle mtoto wake mara alipozaliwa?



61

(Fungu: Ufunuo 12:7-9)
Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka, yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake;



62

nao hawakushinda, wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni.



63

Yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani,aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote;



64

akatupwa hata
nchi, na malaika
zake wakatupwa
pamoja naye.



65

(Fungu: Ufunuo 12:5)
Ufunuo pia inaeleza juu ya mtoto: Naye akazaa mtoto mwanamume, yeye atakayeyachunga mataifa kwa fimbo ya chuma.



66

Na mtoto wake akanyakuliwa hata kwa Mungu,  na kwa kiti chake cha enzi.
Ufunuo 12:5

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli


67

Ni mtoto mmoja tu katika historia ya dunia ambaye atawa chunga mataifa yote kwa fimbo ya chuma na kunyakuliwa hata kwa Mungu, na kwa kiti chake cha enzi, na huyo ni Yesu. Alinena juu ya kuja kwa mara ya pili kwa Kristo,



68

(Fungu: Ufunuo 19:15)
Yohana alisema, Na  upanga mkali hutoka kinywani mwake ili awapige mataifa kwa huo.



69

Naye atawachunga kwa fimbo ya chuma...
Ufunuo 19:15.
Paulo anaeleza jinsi Yesu alivyo nyakuliwa hata kwa kiti cha enzi,



70

(Fungu: Waefeso 1:20)
Wakati Mungu ...alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho. Waefeso 1:20.


71

Vita iliyoanza mbinguni ilihamia duniani. Akifanya kazi kupitia katika Rumi ya kipagani, Shetani alijaribu kuondoa uhai wa Yesu mara alipozaliwa. Herode, liwali wa Kirumi, alitoa tamko kwamba watoto wote wa kiume wenye umri wa miaka miwili kushuka chini wauawe, lakini malaika alimuonya Mariamu na Yusufu kwamba wakimbie na Yesu hadi Misri.


72

Mwovu alimjaribu Yesu wakati wote wa huduma yake, akitegemea kuuzuia mpango wa Mungu wa kuokoa dunia iliyoanguka. Mwili wa Kristo ulining'inia msalabani, Shetani alidhani alikuwa ameshinda pambano.
Lakini kaburi tupu lilikuwa ishara dhahiri ya kushindwa kwa Shetani.

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli


73

Kristo alifufuka na kupaa hadi kwa kiti cha enzi cha Baba yake. Unabii ulikuwa katika ratiba, kama jinsi ulivyotabiriwa! Hali akiwa ameshindwa katika jaribio lake la kumuangamiza Mwana wa Mungu, Shetani aligeuzia hasira yake kwa mwanamke, au kanisa la Kikristo.


74


Wanafunzi wote wa Kristo kasoro mmoja walikufa mauti ya wafia dini.
Kama unataka unataka kumuumiza mzazi, ni ipi namna iliyo chungu kuliko zote?
Kwa kumuumizia watoto wake.
Shetani hangeweza tena kumgusa Yesu.
Alikuwa mbinguni, ndiyo.
Hivyo sasa aliwashambulia wafuasi wa Yesu kwa ukali sana.


75

Na mtume Paulo alikatwa kichwa nje ya kuta za Rumi.
Wakristo waliteswa na kutupwa katika mashimo yenye giza, wengi wakitia muhuri shuhuda zao kwa damu zao.



76

Kwa kadiri wanafunzi walivyokuwa hai, ndivyo na kanisa lilivyosimama imara katika kweli.
Baada ya vifo vya wanafunzi, baada ya muda kupita, baadhi ya wakristo, Wakristo waliiuza imani yao na mafundisho ya uongo yakaingia kanisani.



77

Kuelekea sehemu ya mwisho ya karne ya pili, makanisa yaliyo mengi yalijitwalia mfumo mpya;



78

ule unyofu wa awali ulitoweka kadiri wanafunzi wa zamani walipotulia makaburini mwao.

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli


79

Katika karne ya nne, Mfalme Konstantine alijaribu kuunganisha Ufalme wa Kirumi pamoja kwa kuunganisha wapagani na Wakristo katika mfumo mmoja wa mkuu wa kidini. Matokeo yake, Ukristo ukapendwa sana. Wapagani wakabatizwa na kuingia kanisani wakileta imani zao nyingi na mazoea yao. Kanisa lilipoendelea kukumbatia makosa hayo, lilipoteza mwelekeo wa kusudi lake.



80

Mwana historia mmoja aliandika, Wakristo wapya walikuwa wapagani wale wale wa zamani, kama jinsi mawazo na mazoea yao yalivyokuwa,....ongezeko lao makanisani halikufuta upagani.



81

Kinyume chake, makundi ya wapagani yalipelekea upagani kuhafifisha nguvu za kimaadili za Ukristo uliokuwa katika utaratibu mzuri hadi kiasi cha kuua uwezekano wa kuzaa.
- Karne za Ukristo: Historia kwa Ufupi, uk. 58.


82

Hata hivyo, katika wakati huu Wakristo wengi walisalia kuwa waaminifu kwa kweli za Mungu na wakaapinga mabadiliko yaliyokuwa yameingia katika kanisa.
Walikataa kuuza misimamo yao, na wengi waliteswa kwa sababu ya misimamo yao.
Mara wafalme wa Kirumi wakatoa amri kwamba yeyote aliyekataa mafundisho ya uongo ya kanisa la kiserikali alikuwa amefanya uhalifu ulioadhibiwa tu kwa kifo.



83


(Fungu: Ufunuo 12:13)
Huku akiwa ameyaona haya yote mbeleni, Yohana aliandika,
Na joka yule...alimwudhi mwanamke yule aliyemzaa mtoto mwanamume.
Ufunuo 12:13.
Na ni kitu gani kilichotokea kwa mwanamke?

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli




84

(Fungu: Ufunuo 12:6)
Yule mwanamke akakimbilia nyikani, ambapo ana mahali palipotengenezwa na Mungu,




85

ili wamlishe huko muda wa siku elfu na mia mbili na sitini.
Ufunuo 12:6.
Tambua hapa ya kwamba Mungu anafunua muda ambao watu wake walikuwa wateswe: siku 1,260. Tumegundua tayari ya kwamba kila siku katika unabii wa Biblia huwakilisha muda wa mwaka mmoja halisi.




86

(Fungu: Ezekieli 4:6)
Ezekieli aliandika, ....siku moja kwa mwaka mmoja nimekuagiza.
Ezekieli 4:6




87

Hivyo kugandamizwa kwa watu waamifu wa Mungu, kama kulivyotabiriwa katika Ufunuo, ilikuwa kuendelee kwa miaka 1,260.




88

Historia kwa usahihi kabisa inauthibitisha unabii huu wa Biblia. Mfalme wa Kirumi Justinian aliamuru jenerali wa Kirumi Belisarius kufutilia mbali mamlaka mbili za mwisho za Ki Arian ambazo zilipinga kanisa la Kirumi.




89

Mamlaka ya mwisho katika hizi ilifutiliwa mbali mwaka wa 538 B.K., na Justinian alimtamka askofu wa Rumi kuwa kichwa cha kanisa, msahihishaji mwenye nguvu na wa kweli wa wazushi.
Utawala usio na uvumilivu wa wale walioitwa wazushi ukaanza.

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli


90

Na Wakristo waaminifu walioendelea kudumisha ukweli uliofunuliwa katika Neno la Mungu waligundua ya kwamba njia pekee ya kuihifadhi imani ilikuwa kukimbia, kama jinsi Ufunuo ilivyotabiri.

Mwanamke akakimbilia jangwani.


91


Wa Waldensia, Waalbigensia, na Wakristo waaminifu wengine walikimbilia kwenye Alps katika Italia ya kaskazini na Ufaransa ya kusini, na Wahaguenoti wakasambaa katika Ufaransa yote. Walitulia katika mabonde yaliyojitenga, mapango ya mbali zaidi, na katika milima iliyo inuka zaidi.
Walisakwa kama wahalifu wa kawaida, na wengi waliuawa.
Uhalifu wao? Hawakuacha mafundisho ya Yesu.


92

Mamilioni ya Wakristo waliamua kuuawa badala ya kuiuza imani yao.
Baadhi ya wanahistoria wanakadiria idadi ya waliouawa kufikia milioni 50.
Na wengi wa wale waliouawa waliuawa na wengine waliojiita Wakristo walioamini ya kwamba walikuwa wakitenda mapenzi ya Mungu!


93

Hatimaye ukweli wa Mungu ulishinda.
Biblia iliyotafsiriwa katika lugha ya watu husika na sasa kupitia katika uvumbuzi wa mashine za uchapaji ikasambaa katika dunia nzima.
Ukweli wa Mungu haukuwa ufichike tena. Ulikuwa ufunuliwe sasa!


94

Wanamatengenezo wenye juhudi walilitangaza Neno la Mungu kwa ujasiri. Baadhi kama Huss na Jerome, walichomwa huku wakiwa wamefungwa katika miti.

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli




95


Wengine, kama Luther, Wycliffe, na Tyndale, walisakwa na kuteswa.


96

Hata hivyo, pamoja na uvumbuzi wa Marekani, uhuru mpya na kimbilio jipya vikatolewa kwa Wakristo walioteswa wa Ulaya.



97

Katika pwani za taifa jipya lililozaliwa  kuliwekwa msingi wa uraia na uhuru wa kidini.



98

Kipindi cha maridhiano na mateso kilichotabiriwa katika ufunuo 12 hatimaye kikafikia mwisho wake mwaka 1798.
Kiliisha wakati Napolioni alipomtuma Jenerali Berthier kumchukua papa mateka --miaka kamili 1,260 baada ya mateso kuanza mwaka wa 538.


99

Wakati muda huu wa kinabii ulipofikia mwisho wake,  bado Mungu alikuwa na kundi la waumini waaminifu walioshikilia Biblia na mafundisho yake. Unabii ulitangulia mapema kusema ya kwamba Shetani angegeuzia ghadhabu yake  kwa kanisa la Mungu lililosalia baada ya kipindi hiki cha kinabii:



100

(Fungu: Ufunuo 12:17)
Joka akamkasirikia mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya  wazao wake waliosalia,



101

wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu;
Ufunuo 12:17.

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli


102


Masalio ni sehemu ya mwisho ya kitambaa kinachosalia kutokana na jora...
Vivyo hivyo, masalio wa kanisa la Mungu ni sehemu ya mwisho ya kanisa lile -kanisa linaloendelea kuwepo katika kipindi cha mwisho mara kabla ya Yesu kurudi duniani tena.



103

Hivyo katika kutafsiri fungu hili moja kwa moja, tungesema, Mwovu alighadhibika....akaenda kufanya vita na kanisa la siku za mwisho.

Shetani anaghadhibika kwa kuwa watu wa Mungu bado wanafuata kweli za Mungu katika siku za hizi za mwisho.




104

Yohana anaelezea juu ya tabia mbili ambazo kwazo twaweza kulitambua kanisa hili la siku za mwisho:
Joka akamkasirikia [alimghadhibikia] mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia,



105

wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu; Ufunuo 12:17.
Masalio ni wale wazishikao amri zote za Mungu.



106

Wenye ushuhuda wa Yesu Kristo


107

Lakini je, si kila kanisa linafundisha ya kwamba Wakristo wanapaswa kutii amri za Mungu?
Siyo hivyo kikamilifu! Lakini dini nyingi leo hufundisha washiriki wao, kwa njia moja ama nyingine, kutotii baadhi ya maelekezo ya Mungu.
Kwa mfano, baadhi ya makanisa hufundishwa kuinamia sanamu.
Mengine hudharau utakatifu wa jina la Mungu.

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli



108

(Fungu: Kutoka 20:8-10)
Na sehemu kubwa zaidi ya ulimwengu wa kidini umepoteza muelekeo wa kumbukumbu ya uumbaji iliyoelezwa katika amri ya nne:
Ikumbuke siku ya Sabato, uitakase.




109

Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote;




110

lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako,
Kutoka 20:8-10.



111

(Fungu: Ufunuo 12:17)
Masalio wa Mungu, au kanisa la siku za mwisho, si tu walikuwa watunze amri za Mungu, lakini unabii pia unasema watakuwa na ushuhuda wa Yesu Kristo. (Ufunuo 12:17)



112

(Fungu: Ufunuo 19:10)
Ufunuo 19:10 inasema, ushuhuda wa Yesu ndio roho ya unabii.


113

Kanisa la Mungu la siku za mwisho litakuwa na karama za Roho, ikiwepo ile ya roho ya unabii. Tutajifunza hii karama ya pekee kwa undani zaidi katika wakati wa mbeleni.
Mungu anatoa tabia zingine kadhaa ili kutusaidia katika utafiti wetu wa kanisa lake la siku za mwisho. Watu wake watajihusisha na utume wa kuifikia dunia kwa injili, kwani Yesu aliliagiza kanisa lake:



114

(Fungu: Mathayo 28:19,20)
Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi,

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli



115

mkiwabatiza  kwa jina la  Baba, na Mwana,
na Roho Mtakatifu;



116

na kuwafundisha kuyashika yote
niliyowaamuru ninyi; na tazama



117

mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari..
Mathayo 28:19,20.


118

Amri ya kuhubiri injili ya milele katika dunia nzima inawakilishwa katika Ufunuo 14 na malaika watatu warukao katikati ya mbingu.
Sehemu ya  kwanza  ya jumbe hizi tatu inasisitiza kweli mbili kuu ambazo zinapaswa kuelezwa kwa kila mtu:



119

(Fungu; Ufunuo 14:6,7)
Kisha nikaona
malaika mwingine akiruka katikati ya  mbingu,



120

mwenye injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi -



121

na kila taifa na kabila na lugha na jamaa,-



122

akasema kwa sauti kuu, 'Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja.



123

Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji.'
Ufunuo 14:6,7.



124

Hili ni onyo kwa wale wanaoishi katika saa za mwisho za Dunia kukumbuka ya kwamba siku ya hukumu imekuja.
Hili pia ni kumbusho la kumbukumbu kuu ya uwezo wa Mungu wa uumbaji, Sabato ya siku ya saba.
Sehemu ya pili ya ujumbe huu wenye sehemu tatu unapatikana katika fungu la 8:



125

(Fungu: Ufunuo 14:8)
Kisha mwingine, malaika wa pili, akafuata akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa,



126

maana ndio uliowaowanyeshwa mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake.'
Ufunuo 14:8.
Ujumbe huu unaita watu wa kweli wa Mungu kutengana na ulimwengu uliochanganyikiwa kidini.
Mtizamo wao utaitwa ili kuelekea uasi katika dini leo.
Mwito wa mwisho, na mzito, unatolewa katika sehemu ya tatu ya unabii huu:



127

(Fungu: Ufunuo 14:9,10)
Na mwingine, malaika wa tatu, akafuata, akisema kwa sauti kuu,

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli



128

'Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake,  na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake,



129

yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu......
Ufunuo 14:9,10.



130

Dunia inapaswa ionywe dhidi ya ibada ya mnyama na sanamu yake au kupokea alama yake.



131

(Fungu: Yohana 10:16)
Yesu alisema, Na kondoo wengine
ninao, ambao si wa zizi hili; na hao nao imenipasa kuwaleta;



132

na sauti yangu wataisikia; kisha kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja.
Yohana 10:16.


133

Mungu anao wafuasi wake katika makanisa yote, lakini utakuja wakati ambapo kutakuwa na zizi moja, au kanisa moja peke yake la kweli.
Yesu alisema kondoo wake wataitwa toka katika makundi haya ambayo hayajafuata kwa uangalifu mafundisho ya Neno la Mungu.



134

(Fungu: Ufunuo 18:4)
Yohana wa Ufunuo alitabiri juu ya wakati huo:Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni ikisema, 'Tokeni kwake, enyi watu wangu,



135

msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake.'
Ufunuo 18:4.
Wafuasi waaminifu wa Mungu wataitwa kutoka katika makosa ya kidini na machafuko ambayo yapo katika kipindi cha mwisho wa wakati.
Utataka kugundua  jinsi gani Biblia inaeleza juu ya watu wanaoitwa watoke katika machafuko ya kidini ambayo yatakuwapo kabla tu ya kuja kwa Yesu.



136

(Fungu: Ufunuo 14:12,14)
Hapa ndipopenye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri ya Mungu, na imani ya Yesu.




137

Kisha nikaona, na tazama, wingu jeupe,  na juu ya wingu hilo ameketi mmoja, mfano wa Mwanadamu,




138

mwenye taji ya dhahabu juu ya kichwa chake, na katika mkono wake mundu mkali.
Ufunuo 14:12,14.




139

Hebu na tupitie kwa upesi baadhi ya tabia za maana za kanisa la Mungu kama zinavyoelezwa katika Biblia:



140


Kanisa la Mungu la masalio lilikuwa litokee baada ya mateso ya kutisha ambayo yaliisha mwaka wa 1798.



141


Watakuwa na imani ya Yesu, inayowaongoza kutunza amri zote kumi za Mungu.

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli



142

3. Watatangaza jumbe maalum za maonyo za Ufunuo kwa dunia yote ili kuwaandaa watu kwa ajili ya marejeo ya Yesu.



143

Watakuwa na karama za Roho, ikiwemo karama ya unabii.


144

Makanisa yote yanaweza kufanana kwa mtizamo wa haraka,


145

lakini uendeleapo kujifunza maelekezo ya Mungu juu ya undani wa Neno lake Takatifu, ni rahisi sana kutupilia mbali wale ambao hawana tabia hizi za Kibiblia.
Pengine umekuwa ukitafuta, ukijaribu kuchuja katika machafuko haya ya kidini duniani leo, ukitafuta kanisa la siku za mwisho la Mungu.
Ninaamini ya kwamba lipo kanisa moja la kweli pekee. Hili ni kanisa linaloamini katika Biblia, ambalo kiini chake ni Kristo, utunzaji wa Sabato, kazi ya dunia nzima ihusuyo marejeo ya Kristo.
Ndiyo maana mimi ni muadventista Msabato.
Nina imani kanisa limefikia kiwango cha tabia zote.


146

Kama jinsi tulivyojifunza huu unabii wa ajabu, waweza kuona wazi ya kwamba Mungu anao ujumbe maalum, na watu maalum wa kuubeba ujumbe huu kwa dunia nzima.
Lakini haitoshi kujua tu kweli hizi za kibiblia.


147

Ili kuwa na amani na furaha itokanayo na kutembea kikamilifu na Yesu Kristo, ni muhimu pia kwako kujitokeza na kufuata ukweli kama ambavyo umefunuliwa katika Neno la Mungu, kwani Yesu alisema,

# 20 - Kuwekwa Huru na Kweli



148

(Fungu: Yohana 13:17)
Basi, ikiwa mwayajua hayo, mtakuwa na heri mkiyatekeleza. (John 13:17 [HNKK])
Yohana 13:17.


149

Mungu anakualika ili upate kufanya mojawapo kati maamuzi ya muhimu zaidi katika maisha yako.
Je, waamini ya kwamba umelisikia neno la Mungu likihubiriwa katika mfululizo wa mafundisho haya?
Je, waamini ya kwamba Roho Mtakatifu amekuwa akivuta kwa nguvu moyo wako katika mfululizo huu?
Tunapolisikia neno la Mungu, tunaposikiliza kweli ya Mungu, Roho Mtakatifu anatuvuta kufanya uamuzi.
Je, ungependa kusema, Ndiyo BWANA, ninakubali neno lako. Ndiyo, Yesu, ninataka kuufuata ukweli. Ndiyo, Yesu, ninakubaliana na maongozi ya Roho Mtakatifu. Nitakufuata njia yote sasa. Ninachagua kutembea katika njia ya kweli.
Kama huo ndiyo uamuzi wako, je, waweza kusimama sasa hivi tunapoomba?

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota



1

Mungu Angali Akinena Kupitia kwa Manabii Wake


2

Katika sehemu mbalimbali za dunia, wanasayansi wanaotumia darubini zinazotumia mawimbi sauti kama ya radio
wanasikiliza sauti zinazotoka nje ya anga letu.


3

Wanategemea ya kwamba labda siku moja, watasikia ujumbe kutoka kwa viumbe hawa wenye akili waliopo katika dunia nyingine.


4

Kuna vithibitisho ya kwamba ujumbe umekuwa ukivuma Duniani kwa miaka maelfu sasa - lakini ni wachache wanaousikiliza.
Huu ni ujumbe kutoka kwa Muumbaji wa sayari hii -- ujumbe wa upendo toka kwa Mungu unaojaribu kurejesha watoto wake waasi.



5

Utengano huu kati ya Mungu na wanadamu haukuwepo siku zote.
Kila kitu kilianzia kwa uzuri katika Sayari Dunia -- Dunia iliyo kamili kwa ajili ya watu wawili walio kamili, walioumbwa kwa mfano wa Mungu!



6

Na pale katika nyumba ya Edeni, Mungu alikuja na kutembea na kuzungumza nao uso kwa uso.
Hebu tafakari kama unawaona wakitembea tembea pamoja katika wakati wa jua kupunga jioni!


7

Hivi ndivyo Mungu alivyopanga - uhusiano mzuri wa umoja!
Hakukuwa na cha kuwatenganisha.
Haya lazima yalikuwa ni matembezi ya kupendeza pamoja.

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota




8


Lakini ni jambo la kusikitisha kusema, huu uhusiano wa upendo  na umoja ulidumu tu kwa muda wa sura mbili katika Biblia.


9

Mwanzo, sura ya 3 inatuambia kisa cha kusikitisha. Adamu na Hawa walitenda dhambi.


10

Waliasi dhidi ya sheria ya Mungu ya upendo usio na dosari.
Dhambi hutenganisha. Dhambi na Mungu havikai pamoja.
Adamu na Hawa wasingeweza kuwa na mawasiliano ya moja kwa moja na ushirika na Mungu.


11

Walimsikiliza joka Lusifa na kumtii yeye badala ya Mungu -- na hiyo ndiyo dhambi.



12

(Fungu:  Mwanzo 3:8)
Biblia yasema,Kisha wakaisikia sauti ya BWANA Mungu, akitembea  bustanini  wakati wa jua kupunga;



13

Adamu na  mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, BWANA Mungu asiwaone



14

kati ya miti ya bustani.
Mwanzo 3:8.
Adamu na Hawa walikuwa wamejificha!
Hawakutaka kumkabili Mungu.
Walitaka tu kujificha.
Hicho ndicho dhambi inachotenda.

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota



15

Inatutenganisha na kuharibu uhusiano wa upendo kati ya Mungu na mwanadamu, na kati ya mtu na watu wengine.



16

(Fungu: Isaya 59:2)
Nabii Isaya aliandika: Lakini  maovu yenu yamewafarikisha ninyi na  Mungu wenu,



17

na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone, hata  hataki  kusikia.....
Isaya 59:2.
Ndiyo, dhambi hututenganisha sisi na Mungu, lakini haikututenganisha na upendo Wake.
Mungu alipata njia ya kuendelea kuwasiliana na mwanadamu mwenye dhambi.
Upendo daima hutafuta namna ya kuendelea kuwasiliana!


18

Aliimarisha namna nyingine ya kuwasiliana na watoto wake katika Sayari Dunia -- njia ya kuongoza na kuelekeza, na kufunua mipango yake.
Alichagua wanaume na wanawake ambao angewaamini kuwa wanenaji wake, kuwasiliana upendo wake na mipango yake kwa mwanadamu.


19

Kati ya wale aliowachagua alikuwepo Musa, Miriamu, Samweli, Eliya, Hulda, Debora, Isaya, Yeremia, na wengine wengi.


20

Manabii wa kiume na wa kike walikuwa wanenaji wa Mungu!

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota



21

Hii ilikuwa ni njia ya Mungu ya kusema, Ninakupenda, Ninakujali, na  ninao mpango kwa ajili yako.


22

Biblia inayo taarifa ya majadiliano mengi kati ya Bwana na watu mbalimbali watajwao katika Biblia, lakini hayakuwa majadiliano sawa na majadiliano na ushirika ambao Adamu na Hawa waliufurahia katika Bustani ya Edeni.


23


Wakati fulani Mungu alinena kwa njia  ya Roho Mtakatifu, wakati fulani alinena kwa njia ya malaika watakatifu, na nyakati zingine kupitia kwa watu aliowachagua kuwa wajumbe wake.

Katika kipindi cha miaka 2,500 ya awali ya historia ya mwanadamu, hakukuwa na ufunuo ulioandikwa toka kwa Mungu  kama ambavyo tumeweza kugundua hadi sasa.
Wale waliofundisha juu ya Mungu lazima walishuhudia  kwa njia ya maneno kile alichowaambia.
Hata hivyo, njia iliyopendelewa sana ambayo Mungu alichagua kuitumia kuwasiliana na watu wake



24

(Fungu: Amosi 3:7)
imekuwa ni mkondo wa manabii - wa kiume na wa kike ambao walinena kwa ajili ya Mungu kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu.
Hili si la kushangaza sana, kwani Biblia yasema wazi: Hakika Bwana MUNGU hatafanya neno lolote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake. Amosi 3:7.


25

Hebu tuone jinsi hawa manabii walivyopokea ujumbe:

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota




26

(Fungu: 2 Petro 1:21)
Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu,



27

bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.
2 Petro 1:21
Mungu alikuwa na manabii, kwa kweli, hata kabla ya Gharika kuu ya siku za Nuhu.



28

(Fungu: Yuda 14)
Henoko alitangaza kuja kwa mara ya pili kwa Kristo: Na Henoko, mtu wa saba baada ya Adamu, alitoa maneno ya unabii juu ya hao, akisema,



29

'Angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake, maelfu maelfu.'
Yuda 14.
Henoko ni mtu wa kwanza kutajwa katika Biblia ambaye alikuwa na karama ya unabii.
Lakini walikuwepo wengine!



30

(Fungu: Matendo 3:21)
Biblia yasema, Mungu alinena kwa .....kinywa cha manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu. Matendo 3:21.
Nuhu, nabii mwingine, alitabiri juu ya maangamizi ya dunia kwa gharika miaka 120 kabla haijatokea.


31

Baada ya Gharika, tunaona manabii wengi wa kiume na wa kike - akiwemo Miriamu, Debora, Yeremia, Isaya, Ezekieli, na wengine.
Hawa walikuwa waalimu wa haki. Walikuwa na viongozi wa maadili na wa kiroho, wakinena kwa ajili ya Mungu.

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota



32

Wakati fulani Mungu alifunua mapenzi yake kwa manabii wa kiume na wa kike kwa njia ya njozi, wakati fulani kwa njia ya ndoto, na wakati fulani kwa njia ya Neno la Mungu.
Lakini daima kwa njia ya Roho Mtakatifu.




33

(Fungu: Hesabu 12:6)
Bwana alisema: ....Akiwapo nabii kati yenu, Mimi, BWANA, nitajifunua kwake katika maono;





34

Nitasema naye katika ndoto.
Hesabu 12:6.
Wakati fulani wajumbe wa Mungu walielekezwa wanene kwa niaba ya Mungu; wakati fulani walikuwa waandike au waweke taarifa ya ujumbe kwa ajili yake.
Kwa kweli, Biblia ni matokeo ya huduma ya manabii.
Kila mwandishi alikuwa ni sehemu ya mpango wa Mungu.





35

Wote walinena au waliandika kwa niaba yake Wakiongozwa na Roho wake. Kupitia kwake Mungu alituma barua ya upendo kwa watoto wake duniani.




36

Hii ni njia yake ya kusema,Ninawapenda, na ninataka kuwasiliana nanyi.
Na kwa namna ya pekee anataka sisi tujue ya kwamba anatamani wakati ule ambapo tutakuwa na ushirika naye uso kwa uso!



37

Waandishi wote wa Agano Jipya -- Mathayo, Marko, Luka, Yohana, Paulo, Yakobo, Petro, na Yuda -- walikuwa ni sehemu ya mpango ule.
Wote walikuwa na karama ya unabii.
Kwa kweli, walikuwepo wengine wakati huo waliokuwa wakinena kwa ajili ya Mungu: Simeoni, Agabus, Baranabas, Anna,

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota



38

(Fungu: Matendo 21:9)
na mabinti wanne wa Filipo .....waliokuwa wakitabiri. Hawa wote walikuwa vyombo vya Mungu vilivyotumika kufunua mapenzi yake na kutia moyo kanisa la Kikristo la awali.


39

Kisha Yesu akaja, kueleleza yeye binafsi kwa maneno na matendo jinsi Mungu alivyo hasa. Kamwe dunia haijapata kushuhudia Mwana mawasiliano mzuri kama huyo wa upendo na fikira za Mungu.


40

Karne kumi na tisa zimepita tangu Kalvari, na bado wanaume na wanawake, wavulana na wasichana hupiga magoti chini ya msalaba na kuweka maagano yasiyoisha na kujitoa kwa Mwokozi wa Ulimwengu. Yesu aliporudi mbinguni, Biblia yasema aligawa karama kwa watu -karama ambazo zingeliwatia moyo na kuwaimarisha wafuasi wake:



41

(Fungu: Waefeso 4:8)
Hivyo husema, Alipopaa juu aliteka mateka, Akawapa wanadamu vipawa.
Waefeso 4:8.
Hizi karama zilikuwa zipi?



42

(Fungu: Waefeso 4:11 - 15)
Biblia yasema, Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu.
Waefeso 4:11.



43

Kwa nini Yesu alichagua kutoa karama kwa kanisa? Fungu la 12 lasema, Kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe.

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota




44

Hizi karama zilikuwa zisalie kanisani kwa muda gani?Hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu,



45

hata kufika kwa cheo cha kimo cha utimiilifu wa Kristo.
Fungu la 13.
Biblia yasema ya kwamba karama hizi zingetengeneza msimamo kwa kanisa na kuimarisha watu



46

Ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na upepo wa elimu,



47

kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu.
Fungu la 14.
Tambua mahali ambapo karama ya unabii inaposimama katika orodha ya karama za roho, kama jinsi Paulo anavyoziita.



48

(Fungu: 1 Wakorintho12:28)
Na Mungu ameweka wengine katika kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii,.....
1 Wakorintho 12:28.




49

Karama ya unabii ilikuwa ya pili baada tu ya ile ya utume, lakini ilikuwa iwe ya muhimu sana na karama ya maana katika kusaidia kanisa kutenda kazi sawasawa.

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota


50

Paulo alifananisha karama za Roho na sehemu mbalimbali za mwili wa mwanadamu.
Alionyesha ya kuwa macho, kichwa, mdomo, na sehemu zingine za mwili zote ni za muhimu kwa mwili ili ufanye kazi kwa uzuri na kwa ustadi.
Vivyo hivyo na kanisa.
Bila maono, kwa mfano, kanisa li kipofu!



51

(Fungu: Mithali 29:18)
Pasipo maono, watu huacha kujizuia; Bali ana heri mtu yule aishikaye sheria.
Mithali 29:18.


52

Lakini, wasema, Kitu gani kilitokea kwa karama ya unabii baada ya Kristo kurudi mbinguni na wanafunzi wake wote kufa?


53

Siyo vizazi vingi vilivyopita hadi kanisa lilipokuwa zembe, likiuuza ukweli, na kukosa uaminifu kwa Mungu na sheria yake.
Yeremia anayo taarifa ya kile kilichotokea wakati Israeli walipoasi kwa kipindi fulani:




54

(Fungu: Maombolezo 2:9)
......Wasio na sheria; Naam, manabii wake hawapati maono yatokayo kwa BWANA.
Maombolezo 2:9.


55

Kanisa la awali lilipoendelea kuingiza kanuni za kipagani na tabia zao na kuacha kweli za muhimu za Biblia, karama za kiroho moja baada ya nyingine ziliondolewa.


56

Wakati wa uasi wa kanisa, au wakati wa Zama za Giza, Biblia ilifungwa kwa mnyororo katika madhabahu za kitawa.
Kwa ujumla ziliandikwa katika Kiebrania, Kiyunani na Kilatini.

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota


57

Watu wa kawaida walipigwa marufuku kuhozi  au kusoma Maandiko.
Makasisi (au mapadre) peke yao waliruhusiwa kusoma na kutafsiri Biblia.
Wakristo waaminifu wachache walishikilia Biblia na ukweli wake,
Ijapokuwa kulikuwa na mateso, waliendeleza mbele kazi ya upelekwa na kushiriki sehemu za Maandiko waliyokuwa nayo na watu wengine.
Walipanda mbegu za Matengenezo muda  mrefu kabla ya Wycliffe, Luther, na Huss.



58

Martin Luther na wengine waliitafsiri Biblia katika lugha ya kawaida ya watu. Mateso yalikuja, lakini yalizidisha tu tamaa kubwa kwa ajili ya Neno la Mungu.


59

Na kadiri watu walivyoanza kwa bidii kujifunza Maandiko, kweli za zamani zilizofichwa kwa karne nyingi ziligunduliwa.
Kweli hizi zililetwa mbele za watu, na mwamko mkuu wa kidini ukatokea.


60


Katika kipindi hiki kukatokea msukumo mpya wa kidini - kundi la Wakristo waliojitoa, baadhi Wabaptisti, baadhi Wamethodisti, baadhi Wapresbiteriani, na wengine - wakiyachunguza Maandiko na kusali wapate nuru.



61

Walivyoendelea  kuchunguza Biblia waligundua katika amri ya nne ya Mungu kumbukumbu kuu ya Uumbaji wake - siku Mungu aliyowaomba watu wake kukumbuka.
Walisoma Kitabu cha Ufunuo na kuona maelezo ya watu wa siku za mwisho wa Mungu:

# 21 - JUMBE TOKA MBALI KUPITA NYOTA



62

(Fungu: Ufunuo 14:12)
Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu. Ufunuo 14:12.
Walivyoendelea kusoma na kujifunza mafungu, waliguswa zaidi na utunzaji wa amri za Mungu ikiwemo ya utunzaji wa Sabato ya Biblia.



63

Waliikubali hii kumbukumbu ya uumbaji na kutangaza ukweli wa Sabato kwa dunia



64

Vipi juu ya karama ya unabii?
Je, Mungu angeliinua karama maalum ya unabii kati ya hawa watu wa wakati wa mwisho waitunzao Sabato? Je, Mungu anacho kitu fulani maalum? Je, si sawa kuhitimisha ya kwamba Mungu anaweza kuwa amekuwa na kitu fulani maalum cha kusema kwa kizazi hiki? Je, yawezekana ya kwamba Mungu katika upendo wake kwa ajili yetu leo anataka kudumu katika mawasiliano nasi?



65

(Fungu: Yoeli 2:28,31)
Sikiliza: Hata itakuwa, baada ya hayo,
ya kwamba nitamimina roho yangu
juu ya wote wenye mwili;



66

na wana wenu, waume kwa wake, watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono.



67

....kabla haijaja hiyo siku ya BWANA iliyo kuu na itishayo.
Yoeli 2:28,31.

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota


68

Tambua ya kwamba Mungu alisema hili lingetokea mara tu kabla ya siku Kuu na ya Kutisha ya Bwana -- au kabla tu ya kuja kwa Kristo mara ya pili. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa na karama ya unabii kati yao wakati wa masaa ya mwisho ya historia ya dunia. Akiwasiliana na kanisa la Korintho, Paulo alitoa kauli hii kuhusu wafuasi wa Mungu:



69

(Fungu: 1 Wakorintho 1:7)
Hata hamkupungukiwa na karama yo yote, mkikutazamia sana kufunuliwa kwake Bwana wetu Yesu Kristo.
1 Wakorintho 1:7.



70

Tumekwisha gundua ya kwamba watu wa Mungu katika siku za mwisho watatambulika kama wale ambao watakuwa wame zishika amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu; Ufu. 12:17



71

subira ya watakatifu



72

na kuzishika amri za Mungu



73

na watakuwa na ushuhuda wa Yesu.

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota




74

(Fungu: Ufunuo 19:10)
Tunaambiwa ya kwamba ushuhuda wa Yesu ni roho ya unabii. Ufunuo 19:10. Kwa maneno mengine, ushuhuda wa Yesu ni ushuhuda wa Yesu kupitia kwa karama ya unabii.
Kulingana na Ufunuo, kanisa linalosalia kama mfereji wa mawasiliano katika siku za mwisho linatambulika kwa kuwa na imani ya Yesu, likizitunza amri zote za Mungu, na kubarikiwa kwa karama ya unabii.


75

Ndiyo, bado Mungu anataka kuwasiliana.
Bado angali na neno la kusema kwa kizazi hiki.



76

Lakini waweza kuuliza, Vipi juu ya uwezekano wa udanganyifu?
Twawezaje kujua tofauti kati ya nabii wa kweli wa Mungu na nabii wa uongo?



77

Uwezekano wa udanganyifu umekuwepo daima.
Katika historia yote kumekuwa na manabii wa uongo na wa kweli.
Hatupaswi kujihusisha na wale wa uongo, kama tunajua namna ya kuwatambua wale walio wa kweli.



78


Biblia inatoa tabia maalum
ambazo zinatambulisha nabii wa kweli:



79


Ujumbe wa nabii wa kweli utapelekana kabisa na Neno la Mungu na sheria yake.

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota



80

(Fungu: Isaya 8:20)
Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hakuna asubuhi.
Isaya 8:20.



81

Utabiri wa nabii wa kweli lazima utokee au daima ni lazima utimie!




82

(Fungu: Yeremia 28:9)
....neno la nabii yule litakapotokea, ndipo nabii yule atakapojulikana, kuwa BWANA amemtuma kweli kweli. Yeremia 28:9.



83

Nabii wa kweli hutabiri ili kulijenga kanisa. Mojawapo ya sababu ya Mungu kutoa karama ya unabii ni ili kulijenga kanisa lake. Kama tunataka kugundua karama ya kweli sharti tugundue pia kanisa la kweli. Hizi zimeshikana pamoja.



84

(Fungu: 1 Wakorintho 14:3,4)
Bali yeye ahutubuye, asema na watu maneno ya kuwajenga, na kuwafariji, na kuwatia moyo...



85

bali yeye ahutubuye ( au anayetabiri) hulijenga kanisa.
1 Wakorintho 14:3,4.



86

Nabii wa kweli atamtukuza Kristo kama Mwana wa Mungu na Mwokozi wa wanadamu:

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota



87

(Fungu: 1 Yohana 4:1,2)
Wapenzi, msiiamini kila roho, kwamba zimetokana na Mungu;



88

kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani.



89

....Kila roho ikiriyo kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatokana na Mungu.
1 Yohana 4:1,2.



90

Nabii wa kweli wa kiume au wa kike atajulikana kwa maisha yake na matendo yake.




91

(Fungu: Mathayo 7:16,18)
Mtawatambua kwa matunda yao....



92

Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti mwovu kuzaa matunda mazuri.
Mathayo 7:16,18.


93

Kulingana na mafungu haya, inakuwa dhahiri ya kwamba si kila ajiitaye kuwa nabii wa Mungu ni nabii wa kweli.

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota


94

Ujumbe wa nabii wa kweli, maisha yake na matendo yake lazima viunge mkono na kuimarisha ujumbe wa kinabii katika Biblia na maelekezo na amri za Mungu katika Neno lake Takatifu.
Hivyo bila kujali ni nani anayedai kunena kwa niaba ya Mungu, kipimo hiki kinamhusu!
Kama mtu anapelekana nacho, Mungu ashukuriwe!
Kama sivyo, fuata onyo la Mungu la kuwa macho nao.


95

Hebu nieleze kisa cha jinsi Mungu alivyochagua kuwa na mawasiliano na watu wake. Ulikuwa wakati ambapo walikuwa wakiuambia ulimwengu kweli zile zilizokuwa zimefichwa kwa karne nyingi.
Ulikuwa wakati wa Mwamko Mkuu wa Kidini mapema karne ya 19. Kulikuwa na shauku ya ajabu ya mafundisho ya Biblia na maombi.
Unabii wa Danieli na Ufunuo ulikuwa ukipendwa zaidi.


96

Wanafunzi waaminifu wa Biblia walijifunza unabii huu na hatimaye wakafikia hitimisho ya kwamba Yesu angekuja katika wakati wao.



97

Walipoendelea kujifunza wakafikia katika tarehe ya Oktoba 22, 1844. Hata hivyo, Oktoba 22 ilipita na marejeo ya utukufu ya Yesu hayakutokea.


98

Ulikuwa wakati wa kukatisha tamaa mkuu kuliko wote. Ulizua kujeli, dharau, na kutoeleweka.

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota



99

Baadaye, baada ya sala nyingi na majifunzo zaidi ya Biblia, kundi hili liligundua tarehe ilikuwa sahihi, lakini tukio hailikuwa sahihi!
Walidhania hekalu lililotajwa katika Danieli 8:14 lilikuwa dunia, lakini katika hili walikuwa wamekosea.
Badala ya dunia kutakaswa kwa moto, hekalu la mbinguni lilitakaswa. Hili lilihusisha uthibitisho wa mwisho wa tabia ya Mungu na serikali yake.


100

Watu walivunjika mioyo, kukata tamaa kulionekana kama kusikoweza kubebeka.
Lakini Mungu mwenye upendo kamwe hamuachi mtafiti mwaminifu wa ukweli: na hakuwaacha hawa waumini wa marejeo katika kipindi hiki cha shida. Aliwataka wajue ya kwamba Aliwajali - kwamba aliwapenda na alitaka kuwasaidia. Hivyo katika kipindi hiki nyeti, Mungu alichagua kurejesha karama ya unabii kwa watu wake. Ni kisa cha kusisimua tangia mwanzo!


101

Alimchagua binti dhaifu aliyekuwa na umri wa miaka 17 tu na kumpa njozi ya ushindi ya mpango wa Mungu. Ellen Harmon alipewa njozi yake ya kwanza mara baada ya kukata tamaa kukuu kwa Desemba, 1844.
Alionyeshwa wana marejeo wakisafiri katika njia iliyoinuka kwenda mbinguni na njia hii ikiwa na nuru yenye kung'aa iliyoiangaza njia.


102

Lilikuwa jambo la kutia moyo kiasi gani kwa kundi hili dogo lililosambaa la waumini wa marejeo, ambalo baadaye lingejulikana kama Waadventista wa Sabato.

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota


103

Huyu mwanamke kijana ambaye baadaye alifahamika kama Ellen White kwa sababu ya ndoa yake na mtangulizi wa Waadventista, James White, alikuwa mwaminifu kwa mwito wake. Kwa zaidi ya miaka 70, alinena, aliandika, alifundisha, na alishauri akiongozwa na Mungu. Hata ingawa upana wa huduma yake na ujuzi wake ulikuwa wa kushangaza, kazi yake kuu, kama alivyoieleza, ilikuwa ni kuongoza wanaume na wanawake kwa 'nuru kuu' -- Biblia.




104

Aliandika: Usikivu kidogo tu umewekwa kwa Biblia na Bwana ametoa nuru ndogo ili kuongoza watu waume na wake kwa 'Nuru Kuu.'
-- Huduma ya Uinjilisti wa Vitabu, uk. 125.



105

Alitanguliza Maandiko Mtakatifu kama mahakama ya mwisho ya rufaa katika maswali yote yahusuyo mafundisho ya Biblia.
Kwa wale waliokuwa wakikosoa Neno la Mungu, aliandika:



106

Shikeni Biblia yenu kama isemavyo na mkome ukosoaji wenu kuhusu uthamani wake na mulitii Neno,



107

na hakuna hata mmoja wenu atakayepotea.
Selected Messages, Kitabu cha 1, uk. 18.


108

Hakuna mwanamke hata mmoja ambaye amewahi kuchapa vitabu vingi kama Ellen White alivyochapa vitabu, makala za magazeti, vitini, majarida, na nyaraka binafsi. Ujumbe wake wa ushauri na makaripio yaliyopokelewa toka kwa Mungu yalitolewa kwa watu wake katika kipindi chote cha maisha yake.

# 21 - JUMBE TOKA MBALI KUPITA NYOTA



109

Maandishi yake yanahusisha ushauri katika maisha ya ushindi ya Kikristo, lishe, afya,malezi ya uja uzito, madawa, ndoa na unyumba, uongozi wa watoto, elimu , na mengi, mengi zaidi. Mengi ya maandishi yake sasa yana umri wa zaidi ya miaka mia moja na yamethibitishwa na kupelekana na uvumbuzi wa kisayansi wa kisasa. Amenukuliwa na maprofesa, madaktari, watangazaji wa habari, na wengine kama bingwa katika nyingi ya fani hizi.




110


Dk. Clive M. McCay, marehemu profesa wa lishe katika Chuo Kikuu cha Cornell, alisema: Maandishi ya Ellen G. White yametajwa kwa sababu yanatoa mwongozo kwa ajili ya lishe ambayo inajenga na kuhusisha mwili mzima.

- Chakula cha Asili na Kilimo, Mei, 1958.





111

Nyuma kabisa mwaka wa 1864, Ellen White aliandika: Tumbaku ni sumu idanganyayo sana na iliyoovu zaidi...




112

Ni ya hatari zaidi kwa sababu madhara yake kwa mfumo wa mwili huingia taratibu sana, na hutambulika kidogo kidogo.





113

Hayakueleweka mapema hadi mwaka wa 1957 wakati Jumuiya inayoshughulikia Maradhi ya Moyo ilipotoa hitimisho ya kuwa uvutaji wa tumbaku ni chanzo kikubwa cha sarakani ya mapafu! Wakati wake wale waliokuwa katika fani ya tiba lazima walimhoji, kwani wakati ule ilifikirika ya kwamba tumbaku na sigara vilikuwa ni tiba ya muhimu ya maradhi ya mapafu.


21 - JUMBE TOKA MBALI KUPITA NYOTA

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota




114

Katika mwaka wa 1905 Mama White aliandika ya kwamba kulikuwa na 'vijidudu' vya sarakani. Alitaja:
Watu wanadumu kula
nyama iliyojazwa na vijidudu
vya kifua kikuu na sarakani....




115

Kifua kikuu, sarakani, na maradhi mengine ya kufisha husambazwa kwa njia hiyo.
---- Huduma ya Uponyaji, uk  313.





116

Kwa kweli, leo tungelitumia kwa usahihi zaidi neno kirusi.
Miaka tisini na tatu baadaye, gazeti la Newsweek lilichapisha habari iliyokuwa na kichwa kisemacho Virusi ni wakala wakuu wanaoamsha sarakani





117

Dk. Wendell Stanley, mtaalamu wa virusi na mshindi wa Nishani ya Nobeli,




118

aliendelea kiasi cha kutaja bila kuainisha ya kwamba aliamini virusi ni vyanzo vya sarakani zote za mwanadamu.
--Newsweek, Juni 18, 1956.




119

Mwaka wa 1902, Ellen White alionya ya kwamba San Fransisco na Oakland  itaadhibiwa na  Mungu kwa sababu walikuwa
kama Sodoma na Gomora.
(Manuscript 1902, uk.114)

# 21 - JUMBE TOKA MBALI KUPITA NYOTA



120

Tarehe 18 Aprili, 1906 saa 11:02 alfajiri, tetemeko kuu la San Francisco lilitokea.
Unabii ulikuwa wa kweli.
Uharibifu uliotabiriwa ulitokea kwa hakika kama ulivyotabiriwa.
Mafanikio ya mama White yanashangaza zaidi tunapofikiria juu ya vikwazo vingi na mapungufu yaliyomkabili wakati wote wa maisha yake.



121

Mtu aweza kuhoji kwamba huyu Ellen White alikwa nani na alikuwaje?
Jibu linatupeleka nyuma hadi Novemba 26, 1827.


122

Katika tarehe ile, dada pacha, Elizabeth na Ellen, walizaliwa karibu na kijiji kidogo cha Gorham, Maine, kwa familia ya Eunice na Robert Harmon. Ellen alikuwa wa mwisho kati ya watoto nane.


123

Akiwa na umri wa miaka tisa ajali ilibadili maisha yake milele.
Akirejea nyumbani toka shuleni, Ellen alijeruhiwa vibaya sana kwa jiwe lililorushwa na mwanafunzi mwenzake waliyesoma darasa moja naye.


124

Kwa majuma matatu hakujitambua. Hakuweza kuendelea na shule, na ilionekana kama asingeweza kuishi muda mrefu.
Hakuendelea zaidi ya viwango vya mwanzoni vya shule.

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota


125

Miaka kadhaa baadaye Ellen alitizama nyuma akiwa na hisia mchangayiko katika mwaka wa tisa wa umri wake. Kwa kweli, lilikuwa jambo la  kuvunja moyo kwa kutoweza kuhudhuria shule- kwa kutoweza kukimbia na kucheza na dada zake na kaka zake. Lakini wakati awamu moja ya maisha ilipoonekana kuisha, nyingine ilianza. Ellen akawa mwanafunzi mzuri sana wa Biblia. Alihudhuria kwenye mikutano ya makambi, uamsho, na mikutano ya nyumba kwa nyumba.


126

Baada ya kuhudhuria mikutano ya makambi ya Kimethodisti kule Buxton, Maine, Ellen alibatizwa tarehe 26 Juni, 1842. Akawa mshiriki wa kanisa la Kimethodisti.


127

Baadaye, Ellen na familia yao walihudhuria makambi yaliyofanyika kule Portland, Maine. Mnenaji alikuwa William Miller, kepteni wa zamani wa jeshi, ambaye alikuwa akijifunza Biblia kwa bidii. Kwa sababu alikuwa na shauku na kuja kwa Kristo upesi, yeye na wafuasi wake walibandikwa jina Waadventista au Wafuasi wa Miller.Familia ya Harmon ilishawishika juu ya  ukweli wa ujumbe wa Miller.


128

Hata hivyo, baada ya kukata tamaa kukuu kwa tarehe 22 Oktoba, 1844, wao pia walishanganyikiwa. Ellen alikata tamaa sana. Alilia, alijifunza neno la Mungu ili apate jibu, kama ilivyokuwa kwa wengi wa waumini waadventista.
Na hapo ndipo Mungu alipomuita kuwa nabii. Kimwili, hakuonekana kuwa kama mtu uliyemtegemea kuwa nabii. Alikuwa msichana wa miaka 17, akipambana na kifua kikuu na matatizo ya moyo. Na bado mwezi wa Desemba, 1844, Mungu alichagua kunena kwa Ellen katika njozi. Katika maneno yake mwenyewe, anaeleza mwitikio wake kwa wito huo:

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota



129

Baada ya kupata njozi hii, na Mungu kunipatia nuru, alinisihi niipeleke....lakini nilikataa. Nilikuwa kijana, na nilidhani hawangeweza kuipokea toka kwangu.
- Ellen G. White  Barua ya 3, 1847.


130

Ingawa alijihisi kutostahili na mdhaifu kimwili kulingana na majukumu ya mwito huu toka kwa Mungu, kwa imani alipokea utume huu toka kwa Mungu ambao ungedumu kwa maisha yake yote.


131

Ellen na mumewe James White walitenda kazi pamoja katika kuisambaza nuru hii ambayo Mungu aliitoa.


132

Ushindi wao na kujitoa kwao kunatajwa katika maandishi yake mengi.
Katika maisha yake yote Ellen White alikuwa Mkristo aliyejitoa, mtumishi wa Mungu ambaye hakuchoka, na mama mwenye bidii.
Alipendwa na mumewe, familia yake, na maelfu katika dunia.



133

Tarehe 6 Agosti, 1881, mume wa Ellen James alifariki kule Battle Creek, Michigan.
Ellen alisimama kando ya kaburi lake-akiweka agano la kuendeleza kazi ambayo walikuwa wamejinyima pamoja na kuiendeleza kwa zaidi ya miaka 35!


134

Baadhi ya maandishi mazuri sana na yatia nguvu moyo yalitokea baada ya tarehe hii.
Alitenda kazi peke yake kwa miaka mingine 34.
Huduma yake ya unabii ilimchukua hadi nchi kadhaa -- akiongoza, akielekeza, na kushauri waumini kama jinsi Bwana alivyomuongoza.

21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota



135

Maisha na kazi za Ellen Gould White zilimalizika tarehe 16 July, 1915.
Alikuwa amepita miaka 87 ya umri.
Alizikwa pembeni ya mume wake katika Makaburi ya Oak Hill kule Battle Creek, Michigan. Majuma machache baada ya kufariki kwake, gazeti moja likawa na kauli hii:




136

Hakuonyesha kiburi chochote cha kiroho na hakuwa akitafuta utajiri. Aliishi maisha na kutenda kazi iliyomstahili nabii, mtu wa kutamanika kuliko wote katika warithi wa Marekani. The New York Independent, Agosti 23, 1915.



137

Ndiyo, sauti yake imebaki imetulia katika kalamu yake . Lakini maneno yenye thamani sana ya ushauri, maonyo, maelekezo na yanayotia moyo ya huyu mtu mwaminifu wa Mungu yataendelea kuongoza watu wa Mungu hadi kufikia ushindi wa mwisho!




138

Maisha yake kwa ulimwengu ni karama ya upendo - ujumbe kwa dunia kutokea mahali palipo mbali na ulimwengu, toka kwa Mungu wa upendo ambaye bado anataka 'kuwasiliana' na watoto wake hapa hadi Kristo atakaporejea. Kisha nuru ndogo itafifia tutakaposimama katika nuru ya utukufu wa Uwepo wake kwa mara nyingine tena ili kuona na kushiriki pamoja na Mungu uso kwa uso katika utukufu wake wote!

# 21 - Jumbe Toka Mbali Kupita Nyota


139

Miaka kadhaa iliyopita, katika jangwa kubwa la Bechuana, la Afrika ya kusini aliishi mmojawapo kati ya watu waishio porini aliyeitwa Sukuba. Aliishi maisha ya upweke kama mmojawapo katika kabila la watu walio hama hama. Usiku mmoja wakati wa majira ya baridi alijikokota na kuingia katika kibanda chake akijiandaa kulala. Lakini ghafla usiku ukawa na nuru kuliko mchana. Kulitokea kama mtu aliyeng'aa ambaye alimwambia kuwatafuta watu wa Kitabu.

Lazima atafute watu waliomwabudu Mungu. Sukuba hakuwa na hakika ujumbe huu ulimaanisha nini. Kitabu gani? Angelikisomaje kama angekipata? Lugha ya huyu mtu wa porini ilikuwa na sauti kama 'gh' na zenye vidoko tofauti na lugha nyingine za kiafrika. Haijawezekana kuiweka lugha hii katika maandishi. Lakini huyu aliyeng'aa, kama jinsi Sukuba alivyomuita malaika aliyemtokea, alikuwa amemwambia, Kitabu kinanena. Utaweza kukisoma. Sukuba alisafiri kwa siku kadhaa pamoja na familia yake katika kukitafuta Kitabu. Alifika katika kibanda cha wakulima wa ki bantu na akauliza kama walifahamu watu wenye Kitabu.

Huyu mbantu aliyeulizwa alishangaa kumsikia huyu mtu wa porini akinena kwa namna fulani lugha ya kibantu. Mara moja alimchukua Sukuba na kumpeleka kwa mchungaji wake. Mchungaji aliguswa sana na kisa cha Sukuba. Akasema, Safari yako imefikia mwisho. Sukuba alifurahi sana. Lakini usiku ule yule 'Mwenye Kung'aa' alimtokea tena. Alimwambia kwamba hawa hawakuwa watu aliokuwa anawatafuta.

Sharti atafute kanisa linalotunza Sabato na mchungaji Moye. Mchungaji Moye angekuwa na Kitabu na pia vitabu vya kijani vinne ambavyo kwa hakika ni tisa. Siku iliyofuata Sukuba aliomba kwa ajili ya ishara. Alihitaji maelekezo ya njia kwa ajili ya safari yake. Alipoomba wingu likatokea angani. Sukuba alitembea kulifuata na akalielekea kwa siku saba. Lilitoweka juu ya kijiji kimoja. Hapa Sukuba

akaulizia juu ya Mchungaji Moye na upesi alielekezwa kwa nyumba yake.

Baada ya Sukuba kueleza kisa chake katika lugha yake, Mchungaji Moye aliitoa Biblia yake iliyokuwa imezeeka. Ndicho hicho! Sukuba lisema kwa sauti kubwa. Ndicho hicho! Lakini viko wapi vitabu vinne, ambavyo kwa hakika ni tisa?

Naam, kama ilivyokuja kuonekana, Ellen White miaka kadhaa iliyopita, alikuwa ameandika vitabu (Magombo) tisa ya maelekezo kwa kanisa la Mungu vilivyoitwa Shuhuda kwa Kanisa. Na hivi baadaye viliuganishwa na kuwa vitabu vinne. Utafiti wa Sukuba ukawa umefikia kilele. Alikuwa amewapata watu wa Kitabu. Alikuwa amewapata watu watunzao Sabato, watu waliobarikiwa na karama ya unabii. Hatimaye yeye pamoja na familia yake walimkubali Kristo na kubatizwa. Akawa mmishenari kwa watu wa kabila lake. Mungu anatenda kazi yake kwa njia za kushangaza leo katika kuwaongoza wanaume kwa wanawake kwa kanisa lake la kweli. Ukweli ya kwamba unasikia kisa hiki si ajali. Kama Sukuba, wewe pia unaongozwa. Mungu anakuongoza katika kweli yake. Mungu anakupatia wewe ujasiri wa kuukabili wakati ujao.

Pengine umekuwa ukiutafuta ukweli kwa miaka mingi. Nina amini utafiti wako umefikia kilele chake. Umeongozwa na mbingu hadi kufikia katika mahali hapa. Wewe kama Sukuba, waweza kutamka kwa sauti, Hili ndilo! Kanisa la Mungu!'

Je, hutaki kujiunga na wale wanaotunza amri za Mungu na kuwa na imani ya Yesu? Je, hutaki kujiunga na watu wa Mungu wa wakati wa mwisho? Tafakari ahadi hii kwa makini.

Yawezekana ikawa ni uamuzi wa muhimu zaidi wa maisha yako.

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana



1

Unawezaje  Kulipata  Kanisa la Kweli?



2

Je, umepata kujiuliza kwa nini kuna makanisa mbalimbali mengi hivyo? Mtu wa kawaida huchanganyikiwa. Makanisa mengi hufundisha ya kwamba ndiyo pekee yaliyo na ukweli.
Je, umepata kujiuliza kwamba ni kanisa gani kwa hakika linalofundisha na kuamini ukweli juu ya Mungu?



3

Rafiki, Biblia inayo majibu kwa ajili yetu.
Katika dunia ya mchanganyiko, Neno la Mungu laweza kuaminiwa daima katika kutofautisha kati ya kweli na uongo!



4

Kwa hiyo somo letu wakati huu ni Kwa nini kuna makanisa tofauti tofauti mengi hivi?



5

(Fungu: Amosi 3:7)
Hakika Bwana MUNGU hatafanya neno lo lote, Biblia yasema, Bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake.
Amosi 3:7.



6

Hebu tuelekee kwa neno la Mungu. Kumbuka ya kwamba haidhuru ninawaza nini. Jambo la muhimu tu ni kama lipo katika  Biblia.
Kama lipo katika Biblia, liamini.
Kama halipo katika Biblia, hilo si langu!



7

Kwa kuanza somo letu, hebu tuanze na kitabu cha mwisho cha Biblia - Ufunuo.
Ufunuo, sura ya sita, inanena juu ya wapanda farasi wanne.

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana



8

Hawa wapanda farasi wanne wanawakilisha vipindi tofauti tofauti vya wakati katika historia ya kanisa la Kikristo. Katika vipindi hivi vya wakati, tunaona maendeleo ya makanisa tofauti tulio nayo leo.



9

(Fungu: Ufunuo 6:1)
Kisha nikaona hapo Mwana -Kondoo alipofungua moja ya  zile muhuri saba,



10

nikasikia mmoja wa wale wenye uhai wanne akisema, kama kwa sauti ya ngurumo, 'Njoo!' Ufunuo 6:1.
Historia ya Ukristo sasa inafunuliwa hapa katika sura ya sita.



11

(Fungu: Ufunuo 6:2)
Nikaona, na tazama, farasi mweupe, na yeye aliyempanda ana uta, akapewa taji,



12

ali akishinda tena apate kushinda.
Ufunuo 6:2.


13

Hivyo kanisa la  kwanza ni kanisa la imani inayoshinda. NI farasi mweupe.
Weupe huwakilisha imani safi.


14

Ungelikuwa wakati wa kufurahisha katika ile karne ya kwanza mara baada ya kupaa kwa Yesu.

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana


15

Wanafunzi walikuwa wamejazwa na ujasiri mwingi sana na imani nyingi sana, kwa sababu walikuwa wametembea na kuzungumza na Yesu.
Walikuwa wamemwona akifufuliwa.
Walikuwa wamemwona akipaa kwenda mbinguni.
Walikuwa wamemwona akirejea.
Walikuwa wameamini ahadi zake kwa mioyo yao yote.


16

Walishiriki habari njema, injili, wakiwa na ujasiri mwingi na shauku, kwa ulimwengu mzima.



17

(Fungu: Wakolosai 1:21 -23)
Kwa kweli, habari njema ya wokovu ilihubiriwa kwa kila sehemu ya ulimwengu wa wakati ule. Paulo anasema,
Na ninyi, mliokuwa hapo kwanza mmefarikishwa , tena adui katika nia zenu, kwa matendo yenu mabaya,



18

amewapatanisha sasa,



19

katika mwili wa nyama yake, kwa kufa kwake, ili awalete ninyi mbele zake, watakatifu,



20

wasio na mawaa wala lawama.

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana



21

mkidumu  tu katika ile imani, hali mmewekwa juu ya msingi, mkawa imara;



22

msipogeuzwa  na kuliacha tumaini la Injili mliyoisikia habari zake,



23

ambayo mimi Paulo nalikuwa mhudumu wake.
Wakolosai 1:21 - 23.



24

(Fungu: Matendo 5:14)
Walioamini wakazidi kuongezeka kwa
Bwana, wengi, wanaume na  wanawake.
Matendo 5:14.
Kitabu cha Matendo kinatuambia ya kwamba maelfu walibatizwa kila siku.



25

(Fungu: Matendo 2: 47)
Walioamini wakazidi kuongezeka kwa
Bwana, wengi, wanaume na  wanawake.
Matendo 5:14.
Kanisa lilikuwa ni mwili wa Kristo.


26

Watu walibatizwa kwa Yesu.
Walibatizwa na kuingia katika mwili wake, ambao ulikuwa kanisa.
Ilikuwa ni muhimu sana kwa wanafunzi wa awali kuwa waaminifu kwa Yesu.
Wakati wanafunzi walipoonywa wasifundishe katika jina la Yesu, Biblia yasema:

# 22 - CHAGUZI NI NYINGI SANA



27


(Fungu: Matendo 5:29)
Petro na mitume wakajibu, wakisema, 'Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu.' Matendo 5:29.
Ilikuwa muhimu zaidi kutenda kile alichokisema Mungu, unaona? Kuliko kufuata mapokeo ya wanadamu.


28

Hivyo walikuwa na imani safi, kwa sababu walipata kuwa na Yesu.
Waliamini kile Yesu alichokisema.
Waliamini kile alichokiamini Yesu.
Walifundisha alichokifundisha Yesu.


29

Hiyo ndiyo aina ya imani tunayoihitaji leo - isiyochanganya, imani safi inayotizama mbele kwa marejeo ya Kristo.
Imani inayotizamia habari njema za wokovu kwa marafiki zetu wote na majirani- kwa ulimwengu mzima - ili kutimiza utume mkuu aliotupatia Yesu.
Hiyo ni imani safi.
Hiyo ni imani ya waumini wa kanisa la karne ya kwanza.



30

Kanisa la kwanza lililoshinda kiimani liliwakilishwa na farasi mweupe.
Kipindi hiki kiliishia mwaka wa 100 BK.


31

Je, Yohana aliona nini wakati Yesu alipofungua muhuri wa pili?



32

(Fungu: Ufunuo 6:4)
Akatoka farasi mwingine, mwekundu sana, na yeye aliyempanda alipewa kuiondoa amani katika nchi,

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana



33

ili watu wauane, naye akapewa upanga mkubwa.
Ufunuo 6:4.
Hivyo hapa tumewakilisha imani iliyotiwa damu.


34

Tunajua ya kwamba baada ya mwaka 100 BK, Wakristo walisombwa hadi Rumi, ambapo waliuawa, na wengi wao walifanywa kuwa chakula cha simba katika viwanja vikubwa vya maonyesho na michezo katika Himaya ya Kirumi.



35

Ulikuwa wakati mbaya kiasi gani kwa kanisa la Kikristo! Lakini bado, kanisa liliendelea kukua.Mwana historia mmoja wa wakati ule alisema ilionekana damu ya Wakristo ilikuwa kama mbegu. Watu walipoendelea kuuawa na kutoa maisha yao kwa Yesu, ilionekana kama mbegu iliyokuwa ikipandwa, na wengi zaidi waliinuliwa ili kuchukua mahali pao.
Habari njema ya wokovu ilienea katika Ufalme wote wa Kirumi na katika sehemu zingine zote zilizojulikana za ulimwengu wa wakati ule.




36

Kwa hivyo farasi mwekundu huwakilisha imani iliyotiwa damu. Muhuri wa pili ni kanisa la Kikristo lililokuwepo tangu mwaka 100 BK hadi 323 BK.



37

(Fungu: Ufunuo 6:5)
Hivyo Yesu alifungua muhuri wa tatu -- kipindi cha tatu cha kanisa la Kikristo.
Na alipoifungua muhuri ya tatu, nikamsikia yule wa tatu mwenye uhai akisema, 'Njoo!....'



38

Nikaona, na tazama, farasi mweusi, na yeye aliyempanda ana mizani mkononi mwake.
Ufunuo 6:5.

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana


39

Huyu farasi mweusi anawakilisha imani iliyouzwa.




40

(Fungu: Matendo 20:29,30)
Najua mimi ya kuwa baada ya kuondoka kwangu mbwa mwitu wakali wataingia kwenu, walisilihurumie kundi.



41

tena katika ninyi wenyewe watainuka watu wakisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao. Matendo 20:29,30. Huu ni wakati wa kusikitisha sana kwa kanisa la Kikristo.


42

Huu ni wakati wa imani iliyouzwa - wakati upagani unapoungana na Ukristo.
Danieli alitabiri hili.



43

(Fungu: Danieli 8: 12)
Na jeshi likatolewa kwake pamoja na sadaka ya kuteketezwa ya daima,



44

nayo ikaiangusha kweli hata chini; ikatenda ilivyopenda na kufanikiwa.
Danieli 8:12.


45

Ukweli wa kwanza wa muhimu uliopotea katika kipindi hiki ulikuwa wa wokovu kwa imani pekee katika Yesu.
Wokovu kupitia kwa Kristo uliondolewa na badala yake kukawa na matakwa ya kanisa.

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana



46

Kama utakumbuka kama tulivyojifunza kabla, wokovu, kulingana na Biblia, ni karama ya bure. Hii ni karama, kwa sababu sisi sote tumetenda dhambi, na hatustahili kabisa. Tunastahili kufa, kwa sababu mshahara wa dhambi ni mauti.
Lakini karama ya Mungu ni uzima wa milele.



47

Tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu. Hiyo ni injili isiyochanganya.



48

Ili kupokea karama ya bure, yote tunayohitaji kutenda ni kumwalika Yesu katika mioyo yetu.



49

Kisha hutusamehe dhambi zetu zote.



50

Na pili, Atatupatia uwezo wa kuacha dhambi. Atatupatia uwezo wa kutembea katika hatua zake.


51

Lakini huu ukweli ulio wazi wa wokovu, hii injili isiyochanganya kama ilivyo katika Yesu, katika kipindi hiki wakati imani ilipouzwa, ilibadilishwa na badala yake kuwekwa matakwa ya kanisa.


52

Badala ya kukabili kwa ujasiri kiti cha enzi cha Mungu, kwa kupokea neema yake na msamaha, badala ya kuungama dhambi kama jinsi Biblia isemavyo jinsi ya kutenda,  Wakristo waliambiwa ya kwamba walihitaji kulipa ili dhambi zao zisamehewe.

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana



53

(Fungu: 1 Yohana 1:9)
Lakini Biblia yasema, Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.


54


Wakristo waliambiwa ya kwamba walikuwa waende kwa padri. Walikuwa waende kwa mtu.
Hawangeweza tena kwenda kwa ujasiri mbele za kiti cha enzi cha Mungu.
Wokovu ulifanywa kuwa mgumu zaidi.
Na watu walikubali uuzaji huu wa imani, kwa sababu hawakuwa na Maneno ya Mungu.


55

Ilikuwa ni kinyume cha sheria, kwa kweli, katika kipindi hiki kwa wao kuwa na Neno la Mungu. Nyumba na mashine kubwa za uchapaji zilikuwa hazijavumbuliwa bado, hivyo ilikuwa vigumu kupata hata kisehemu kidogo cha maandiko. Watu wengi walikubali kile kanisa lilichowaambia, na imani ya Kikristo ikachafuliwa.


56

Ilikuwa ni kinyume cha sheria, kwa kweli, katika kipindi hiki kwa wao kuwa na Neno la Mungu. Nyumba na mashine kubwa za uchapaji zilikuwa hazijavumbuliwa bado, hivyo ilikuwa vigumu kupata hata kisehemu kidogo cha maandiko. Watu wengi walikubali kile kanisa lilichowaambia, na imani ya Kikristo ikachafuliwa.



57

(Fungu: Kutoka 20:4,5)
Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni,



58

wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia.

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana



59

Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu;



60

nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao,
Kutoka 20:4,5.


61

Huu ndio wakati ambapo sanamu ziliingia kanisani. Amri kumi zilikuwa zimeweka wazi kabisa ya kwamba ilikuwa si sahihi kuabudu kitu kingine chochote isipokuwa Mungu Peke Yake.


62

Ukweli wa tatu wa Biblia uliouzwa wakati huu ulihusiana na amri ya nne na siku ya ibada. Tambua jinsi Biblia isemavyo juu ya Danieli na jinsi alivyoliona hili:



63

(Fungu: Danieli 7:15)
Basi, mimi Danieli, roho yangu ilihuzunika mwilini mwangu, na hayo maono ya kichwa changu yakanifadhaisha.
Danieli 7:15.


64

Umeona jinsi ambavyo Konstantine alisimika sheria ya kwanza ya Jumapili: kubadilishwa kwa siku ya ibada toka Sabato ya siku ya saba hadi siku ya kwanza ya juma, Jumapili.




65

(Fungu: Yohana 14:15)
Lakini kumbuka, Yesu alisema,Mkinipenda, mtazishika amri zangu. Yohana 14:15.
Na bado katika kipindi hiki cha imani iliyouzwa, upendo kwa Yesu ulipoa, na watu wengi walifuata mapokeo badala ya kumfuata Mungu.

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana


66

Kanisa lilikubali mapatano kuhusu Sabato na likajaribu kuibadili siku ya ibada.
Tarehe 21 Mei, 1995, Gazeti la Sentinel la kanisa la Kikatoliki la Mtakatifu Catherine lilisema,



67

Pengine jambo la ujasiri zaidi, badiliko la kianamapinduzi lililokubwa lililowahi kutokea lilitokea katika karne ya kwanza. Siku takatifu,




68

Sabato, ilibadilishwa toka
siku ya Jumamosi kwenda siku
ya Jumapili....siyo kutokana
na maelekezo yoyote yaliyopo katika
Maandiko, lakini kutokana na hisia
ya kanisa ya mamlaka yake......




69

Watu wanaofikiria ya kwamba Maandiko yanapaswa kuwa mamlaka ya pekee, wanapaswa kwa hekima wawe Waadventista wa Sabato na watunze siku ya Jumamosi kama takatifu.



70

Ibada Jumapili, siku ya kwanza ya juma, haipo katika Biblia. Wasomi katika dunia nzima hulikubali hilo!



71

Badiliko lililetwa kama ambavyo tumeona, na mfalme wa Himaya ya Kirumi, Konstantine, mwaka wa 320 BK, na kanisa lilikubali badiliko hili.


72

Rafiki zangu, kama tunataka kutenda jinsi Biblia isemavyo, na tuwe Waadventista wa Sabato! Katika kipindi hiki cha mapatano, siku ya kipagani ya jua iliwekwa badala ya Sabato Takatifu ya Biblia.

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana



73

Historia ya Kanisa la Mashariki, uk. 184, inasema,
Sarafu zake ( Konstantine)
zilikuwa na herufi katika
upande mmoja za jina la Kristo,
na upande mwingine,
sura ya mungu-mtu.....




74

kana kwamba hakuweza kuachilia mbali ufadhili wa ung'avu wa jua. Je, hili si jambo la kushangaza?


75

Mungu analiweka wazi kabisa katika amri zake:




76

(Fungu:Kutoka 20:11)
Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi na bahari na vyote vilivyomo,



77

akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya sabato akaitakasa.
Kutoka 20:11.


78

Mungu anaweka wazi ya kwamba anataka watu wake watunze siku ya saba kama Sabato takatifu.
Nyuma katika mwanzo kabisa, Biblia yasema,



79

(Fungu: Mwanzo 2:3)
Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana




80

kwa sababu katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kuifanya.
Mwanzo 2:3.



81

Kama Mungu Muumbaji



82

aliibariki siku,



83

kama aliiweka siku moja
pembeni,




84

kama aliifanya siku moja kuwa takatifu zaidi ya siku nyingine, hivyo rafiki zangu, mwanadamu hana haki, wala hana mamlaka ya kuibadili! Inakuwa ni swala la ibada, ni swala la utii kama ni kwamba tufuate mapokeo ya mwanadamu au tutende kile alichokisema Mungu.



85

Hiki basi ni kipindi cha imani iliyouzwa. Kipindi hiki cha kanisa kilikuwa kuanzia mwaka wa 323 BK hadi mwaka wa 536 BK.


86

Sasa tunakwenda kwa hatua ya nne ya Kanisa la Kikristo, ambayo ni farasi wa kijivu.

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana



87

(Fungu: Ufunuo 6:7,8)
Na alipoifungua muhuri ya nne, nikasikia sauti ya yule mwenye uhai wa nne akisema,
'Njoo!



88

Nikaona, na tazama, farasi wa rangi ya kijivujivu, na yeye aliyempanda jina lake ni Mauti, na Kuzimu akafuatana naye.



89

Nao wakapewa mamlaka juu ya robo ya nchi, waue kwa upanga




90

na kwa njaa na kwa tauni na kwa hayawani wa nchi.
Ufunuo 6:7,8.



91

Imani iliyokufa - muhuri wa nne.
Huu ulikuwa ni wakati wa muungano wa kanisa na serikali. Ufalme 'mtakatifu' wa Kirumi ulikuwa umeendelea kikamilifu sasa, na haikuwa tu ni serikali ya kidini bali pia ilikuwa ni serikali ya kisiasa.
Hapo tunaona muunganiko basi, wa kanisa na siasa.



92

Kwa ufupi angalia kauli hii: Ukristo ukawa ni dini iliyothibitishwa katika Ufalme wa Kirumi na kuchukua nafasi ya upagani.



93

Ukristo, kama jinsi ulivyokuwa wakati wa Zama za Giza, unaweza kuitwa 'upagani uliobatizwa'.
 - Historia ya Kanisa, Karne ya 2, sura ya 2, sehemu ya 7.

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana


94

Kumbuka, katika wakati huu watu hawakuwa na uhuru wa kusoma Neno la Mungu.
Ilikuwa kwa kweli kinyume na sheria, na kama tuivyosema, mashine za uchapaji zilikuwa hazijazinduliwa bado.


95

Watu walifuata mapokeo.
Walifuata upagani na sherehe ambazo zilikuwa zimeingia katika kanisa.
Hii ni kweli ya kihistoria ambayo ninaieleza.



96

Kanisa pekee lililoendelea kuwepo likawa la Kikatoliki.
Na tena, hii si ukosoaji wa mtu fulani mmoja mmoja - ni swala la mfumo !
Tunao watawa wengi wa Kikatoliki na mapadri na waumini wa Kikatoliki duniani ambao wanampenda Yesu sana na wanautafuta ukweli. Ni muhimu kuelewa kwa nini tupo pale tulipo sasa hivi.


97

Huu ulikuwa wakati mbaya sana wa mapatano, wakati wa kutisha wa uteswaji wa watu wa Mungu.



98

Hii ndiyo sababu kipindi hiki kinaitwa Zama za Giza.
Wakristo milioni hamsini waliuawa kwa sababu ya imani yao.



99

Tazama hapa hatua za mapatano:



100

mapokeo,

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana



101

toba,



102

na misamaha ikaingia katika kanisa.
Uliweza kulipa fedha na kulipa kwa ajili ya msamaha ili kama inavyosadikiwa, ndugu zako watoke katika pagatori, au ungeweza kujilipia mwenyewe, ili kwamba usiende pagatori unapokufa. Huu ni mfano tena wa upagani katika kanisa la Kikristo.



103

Hakuna katika Neno la Mungu kitu kama pagatori. Sanamu ziliingia katika kanisa - kama jinsi ilivyokuwa katika swala la madaraja kanisani na masharti ya kanisa.
Je ukweli wa Mungu ungeendelea kukanyagwa chini milele? Tunahoji. Hakika, la, kwa sababu nuru ya ukweli ingepenya katikati ya giza. Na hatua zingechukuliwa katika kuweka daraja la kuunganisha kweli zilizopotea katika Zama za Giza.



104

Wakati wa Matengenezo, imani safi ya Yesu ilianza kugunduliwa tena.


105

Waliokuwa wa kwanza kuchukua hatua katika Zama za Giza za miaka ya 1400 walikuwa ni Wawaldensia.


106

Waligundua tena Neno la Mungu, Biblia. Biblia ni muhimu sana. Kama tusingelikuwa na Neno la Mungu, kama tusingelikuwa na barua za upendo kwa ajili yetu tunazozipata katika Biblia, tusingelikuwa na mwelekeo katika maisha.

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana


107

Kule kaskazini mwa Italia, tunapata kisa cha wa - waldensia walioiamini Biblia.
Waldensia wangeliandika Maandiko kwa mkono na kutoa sehemu zake kwa watoto wao. Kwa kutumia mafungu haya yaliyoshonwa katika mavazi yao, watoto walifanikiwa kwenda katika majiji makubwa ya Ulaya. Walishiriki mafungu haya ya Biblia pamoja na marafiki zao waliowapata katika masoko na katika vyuo.


108

Hata hivyo, matokeo yake, kama walikamatwa, yalikuwa ni mazito-walichomwa wakiwa wamefungwa katika miti.
Ingawa wengi walipoteza maisha yao, Wawaldensia walitafakari kuwa ni upendeleo wa pekee kuwa katika hali hiyo ili kazi ya Mungu iendelee kuwa hai.


109

Baada ya Waldensia, alikuja mwanamatengenezo, mwanafunzi wa Biblia kule Prague aliyeitwa John Huss.
Huss, pamoja na rafiki yake Jerome, waligundua ya kwamba ilikuwa ni muhimu zaidi kumtii Mungu zaidi ya kutii kanisa au kutii mwanadamu.


110

Kwa sababu ya msimamo wao wa utii, wa kuamini ya kwamba tunapaswa kutenda  kile Mungu anachotuambia tukitende badala ya kufuata mapokeo ya kanisa, walichomwa hadi kufa,
Majivu yao yalitupwa katika mto uliotiririka kwenda katika Bahari ya Mediteranian.
Zaidi kwa namna iyo hiyo, Matengenezo yalitiririka toka katika chanzo chake hadi kwenda dunia nzima.


111

Baada ya Huss na Jerome kuchomwa hadi kufa, mtu mmoja wa Ujerumani aliyeitwa Martin Luther aliugundua ukweli wa Biblia wa wokovu kwa njia ya neema peke yake.

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana



112

Baadhi ya watu huuliza swali, Kwa nini Luther hakugundua kweli  zote zilizopotea wakati wa Zama za Giza?
Na Biblia inajibu,



113

(Fungu: Yohana 16:12)
Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi  kuyastahimili
hivi sasa.



114

Kupata tena kweli za Biblia zilizopotea kulichukua muda mrefu-ilikuwa ni hatua kwa hatua.
Ilichukua miaka mamia kwetu kupoteza imani ya Yesu nyakati za Zama za Giza.
Na ilinglichukua pia miaka mingine mingi tena kugundua tena kweli hizi.


115


Wakati Luther alipokufa, waumini wake walichukua kile alichokisema na kuunda kanisa la Kilutheri. Kwao, Matengenezo yalikomea katika kifo cha Luther.


116

Kutokea Ujerumani, tunasafiri hadi Geneva, Uswisi, na kumpata mwanafunzi wa Biblia aliyeitwa John Calvin ambaye,


117

katika majifunzo yake, aligundua ya kwamba Wakristo si tu kwamba hupokea neema na msamaha na kwamba wanapaswa kuja kwa ujasiri mbele za kiti cha rehema, bali pia , ni muhimu kwao kukua katika Kristo.


118

Hivyo Calvin alifundisha fundisho la ukuaji, ambalo wengine huliita  utakaso.
Tunapomkubali Yesu, anatupatia uwezo wa kushinda dhambi.

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana


119

Wakati John Calvin alipokufa, wafuasi wake walichukua kile alichokisema na kuunda kanisa la Kipresbyterian.
Hivyo ukweli, unaona, tangu ulipopotea katika Zama za Giza, uliendelea kuvumbuliwa tena.


120

Baada ya wakati wa Calvin, kulikuwa na kundi la Wakristo katika sehemu mbalimbali za Ulaya kaskazini waliojifunza Biblia zao na kufikia hitimisho ya kwamba badala ya kunyunyiziwa kama watoto,


121

ubatizo unapaswa kufuata mfano wa Yesu, kwa huwo kuwa uamuzi wa mtu pekee na kutendwa kwa njia ya kuzamisha.
Waliitwa Wa -Anabaptist.


122

Ubatizo kwa njia ya kuzamisha - kuwekwa moja kwa moja ndani ya maji kama Yesu alivyofanya ulikuwa ni ukweli wa muhimu sana uliokuwa umepotea wakati wa Zama za Giza, kama ambavyo unawakilisha kifo katika dhambi na kuwa hai katika Mungu.



123

(Fungu: Warumi 6:3,4)
Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake?



124

Basi tulizikwa  pamoja naye  kwa njia ya ubatizo katika  mauti yake,



125

kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.
Warumi 6:3,4.

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana



126

Na ili kubatizwa kama Yesu alivyobatizwa,




127

tunapaswa kujifunza juu yake,



128

tuungame dhambi
zetu,



129

na tumkubali Yesu kama Mwokozi wetu.
Wengi wa wa-Anabaptisti walipoteza maisha yao, kwa sababu waliamini ya kwamba wana paswa kutembea katika nyayo za Yesu na kubatizwa kama Yeye alivyobatizwa.


130

Kutokea katika mwanzo huu mnyenyekevu, kanisa la Kibaptist liliundwa.



131

(Fungu: Mathayo 28:18,19)
Yesu akaja kwao akasema nao, akawaambia, 'Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.



132

Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi,



133

mkiwabatiza kwa jina la Baba na Mwana, na Roho Mtakatifu'.
Mathayo 28:18,19.

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana


134

Yesu alitoa agizo kwa kanisa Lake kuwa liende na kufundisha na kubatiza na kufanya watu kuwa wanafunzi.
Wa baptisti wa matengenezo walikuwa wakifuata na kutimiza agizo, kama tutendavyo leo!


135


Unaona, kila mmoja wa hawa wana matengenezo alikuwa akivumbua upya kweli ambazo zilikuwa zimepotea wakati wa Zama za Giza.
Walipogundua upya kweli hizi, wafuasi wao waliungana pamoja katika kile kilichokuja kufahamika baadaye kama madhehebu ya Kiprotestanti kama vile Walutheri, Wapresbyterian, na Wabaptisti.


136

Hatimaye, kule Uingereza, mtu aliyeitwa John Wesley alianza kujifunza Biblia yake.


137

Ndugu yake, Charles, aliandika nyimbo nzuri sana juu ya Yesu, na walihisi ni bora ziimbwe kanisani.Waligundua pia ya kwamba haikuwa tu muhimu kukubali karama ya bure ya wokovu, kuwa watii kwa Mungu, na kubatizwa na kukua katika neema, lakini hali msingi umewekwa katika Neno la Mungu, waligundua kwamba ni muhimu kuwa watakatifu.
John Wesley alikuwa mwanamatengenezo mkuu, na mara alipokufa, wafuasi wake walichukua kile ambacho yeye na wana matengenezo wengine walichokifundisha na kuunda kanisa la Kimethodisti.



138

Kisha katika sehemu mbalimbali za dunia kama vile Amerika ya kusini, Ulaya, na Amerika ya Kaskazini, watu walianza kujifunza kuhusu kuja kwa mara ya pili kwa Yesu.

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana


139

Mtu aliyeitwa William Miller, wa Amerika ya Kaskazini, alijifunza juu ya ahadi za Yesu za Yohana 14. Alijifunza pia unabii wa Danieli na Ufunuo, na alielewa ya kwamba Yesu alikuwa anakuja upesi sana.




140

Hivyo katika msingi wa



141

Wawaldensia walifundisha juu ya Biblia,




142

Kile ambacho Huss alikifundisha juu ya utii,




143

kile Luther alichofundisha juu ya neema,



144

kile Calvin alichofundisha juu ya utakaso au ukuaji,



145

kile Waanabaptisti walichofundisha juu ya ubatizo,

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana



146

na wakati Wesley alipofundisha juu ya utakatifu, Miller aliongezea katika haya fundisho lingine muhimu sana: ukaribu wa kuja kwa mara ya pili kwa Kristo.



147

Baada ya wakati wa Miller, msukumo wa kiadventista uliendelea.
Rafiki zake pia waligundua ya kwamba wakati watu wanapokufa wakimwamini Yesu, hulala katika Yesu, wakisubiri ufufuo. Kama Biblia ifundishavyo wazi, tunalala hadi wakati ule wa ufufuo tutakapoitwa tutoke katika kaburi.
Itakuwa asubuhi njema kiasi gani kuunganishwa na wapendwa!




148

Waadventista wa awali waligundua toka kwenye Biblia:




149

1. Mauti ni usingizi.



150

2. Yesu anakuja.



151

3. Atawafufua wafu wakati wa ufufuo:

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana



152

(Fungu: 1 Wathesalonike 4:16)
Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu,na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza.
1 Wathesalonike 4:16.



153

(Fungu: Yohana 14:15)
Baada ya wakati wa William Miller, waumini katika kuja kwa Yesu mara ya pili wao pia waligundua maneno  Yesu  yaliyomo katika Yohana 14:15: Mkinipenda, mtazishika amri zangu.
Unaona, sisi sote tunapaswa tutake kuwa na uhusiano wa upendo na Yesu. Kwa sababu tunampenda, tunataka kutunza amri zake zote. Siyo tu baadhi ya hizo, bali kila moja ya hizo.



154

(Fungu: Mathayo 15:9)
Tazama kile Yesu alichokisema katika Mathayo 15:9; Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.
Ni kweli kiasi gani hiyo leo.
Watu hufundisha mafundisho na amri za wanadamu.



155

Lakini haijali watu wanasema nini. Lililo la muhimu ni lile Mungu analolisema.



156

Tunapofikia katika swala la ibada, lazima tumwabudu Mungu katika siku ya Sabato ambayo ameiweka pembeni kwa ajili yetu. Ni siku  ya  pekee ambayo ametupatia. Kama jinsi mafundisho haya ya pekee  yalivyogunduliwa  katika Biblia, watu wajifunzao kweli hizi  hatimaye waliunganika pamoja na kuunda kanisa la Waadventista wa Sabato. Isaya 58:13 na 14 ilitabiri ya kwamba kungekuwa na msukumo kwa ajili ya kukarabati ufa uliojengeka katika sheria ya Mungu. Fungu hili hunena juu ya siku ya pekee:

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana




157

(Fungu: Isaya 58:13,14)
Kama ukiugeuza mguu wako usihalifu sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu wangu,



158

ukiita sabato siku ya furaha, na siku takatifu ya BWANA yenye heshima; ukiitukuza,




159

kwa kutokuzifanya njia zako mwenyewe; wala kuyatafuta yakupendezayo,wala kusema maneno yako mwenyewe;




160

ndipo utakapojifurahisha katika BWANA;




161

nami nitakupandisha mahali pa nchi palipoinuka;



162

nitakulisha urithi wa Yakobo baba yako; kwa maana kinywa cha BWANA kimenena hayo.


163

Bwana anatuambia wazi kabisa ya kwamba hatupaswi kufanya kazi katika siku hiyo. Hatupaswi kufanya biashara katika siku hiyo. Hatupaswi kutafuta anasa zetu wenyewe katika siku hiyo.

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana


164

Ni siku takatifu.
Tunapomuweka Mungu kuwa wa kwanza katika Sabato, uzoefu wetu utakuwa wa kupendeza. Sabato inakuwa ya kusisimua.
Mungu hachukui toka kwetu-Yeye anatupatia mbaraka wa pekee. Ni kama siku ya malipo.
Anasema atasababisha tuweze kutembea katika mahali palipo inuka pa dunia. Ni mbaraka kiasi gani atatupatia kama tutamuweka kuwa wa kwanza na bora kuliko vyote katika maisha yetu -kama tukimfuata na kutunza Sabato kama atuombavyo.



165

Hivyo kwa kila kweli ambayo Mungu ametufundisha katika Biblia, Shetani ametengeneza bandia yake - uigizaji wa uongo.


166

Mungu anasema tunapokufa, tunalala katika kaburi. Bandia ya Shetani ni kwamba tunakwenda mbinguni au jehanamu au pagatori tunapokufa.


167

Mungu anasema ubatizo ni kwa njia ya kuzamisha.
Shetani anasema yawezekana kwa njia ya kunyunyizia.
Mungu alitupatia kweli yake kuhusu afya.
Shetani anasema sheria za afya zilitufutwa.
Kwa kila kweli ipo bandia yake.
Na hilo hutengeneza mchanganyiko.



168

(Fungu: Ufunuo 18:2)
Kitabu cha Ufunuo kinanena kuhusu hilo: Akalia kwa sauti kuu, akisema, 'Umenguka, umeanguka Babeli ule ulio mkuu,

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana



169

umekuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu, na ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza!'
Ufunuo 18:2.
Babeli, katika unabii, humaanisha machafuko ya kidini. Na tizama mwito uliowekwa hapa.



170

(Fungu: Ufunuo 18:4)
Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, 'Tokeni kwake, enyi watu wangu,



171

msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake.'
Ufunuo 18:4.



172

Mungu anaita watu wake watoke katika machafuko, ili wasiwe washiriki katika dhambi zake.
Rafiki zangu, Yesu anakuta wewe sasa.
Sasa ndiwo wakati wa kusimama kwa ajili ya Yesu!



173

(Fungu: Matendo 2:47)
Tazama Neno la Mungu: Wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku
kwa wale waliokuwa wakiokolewa.



174


(Fungu: 1Wakorintho 12:13)
Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru;



175

nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja.
1 Wakorintho 12:13.

# 22 - Chaguzi ni Nyingi Sana



176

(Fungu: 1 Wakorintho 1:18)
Kwa sababu neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuzi,



177

bali kwetu  sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu.
1 Wakorintho 1:18.


178

Tunaitwa tutoke katika Babeli ili tutende yaliyo sahihi. Je, humpendi Yesu wako?
Anarudi upesi sana kutuchukua kwenda nyumbani kwetu mbinguni ambako amepaandaa kwa ajili yetu sasa.
Je, hupendi kumfuata njia yote?
Kama jinsi ambavyo usiku wa leo, ni wazi kuona ya kwamba Yesu kupitia katika maisha yake na mafundisho yake alifunua kweli yake aliyokusudia ya kwamba ijulikane kwa wafuasi wake na waifuate.
Tumegundua ni nani anayefanya vita dhidi ya kweli na kanisa la Kristo, akitesa, akichanganya, na kuweka bandia ya ile kweli ambayo Kristo amelipa kanisa.
Tumeona katika majifunzo yetu ya Biblia na historia ya kwamba Kristo anawaongoza watu wake warejee katika kweli ambayo hapo mwanzo alilipa kanisa Lake.
Anawaita watu watoke katika machafuko ya kidini na kuingia katika kweli iliyofunuliwa katika kazi yake takatifu.
Je, hungependa sasa hivi, kuitikia malaika zake wanaoita .. tokeni kati yake enyi watu Wangu! Je, hutaki sasa hivi kuwa sehemu ya kanisa la Mungu, ...Linalozishika amri za Mungu na kuwa na imani ya Yesu?

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.



1

Jinsi ya Kuepuka Mapigo 7 ya Mwisho.


2

Mahali palikuwa Misri -  taifa lililokuwa limeendelea sana wakati huo. Mwaka - 1445 K.K. Kwa miaka 215 wana wa Israeli walikuwa wameishi pale karne ya mwisho katika utumwa mchungu. Mafarao waliokuwa marafiki waliokuwa wamemjua na kumpenda Yusufu walikuwa wameshapita na kuingia katika makaburi yao kitambo.



3

Watawala wapya walitizama wana wa Israeli waliokuwa wakiongezeka kwa kasi kama tishio kwa usalama wa taifa, wakihofu ya kwamba katika tukio la vita, Wana wa Israeli wataunganisha nguvu zao na maadui wa Misri. Hivyo wana wa Israeli waliwekwa katika utumwa, wakalazimishwa kuwa watumwa chini ya ukatili wa Wamisri.




4

Lakini, Biblia yasema, Lakini kwa kadiri walivyowatesa,



5

ndivyo walivyozidi kuongezeka na kuzidi kuenea. Kutoka 1:12.



6


...Wana wa Israeli wakaugua kwa sababu ya ule utumwa,



7

wakalia; kilio chao kikafika juu kwa Mungu kwa sababu ya ule utumwa.

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.



8

Mungu akasikia kuugua kwao, Mungu akakumbuka agano lake alilolifanya na Ibrahimu na Isaka na Yakobo. Kutoka 2:23,24.


9

Ilikuwa ni zaidi ya miaka 400 tangu Mungu alipofanya agano na Ibrahimu kuhusu vizazi vyake na ukombozi wao. Sasa, hatimaye, siku ilikuwa imekuja. Mungu alikuwa tayari, na mkombozi wake alikuwa tayari!


10

Walikutana --Mungu na Musa. Siyo katika Ikulu, wala siyo katika kivuli cha ihramu kubwa, lakini nje katika jangwa la Midiani kando ya kichaka kilichokuwa kikiwaka moto.




11

BWANA akasema, 'Hakika nimeyaona mateso ya watu wangu walioko Misri,




12

nami nimesikia kilio chao  kwa sababu ya wasimamizi wao; maana nayajua maumivu yao.



13

nami nimeshuka ili niwaokoe..... Kutoka 3:7,8. Akinena na Musa, Mungu alisema:



14

Haya, basi, nitakutuma kwa Farao,



15

ili upate kuwaokoa watu wangu, hao wana wa Israeli, katika Misri. Kutoka 3:10.

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.


16

Ilikuwa miaka arobaini tangu Musa alipoondoka Ikulu pale Misri. Miaka arobaini tangu aliponena lugha ya Kimisri! Kwa kweli, kwa kipindi chote kile, alikuwa amechunga kondoo nje katika jangwa pweke. Ile hali ya kujiamini binafsi aliyokuwa nayo akiwa kama mwana wa mfalme kule katika baraza la Misri, ilikuwa imepotea. Biblia yasema,



17

MUSA alifundishwa mambo yote ya hekima ya Wamisri akawa mashuhuri kwa maneno na matendo. (Matendo 7:22 HNKK)


18

Lakini katika jangwa, Musa alijifunza zaidi ya unyenyekevu. Kwa kuwachunga kondoo, alijifunza uvumilivu na uungwana. Sasa Mungu aliona ya kwamba Musa alikuwa tayari kuwakomboa Israeli na kutumia kuwaangalia kama baba watu wake.
Kwa unyenyekevu Musa alitii maelekezo ya Mungu na kukubali kile ambacho kwa wakati ule kilionekana kuwa kazi isiyowezekana.


19

Kwa kumsaidia Musa akamilishe hii kaziya ajabu, Mungu alimuelekeza Haruni, kaka yake Musa (ambaye aliwahi kuwa mtumwa Misri),kutoka na kwenda kukutana na Musa. Si tu kwamba Haruni alikuwa amuunge mkono Musa kwa kuwepo kwake pamoja naye, lakini Mungu alimteua Haruni kuwa mzungumzaji wa Musa, kwani Musa pia alikuwa hajatumia lugha ya Kimisri kwa miaka mingi.

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.


20

Hawa ndugu wawili waliingia Ikulu ya Farao wakidai kuwa mabalozi waliotumwa na Mungu. Walinena katika Jina lake na kutaja uwezo wake. Mtizamo wa mtawala huyu mwenye kiburi lazima ulikuwa wa pekee kwa muda mfupi. Mbele yake walisimama ndugu wawili, mmoja akiwa mchungaji mnyenyekevu wa ki Midiani, aliyekuwa bado akitembelea fimbo ya kichungaji, na mwingine Muebrania mtumwa aliyetoka katika mazingira ya kawaida pale. Wote wawili walikuwa wakitangaza uwezo mkuu wa Mungu waliyekuwa wakimtumikia. Wakati Haruni aliposema ya kwamba walikuwa wamekuja na ujumbe toka kwa Bwana uliomuomba Farao kuacha watu waende, Farao alikoroma kwa ghadhabu:



21

'BWANA ni nani, hata niiisikilize sauti yake, na kuwapa Israeli ruhusa waende zao?



22

Mimi simjui BWANA, wala sitawapa Israeli ruhusa waende zao.' Kutoka 5:2.
Hali akiwa na maelfu ya watumwa pamoja naye, Farao kwa uwazi hakuwa na makusudio ya kupoteza ule utumishi wa bure. Ombi la Haruni lilileteleza mwitikio mkali. Mfalme alizidisha mzigo wa kazi kwa Wana wa Israeli.


23

Lakini mara ile Mungu angemruhusu Farao mwenye kiburi kujua Bwana ni nani na jambo fulani kuhusu nguvu au uwezo wake. Farao alionywa na Musa na Haruni ya kwamba Mungu angetuma mapigo moja baada ya jingine juu ya Misri hadi watu wake watakapochiliwa toka utumwani. Halafu ujumbe wa Bwana kwa Farao ulikuwa:



24

Katika jambo hili utanijua ya kuwa mimi ndimi BWANA...
Kutoka 7:17.

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.


25

Haikuchukua muda hadi mapigo yalipoanza kuanguka. Kumi kwa uhakika! Kabla ya kila pigo kuanguka, Musa na Haruni walimuonya Farao juu ya hukumu iliyokuwa ije, wakitegemea angelichagua kuwaacha wana wa Israeli, hivyo ajiokoe mwenyewe na watu wake kutoka katika maafa. Lakini Farao alikuwa mkaidi akishupaa  katika njia yake ya mawazo. Na,  kwa  kulingana na ahadi Yake, misiba ya pekee ikawatembelea Wamisri.




26

Kwanza, Mto Naili, unaoabudiwa na Wamisri kama mmoja wa miungu yao, uligeuka damu wakati Haruni alipoyapiga maji kwa fimbo. Samaki wakafa, na maji mengine yote katika Miisri yakawa damu kwa siku saba. Lakini Farao alikataa kuwaachilia watu wa Mungu kwenda!



27

Kilichofuata, ni pigo la vyura ambavyo viliiathiri nchi. Mamilioni yao katika chakula, katika vitanda, kila mahali! Na bado, mfalme mkaidi alikataa kuwaacha Israeli waende.



28

Pigo la chawa lilifuatia. Lakini huyu mtawala katili asingekubali kuwaruhusu watu hawa waende. Tambua ya kwamba mapigo ya kwanza matatu yalianguka kwa Waebrania na Wamisri: hata hivyo, mapigo saba ya mwisho yalianguka tu kwa Wamisri.



29

Nami siku hiyo nitatenga nchi ya Gosheni, watu wangu wanayokaa, ili hao mainzi wasiwe huko,



30

ili kwamba upate kujua wewe ya kuwa mimi ndimi BWANA  kati ya dunia.

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.



31

Nami nitatia mpaka kati ya watu wangu na watu wako; ishara hiyo italetwa kesho. Kutoka 8:22,23.


32

Hatua iliyofuata ilikuwa ya pigo la inzi ambao walilijaza jumba la Farao.


33

Baada ya mainzi, pigo la kutisha kabisa liliikumba nchi, likiangamiza wanyama wote waliokuwa katika mashamba. Kufikia sasa, Farao alikuwa na mdadisi sana. Je, mifugo ya Waebrania iliangamia pia - au ililindwa kama jinsi Musa alivyotabiri?




34

Farao akatuma watu, na tazama hapana  mmoja aliyekufa katika wanyama wa wana wa Israeli.



35

Lakini moyo wa Farao ulikuwa mzito, wala hakuwapa hao watu ruhusa waende zao.
Kutoka 9:7.



36

Pigo la sita lilileta majipu juu ya wanyama na watu, lakini bado mfalme katili alikataa kuachilia wana wa Israeli.


37

Unabii uliofuata ulitabiri pigo la mvua ya mawe.

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.



38

Hata hivyo, Mungu aliahidi ya kwamba wote ambao wangejilinda, wao wenyewe na wanyama wao wasinge kufa. Habari ilienea kwa kasi sana katika Misri na Wamisri wengi walijificha, pamoja na wanyama wao. Mvua ya mawe ikaja, ikichanganyika na radi na ngurumo, na wote walioshindwa kujiandaa kwa ajili yake walikufa!



39

Wamisri waliona wazi ya kwamba dunia ilikuwa chini ya utawala wa Mungu aliyehai, na ya kwamba usalama wao pekee ulikuwa katika kumtii Yeye. Kwa muda mfupi, Farao kwa kweli alicheza cheza na wazo la kumtii Mungu na kuwaacha watu wale waende, lakini kadiri mapigo yalivyopungua, vivyo ndivyo na makusudio mazuri ya Farao yalivyokwisha.



40

Musa alimuonya Farao ya kwamba kama angekataa kuwaruhusu wana wa Israeli waende, pigo ambalo lingefuata lingekuwa la makundi ya nzige. Hali wakitishika kwa wazo la kuwa na mapigo zaidi, washauri wa Farao walimbembeleza ili awaache hawa watumwa waende, lakini mfalme bado alikataa.Na nzige wakaja kama walivyotabiriwa.


41

Kisha zikaja siku tatu za giza lililokuwa zito kiasi ambacho lilihisika, lakini Farao muasi aliendelea kumkaidi Mungu wa mbinguni.


42


Musa alitaja ya kwamba pigo moja zaidi lingemwagwa juu ya Wamisri - la mwisho ambalo lisingepaswa kudharauliwa kirahisi. Malaika mwangamizaji alikuwa apite katika nchi usiku wa manane na ange ua wazaliwa wa kwanza wote katika Misri - wote wa watu na wanyama.

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.




43

Kwa mara nyingine tena, Waebrania walikuwa waachwe, wasiguswe. Lakini safari hiii haikutosha kuwa Muebrania au kuishi Gosheni. Ili kuepuka ukumu ya kifo, kila familia iliagizwa kuchinja mwana - kondoo na kisha kunyunyiza sehemu ya damu yake katika miimo ya (milango) ya nyumba zao kama ishara ya imani yao na utii wao kwa Mungu. Na Mungu akaahidi:



44

Nami nitakapoiona ile damu, nitapita juu yenu;



45

lisiwapate pigo lolote likawaharibu, nitakapoipiga nchi ya Misri. Kutoka 12:13.


46

Ilikuwa picha ya kuvutia kiasi gani kuiangalia usiku ule! Maelfu ya familia za Waebrania na Wamisri wengi walisimama katika miimo ya milango ya nyumba zao wakitizama baba, hali akishikilia bakuli kubwa lenye damu mkono mmoja na kitawi cha hisopo katika mkono mwingine, akinyunyiza miimo ya mlango. Na mtu anaweza kufikiria ya kwamba kati ya watizamaji makini kabisa usiku huu walikuwa hawa wazaliwa wa kwanza.



47

Hata ikawa usiku wa manane BWANA akawapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri,



48

tangu mzaliwa wa kwanza wa Farao aliyeketi katika kiti chake cha enzi, hata mzaliwa wa kwanza wa mtu aliyefungwa katika nyumba ya wafungwa.

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.



49

na wazaliwa wa kwanza wote wa wanyama. Kutoka 12:29.


50

Hata hivyo, hakuna nyumba hata moja iliyokuwa na damu iliyopakwa katika miimo ya milango kwa kutii agizo la Mungu ambayo iliguswa na pigo.


51

Pote katika ufalme huu mkubwa wa Misri vilio vya waombolezaji vilisikika. Na kwa miguu inayotetemeka na neva zinazoduwaa, Farao alikumbuka jinsi alivyomdharau Mungu wa Waebrania na kuunguruma kwa kejeli:



52

...BWANA ni nani, hata niisikilize sauti yake, na kuwapa Israeli ruhusa waende zao? Kutoka 5:2. Sasa alijua. Kwa unyenyekevu, yeye pamoja na washauri wake waliwaita wale ndugu wawili wa Kiebrania na kuwasihi wawachukue wana wa Israeli na kuiacha nchi ya Misri kwa haraka, kwani waliogopa ya kwamba wao wote walikuwa wanakwenda kufa!



53

Ilipofika usiku wa maanane, watu wa Mungu-wale waliokuwa wamemchagua kama mkombozi wao-waliwekwa huru. Na kama jinsi Mungu alivyoamuru, walikuwa wamejiandaa kwa ajili ya wakati huu. Hali wakiwa wameshavaa viatu miguuni mwao na makoti katika migongo yao, walikuwa tayari kwa ajili kutoka kuliko kukuu. Walikuwa njiani mwao kuelekea katika Nchi ya Ahadi!


54

Naam, wasema, hicho ni kisa cha kuvutia, lakini ni cha muhimu vipi kwetu sisi tuishio katika karne ya ishirini? Chaweza kuonekana kana kwamba hakina umuhimu, lakini si hivyo. Kwa kweli chaweza kuwa cha muhimu sana.

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.


55

Unaona, katika Agano Jipya, tunakuta unabii wa kushangaza kabisa utoao kwa undani matukio ya mwisho yatakayotokea katika dunia. Unabii huu unaweka wazi kabisa ya kwamba, kwa mara nyingine tena, mapigo yataanguka - lakini katika kiasi kikubwa zaidi na cha kutisha.


56

Ndiyo, kulingana na unabii wa Biblia, historia itarudiwa. Siyo kwa mapigo kumi, lakini saba ambayo yataweka kilele cha ukombozi wa watu wa Mungu. Siyo kutoka Misri bali kutoka katika sayari iliyoasi.


57

Lakini, kama jinsi wana wa Israeli walivyovumilia katika kipindi cha mateso kabla ya ukombozi wao wa utukufu toka Misri na kushuhudia mapigo yakiwaangukia Wamisri,


58

Vivyo hivyo watu wa Mungu watashuhudia kumwagika kwa mapigo saba ya mwisho kwa waovu kabla ya kuja kwa Kristo.
Nabii Danieli anaelezea kipindi hiki cha taabu kwa namna hii:



59

Wakati huo Mikaeli atasimama, jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako;



60

na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lililopoanza kuwapo taifa hata wakati huo:



61

na wakati huo watu wako wataokolewa; kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile. Danieli 12:1

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.


62

Injili ya milele itakuwa imehubiriwa kwa dunia yote. Mwito wa malaika wa pili wa tokeni Babeli au kuonya juu ya mifumo ya uongo ya ibada itakuwa imetolewa. Na kwa kila mtu malaika wa tatu anasema:



63

Yeyote anayemwabudu yule mnyama na sanamu yake na kukubali kutiwa alama yake juu ya paji la uso wake au juu ya mkono wake, (Ufunuo 14:9 HNKK)



64

yeye mwenyewe atakunywa divai ya ghadhabu ya Mungu, .......... (Ufunuo 14:9,10)



65

Hili ndilo onyo la kutisha zaidi katika Biblia ambalo limewahi kutolewa kwa wanadamu. Lakini haitakuwa hivyo hadi maswala yamewekwa bayana mbele za wakazi wa dunia na kuletwa katika swala la uchaguzi kati ya amri za Mungu na amri za wanadamu, ndipo ye yote yule atapokea alama ya mnyama, au kunywa mvinyo ya ghadhabu ya Mungu.


66

Lakini hilo likikamilika, mlango wa rehema hufungwa daima kwa wanadamu wote.



67

(Ufunuo 22:11 HNKK)
Na tangazo la muhimu litawekwa:
Kwa sasa anayetenda mabaya na aendelee kutenda mabaya, na aliye mchafu aendelee kuwa mchafu.



68

Mwenye kutenda mema na azidi kutenda mema, na aliye mtakatifu na azidi kuwa mtakatifu. Ufunuo 22:11.

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.


69

Kazi ya Kristo kama Kuhani Mkuu mbinguni imemalizika. Kila kesi imeamuliwa kwa ajili ya uzima wa milele au kwa ajili ya mauti ya milele. Mlango wa rehema wa Mungu umefungwa! Sasa ni uzoefu wa yule mkaaji wa dunia  uitwao wakati wa taabu ulionenwa na nabii Danieli.


70

Na sikiliza, Rafiki, Mungu hatanyakua watu wake hadi mapigo yameisha. Watakuwa hapa hapa duniani hadi mwisho! Watalindwa wakati wa mapigo, kama jinsi ilivyokuwa kwa wana wa Israeli, lakini hawatakuwa huru na matatizo na taabu. Utakuwa wakati wa taabu kwa kila mmoja.



71

Na, Rafiki, maelezo yaliyo dhahiri zaidi ya kipindi hiki cha historia ya dunia hayawezi kufikia ukubwa wa ukweli wa mambo wenyewe, wakati waovu wakinywa kikombe cha ghadhabu ya Mungu isiyochanganyika na rehema.
Yohana alipewa picha ya mambo kabla; jinsi utakavyokuwa  wakati huu wa taabu kabla tu ya kurudi kwa Yesu na ukombozi wa watu wake.



72

(Ufunuo 15:1 HNKK)
Kisha nikaona ishara nyingine mbinguni, kubwa na ya kushangaza.



73

Palikuwa hapo malaika saba wenye mabaa makubwa saba ya mwisho. Kwa mabaa hayo makubwa saba, ghadhabu ya Mungu imekamilishwa. (Ufunuo 15:1)
Na tena Yohana aliandika:



74

Kisha nikasikia sauti kubwa kutoka Hekaluni ikiwaambia wale malaika saba, 'Nendeni mkamwage mabakuli hayo saba ya ghadhabu ya Mungu duniani.'

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.



75

mkamwage mabakuli hayo saba ya ghadhabu ya Mungu duniani.'  Ufunuo 16:1.




76

Lakini, unahoji, haya mapigo ya kutisha ni yapi ambayo yanapaswa kumwagwa na malaika saba juu ya waovu? Hilo ni swali zuri. Tunaposoma juu ya mapigo, utatambua  kufanana kukubwa na yale yaliyoangukiwa Misri. Hebu tusome kile akisemacho Yohana juu ya malaika wa kwanza



77

(Ufunuo 16:2 HNKK)
Basi, malaika wa kwanza akaenda akamwaga bakuli lake juu ya nchi.



78

Mara madonda mabaya na ya kuumiza sana yakawapata wote waliokuwa na alama ya yule mnyama,




79

na wale walioiabudu sanamu yake. (Ufunuo 16:2 HNKK)


80

Pengine haya majipu yanafanana na yale majipu na madonda ambayo Wamisri wakati wa pigo la saba waliteseka nalo. Au labda yangeliweza kufanana na yale ambayo Ayubu aliyapitia.


81

Je, waweza kufikiria uzito na athari ya pigo la namna hiyo? Shule zingefungwa.

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.


82

Viwanda vingelifungwa. Maduka yasingeliweza kunguliwa.


83

Hosptali zingefurika kwa watu wenye hitaji la huduma  ya dharura, lakini waganga walio wengi wangeteseka kwa matatizo yayo hayo.
Na kisha, wakati watu wangali wakiteseka kutokana na majipu yao, baa lingine linawapiga!




84

Kisha malaika wa pili akamwaga bakuli lake baharini. Nayo bahari ikawa damu tupu kama damu ya mtu aliyekufa, na viumbe vyote hai baharini vikafa. (Ufunuo 16:3  HNKK).



85

Ni picha ya ajabu kiasi gani, harufu ya kutisha kiasi gani, viumbe wa baharini wakilala katika pwani za bahari. Watu watakuwa wakijikwaa juu ya wengine katika kasi kali toka katika pwani hizi. Lakini pigo la tatu linahusiana kwa karibu sana na lile la pili.




86

Malaika wa tatu akamwaga bakuli lake katika mito na chemchemi za maji, navyo vikageuka damu. (Ufunuo 16:4 HNKK)


87

Hebu tafakari!  Mtu anafungulia bomba la maji ili apate maji ya kunywa, badala ya maji, damu inatoka! Hii inakuwa balaa gani! Je, kuna baya zaidi ya hilo? Lakini kwa ghadhabu na kutisha kama jinsi ambavyo mapigo ya mwisho yawezavyo kuwa, haki ya Mungu inathibitishwa kikamilifu. Kwani malaika anatamka:



88

(Ufunuo 16:5 HNKK)
Ewe mtakatifu, Uliyeko na uliyekuwako! Wewe ni mwenye haki katika hukumu hii uliyotoa.

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.




89

Maana waliimwaga damu ya watu wako na ya manabii,




90

nawe umewapa damu wainywe; wamestahili hivyo! Ufunuo 16:5,6.
Wakati huu, wakati ambapo waovu wanaangamia kwa sababu ya kutokuwa na chochote cha kunywa isipokuwa damu, ahadi hutamkwa kwa yule atembeaye kwa haki:




91

...atapewa chakula chake; maji yake hayatakoma. Isaya 33:16.



92

Na kisha Biblia husema juu ya malaika wa nne aliyemwaga bakuli lake:
Na huyo wa nne akakimimina kitasa chake juu ya jua, nalo likapewa kuwaunguza wanadamu kwa moto.



93

Wanadamu wakaunguzwa maunguzo makubwa, nao wakalitukana jina la Mungu aliye na mamlaka juu ya mapigo hayo:



94


wala hawakutubu wala kumpa utukufu. Ufunuo 16:8,9.
Kisha, malaika wa tano akamimina kitasa chake juu ya makao makuu ya mnyama:



95


Na huyo malaika wa tano akakimimina kitasa chake juu ya kiti cha enzi cha yule mnyama ; ufalme wake ukatiwa giza:

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.



96

wakatafuna ndimi zao kwa sababu ya maumivu,




97

wakamtukana Mungu wa mbingu kwa sababu ya maumivu yao, na kwa sababu ya majipu yao; wala hawakuyatubia matendo yao



98

na kwa sababu ya majipu yao; wala hawakuyatubia matendo yao. Ufunuo 16:10, 11.




99

Kwa fungu hili tunagundua ya kwamba haya mapigo si yote yaliyo kwa ajili ya dunia nzima, na wala si yote yanayoua mara moja, kwa sababu hapa tunaona ya kwamba wale waliokuwa katika pigo la tano bado wangali wakitaabika na majipu ya pigo la kwanza. Inaonekana haya mapigo yanaanguka moja baada ya jingine badala ya kuanguka kwa wakati mmoja yote, lakini athari zake hudumu kutoka moja hadi jingine. Katika pigo la sita ndipo tunakuta pambano kuu la mwisho, Har magedoni:



100

(UFUNUO 16:12)
Kisha malaika wa sita akamwaga bakuli lake juu ya mto mkubwa uitwao Frati.



101

Maji yake yakakauka, na hivyo njia ilitengenezwa kwa ajili ya wafalme wa mashariki.

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.



102

(Ufunuo 16:13 HNKK)
Kisha nikaona pepo wabaya watatu walio kama vyura, wakitoka kinywani mwa yule joka, kinywani mwa yule mnyama,




103

na kinywani mwa yule nabii wa uongo.




104

(Ufunuo 16:14 HNKK)
Hawa ndio roho za pepo wafanyao miujiza.



105

Ndio wanaokwenda kwa wafalme wa ulimwengu wote



106

na kuwakusanya pamoja kwa ajili ya vita kuu Siku ile ya Mungu Mwenye Uwezo. Ufunuo 16:12 - 14. Na Ufunuo 16:16 inasema:



107

Basi, roho hao wakawakusanya hao wafalme mahali paitwapo kwa Kiebrania Har-magedoni. Dunia nzima itahusishwa katika hili pambano la mwisho. Yohana aliandika:



108

(Ufunuo 19:11)
Kisha nikaona mbingu zimefunguliwa; na huko alikuwako farasi mmoja mweupe,



109

na mpanda farasi wake aliitwa Mwaminifu na Kweli. Huyo huhukumu na kupigana kwa ajili ya haki

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.



110

Na majeshi yaliyo mbinguni yakamfuata, wamepanda farasi mweupe na kuvikwa kitani nzuri, nyeupe , safi.



111

(Ufunuo 19:15 HNKK)
Upanga mkali hutoka kinywani mwake, na kwa upanga huo atawashinda mataifa.



112

. .....Yeye ndiye.... (mwenye) kuikamua divai katika chombo cha kukamulia zabibu za ghadhabu kuu ya Mungu Mwenye Uwezo.  Ufunuo 19:11,14,15.



113

(Ufunuo 16:17)
Kisha malaika wa saba akamwaga bakuli lake hewani. Sauti kubwa ikasikika kutoka kwenye kiti cha enzi, Hekaluni,



114

ikisema, Mwisho umefika!



115

Kukatokea umeme, kelele, ngurumo na tetemeko kubwa la ardhi ambalo halijapata kutokea tangu Mungu alipomuumba mtu.



116

Visiwa vyote vikatoweka, nayo milima haikuonekena tena. (Ufunuo 16:20)



117

Mvua ya mawe makubwa yenye uzito wa kama kilo hamsini kila moja, ikawanyeshea watu

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.



118


Nao wakamtukana Mungu kwa sababu ya mapigo ya mvua hiyo ya mawe. Naam, pigo la mvua hiyo ya mawe lilikuwa kubwa mno.
Ufunuo 16:17-18,20-21.


119

Wasomi wengi huweka uzito huo wa talanta kwenye kilo kama 50. Hakuna awezaye kufikiria jinsi uharibifu wa hiyo mvua ya mawe utakavyokuwa.


120

Lakini Biblia yasema kwamba Bwana mwenyewe ataingilia kati pambano akisafiri katika anga na majeshi ya mbinguni ili kuwakomboa watu wake toka katika sayari iliyoasi.


121

Lakini, unauliza, nawezaje kuwa na hakika ya ulinzi wa Mungu wakati mapigo yaanzapo kumwagika? Ipo njia moja tu.


122

Unaona, watu waliokombolewa kutoka katika pigo la mwisho katika Misri walikuwa wameeleleza imani yao na utii wa o kwa Mungu kama Mkombozi wao kwa kupaka damu ya mwana kondoo katika miimo ya milango ya nyumba zao. Wakati malaika aangamizaye alipopita  juu ya nyumba zao, walikuwa salama katikati ya uangamivu. Walikuwa wamefuata maelekezo ya Mungu na walikuwa wamefanya maandalizi ya muhimu.


123

Na tena, watu wa Mungu wataokolewa wakati mapigo yakimiminwa kama watakuwa wamemkubali Mwana - Kondoo wa Mungu kama kafara yao na kuruhusu damu yake kuwatakasa toka katika dhambi.

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.


124

Kwa jinsi tuishivyo, tunachagua leo sehemu gani tutakayokuwa  sehemu ya Mungu, au sehemu ya malaika muasi. Na rafiki, wakati malaika waangamivu wakianza kazi, watu watakuwa wamechelewa sana kubadili kambi! Mlango wa rehema utakuwa umefungwa tayari milele.
Je, hutajiweka mwenyewe katika kambi ya Mungu, chini ya ulinzi wa damu ya Yesu sasa? Maneno ya kusikitisha zaidi yatakayonenwa na watu hupatikana katika Yeremia 8:20.




125

Mavuno yamepita, wakati wa hari umekwisha, wala sisi hatukuokoka!


126

Kisa kinaelezwa cha fundi mwashi wa Australia ambaye alijenga kibanda chake katika kingo za msitu. Hakikuwa kikubwa lakinikilikuwa nyumbani kwake. Siku moja, aliporejea toka kazini mwake,


127

alistushwa na kuvunjika moyo kwa kukuta kaibanda chake kidogo kikiwa katika hali ya magofu. Yote yaliyokuwa yamesalia ni vipande vipande vya miti viliyokuwa na majivu na kuungua, pamoja na vyuma, vilivyojaa masizi ya moto. Alitembelea mahali ambapo kibanda chake cha kuku kilipokuwa kikisimama.


128

Yote aliyokuta ilikuwa ni mabonge ya majivu na nyaya ziliaoungua. Kama aliyejilazimisha alipekua vifusi. Kisha, hali akitizama chini katika miguu yake, jicho lake lilinasa bonge la manyoya yaliyopapurwa na moto. Kama kwa uvivu akapiga teke.Na unadhani kitu gani kilitokea?

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.



129

Vifaranga vinne vizuri vilivyojikusanya pamoja, ambavyo kwa muujiza hivi vililindwa kwa mbawa za mama yao mwenye upendo.
Katika lugha iliyo nzuri na ya kupendeza zaidi ya Maandiko, Mungu anaeleza kile anachotaka kukitenda kwa kila mmoja wa watoto wake duniani wakati mapigo yakimwagwa.




130

Aketiye mahali pa siri pake aliye juu;




131

Atakaa katika uvuli wake Mwenyezi......




132

Kwa manyoya yake atakufunika, Chini ya mbawa zake utapata kimbilio;




133

Uaminifu wake ni ngao na kigao. Zaburi 91:1,4.
Ndiyo, Mungu ametoa uhakika wa ajabu kwa wale wanaochagua kumfuata Yeye:



134


Hutaogopa hofu ya usiku, wala mshale urukao mchana;



135


Wala tauni ipitayo gizani,
wala uele uharibuo adhuhuri.

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.




136

Ijapo watu elfu waanguka ubavuni pako, naam kumi elfu mkono wako wa kuume! Hata hivyo hautakukaribia wewe.




137

Ila kwa macho yako utatazama na kuyaona malipo ya wasio haki.




138

Kwa kuwa Wewe BWANA ndiwe kimbilio langu; Umemfanya Aliye juu kuwa makao yako;



139

Mabaya hayatakupata wewe, wala tauni haitaikaribia hema yako.



140

Kwa kuwa atakuagizia malaika zake wakulinde katika njia zako zote....
Zaburi 91:5 - 11.



141

Je, kuna jambo la  lenye uhakika kuliko hilo? Je, hungependa kuwekewa ulinzi na usalama chini ya mbawa za Mwenyezi wakati mapigo yakianza kumiminwa? Wakati hakuna mahali pa kujificha? Baba yako wa Mbinguni anataka kukulinda na kukuokoa katika saa ya taabu na uangamivu.

# 23 - Kupona katika Taabu Ijayo.


142

Unapotoa maisha yako kwake, anao uwezo wa kukulinda kama mama kuku akusanyaye vifaranga vyake chini ya mbawa zake. Uamuzi ni wako. Ninao uhakika ya kwamba Mungu angelipenda kufanya uamuzi kwa niaba yako ili uweze kuwa naye milele zote, lakini hawezi kulifanya hilo. Wewe ndiwe peke yako uwezaye kufanya uamuzi huo. Usisubiri, Fanya hilo sasa.

# 24 - Uovu Katika Minyororo



1

Wakati Ambapo Mwovu Hawezi Kujaribu Tena


2

Kundi la wavumbuzi  wa Aktiki walikwama katika kisiwa kitupu chenye miamba. Masurufu yao yalikuwa yakimalizika kwa upesi. Walikuwa wamekula mego za mwisho za chakula.
Mafuta yao nayo yalikuwa katika kuisha.
Baridi ilikuwa ikiongezeka na walikuwa katika kuganda. Walijiandaa kwa ajili ya hali mbaya kuliko zote.
Walijua ya kwamba  kifo kilikuwa kikija upesi.
Pale tu walipokata tamaa,


3

mmoja wa hawa wavumbuzi waliokuwa katika kufa akatambua kiwingu cha moshi upeoni mwa macho. Mtu fulani alikuwa amenasa mawimbi yao ya redio ya masafa mafupi. Msaada ulikuwa njiani. Ukombozi ulikuwa unakuja.
Kile kiwingu kidogo cha moshi kilichoonekana upeoni ndicho tu walicho hitaji kiwatie moyo wadumu pale.
Karibuni ndoto mbaya ya hatari hii ya kutisha ingekwisha.
Karibuni wangekuwa salama  katika joto la chombo cha wokovu wao, na kisha muda mfupi baadaye wangekuwa nyumbani.
Nyumbani hatimaye!

# 24 - Uovu Katika Minyororo




4

Kitabu cha mwisho cha Biblia, Ufunuo, kinafunua ya kwamba msaada uko njiani. Hivi karibuni, sisi pia, tutakombolewa.
Ndoto ya muda mrefu ya dhambi itakwisha. Tutakombolewa, na Shetani atafungwa. Tutanyakuliwa angani kumlaki Yesu, na Shetani atafungwa na mazingira hapa duniani,
Tutapokea kautli ya uzima wa milele, na Shetani na wafuasi wake watapokea kauli ya uangamivu wa milele.





5

Kila mara, jaji ama jopo la majaji mahali fulani duniani hutoa kauli ya hukumu kwa mtu ili kutumikia kifungo cha muda mrefu, ili kuonyesha ghadhabu dhidi ya uhalifu.
Hukumu ya vifungo vya maisha vitatu ama vinne mfululizo au hata hukumu ya kifungo cha miaka 99 wakati mtu yupo katika umri wa kustaafu hutolewa bila matumaini bayana kama kweli vitatumikiwa kikamilifu.



6

Lakini kupitia kwa jaji ama jopo la mahakimu, hukumu inaeleza ghadhabu ya jamii mahususi kwa uhalifu wa kutisha.




7

Je, wajua ya kwamba wakati unakuja hivi karibuni ambapo Jaji atatoa hukumu ya miaka 1000 na mhalifu ataitumikia kila siku ya hukumu hiyo?




8

(Fungu: Ufunuo 20:1-3)
Sikiliza maneno haya yatokayo katika Biblia:
Kisha nikaona malaika akishuka kutoka mbinguni, mwenye ufunguo wa kuzimu, na mnyororo mkubwa mkononi mwake.

# 24 - Uovu Katika Minyororo



9

Akamshika yule joka, yule nyoka wa zamani, ambaye ni Ibilisi na Shetani, akamfunga miaka elfu.



10

akamtupa katika kuzimu, akamfunga, akatia muhuri juu yake,



11

asipate kuwadanganya mataifa tena, hata ile miaka elfu itimie.



12

na baada ya hayo yapasa afunguliwe muda mchache. Ufunuo 20: 1-3.


13


Hapa tunaona ya kwamba Mungu anao mpango wa kumshughulikia huyu mhalifu mkuu kuliko wote katika ulimwengu ambaye amepata kuwepo ambaye anahusika moja kwa moja na kila dhambi na uhalifu uliopata kuwepo katika dunia.
Lakini wakati unakuja ambapo atafungwa kwa miaka 1,000!
Miaka elfu moja katika mahali pabaya palipoharibika kuliko pote katika ulimwengu.
Mara nyingi kipindi hiki hufahamika kama Mileniam.



14

Mileniam ni nini?

# 24 - Uovu Katika Minyororo




15

Hiki kipindi cha miaka elfu huitwa mileniam, kutokana na maneno mawili ya Kilatini, mille, limaanishalo elfu moja, na annum, limaanishalo mwaka.


16

Unabii pia unatuambia ya kwamba Shetani atafungwa kwa



17

na kwamba atafunguliwa kwa muda mfupi ili kuuhakikishia ulimwengu ya kwamba hata baada ya miaka 1,000, hajabadilika bado ni yule yule mwovu. Ili kuweza kuamini unabii huu na kuona umuhimu wake kikamilifu, tunahitaji kuona jinsi gani unaanza na jinsi gani unaisha na kitu gani kinachotokea katika kipindi kilicho kati kati yake.



18

Niache nitoe kauli hii sasa, na kisha nitaendelea kuhakikisha ukweli wa kauli hii.
Mileniam imefungwa kati ya fufuo mbili:



19

1) Ufufuo wa uzima mwanzoni mwa kipindi hicho,



20

na
2) Ufufuo kwa ajili ya adhabu ya milele mwishoni mwa wakati huo.



21

(Fungu: Yohana 5:25)
Siku moja Yesu alikuwa akifundisha wanafunzi wake juu ya mauti, akasema: Amin, amin, nawaambia, ...Saa inakuja, na sasa ipo,



22

wafu watakapoisikia sauti ya  Mwana  wa Mungu, na wale waisikiao watakuwa  hai.
Yohana 5:25.
Hapo umeliona hilo.
Wafu wataisikia sauti yake na kuishi.
Hiyo ina maana, wafu wote watafufuliwa.
Najua hilo laweza kuja kama jambo la kushtua kwa baadhi yenu, kwa sababu mlidhani ya kwamba  wafu wenye haki peke yake watafufuliwa.
Tambua jinsi Kristo anavyolieleza katika  hili fungu la 28 na fungu la 29 la sura hii hii:



23

(Fungu: Yohana 5:28,29)
Msistaajabie maneno hayo; kwa maana saa yaja,ambayo watu  wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake,



24

Nao watatoka;wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa  hukumu.



25

na wale waliotenda mabaya
kwa ufufuo wa  hukumu. Yohana 5:28,29.



26

Tambua fufuo hizi mbili.  Wa kwanza,  ni ufufuo wa wale waliotenda mema, na wa pili ni wa  kwa ajili ya hukumu ya milele.


27

Sikiliza kile Biblia isemacho juu ya wale watakaokuwa katika ufufuo wa kwanza:

# 24 - Uovu Katika Minyororo



28

[Fungu: Ufunuo 20:6 (katika Kiswahili ni fungu la 6 pekee; ni tofauti na KJV ya kiiingereza ambapo maneno yanayofuata huwa yapo katika fungu la 5 na la 6)]....Huo ndio ufufuo wa kwanza.



29

Heri, na mtakatifu,ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo  wa kwanza; juu ya hao mauti ya pili haina nguvu;



30

bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja naye hiyo miaka elfu. Ufunuo 20:5,6.


31

Hili linapelekana na lile Paulo alilowaambia Wathesalonike.
Tambua jinsi anavyoeleza juu ya kuja kwa Kristo mara ya pili.



32

(Fungu: 1 Wathesalonike 4: 16,17)
Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka toka mbinguni na  mwaliko, na sauti ya malaika mkuu,



33

na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza.



34

Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana milele.



35

Na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele. Mafungu 16,17.

# 24 - Uovu Katika Minyororo


36

Ni maelezo matamu kiasi gani juu ya ufufuo.
Utatambua ya kwamba wale waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza,
kisha wafuasi wa Kristo walio hai watanyakuliwa pamoja nao katika mawingu ili kumlaki Bwana hewani!



37

(Fungu: Yohana 11:25)
Siku ile itatimia ahadi iliyotolewa na Yesu,Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa,
atakuwa anaishi;
Yohana 11:25.


38

Ndiyo, wenye haki waliokufa watafufuliwa toka kwenye makaburi yao wakati Yesu akirudi.



39

(Fungu: Isaya 26:19)
Isaya analielezea tukio hili la shangwe:...Amkeni, kaimbeni, ninyi
mnaokaa mavumbini,....nayo ardhi itawatoa waliokufa. Isaya 26:19.
Itakuwa siku ya utukufu kiasi gani!


40

Akina mama wakikutanishwa tena na watoto wao wachanga waliokufa. Waume na wake zao wakiunganishwa tena.
Wana na mabinti wakiunganishwa na Mama na Baba!
Je, tukio lingekuwa na mguso zaidi ya huo ?



41

(Fungu: Yohana 14: 2,3)
Kisha ile ahadi ya ajabu ambayo Kristo aliifanya muda mrefu uliopita itatimia: ......Naenda kuwaandalia mahali.



42

Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu;

# 24 - Uovu Katika Minyororo



43

ili nilipo mimi, nanyi muwepo.
Yohana 14:2,3
Hapa ndipo watakaookolewa watakapotumia mileniam!



44

(Fungu: Ufunuo 20:6)
Tutakuwa tukifanya nini? Yohana anatuambia Heri, na mtakatifu, ni yeye aliye na  sehemu katika ufufuo wa  kwanza; juu ya  hao mauti ya
pili haina nguvu;:



45

bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala  pamoja naye
miaka elfu. Ufunuo 20:6.
Pembeni ya furaha isiyoelezeka ya ushirika pamoja na Kristo na wafuasi wake, Yohana anatoa maelezo zaidi juu ya kile watakachikuwa wakikifanya wakati huu wa mileniam:



46

(Fungu: Ufunuo 20:4)
Kisha nikaona viti vya enzi, wakaketi juu yake, nao wakapewa hukumu;.....
Ufunuo 20:4.
Mungu wa ulimwengu wote mwenye hekima au ujuzi wote, mwenye uwezo wote amewahusisha wanaume na wanawake walioanguka katika kazi takatifu ya kuwahukumu malaika walioanguka na watu waliopotea.



47

(Fungu: 1 Wakorintho 6:2,3)
Paulo anasema: Au hamjui ya  kwamba watakatifu watauhukumu  ulimwengu?....



48

Hamjui ya kuwa  mtawahukumu  malaika?......  1 Wakorintho 6:2,3.

# 24 - Uovu Katika Minyororo




49

Itakuwa wazi mara moja ya kuwa Mungu ni mwenye haki na mwema na asiye na upendeleo.
Kwa miaka maelfu Shetani amekuwa akimshitaki Mungu ya kwamba hatumii haki, na hana upendo, na si mwenye haki.
Miaka ya mileniam italiwekea mwisho swala hili, na kuithibitisha tabia ya Mungu mbele za ulimwengu wote!
Lakini kwa nini tuhitaji kuhukumu malaika waovu na wenye dhambi waovu?
Je, hawajahukumiwa kabla ya kuja kwa Kristo?


50

Ni kweli,  lakini je umepata kujiuliza juu ya mshangao utakao kuwa nao kama utamtafuta mtu fulani mbinguni uliyetegemea kumwona pale -- halafu ugundue ya kwamba amepotea milele?
Waweza  kuiwekea maswali haki ya Mungu.


51

Wakati wa mileniam, taarifa za waliokufa zitafunguliwa.
Siri zilizovungwa sana na makusudi yaliyofichwa katika mawazo ya kila mtu vitawekwa wazi.
Upendo wa Mungu na haki yake vitathibitishwa.



52

(Fungu: Ufunuo 16:7)
Watakaokuwa wakichunguza taarifa watasalia tu na mwitikio mmoja:.....Naam,  Bwana
na Mungu Mwenyezi,  ni za kweli, na za haki, hukumu zako. Ufunuo 16:7.


53

Waweza kuwa unajiuliza kitu gani kilitokea kwa wale waliokutwa hai wakati Kristo akija, lakini hawakupata wokovu. Ufunuo sura ya 19 inaeleza juu ya kuja kwa mara ya pili kwa Kristo na kuangamizwa kwa wale ambao hawakuokolewa katika maneno haya:



54

(Fungu: Ufunuo 19:21)
Na wale waliosalia waliuawa kwa upanga utokao

# 24 - Uovu Katika Minyororo



55


katika kinywa  chake.....
Ufunuo 19:21


56

Hakuna uwezekano wa waliopotea kuweza kusimama mbele za utukufu wa Kristo ajapo pamoja na malaika zake watakatifu.



57

Malaika mmoja tu alikuja kwenye kaburi la Yesu, na askari wa Kirumi wakawa kama wafu.



58

(Fungu: Yeremia 25:33)
Biblia yasema, Na waliouawa  na  BWANA siku ile watakuwapo, toka upande  mmoja wa dunia  hata upande wa  pili.



59

hawataliliwa, wala kukusanywa,  wala kuzikwa; watakuwa samadi juu  ya uso wa nchi.
Yeremia 25:33.


60

Wakati wa kuja kwa mara ya pili kwa Kristo, wenye haki wanafufuliwa  na kubadilishwa kumlaki Yesu mawinguni,


61

wasiookolewa watauawa kwa mng'ao wa utukufu wa kuja kwake -- kwa upanga utokao katika kinywa chake.
Mtu atauliza swali, Vipi juu ya wasiookolewa ambao bado wako katika makaburi yao?
Jibu linatolewa katika fungu la tano la Ufunuo, sura ya 20:

# 24 - Uovu Katika Minyororo



62

(Fungu: Ufunuo 20:5)
Hao wafu waliosalia  hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu.


63

Sura inaanza kueleweka.
Picha kubwa inaanza kuonekana bayana juu ya kile kitakachotokea wakati Yesu Kristo akirudi:



64

Haya ndiyo matukio yanayokuwepo wakati wa kuja kwa Kristo



65

1. Yesu atarejea, pamoja na malaika watakatifu wote (Mathayo 25:31).



66

2. Wafu katika Kristo watafufuka kwanza (1 Wathesalonike 4:16).



67

3. Watakaookolewa walio hai wananyakuliwa kumlaki Yesu katika anga.( 1 Wathesalonike 4:17).



68

4.Walioookolewa wanakwenda nyumbani pamoja na Yesu na kutawala pamoja naye kwa miaka 1,000. (Ufunuo 20:4,6).



69

5. Wale ambao hawakuokolewa wanauawa kwa mng'ao wa kuja kwa Kristo (Yeremia 25:33).

# 24 - Uovu Katika Minyororo



70

6. Waovu waliokufa hawafufuliwi hadi baada ya miaka 1,000 (Ufunuo 20:5).




71

7.Shetani anafungwa  miaka 1000 kwa mnyororo wa mazingira -hakuna wa kumjaribu wala wa kuteketeza !



72

Wenye haki wako mbinguni,
na waovu wote wamekufa.
Kila mmoja amekwenda!
Kila mahali ni uharibifu.  (Yeremia 4:23-26).


73

Dunia hii inakuwa gereza la shetani.
Biblia yasema ya kwamba Shetani aliwekwa katika shimo lisilo na mwisho kwa mileniam.
Je, anatiwaje mnyororo?
Kwa mnyororo wa mazingira yanayofanya isiwezekane  kwake yeye  kujaribu na kuangamiza yeyote kwa miaka 1,000.


74

Wale ambao wamemfuata Shetani wakati wa maisha yao hapa duniani wanauawa wakati wa kuja kwa mara ya pili kwa Kristo, au wanasalia katika makaburi hadi ile miaka elfu iishe.


75

Waliookolewa ni wale wote walio na Kristo kwa miaka elfu.


76

Mwovu anao tu wale malaika waovu kuwajaribu na kuwapotosha , na wao,
baada ya miaka 6,000, ni wabaya  kama
alivyo yeye.

# 24 - Uovu Katika Minyororo



77

Dunia hii inakuwa gereza lake.
Alitaka kuonyesha jinsi gani ambavyo angeutawala ulimwengu, hivyo akachukua utawala toka kwa Adamu na Hawa kwa udanganyifu, lakini sasa kila mmoja atakuwa tayari kuona ya kwamba ni mtawala wa namna gani!




78

(Fungu: Ufunuo 20:3)
Utakumbuka ya kwamba Ufunuo 20:3 inasema: Akamtupa katika kuzimu, akamfunga, akatia muhuri juu yake,




79

asipate kuwadanganya mataifa tena, hata ile miaka elfu itimie;




80

na baada ya hayo yapasa afunguliwe muda mchache. Neno la asili la Biblia ya awali limaanishalo shimo ni abussos.
Hili ndilo neno pia lililotumika katika Agano la Kale kueleza juu ya dunia katika hali isiyo na utaratibu na umbo linaloeleweka kabla Mungu hajaumba dunia hii nzuri.




81


(Fungu: Yeremia 4:23)
Ni neno lili hili lililotumika katika kitabu cha Yeremia: Naliiangalia nchi,na tazama, ilikuwa ukiwa, haina watu; naliziangalia mbingu, nazo zilikuwa hazina nuru.
Yeremia 4:23.




82


Ndiyo, dunia ni abusos au shimo lisilo na mwisho. Patakuwa mahali penye giza!
Sasa, tambua jambo jingine ambalo Yeremia analisema juu ya wakati huu:

# 24 - Uovu Katika Minyororo



83

(Fungu: Yeremia 4:24, 25)
Naliiangalia milima, na  tazama, ilitetemeka, na milima  yote ilisogea huko na huko.



84

Nikaangalia,  na  tazama, hapakuwa na mtu hata mmoja, na ndege wa angani
wamekwenda zao.
Yeremia 4:24,25.
Utatambua pia ya kwamba fungu lilisema, Hapakuwa na mtu.




85

(Fungu: Yeremia 4:26)
Na tena Yeremia anasema,Nikaangalia,
na tazama, shamba lililozaa sana  limekuwa ukiwa,



86

na miji yake  yote  ilikuwa imebomoka
mbele za  BWANA, na  mbele za hasira  yake kali.
Mafungu 26,27.


87

Hiyo inaonyesha kweli jinsi patakavyokuwa mahali pa kuogofya kupata likizo kwa miaka elfu, je, unakubaliana nami?
Shetani na malaika zake hawana la kufanya ila kurandaranda  huku na huko gizani, wakiwa katika sayari yenye giza, iliyoharibika, na yenye ukiwa na wakati huo wakitafakari matokeo ya uasi wao dhidi ya Mungu!



88


Sasa hebu na tupitie matukio yanayoendelea wakati wa miaka elfu (Mileniam):



89

1. Dunia ina ukiwa na uharibifu.

# 24 - Uovu Katika Minyororo




90

2.Wote ambao hawakuokolewa wamekufa, wameuawa kwa utukufu wa kuja kwa Yesu.




91

3. Wote waliookolewa wako mbinguni wakitawala na Kristo.



92

4. Shetani amefungwa katika sayari hii iliyoharibika ili autafakari uasi wake.


93

Je, Shetani atabadilika?
Habari gani juu ya malaika aliowaongoza katika uasi?
Je, watachagua kumfuata Yeye tena- au watachagua kumfuata Kristo sasa?
Sababu mojawapo iliyomfanya Mungu kuchagua kuiweka mileniam katika ratiba yake ni kutaka kuuhakikishia ulimwengu ya kwamba kama mwovu, malaika zake, na wale ambao wamechagua kumfuata hapa duniani wangepewa nafasi nyingine, bado wangefanya uamuzi huo huo na kuchagua kumfuata bwana huyo huyo.


94


Wangekataa mpango wa wokovu hata kama wangelikuwa na nafasi elfu za kuukubali.



95

Je, Biblia yasema nini juu ya uchaguzi wao?

# 24 - Uovu Katika Minyororo



96

(Fungu: Ufunuo 20:7,8)
Jibu linatolewa katika Ufunuo 20:7,8: Na hiyo miaka elfu itakapokwisha, Shetani atafunguliwa, atoke kifungoni mwake;



97

naye atatoka kuwadanganya mataifa walio katika pembe nne za nchi,.........



98

kuwakusanya kwa vita, ambao hesabu yao ni kama mchanga wa bahari.
Ufunuo 20:7,8.
Pengine unashangaa watu wote hawa watatokea wapi watakao kuwa katika pambano hili.



99

(Fungu: Ufunuo 20:5)
Kumbuka tunasoma katika sura ya 20 ya Ufunuo, fungu la 5: Hao wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu.


100

Ndiyo, wafu waliosalia ama wafu ambao hawakuokolewa wanafufuliwa katika ufufuo kwa ajili ya adhabu ya milele mwishoni mwa mileniam. Itakuwa picha ya ajabu kiasi gani kuona wafu walio waovu waliofufuliwa katika idadi yao kubwa, waovu wote tangu siku za Adamu hadi kuja kwa Yesu mara ya pili.



101

(Fungu: Ufunuo 20:8)
Yohana anasema, .......ambao hesabu yao ni kama mchanga wa bahari.
Ufunuo 20:8.


102

Wakati huu huu Jiji Takatifu, Yerusalemi mpya, pamoja na Kristo na waliookoka, wanakuja duniani mwishoni mwa mileniam!
Jiji hili litakuwa ndilo shabaha ya hasira ya shetani, kwani Biblia yasema,

# 24 - Uovu Katika Minyororo



103

(Fungu: Ufunuo 20:7,8)
Na hiyo miaka elfu itakapokwisha, Shetani atafunguliwa, atoke kifungoni mwake,



104

naye atatoka kuwadanganya mataifa walio katika pembe nne za nchi.....



105

kuwakusanya kwa vita....
Ufunuo 20:7,8.


106

Sasa Shetani na malaika zake waovu wanatoka tena kuwadanganya waovu!
Hajabadilika hata kidogo!
Kwa mara nyingine wasiookolewa wanamchagua Shetani kama kiongozi wao.
Mwovu anawapanga kama jemadari mkuu, wanakuwa katika jeshi moja kubwa lililo na shabaha ya kuichukua Yerusalemi mpya kwa nguvu.
Hili ni pambano la mwisho la dunia!
Jeshi kubwa, chini ya uongozi wa malaika muasi, linasonga mbele!


107

Hebu na tusome kile Biblia inachokisema kitatokea:



108

(Fungu: Ufunuo 20:9)
Wakapanda juu ya upana wa nchi wakaizingira kambi ya watakatifu, na mji huo uliopendwa.

# 24 - Uovu Katika Minyororo



109

Moto ukashuka kutoka
mbinguni, ukawala.
Ufunuo 20:9.



110

Pambano limekwisha! Inasikitisha kiasi gani wakati ambapo hali hii ingelikuwa tofauti kabisa!
Kitu gani kinachotokea kwa mwovu? Biblia inatuambia:



111

(Fungu: Ufunuo 20:10, 14,15)
Na yule Ibilisi, mwenye kuwadanganya,
akatupwa katika lile ziwa la moto na kiberiti,.....



112

Mauti na kuzimu zikatupwa katika
lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili.



113

Na iwapo mtu ye yote hakuonekana
ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa
katika lile ziwa la moto.
Ufunuo 20:10, 14,15.
Petro aliuona moto huu katika njozi na kuandika:



114

(Fungu: 2 Petro 3:10)
...Katika siku hiyo mbingu zitatoweka
kwa mshindo mkuu, na viumbe vya asili
vitaunguzwa, na kufumuliwa,



115

na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea.
2 Petro 3:10
Shetani, malaika zake waovu, na wenye dhambi
watakuwa wametoweka milele!


116

Twaweza kuwa na jamaa, marafiki, au watu tulio
wajua na kuwapenda sana ambao watatoweka milele.
Kwa kweli, tutalia. Vinginevyo ingekuwaje?

# 24 - Uovu Katika Minyororo




117

(Fungu: Ufunuo 21:4)
Lakini, habari njema ni hii: Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena;




118

wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.
Ufunuo 21:4.



119

Ni umilele wenye utukufu kiasi gani ambao Mungu anawaahidi watakaookolewa!
Mawazo ya kibinadamu hayawezi kuelewa utukufu na uzuri wa Paradiso ambayo Mungu anaandaa kwa ajili ya wale wampendao na walio tayari kumfuata!
Na kufikiri ya kwamba yote haya, waovu wangeyafaidi, lakini ilionekana kwao kuwa vigumu sana!
Hawakuwa tayari kumchagua Kristo kama Mwokozi wao na Bwana.
Ni kundi gani utakalokuwa kwalo katika siku ile, rafiki?
Siku ile itakapofika, utakuwa umechelewa sana kubadilisha makundi.
Hata katika mwanzo wa miaka elfu, wakati Yesu ajapo, utakuwa tayari umechelewa sana.
Itakuwa umechelewa sana hata kama utakufa kwa ghafula bila kujiandaa.
Njia ya pekee ya kujua kwa uhakika ya kwamba u kati ya wenye haki mwishoni mwa mileniam ni kuutoa moyo wako wote na maisha yako yote kwa Yesu sasa - LEO!

# 24 - Uovu Katika Minyororo


120

Kama ungependa kutoa maisha yako kwa Yesu kikamilifu kabisa, ningependa uje hapa mbele kwa ajili ya ombi la pekee.
Kama unalo tatizo katika maisha yako, njoo mbele kwa ajili ya ombi sasa hivi.
Kama unayo tabia fulani au mazoea fulani ambayo unahitaji ushindi juu yake, njoo mbele kwa ajili ya sala.
Yesu atakusikia. Yesu atajibu. Nitasubiri kwa dakika moja, lakini njoo, na uje sasa hivi.

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!



1

Mbingu ni Hakika


2

Kisa kinaelezwa cha msichana mdogo aliyeishi katika jiji maisha yake yote. Kwa sababu ya nuru ya taa za jiji ambayo iliangaza anga,  hakupata kuwa na wasaa wa kuona nyota.
Wakati mmoja wa kiangazi mama yake alimchukua kwa likizo hadi sehemu  ya mashambani.


3

Jioni baada ya jua kutua, nyota ziling'aa kama almasi katika anga usiku. Huyu msichana mdogo alitizama juu na kushangaa. Uzuri wa mng'ao wa anga lililojaa nyota zilizosambaa ulimmaliza nguvu.
Alisema kwa mshangao, Ah, mama, kama mbingu hii ni nzuri hivi katika sehemu hii mbaya, ikoje katika sehemu nzuri?



4

Somo la mbingu limekamata mawazo ya wanaume na wanawake katika dunia nzima kwa karne nyingi.
Je, mbingu ikoje kwa kweli?
Je, ipo kweli?
Kama ndivyo, iko wapi, na ikoje huko ilipo?


5

Baadhi ya watu hawaamini katika mbingu.
Wengine husema ziko mbingu tatu, au hata saba.
Baadhi husema unakwenda mbinguni  unapokufa.


6

Baadhi husema la, unakwenda mahali paitwapo pagatori kwanza, kisha labda mbinguni baadaye.


7

Baadhi husema mbingu si mahali halisi, lakini ni ile tu hali ya mawazo.

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!


8

Wapo wale waaminio ya kwamba hatimaye, kila mtu atafika mbinguni. Baadhi husema watu wachache sana watafaulu kufika pale.
Mchanganyiko mwingi sana! Maoni mengi sana!



9

Kwa nini yawepo maoni tofauti tofauti mengi hivi kuhusu mbingu?
Kwa nini maoni yawe na tofauti nyingi hivi na dhana zote hizi wakati Biblia inalifanya neno hili kuwa wazi kabisa?


10

Kwa kweli, je, wajua ya kwamba Biblia imejaza maelezo ya ndani kabisa juu ya mbingu?
Mungu anatutaka tujue jinsi mbingu ilivyo ili tukusudie kuwa pale!
Mbinguni si mahali pa siri ambapo Mungu anatuficha tusipajue.


11

Katika majengo mengi makubwa, kuna ufunguo unaofaa kufungulia kila kufuli au kitasa cha kila mlango.



12

Mwenye jengo anayo funguo iitwayo funguo kuu. Funguo ile moja inafaa kwa milango yote.



13

Mungu anao ufunguo mkuu ufunguao siri na mafumbo juu ya mbinguni, na ufunguo huo mkuu ni Biblia-- chanzo chetu kikuu cha taarifa.
Ni jambo la kupendeza ya kwamba hatuhitaji kutegemea dhana za kibinadamu au maoni yao.
Hatuhitaji kuchanganyikiwa juu ya ukweli halisi uanaohusu mbingu.


14

Mtume Petro aliandika juu ya chanzo hiki muhimu cha taarifa.

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!



15

(Fungu: 2 Petro 1:19)
Nasi tunalo lile neno la unabii lililo
imara zaidi, ambalo, mkiliangalia, kama taa ing'aayo
mahali penye giza, mwafanya vyema,



16

mpaka kutakapopambazuka na nyota ya
asubuhi kuzuka mioyoni mwenu.
2 Petro 1:19.




17

Mungu amefunua katika neno lake:
Mahali Mbinguni palipo
Jinsi mbinguni patakavyokuwa
Mahali makao makuu yatakapokuwa
Mambo watu watakayoyafanya pale
Jinsi watu watakavyokuwa pale
Mahali watakaookolewa watakapoishi
Jinsi Jiji la Makao makuu litakavyoonekana



18

Sasa hebu na tuchukue ufunguo mkuu wa Mungu - Biblia, na tugundue wakati halisi ujao ambao Mungu ameuandaa kwa ajili ya watu wake.


19

Katika kitabu cha mwisho cha Biblia, Ufunuo, Mungu Mwenyewe alifunua kwa Yohana picha ya wakati ujao.
Yohana anaeleza alichokiona:



20

(Fungu: Ufunuo 21:1,2)
Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa
maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza
zimekwisha kupita,



21

Wala hapana bahari tena.

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!



22

Nami nikauona mji ule mtakatifu,
Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu,



23

umewekwa  tayari,kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa  kwa mumewe.
Ufunuo 21:1,2.


24

Mandhari chache huwakilisha furaha na uzuri kama wa bibi-arusi ajiandaaye kwa siku yake ya arusi!


25

Hapa nyumbani mbinguni siyo kitu tu ambacho Yohana peke yake alikiona - manabii wote wa Mungu katika vizazi vyote wamekuwa wakijua kupahusu.
Sikiliza:



26

(Fungu: Matendo 3:20, 21)
Apate kumtuma Kristo Yesu mliyewekewa tangu zamani;



27

ambaye ilimpasa kupokewa mbinguni hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote,



28

zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu.
Matendo 3:20,21.

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!




29

NI VITU GANI AMBAVYO MUNGU ATAVIFANYA UPYA?
Mungu atafanya upya kila kitu ambacho Adamu na Hawa walipoteza!
Dunia ilitoka mikononi mwa Muumbaji ikiwa na utukufu na ukamilifu, ikiwa nzuri zaidi ya maelezo.


30


Muumbaji mwenyewe alikuwa ameisanii na kuiremba nyumba ya Adamu na Hawa, Bustani ya Edeni, paradiso. Mungu alikuwa amewapatia utawala hapa duniani.


31


Walikuwa na afya kamili, upendo, furaha, shangwe, na ushirika wa uso kwa uso na Mungu.
Kila kitu kilikuwa ni amani na shwari.
Wasingeliugua wala kufa kamwe kama wangelichagua kutii maelekezo ya Mungu.


32

Na maelekezo yake yalikuwa: Msile katika mti uliopigwa marufuku katika Bustani ya Edeni, mkifanya hivyo mtakufa.


33

Lakini walichagua kula katika mti ule.
Walimsikiliza malaika muasi katili na mdanganyifu, aliyeitwa Shetani badala ya kumsikiliza Mungu mwenye upendo na mwenye kujali.


34

Baadaye, kwa mara ya kwanza katika maisha yao, walijisikia kuwa na hatia, wenye aibu, na wenye hofu.
Ilikuwa siku ya msiba kuliko zote katika historia ya Sayari Dunia.
Kwa kutotii kwao, walipoteza kila kitu: nyumba yao ya bustanini, utawala wao wa Dunia, na ruhusa ya kula katika Mti wa Uzima.
Kwa kutoweza kula katika Mti wa Uzima, ni hakika wangekufa.

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!



35

Hawakuweza tena kuwa na uzima wa milele.
Furaha yao, upendo wao, ushirika wao na Muumbaji vingeisha.
Dunia yetu iliyokuwa kamili ikaharibiwa na laana ya dhambi.
Dunia ikawa mahali pa huzuni na taabu, mahali pa maradhi na mauti.
Wakiwa si wakuu tena, Adamu na Hawa wakawa watumwa.




36

(Fungu: Warumi 6:16)
Paulo anasema, Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii,




37

mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii.....
Warumi 6:16.
Lakini, Mungu anayependa na kujali alielewa.
Joka alikuwa amemdanganya Adamu na Hawa.
Mungu aliwapenda sana hakuweza kuwaacha watoto wake waliokosa bila tumaini.




38

Katika malango ya bustani, Mungu alimuahidi Adamu na Hawa ya kwamba siku moja Mwana Wake, Mbegu ya Mwanamke, angekuja na kufa kwa ajili yao ili wapate kurejeshwa katika Familia ya Mungu na kuwa na uzima wa milele.




39

(Fungu: Mwanzo 3:15)
Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake;




40

huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino. Mwanzo 3:15.

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!



41

Kadri vizazi vilivyopita na watu walivyozidi duniani, dhambi pia ilizidi.
Mwanadamu alikuwa hata amekaribia kumsahau Mungu na ahadi yake.



42

(Fungu: Mwanzo 6:5)
Watu wakawa waovu na wenye tabia mbaya na BWANA akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani



43


na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu siku zote.
Mwanzo 6:5.


44

Hatimaye ikawa muhimu kwa Mungu kuwaangamiza waovu katika Gharika Kuu ili kudumisha uhai duniani.
Watu wanane peke yake walipona!
Baada ya Gharika Kuu, havikuwa vizazi vingi kabla watu hawajawa waovu tena.


45

Ili kutunza watu watakatifu hapa duniani, Mungu alimuita Ibrahimu na familia yake toka kwa Uru ya Wakaldayo iliyokuwa na ibada ya sanamu na uovu. Familia yake bila shaka ingekuwa ovu pia kama ingesalia pale katika lile jiji.



46

(Fungu: Mwanzo 12:1,2)
Bwana alimwambia Ibrahimu, Toka wewe katika nchi yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha;



47

nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka. Mwanzo 12:1,2.

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!


48

Ibrahimu alikuwa tayari kuacha starehe ya nyumba yake ya Kikaldayo. Hakujua alipokuwa akienda, lakini alikuwa na fununu kidogo ya kile Mungu alichokuwa nacho kwa ajili yake.



49

(Fungu: Waebrania 11:9,10)
Kwa imani alikaa ugenini katika ile nchi ya ahadi, kama katika nchi isiyo yake,



50

akikaa katika hema pamoja na Isaka na Yakobo, warithi pamoja naye wa ahadi ile ile.




51

Maana alikuwa akiutazamia mji wenye misingi, ambao mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu. Waebrania 11:9, 10.
Mungu aliahidi kumpatia Ibrahimu na watoto wake yote ambayo Adamu na Hawa walikuwa wamepoteza.


52

Manabii wa vizazi vyote waliamini na kuutazamia wakati wa kufanywa upya vitu vyote.
Mungu anaorodhesha baadhi ya walio kwenye Ukumbi wa Imani katika Biblia katika



53

Waebrania, sura ya 11. Ibrahimu, Henoko, Nuhu, Habili, Isaka, Rahabu, Daudi, na Samweli ni baadhi tu ya watu wakuu wa imani walioamini katika ahadi ya Mungu ya kurejesha kile Adamu na Hawa walichopoteza. Tambua jinsi Biblia isemavyo kuhusu mashujaa hawa:



54

(Fungu: Waebrania 11:13,16)
Hawa wote wakafa katika imani, wasijazipokea zile ahadi, bali wakaziona tokea mbali na kuzishangilia, na kukiri.....

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!



55

Lakini sasa  waitamani nchi  iliyo bora, yaani, ya mbinguni. Kwa  hiyo Mungu haoni haya kuitwa Mungu wao;



56

maana  amewatengenezea  mji. Waebrania 11:13,16.


57

Isaya, nabii mkuu kabisa kati ya manabii wote wamtabirio Masihi, anatupatia maelezo ya kusisimua juu ya marejesho ambayo Mungu ameandaa,
Hebu tutizame mambo ambayo Mungu alimfunulia Isaya:



58

(Fungu: Isaya 65:17)
Maana, tazama, mimi  naumba mbingu mpya na nchi mpya;



59

na mambo ya kwanza hayatakumbukwa, wala hayataingia moyoni.
Isaya 65:17.



60

(Fungu: Isaya 60:18)
Na tena: Jeuri haitasikiwa tena
katika nchi yako, Ukiwa na uharibifu hazitakuwa mipakani mwako;



61

Bali utaziita kuta zako, Wokovu, na malango yako, Sifa.
Isaya 60:18.

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!



62

Hebu fikiria - HAKUNA ujeuri pale! Ni amani tu na mapatano!
Je, hilo siyo jambo la AJABU kuliwaza?
Hakuna hitaji pale la kupata silaha ili kututetea na kujilinda sisi wenyewe.
Hakuna wabakaji wala wevi!
Na je, haitakuwa ajabu kutembea katika ile mitaa ya dhahabu na bila kuwa na wasiwasi juu ya kuvamiwa au kunyang'anywa?
Lakini hilo siyo yote ambayo nabii aweza kutuambia.
Sikiliza:




63

(Fungu: Isaya 11:6)
Mbwa-mwitu atakaa pamoja na mwana-kondoo, na chui atalala pamoja na mwana mbuzi...........



64

na mtoto mdogo atawaongoza.
Isaya 11:6.


65

Sasa hebu sikiliza kwa kile Biblia ikisemacho juu ya Sayari Dunia wakati ikiwa imerejeshwa katika uzuri wake wa awali:



66

(Fungu: Isaya 33:24)
Wala hapana mwenyeji atakayesema,
'Mimi mgonjwa'....
Isaya 33:24.
Hakuna magonjwa ya moyo, hakuna sarakani, hakuna maradhi yatokanayo na kutopatana na vitu ama vyakula fulani- yaani afya kamili milele!
Je, hiyo si habari njema?

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!



67

(Fungu: Isaya 35:5)
Ndipo macho ya vipofu yatafumbuliwa.... Isaya 35:5.
Bila ya shaka jambo la kwanza aliyekuwa kipofu atakalotaka kuliona litakuwa uso wa Yesu!
Ah, itakuwa siku ya utukufu kiasi gani kwa wale waliokuwa vipofu!



68

(Fungu: Isaya 35:5,6)
....Masikio ya viziwi yatazibuliwa. Isaya 35:5.



69

Ndipo mtu aliye kilema ataruka-ruka kama kulungu... Isaya 35:6.
Hakuna tena viti vyenye gurudumu vya walemavu!
Hakuna tena mikongojo ya kwapani ! Kila mmoja atakuwa na mwili usio na dosari.



70

(Fungu: Isaya 35:6)
......na ulimi wake aliye bubu utaimba: Isaya 35:6. Si tu kwamba watazungumza, bali wataimba!
Itakuwa siku ya furaha kiasi gani!
Lakini kuna habari ya ajabu zaidi!



71

(Fungu: Isaya 35:1)
Nyika na mahali palipo ukiwa patafurahi; jangwa litashangilia na kuchanua maua kama waridi. Isaya 35:1.
Nchi mpya itakuwa mahali pazuri kiasi gani!



72


(Fungu: Isaya 65:21,22)
Nao watajenga nyumba, na kukaa ndani yake; watapanda mizabibu na kula matunda yake,



73

Hawatajenga akakaa mtu mwingine ndani yake; hawatapanda, akala mtu mwingine;

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!



74

Maana kama  siku za mti  ndivyo zitakavyokuwa siku za watu  wangu, na wateule wangu wataifurahia kazi ya mikono yao muda wa siku nyingi.
Isaya 65:21,22.


75

Inaonekana dhahiri kwamba mbinguni patakuwa mahali halisi na watu halisi wakitenda mambo halisi, sivyo?
Kwa kweli, tutakuwa na majina yetu wenyewe, na watu watatujua!



76

(Fungu: Isaya 66:22,23)
'Kama vile mbingu mpya  na nchi mpya, nitakazofanya, zitakavyokaa mbele zangu, asema BWANA,



77

ndivyo uzao  wenu na jina  lenu litakavyokaa.'
Isaya 66:22.



78

'Na itakuwa,  mwezi mpya hata mwezi mpya, na sabato  hata sabato,



79

wanadamu wote  watakuja kuabudu mbele zangu,' asema BWANA.
Isaya 66:23.
Nchi mpya patakuwa ni mahali pa furaha, mahali pa shangwe, kwa ajili ya Mungu na watu wake.



80

(Fungu: Isaya 35:10)
Na hao  waliokombolewa  na BWANA watarudi, watafika  sayuni wakiimba;

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!



81

na furaha ya milele itakuwa juu ya vichwa vyao; nao watapata kicheko na furaha, huzuni na kuugua zitakimbia. Isaya 35:10.
Je, hili halionekani kusisimua?


82

Itakuwa ni sherehe ya shangwe, ajabu wakati waliookolewa kila mmoja wao akija kila Sabato kwenye Jiji takatifu kusifu na kuimba na kuwa na ushirika huu mzuri.


83

Yesu alisema anatujengea kila mmoja wetu jumba. Tutafurahia hilo, lakini Isaya pia alisema sisi pia tutajenga nyumba!
Naam, inaonekana kama labda tutakuwa na nyumba ya mashambani ambayo tutaijenga sisi wenyewe, na kisha kila mwishoni mwa juma tutakwenda makao makuu ya Nchi Mpya na kutumia majumba yetu katika jiji.



84

Picha ya mbinguni iliyopo katika Biblia i wazi. Mungu ataumba mbingu mpya na nchi mpya. Jiji Takatifu, Yerusalemu Mpya, litashuka toka kwa Mungu toka mbinguni.
Dunia, sayari hii ambayo sasa i katika uasi, iliyoanguka katika dhambi, itakuwa makao makuu ya ulimwengu wote.
Yaweza kukushangaza, lakini dunia hii itakuwa ni nyumbani kwa watakaookolewa. Yesu alilisema hivi.



85

(Fungu: Mathayo 5:5)
Heri wenye upole; maana hao watairithi nchi. Mathayo 5:5.
Mungu atairejesha Sayari Dunia katika hali yake ya awali ya ukamilifu, na itakuwa Nchi Mpya yenye utukufu kiasi gani!



86


Pengine waweza kumbuka ahadi za ajabu alizozitoa Yesu kwa wanafunzi na wafuasi wake wa karne zote kabla hajarejea mbinguni:

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!



87

(Fungu: Yohana 14:1-3)
Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi.




88

Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia...



89

Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu;




90

ili nilipo mimi, nanyi muwepo.
Yohana 14:1-3.



91

(Fungu: Mathayo 6:9,10)
Sala kielelezo ambayo Yesu aliwafundisha wanafunzi wake inasema, Ufalme wako uje,
Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.
Mathayo 6:10.
Hapa tunaona ya kwamba Yesu anatuuliza tusali kwa ajili ya kurejeshwa kwa mambo yote.


92

Sasa, hebu na tufikirie kwa undani zaidi jiji kubwa ambalo Yohana aliliona katika njozi katika kisiwa cha Patmo. Yaonekana kama vile nabii alikuwa na wakati mgumu kupata maneno ya kueleza uzuri na ufahari wa Jiji Takatifu. Biblia yasema kwamba:



93

(Fungu: 1 Wakorintho 2:9)
....Mambo ambayo jicho halikuyaona
wala sikio halikuyasikia, ( wala hayakuingia
katika moyo wa mwanadamu,)

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!



94

Mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao.
1 Wakorintho 2:9.
Lakini hebu ngoja kidogo.
Watu wengi hushindwa kusoma fungu linalofuata lisemalo,



95

(Fungu: 1 Wakorintho 2:10)
Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho. ...


96

Unaona? Mungu amefunua mambo haya kwa Roho Mtakatifu aliyewaambia manabii, walioyaandika haya kwa ajili yetu.
Bila ya shaka, nusu haijaelezwa!



97

Marafiki, hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa Yohana na Isaya na manabii wote.
Ndiyo kweli yote-- na nusu haijaelezwa!
Wakati Yohana anapofungua undani wa Jiji Takatifu, inaonekana kama hekaya tu.
Lakini tunalo Neno la Mungu juu ya hilo! Haya ndiyo aliyoyaona Yohana.



98

Yohana alisema aliona mbingu mpya na nchi mpya, na kwamba hapakuwa na bahari tena.
Kisha akaona Jiji Takatifu likishuka toka mbinguni.
Ndipo anatuambia yote juu ya Jiji:



99

(Fungu: Ufunuo 21:1-3, 11, 17,21)
Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita, wala hapana bahari tena. Ufunuo 21:1.



100


Nami nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe. Ufunuo 21:2.

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!




101

Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile
kiti cha enzi ikisema, 'Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu,



102

naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye mwenyewe, Mungu pamoja nao, atakuwa Mungu wao.'
Ufunuo 21:3.




103

.....mwangaza wake ulikuwa mfano wa kito cha thamani nyingi kama kito cha yaspi,
safi kama bilauri.
Ufunuo 21:11.




104

Akaupima ukuta wake, ukapata dhiraa mia na arobaini na nne [mita 66]....... (Fungu la 17).



105

Na ile milango kumi na miwili ni lulu kumi na mbili...... (Fungu la 21)
Kumbe yapo malango ya lulu!



106

(Fungu: Ufunuo 21:12,21,23)
...ukuta mkubwa, mrefu,...na majina yameandikwa ambayo ni majina ya
kabila kumi na mbili za Waisraeli. (Fungu la 12).



107

...Na njia ya mji ni dhahabu safi kama kioo kiangavu. (Fungu la 21).



108

Na mji ule hauhitaji jua wala mwezi kuuangaza, kwa maana utukufu wa Mungu huutia nuru, na taa yake ni Mwana-Kondoo.
(Fungu la 23).

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!



109

(Fungu: Ufunuo 22:1,2,5)
...mto wa maji ya uzima, wenye kung'aa kama bilauri, ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo.




110

.....Na upande huu na upande huu wa ule mto, ulikuwapo mti wa uzima, uzaao matunda yake kila mwezi; .........



111

Wala hapatakuwa na usiku tena;... Uf. 22:5
Kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo kitakuwa katika makao makuu - Yerusalemu mpya.




112

(Fungu: Ufunuo 22:3)
Wala hapatakuwa na laana yoyote tena. Na kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo kitakuwamo ndani yake.... Ufu. 22:3.
Na moja ya zawadi za ajabu zaidi inapatikana katika Ufunuo 21:4:



113

(Fungu: Ufunuo 21:4)
Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo,



114

wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita. Ufunuo 21:4.
Pengine unashangaa ya kwamba ukubwa wa Jiji Takatifu utakuwaje.



115

(Fungu: Ufunuo 21:16)
Yohana anaeleza undani halisi wa ukubwa wa jiji: Na ule mji ni wa mraba, na marefu yake sawasawa na mapana yake.

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!



116

Akaupima mji  kwa ule mwanzi; ulikuwa kama maili elfu na mia  tano;........
Ufunuo 21:16.



117

[Maili tano ni sawa na kilomita nane kwa hiyo maili 1,500 za mraba ni sawa na kilomita 2,400 mraba].
Majiji ya kale yalikuwa yakipimwa kwa umbali wa mzunguko wa nje wa kuta zake.
Hivyo jiji lingekuwa takriban  Km 600 au maili 375 kila upande.
Na pengine unashangaa kama jiji hili litakuwa la kutosha kwa watakaookolewa.


118

Jiji la Tokyo lina wakazi takriban milioni 35 waishio katika jiji hili.



119

Sehemu Kuu ya Jiji la New York ina tunza wakazi milioni 20.


120

Seoul (Korea) na Jiji la Mexico  pia yana karibu ya watu milioni 20 kila moja.



121

Mwana mahesabu mmoja amekadiria ya kwamba Yerusalemu Mpya, hata hivyo, yaweza kutunza wakazi bilioni mbili!
Kwa maneno mengine, kutakuwa na nafasi kwa kila atakayetaka kuwa pale.
Lakini ni kitu gani kitakachotushughulisha  katika mahali pa ajabu kiasi hicho?

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!



122

Bila uhalifu, wala maradhi, bila njaa au ugonjwa-- amani tu na mapatano milele!
Inaonekana kama tutaweza kutenda mambo mengi sana: Kujenga nyumba mashambani kulingana na ndoto zetu, kupanda bustani yetu wenyewe.


123

Yesu, Muumbaji, atakuwa pale kutufungulia mafumbo ya Uumbaji.
Daima tutakuwa tukijifunza mambo mapya.
Tutaweza kusafiri wakati wowote tupendao.


124

Tutakua na wasaa wa kuwa na marafiki zetu na wale tuwapendao.
Na kila Sabato tutakuwa tukimsifu Mungu na tukiimba pamoja na malaika na Yesu -- wakati wetu wa pekee wa kushiriki pamoja na Bwana wetu.
Ndiyo, waweza kuuliza, Twawezaje kuwa na uhakika ya kwamba tutakuwa pale?
Jibu ni rahisi.
Biblia, ufunguo wetu mkuu, yasema:



125

(Fungu: Wagalatia 3:29)
Na kama ninyi ni wa Kristo, basi mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi.
Wagalatia 3:29.


126

Kwa maneno mengine, ukimkubali Yesu kama Mwokozi wako ahadi ambayo Mungu alimpa Ibrahimu ni yako pia.
Tunapojifunza Biblia, inapendeza kutambua ya kwamba



127


Sura tatu za awali zinaeleza jinsi Mungu alivyoiumba dunia na nyumba ya Adamu na Hawa iliyokuwa kama paradiso. Lakini Adamu na Hawa wakapoteza vyote.

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!



128

Sura tatu za mwisho za Biblia zinatupatia picha kabla haijatokea ya mpango wa Mungu wa kurejesha kile Adamu na Hawa walichopoteza- kesho yenye kupendeza ambapo ndoto zetu njema sana zitakapotimia!


129

Miaka kadhaa iliyopita, mashua iliyokuwa ikisafirisha kondoo ilipotea kwenye ukungu katika Bahari ya Kaskazini. Mashua iliambaa ambaa bila mwelekeo kwa muda wa siku tatu. Kondoo waliokuwemo wakakataa kula majani yaliyokaushwa. Walikimbilia upande mmoja na kuanza kulia. Wakaendelea baa baaa baaaaa baa. Nahodha na mabaharia walishangaa sana. Walijiuliza kwanini? Mara ukungu ukatoweka. Mashua ilikuwa yadi chache karibu ya pwani ya Scotland.

Kondoo walikuwa wamepata harufu ya nyasi mbichi zilizokuwa zimekatwa vizuri na kuwekwa katika mashamba mazuri ya Scotland. Walikataa kula zile nyasi zenye umri wa siku kadhaa, nyasi kavu ambazo wenyewe walikuwa wamejaribu kuwalisha.



130

Tunapopata harufu ya mbinguni, tunarekebisha vipaumbele vyetu. Tupatapo harufu ya umilele, kila kitu hupangika mahali pake. Tunatamani nchi nyingine. Tunataka kuwa katika pwani ya umilele. Je, unatamani sana nyumbani mbinguni? Je, una tamani kuwa pale?

Je, ni tamaa ya moyo wako kuishi pamoja na Kristo katika utukufu milele? Je, ungelipenda kusema, Ndiyo, Bwana, ninataka kuwa pamoja nawe. Ninatamani kuwa pamoja nawe milele na milele na milele?



131

(Fungu: Ufunuo 22:17)
Mungu anakupatia mwaliko: Na Roho na Bibi-arusi wasema, 'Njoo!' Ufunuo 22:17.

# 25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!


132

Usiliweke pembeni!
Waweza kuwa sehemu ya kesho ya ajabu sana ya Mungu. Mkaribishe moyoni mwako na mbinguni patakuwa nyumbani kwako!

25 - Yaliyo Bora Zaidi Yanakuja!